

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Kumi na Nne - Tarehe 6 Mei, 2016**

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

**DUA**

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

**MHE. VICKY P. KAMATA (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA):**

Taarifa ya Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

**MHE. CECILIA D. PARESSO (K.n.y MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI):**

Taarifa ya Msemadi Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

**NAIBU SPIKA:** Katibu!

**NDG. JOSHUA CHAMWELA- KATIBU MEZANI:** Maswali.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 110

### **Utengenezaji wa Barabara ya Kutoka Njanne hadi Nandete kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE** aliuliza:-

Moja ya matukio makubwa ya kihistoria katika nchi yetu ni vita ya Majimaji iliyopiganwa kati ya mwaka 1905 – 1907 kati ya Watanganyika na Wajerumani. Pamoja na kufahamu kwamba vita hivyo vilienea katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu, lakini vilianza katika Kijiji cha Nandete, Wilaya ya Kilwa; Serikali inaonesha jitihada mbalimbali ya kuienzi historia hiyo, ikiwa ni pamoja na kujenga mnara katika Kijiji hicho:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza barabara ya kutoka Njanne hadi Nandete kwa kiwango cha lami ili kulifanya eneo hilo la kihistoria kufikiwa kwa urahisi na kuliongezea umaarufu kwa kutembelewa na watalii hususani wa kutoka Ujerumani jambo ambalo litaiongezea mapato Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa na Taifa kwa ujumla.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vedasto Edgar Ngombale, Mbunge wa Jimbo la Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa kujenga barabara ya lami kwenda eneo hili la kihistoria ni la msingi, lakini kwa sasa wakati Serikali inajenga barabara kuu zote nchini kwa kiwango cha lami hasa zikiunganisha Makao Makuu ya Mikoa yote. Hata hivyo, Serikali imekuwa ikitenga bajeti ya fedha kwa ajili ya matengenezo ili kuifanya ipitike wakati wote.

Kupitia Wakala wa barabara Mkoa wa Lindi, katika mwaka wa fedha 2015/2016, zilitengwa shilingi milioni 58.8 kwa ajili ya matengenezo ya kawaida kilomita 43 na matengenezo ya muda maalum kwa kiwango cha changarawe urefu wa kilomita sita, kwa jumla ya gharama ya shilingi milioni 192.3. Matengenezo ya barabara hii yameanza chini ya Mkandarasi Ungando Contractors Company wa Kibiti – Rufiji. Aidha, katika bajeti ya mwaka 2016/2017, barabara hii iko katika mpango wa kufanyiwa matengenezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa kilomita 10 zinazohudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, katika mwaka 2015/2016, zimetengwa shilingi milioni 70 ambazo zitatumika kwa ajili ya matengenezo ya muda maalum kwa urefu wa kilomita nane. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, zimetengwa shilingi milioni 967.6 ambazo zitatumika kwa ajili ya matengenezo ya barabara katika Wilaya ya Kilwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Vesto Ngombale swalii la nyongeza.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa vita ya Majimaji au harakati za awali za kudai uhuru wa Tanganyika zilitokana na chokochoko na misingi imara ya kukataa kuonewa na kudai uhuru kulikofanywa na majemedari wetu wakati wa vita vya Majimaji. Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga barabara hii ili kuwawezesha Watanzania kwenda katika eneo hilo wakajifunze namna gani nchi yetu ilivyojengwa katika misingi ya kudai haki? (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa kuwa barabara hii haipitiki kabisa Serikali ina mpango gani wa kuweka lami katika sehemu korofi kwa mfano mlima Ndunu, Mlima Ngoge pale Chumo, Mlima Kinywanyu na Mlima Karapina pale Kipatimu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba umuhimu wa barabara hii na Mheshimiwa Mbunge amesema kwamba sehemu hii ndiyo chemichemi za harakati ya ukombozi wa nchi yetu. Naomba nikiri kwamba, kuna maeneo mengi sana ya kijigrafia ambayo wakati wa uhuru kama Tanzania tulipokuwa tunaenda katika mchakato walishiriki kwa kiwango kikubwa sana katika kufanikisha uhuru wa nchi yetu, nawapongeza sana ndugu zetu wa Kilwa katika hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakiri wazi kwamba kwa sababu umuhimu wa barabara hii kama nilivyosema awali katika jibu langu, tukirejea tena marejeo ya llani ya Chama cha Mapinduzi, lengo lake kubwa ni kuhakikisha wananchi wanafikiwa wa maeneo mbalimbali. Mheshimiwa Ngombale tutafanya juhudii siyo hapo Kilwa tu, isipokuwa maeneo mbalimbali. Ndiyo maana Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilikuwa ikifanya mikakati katika maeneo mbalimbali, tulianza hasa katika miji tumeenda katika halmashauri, lengo letu ni kwamba maeneo mbalimbali yaweze kufikika chini ya miradi yetu ambayo sasa hivi tuna mradi wa *TSP Project* ambayo inahusisha ujenzi wa miundombinu ya barabara za lami katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili litakuwa katika mpango wetu, mkakati mpana wa kuhakikisha Halmashauri nyingi zinafikiwa na haya ni mambo ambayo tunayafikiria, ndiyo maana hata ukiangalia bajeti yetu ya mwaka huu tuna bajeti takribani ya bilioni 43 kwa ajili ya kuondoa vikwazo, lakini bilioni zaidi ya 200 kwa ajili ya kuhakikisha Halmashauri ziweze kufikiwa vizuri. Kwa hiyo, ni mambo ambayo Serikali yetu inayaangalia na ndani ya miaka mitano tuna imani tutafanya mambo makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lile la kuhusu sasa vile vipande korofi ikiwezekana viwekewe lami na najua Halmashauri ya Kilwa jinsi gani jiografia yake ilivyo na wakati mwingine malori yanashindwa kupanda. Tutawaelekeza wenzetu wa TANROAD ambao tunashirikiana nao kwa karibu zaidi na barabara takribani kilomita 48 zinahudumiwa na TANROAD, tutahakikisha Serikali inayapa kipaumbele yale maeneo korofi ambayo mvua ikinyesha barabara hazipitiki kwa kuyafikiria kwa jicho la karibu zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gekul

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swalii moja la nyongeza. Pamoja na mikakati ya Serikali kujenga barabara za lami, lakini kuna ahadi ya Mheshimiwa Rais ambayo aliitoa katika maeneo yetu wakati anaomba kura, ya ujenzi wa barabara za lami. Katika Bunge hili tuliomba tupatiwe *time frame* kwamba ni muda gani hizi ahadi zinatekelezwa. Nataka kufahamu ni lini Mheshimiwa Waziri atatuletea ratiba ya ujenzi wa barabara hizo za lami kwa ahadi ya Rais ili tufuatilie kwa karibu ikiwemo Jimbo langu la Babati Mjini kilomita ishirini za lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI jibu fupi tafadhal!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ni lini, kifupi *time frame* ya ujenzi wa utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, imeainishwa ndani ya miaka mitano 2015-2020. Jukumu letu kubwa ni kuhakikisha ndani ya kipindi hiki zile ahadi ambazo tumeahidi kwa kadri ilani yetu ilivyojielekeza, tutajitahidi kwa kadri iwezekanavyo, ili mwisho wa siku tuone kwamba ilani yetu imetekelizwa kwa ajili ya kuwapatia wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania maendeleo ya kutosha na siyo Babati peke yake, isipokuwa kwa Tanzania nzima kwa mujibu wa Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi.

Na. 111

### **Kurekebisha Mishahara ya Walimu Waliopandishwa Vyeo**

**MHE. DOTO M. BITEKO** aliuliza:-

Je, kwa nini Serikali inachukua muda mrefu sana kurekebisha mishahara ya Walimu baada ya kupandishwa vyeo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko, Mbunge wa Bukombe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba miaka ya nyuma kulikuwepo na ucheleweshaji wa kurekebisha mishahara kwa kuwa mfumo wa taarifa za kiutumishi na mishahara wa wakati huo ulimtaka kila Mwajiri kuwasilisha marekebisco ya Watumishi wake Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka 2012 Mfumo huu wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara uliimarishwa kutoka Toleo la 7 kwenda Toleo la 9 la Lawson ambapo mwajiri alisogezewa huduma ya kufanya marekebisco mbalimbali ya kiutumishi yanayotokea katika ofisi yake bila ya kulazimika kusafiri kwenda Dar es Salaam. Utaratibu huu umekuwa na manufaa ambapo kwa sasa mabadiliko mbalimbali ya kiutumishi yanafanywa na mwajiri kwa kuzingatia mzunguko wa malipo ya mishahara kwa kila mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na utaratibu huu mzuri, mazingira machache yanayoweza kuchelewesha marekebisco ya mishahara kufanya kwa wakati, kutokana na kuingizwa kwa taarifa za watumishi kwenye mfumo baada ya orodha ya malipo ya mishahara katika mwezi husika kufungwa, au waajiri kufanya mabadiliko bila ya kuweka taarifa muhimu hususan viambatisho kama vile barua za kupandishwa cheo na taarifa kutumwa, zikiwa na makosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujitia Bunge lako Tukufu, kuwataka waajiri wote kufanya marekebisco ya mishahara kwa watumishi wote kwa wakati kama ambavyo imekuwa ikielekezwa na Serikali ili kuепusha ucheleweshaji wa haki za watumishi.

**MHE. DOTO M. BITEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake, vilevile niwashukuru sana ndugu Thadei Mushi kwa namna wanavyotupa ushirikiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili madogo ya nyongeza; kwa kuwa Serikali inafahamu baada ya kuwa imempandisha daraja Mwalimu na kumrekebishia mshahara inachukua muda mrefu sana. Utumishi hawaoni kuwa nao imefika wakati wachukue ile model wanayochukua watu wa Nishati na Madini iijulikane kabisa kwamba ukipandishwa daraja kwa kipindi fulani mshahara wako utakuwa umerekebishwa ili watumishi hawa wawe na uhakika?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, kwa kuwa malimbikizo ya mshahara baada ya kurekebishwa mshahara yanachukua muda mrefu, Serikali inawaambia nini watumishi wa umma hususan Walimu kwamba watalipwa lini, kwa uharaka zaidi malimbikizo ya mshahara haya ambayo yanachukua miaka mingi sana kabla ya kulipa?

#### **WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI NA UTAWALA**

**BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza kabisa nimshukuru kwa namna ambavyo amekuwa akifuatilia sana masuala mazima ya ustawi na maslahi ya utumishi wa umma hususan Walimu. Natambua ametokana na Chama cha Waalimu Tanzania, nakupongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Biteko alitaka kufahamu endapo Serikali labda kwa nini isifikirie mtumishi anapopandishwa daraja moja kwa moja aweze kuwa amefanyiwa marekebishesho yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nilieleza kinachofanyika kuititia Mfumo huu wa Taarifa za Kiutumishi na nashukuru kwamba ameweza kumpongeza Afisa Utumishi aliye kati Wilaya ya Bukombe kwa kazi nzuri anayoifanya, wanapokuwa Kamati ya Ajira imeshampatia barua ya kupandishwa cheo, kinachofanyika wana-post katika mfumo huu wa Lawson wa taarifa za kiutumishi na mishahara, lakini ni jukumu sasa la Utumishi kuhakikisha kwamba, mtumishi huyu aliye pandishwa cheo kwanza taarifa zake za tathmini kwa uwazi kwenye OPRAS zipo, kuhakikisha kwamba katika muundo wa utumishi kweli anastahili kupanda katika ngazi hiyo na kuto kana na sifa na uzoefu amba o umeainishwa katika muundo wa maendeleo ya utumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuhakikisha kwamba ni kweli ana utendaji mzuri pamoja na uadilifu. Bado naendelea kuhimiza niwaombe sana waajiri pamoja na Maafisa Utumishi amba wanasi mamia suala zima la mfumo huu, kuhakikisha kwamba wanapandisha kwa wakati vilevile wanafanya marekebishesho kwa wakati kwa kuzingatia maelekezo mbalimbali ambayo tumewapatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa madeni ya Walimu napenda tu kusema kwamba kwa kiasi kikubwa madeni haya yamelipwa, zaidi ya

Walimu 13,000 tayari malimbikizo yao wameshalipwa ya mishahara, vilevile kwa upande wa Hazina madeni mbalimbali yamekuwa yakilipwa. Bado naendelea kusisitiza tena kuhakikisha kwamba, waajiri wanalipa kwa wakati malipo haya na kuhakikisha kwamba wanayatengea bajeti katika mwaka husika, vile vile wapandishe watumishi kwa kuzingatia muundo na kwa kuzingatia kwamba wana ikama hiyo na bajeti kwa sababu wasipofanya hivyo ndiyo maana wanasababisha malimbikizo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile changamoto nyingine ambayo tumekuwa tikiipata, unakuta mfumo wetu wa Lawson una-calculate automatic arrears, wakati huo huo unakuta Mwajiri mwingine naye analeta manual arrears, kwa hiyo tusipokuwa makini kufanya uhakiki unaweza ukajikuta umemlipa mtumishi mmoja malipo ambayo hayastahiki. Bado naendelea kusisitiza kwamba, Serikali inatambua umuhimu wa watumishi na itakuwa ikiendelea kulipa kila mara kwa kadri ambavyo uwezo umekuwa ukiruhusu.

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Khamis Mtumwa Ali, Mbunge wa Kiwengwa, sasa aulize swali lake. Mheshimiwa Khamis Mtumwa Ali! Hamna anayetaka hata kumuulizia swali lake maana simuoni. Mheshimiwa Khatib!

Na. 112

### **Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**

**MHE. KHATIB SAID HAJI (K.n.y. KHAMIS MTUMWA ALI)** aliuliza:-

Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inafanya ukaguzi katika Taasisi za Tanzania Bara na Zanzibar:-

Je, Ofisi hii inashirikiana vipi wakati wa kufanya ukaguzi wa Taasisi za Muungano na Ofisi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Zanzibar?

### **NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khamis Mtumwa Ali, Mbunge wa Jimbo la Kiwengwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inafanya ukaguzi katika Taasisi zote za Serikali za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Ibara ya 143 (2)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya mwaka 1977. Ibara hiyo ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

inampa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, mamlaka ya kufanya ukaguzi wa hesabu za mihimili yote mitatu ya dola, Serikali, Bunge na Mahakama na kutoa ripoti ya ukaguzi angalau mara moja kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mipaka ya kufanya kazi baina ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Jukumu la ukaguzi wa Taasisi za Muungano lipo kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Wakati jukumu la Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ya Zanzibar ni kukagua Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mipaka hiyo ya kazi, kumekuwepo na ushirikiano katika kufanya ukaguzi wa pamoja kati ya Ofisi hizi kuu mbili kwa lengo la kujenga uwezo na kubadilishana uzoefu. Kwa mfano ukaguzi wa ujenzi wa Ofisi za Wabunge kwenye Majimbo, ukaguzi wa bahari ya kina kirefu na mradi wa kupambana na UKIMWI Zanzibar. Ukaguzi wa miradi hii ulifanywa kwa ushirikiano wa pande zote mbili.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri amejibu baadhi ya maeneo ambayo Mkaguzi Mkuu wa Muungano amekuwa akiyafanya ukaguzi. Kwa nini mpaka sasa Mfuko wa Kuchochera Maendeleo wa Jimbo, haujawahi kufanyiwa ukaguzi na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hilo tu. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema ukaguzi wa Mfuko wa Jimbo hufanywa na Mkaguzi Mkuu na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini kwa pamoja huwa wanashirikiana kufanya ukaguzi huu na Mkaguzi wa Zanzibar, kwa upande wa Zanzibar. Kwa swali lako la kwa nini, nina imani kuwa Mfuko huu utafanyiwa ukaguzi pale muda utakapofika na ukaguzi huo utafanyika.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Mkaguzi Mkuu huwa anakagua mashirika mengine, lakini ningependa kujua au kwa niaba ya wengine pia, yeye huwa anakaguliwa na nani?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mkaguzi Mkuu naamini yeye pia hujikagua mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango.

Na. 113

### **Kupunguza Misamaha ya Kodi Nchini**

**MHE. UPENDO F. PENEZA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kupunguza misamaha ya kodi kufikia asilimia moja (1%) ya GDP?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Upendo Furaha Peneza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, azma ya Serikali ya kupunguza misahama ya kodi kufikia asilimia moja ya pato la Taifa ni mkakati unaotekelezwa kwa awamu na kwa kuzingatia mazingira ya kiuchumi, kijamii na sheria zilizopo. Juhudi za kutekeleza azma ya kupunguza misamaha ya kodi zilianza kufanyika mwaka 2010/2011 baada ya kubaini kuwa, kwa wastani misamaha yetu ilikuwa imefikia takribani asilimia 3.2 ya pato la Taifa kwa mwaka, katika kipindi cha mwaka 2006/2007 hadi 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2009/2010 Serikali iliamua kupitia upya sheria zinazohusu misamaha ya kodi ili kuondoa misamaha ambayo haikuwa na tija katika Taifa letu. Katika mapitio hayo Serikali ilibaini kuwa takribani asilimia 60 hadi asilimia 64 ya misamaha yote ya kodi ilikuwa inatokana na kodi ya ongezeko la thamani – VAT. Baada ya kubaini hali hiyo, Serikali kupitia Bunge lako Tukufu ilifanya maboresho ya Sheria ya VAT, Sura ya 148 na kuondoa misamaha ambayo haikuwa na tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua mbalimbali ambazo zimechukuliwa, hususan za kurekebisha upeo wa misamaha inayotolewa chini ya Kituo cha Uwekezaji – TIC na Sekta ya Madini, zimesaidia kupunguza misamaha ya kodi hadi kufikia asilimia 1.9 ya pato la Taifa kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 kiasi cha kodi kilichosamehewa ni shilingi milioni 564,106.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mwenendo huu ni matarajio yetu kuwa kiasi cha msamaha wa kodi katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 kitakuwa ni shilingi milioni 752,141.9 sawa na asilimia 0.84 ya pato la Taifa. Kutungwa upya kwa Sheria ya VAT ni eneo moja ambalo limeleta ufanisi mkubwa katika kutimiza azma yetu ya kupunguza misamaha ya kodi, hadi kufikia asilimia moja ya pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, baadhi ya misamaha ya kodi haiepukiki katika mifumo ya kodi hapa nchini na popote duniani. Suala la msingi ni kuwa Serikali itahakikisha kuwa misamaha yote ya kodi inatolewa kwa mujibu wa Sheria za Kodi zilizopo.

Katika siku za usoni usimamizi wa misamaha utajengwa katika mifumo imara ya udhibiti inayozingatia matumizi ya teknolojia. Lengo la muda mrefu ni kuweka mfumo wa misamaha ya kodi unaokubalika Kimataifa, pia misamaha hiyo iwe ni ile inayochochea ukuaji wa uchumi na ustawi wa jamii.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Kwa kuwa, ulipaji wa kodi ni suala la kizalendo na kwa kuwa, suala la ulipaji wa kodi ni wajibu wa kila mwananchi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile kwa kuwa Wabunge, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Majaji, ni wanufaika kutokana na mishahara na faida mbalimbali tunazopata kutokana na kodi ambazo wananchi wanalipa.

Je, ni lini Serikali sasa italeta marekebisho ya *Income Tax* inayompa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Rais wa Zanzibar msamaha wa kodi kwenye mishahara yao? Pia ni lini Serikali italeta marekebisho kwenye sheria inayowapa Majaji wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania misamaha ya kodi kwenye mishahara yao ili wote kwa pamoja tutimize wajibu wa kiraia wa kulipa kodi? Ahsante. (Makofii)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyokiri yeye mwenyewe kulipa kodi ni haki ya kila mtu na ni wajibu wa kila mtu. Napenda kumhakikisha Mheshimiwa Upendo pamoja na Bunge lako Tukufu kwamba, muda sahihi utakapofika wa kuleta marekebisho ya Sheria hii tutaleta hapa Bungeni na marekebisho yatafanyika na watu wote watalipa kodi kwa msingi sahihi unaotakiwa. Pia naomba nimkumbushe kuwa, siyo kwamba Mheshimiwa Rais halipi kodi! Mheshimiwa Rais analipa kodi. Nashukuru.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, *Income Tax* ya mwaka 2004, Mheshimiwa Rais halipi kodi!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Peneza, huo siyo utaratibu. Mheshimiwa Kiula swali la nyongeza!

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi kuuliza swali la nyongeza. Ili misamaha ya kodi iweze kupungua kufikia asilimia moja ni pamoja na kuhakikisha kwamba sheria zilizopitishwa na Bunge hili zinatikelezwa kikamilifu. Kumekuwa na *parallel system*, mfano *TIC* kumekuwa na kikao cha *TIC* na *TRA* ambapo *TIC* ikipokea maombi ya wale wanaoitwa

Strategic Investors wanakaa kikao na wanachagua baadhi ya bidhaa wanazipa msamaha wa kodi. Jambo hili litakoma lini kufanyika? Kwa sababu, pia, linawaweka katika mtego wafanyakazi wa Mamlaka ya Mapato ambao wakishiriki kikao hicho ambacho kinatoa msamaha...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa naomba ufupishe swali lako ni la nyongeza, naomba ufupishe.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, lini Serikali itahakikisha kwamba, Sheria za Kodi zinatekelezwa kama zilivyopitishwa na Bunge? Kusiwe kuna parallel system?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumhakikisha kwamba, sheria hizi zinatekelezwa kama ambavyo zimepitishwa na vikao hivi huwa vinafanya kwa pamoja kati ya wataalam wetu waliopo kwenye TIC na wale wa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Inapofikia sehemu ya discussion kuhusu kodi wataalam hawa hukaa pamoja kuona ni jinsi gani ya kutoa misamaha hii ya Kodi. Hakuna sehemu ambako Wataalam wa upande mmoja hukaa peke yao katika kufikia maamuzi haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalithibitishia Bunge lako sheria zetu kama zinavyopitishwa na Bunge zinatekelezwa kama tulivyopitisha.

Na. 114

### **Mkoa wa Katavi Kutokuwa na Viwanda**

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE (K.n.y. MHE. TASKA R. MBOGO)** aliuliza:-

Mkoa wa Katavi ni mionganini mwa Mikoa ambayo haina kiwanda hata kimoja;

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga viwanda katika Mkoa wa Katavi?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa wanawake na vijana wa mkoa huo?

### **WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa ya sensa ya viwanda iliyofanyika mwaka 2015 ni kweli kuwa Mkoa wa Katavi hauna viwanda vikubwa. Hata hivyo, Mkoa huo una jumla ya viwanda vidogo 221 ambapo kila kiwanda kina uwezo wa kuajiri wafanyakazi wasiozidi 10. Aidha, Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (*SIDO*) linatoa huduma katika viwanda vidogo vya usindikaji wa vyakula na asali vipatavyo 26, viwanda vidogo vya kukoboa mpunga tisa, viwanda vya kusaga unga 11 na viwanda vidogo vya kubangua karanga saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na juhudzi za Serikali za kuhamasisha na kuboresha mazingira yanayovutia wawekezaji wa ndani na nje, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Katavi kuwa, tutaongeza juhudzi za kutekeleza jukumu la kuhamasisha viwanda kwenda Katavi. Aidha, nimwombe Mheshimiwa Mbunge na wadau wote wa maendeleo kusaidiana na Serikali kuhamasisha ujenzi wa viwanda Mkoa wa Katavi kwa kulenga malighafi zinazopatikana sehemu hiyo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia *SIDO* imeendelea kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa wananchi wa Mkoa wa Katavi wakiwemo wanawake na vijana. Kati ya mwaka 2007 mpaka 2015 *SIDO* ilitoa mafunzo yenye nia ya kutoa maarifa na kujenga uwezo wa stadi kwa wajasiriamali wapatao 520. Mafunzo hayo yalitolewa katika nyanja zifutazo:-

Utengenezaji wa mizinga ya nyuki ya kisasa, usindikaji wa vyakula, utengenezaji wa sabuni, utengenezaji wa chaki, mafunzo juu ya ujasiriamali, utengenezaji wa majiko ya kisasa yanayotumia nishati ndogo, mfumo wa ufuatiliaji bidhaa za asali, utengenezaji wa mitambo ya kukausha mazao ya kilimo yanayotumia nishati ya jua na usimamizi wa masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, *SIDO* imekwishapata ofisi ya kufanya kazi katika Mkoa wa Katavi kwa lengo la kusogea huduma karibu na wananchi. Hatua hiyo itapanua wigo wa utoaji mafunzo ya ujasiriamali na usindikaji wa vyakula kwa wanawake na vijana katika Mkoa wa Katavi.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza maswali ya nyongeza. Kwanza napenda kuishukuru Serikali kwa kutambua uwezo wa wajasiriamali wa Mkoa wa Katavi ambaeo bado wana viwanda vidogovidogo, lakini kwa kuwa, Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi inalenga uchumi wa kati, je, Serikali inasema nini kuwekeza sasa katika viwanda vikubwa kutokana na malighafi zinazopatikana Mkoa wa Katavi ili tuweze kufikia malengo ya uchumi wa kati?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili; kwa kuwa, Mkoa wa Katavi una wanyama wengi wafugwao hususan ng'ombe. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwekeza kiwanda cha kusindika mazao ya ng'ombe, hasa katika Jimbo la Kavuu?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu haja ya kujenga Kiwanda cha Nyama Katavi na Sumbawanga kule, Mheshimiwa Mbunge Wataalam wa Wizara yangu leo wako hapa *full team*, unione na uwasiliane na Mheshimiwa Zungu kuna Mwekezaji anatafuta mahali pa kujenga viwanda vikubwa vyta nyama, nikupe offer leo hii tuonane, huyo mwekezaji aende Katavi na Sumbawanga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Serikali kujenga viwanda vikubwa. Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe, ananishawishi kusoma hotuba yangu kabla ya wakati! Mkakati wetu ni kuhakikisha viwanda vidogo sana tunavipa nguvu viwe viwanda vidogo na viwanda vidogo viwe viwanda vyta kati na viwanda vyta kati viende viwe vikubwa, tunafanya *business graduation*. Kwa hiyo, tutawapeleka taratibu hasa wazawa, kusudi twende sambamba tufike kwenye viwanda vikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la msingi kama kuna malighafi ambayo inatupa faida ya kiulinganisho niko tayari wakati wowote tusaidiane Wabunge na Serikali ya Katavi, mniambie nini kinawapa faida ya kiulinganisho ili kusudi nilete wawekezaji. Wawekezaji wote watakuwa hapa mpaka Jumatatu, kila mtu ajichukulie wa kwake pale nje.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii niulize swalifupi. Kwa kuwa, suala la Katavi linafanana sana na la Mkoa wa Kigoma ambao hatuna kiwanda hata kimoja na rasilimali ziko za kutosha, hususan katika Jimbo la Buyungu ambako kuna rasilimali kama mihogo, mpunga na kadhalika. Je, Waziri yuko tayari kuja kujenga viwanda katika Wilaya ya Kakonko? Ahsante.

**WAZIRI WA VIWANDA BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haijengi viwanda! Serikali inahamasisha Wawekezaji wa ndani na nje ya nchi waje kujenga viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwape habari nzuri Kigoma; kuna kampuni inaitwa Kigoma Sugar, tumewapa hekta 47,000 watajenga Kiwanda cha Sukari kinachozalisha tani 120,000 watakapoanza kazi, nimewaambia ifikapo Septemba matrekta yote yaende kulima kwetu Kigoma ili kusudi tuzalishe sukari. Mambo mazuri yanakuja Kigoma. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shekilindi swalifupi!

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa, Wilaya ya Lushoto inafahamika kwamba ni ya kilimo cha matunda na mbogamboga. Je, ni lini Serikali itajenga kiwanda cha matunda na mbogamboga katika Wilaya ya Lushoto, ili mazao yale yasiendelee kuharibika?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wanamilazimisha kufungua bajeti yangu kabla ya muda, lakini anayelipa mahari anayo ruhusa ya kumwangalia mwari hata kabla ya siku ya harusi!

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kiwanda kinaitwa Sayona kitawekwa Mkoa wa Pwani, kitakuwa na uwezo wa kusindika tani 25,000 kwa mwaka. Kitachukua matunda yote ya ukanda wa Pwani mpaka ukanda wa Ziwa. Kuna kiwanda kinaitwa Osasuna kitajengwa Handeni kwa Msisi, kitaanza kuchakata Nanasi, kitakuwa na uwezo wa kulima nanasi kwa shamba la mwekezaji hekta 3,000 lakini out growers watapewa hekta 17,000 kumzunguka na yule mwekezaji atawajibika kuwasaidia wananchi wazawa namna ya kulima kisasa. Mwaka 2018 Novemba, tunaanza kutoa juice ya kwanza.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea! Mheshimiwa Innocent Seba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, sasa aulize swali lake!

Waheshimiwa Wabunge, naomba tuongee kwa sauti ya chini tafadhalii kwa sababu kuna kelele sana humu ndani.

Na. 115

### **Masoko ya Kimataifa ya Nkwenda na Murongo**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliuliza:-

Ujenzi wa masoko ya Kimataifa yaliyokuwa yakijengwa huko Nkwenda na Murongo yamesimama kwa muda mrefu sana na wananchi wa Wilaya ya Kyerwa walitegemea masoko hayo kwa ajili ya kuuzia mazao yao mbalimbali:-

Je, ni nini kimesababisha kusitishwa kwa ujenzi wa masoko hayo? Na ni lini sasa ujenzi utafufuliwa na kukamilishwa ili kutoa fursa za kufanya biashara na kwa majirani zetu pia?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Seba Bilakwate, Omwanawumkazi, Mbunge wa Kyerwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa miundombinu ya masoko nchini hususan masoko ya mipakani, yakiwemo masoko ya Nkwenda na Murongo ni moja ya maeneo ya kipaumbele cha Serikali yetu. Masoko hayo yakikamilika yatakuwa ni kichocheo kwa wakulima kuzalisha zaidi na wafanyabiashara kuza kwa uhakika, kutokana na kunufaika na soko la pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, masoko ya Kimataifa ya Nkwenda na Murongo ni kati ya masoko matano ambayo yalikuwa yanajengwa kwa kutumia fedha za mradi wa wawekezaji katika Sekta ya Kilimo Wilayani (*District Agricultural Sector Investment Project - DASIP*).

Mheshimiwa Naibu Spika, masoko mengine yaliyonufaika na mradi huo ni Kabanga - Ngara, Lemagwe - Tarime na Busoka - Kahama. Ujenzi wa Masoko hayo ulifika kiwango cha kati ya asilimia 45 mpaka 65 kwa ujenzi na kusimama baada ya mradi wa *DASIP I* kufikia ukomo wake mwaka 2013 na Benki ya Maendeleo ya Afrika iliyokuwa ikifadhili ujenzi huo kusitisha utoaji wa fedha kwa ajili ya mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo jitihada zinafanyika ili kuendelea na mradi wa *DASIP* awamu ya pili ili pamoja na mambo mengine tuweze kukamilisha ujenzi wa masoko yote yaliyokusudiwa yakiwemo masoko ya Nkwenda na Murongo. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kutoka vyanzo vya ndani na wahisani wengine ili kumalizia ujenzi wa masoko hayo muhimu kwa uchumi wa nchi yetu. Kazi ya kuendeleza ujenzi na kukamilisha masoko hayo itaanza pindi Serikali itakapopata pesa hizo.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pia namshukuru Mheshimiwa Waziri lakini sijaridhika na majibu yake. Niliuliza ni lini masoko haya yatafufuliwa kwa sababu haya masoko ni muhimu kwa ajili ya wananchi wa Kyerwa na Waziri mwenyewe anajua wananchi wa Kyerwa wanapata shida hawana mahali pa kupeleka mazao yao. Naomba anieleze ni lini masoko haya yatafufuliwa yaanze kujengwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, naomba Naibu Waziri awaeleze wananchi wa Jimbo la Kyerwa na Watanzania ambao wanunuwa na masoko haya, je, Serikali imetenga pesa kwenye Bajeti ya mwaka huu wa fedha 2016/2017 kwa ajili ya masoko haya kukamilika?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Innocent Bilakwate ameuliza nijibu ni lini? Nimemweleza, *DASIP I* ilikoma, nimewasiliana na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwamba Mpango wa *DASIP II* haujaanza, utakapoanza tuwaweke watu wa Karagwe na Kyerwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina maslahi na sehemu hizi, napenda niseme ukweli, msema ukweli ni mpenzi wa Mungu. Katika bajeti sijaweka lolote kwa ajili ya masoko haya ya Nkwenda na Murongo, lakini kwa ajili ya Nkwenda na Murongo tumeandaa utaratibu ambapo wakulima wa mazao wa Karagwe, hasa maharage tutawaunganisha moja kwa moja na wanunuzi wa Oman na Innocent Bashungwa nimemteua aratibu shughuli hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tuendelee na Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 116

### **Ukosefu wa Maji Safi na Salama**

**MHE. TUNZA I. MALAPO** aliuliza:-

Wananchi wa Jimbo la Nanyamba kwa muda mrefu wamekuwa wakipata shida ya ukosefu wa maji safi na salama:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wananchi hao wanapata maji safi na salama?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalumu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mpango wa kufanya upanuzi wa mradi wa maji wa Kitaifa wa Makonde kutokea katika Kijiji cha Chikunda kuititia Kijiji cha Nyundo hadi Dihamba. Wakazi wapatao 49,206 waishio katika Vijiji 49 vya Halmashauri ya Nyanyamba na Vijiji saba vya Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara watanufaika na mradi huo utakapokamiliika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na tathmini ya awali, upanuzi wa mradi huo utagharimu kiasi cha shilingi billioni 11.4. Utekelezaji wa mradi huo unategemea upatikanaji wa fedha zitakazotengwa na Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Halmashauri ya Nyanyamba ina mpango wa kufanya ukarabati wa miundombinu ya bomba katika miradi ya maji iliyojengwa kwa ufadhili wa AMREF ipatayo 17 inayotumia nishati ya nguvu za juu. Ukarabati huo unatarajiwa kugharimu shilingi milioni 719 na unakadirwa

kuwanufaisha wakazi wapatao 15,433 waishio katika Jimbo la Nanyamba na hivyo kuongeza kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Halmashauri ya Mtwara Vijijiini inaendelea na utekelezaji wa miradi ya maji ya Mbembelo - Mwang'anga na Nanyamba - Maranje. Miradi hii itanufaisha Vijiji vya Mwang'anga, Mbembaleo, Mwamko, Maranje, Mtimbwilimbwi, Mtopwa, Mtiniko, Shaba, Mbambakofi na Mnivata vyenye wakazi wapatao 20,166. Miradi hii itakapokamilika upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wa Halmashauri ya Nanyamba utaongezeka kutoka asilimia 43 hadi asilimia 80.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu hayo ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

(a) Naomba anieleze ni tatizo gani linalofanya Mji huu usipate maji ya kutosha na ya uhakika wakati vyanzo vya maji viro?

(b) Pia ni lini wananchi hawa waliotheseka kwa muda mrefu hasa wanawake watapata maji safi na salama? Nataka *time frame*, ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni matatizo gani yanafanya wananchi hawa wasipate maji. Ni kweli kabisa kwa bahati nzuri Mheshimiwa Mbunge ni shahidi, katika Mikoa na Wilaya ambayo nilitembelea ni pamoja na Wilaya ya Nanyamba. Maeneo yale yana vyanzo vikubwa vya maji vya Mitema na Mkunya. Tatizo ni kwamba huko nyuma tulikotoka upatikanaji wa fedha ulikuwa kidogo siyo mzuri na kwa sababu tumekuwa tunaishi kwa kutegemea wafadhili vile vile. Hilo ndilo ambalo limefanya miradi ile isiweze kukamilika na kutoa maji yale yanayotakiwa kwa matumizi ya wananchi wa Nanyamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ameuliza ni lini. Sasa hivi tumeingia kwenye program ya pili ya maendeleo ya maji ambayo tunatarajia Serikali inatenga fedha na tunaanza kutenga fedha kuanzia mwaka ujao wa fedha, pia wafadhili wametuahidi na kuna juhudini kubwa ambayo inafanywa na Serikali kupitia Waziri wa Fedha, Iakini na Mwanasheria wa Serikali pia ambapo tunaongea na wafadhili waweze kutupatia pesa ili tuweze kukamilisha hii miradi ya Mito ya Mitema na Nanyamba ambayo itahakikisha kwamba vyanzo vya Mitema na Mkunya ili tuweze kuhakikisha maji yanapatikana kwa hizi Wilaya za Nanyamba pamoja na Tandahimba.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndassa swali la Nyongeza

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri, anajua kwamba Mradi Mkubwa wa Maji wa Ziwa Victoria unaanza katika Kitongoji cha Ihelele, Kijiji cha Nyahumango. Cha kusikitisha Mheshimiwa Waziri, sina tatizo na maji kwenda Nzega, kwenda Kahama au sehemu nyingine, pale kwenye chanzo cha maji Ihelele penye matanki makubwa kuna kituo kimoja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri, hivi ungekuwa wewe ndiyo mwenye Jimbo hilo na una Waziri ungejisikiaje?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningekuwa sijafanya ziara ningeshtuka sana, lakini kwa sababu sijawahi kwenda kwenye eneo hilo nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba nitaenda nikaone kwa nini vijiji ambavyo vinazungukwa na matenki makubwa ya maji havipati maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa ziara yangu Mkoa wa Mtwara, nilikwenda eneo la Mbwinji. Eneo la Mbwinji lina matanki makubwa sana ya maji ndiyo chanzo cha maji, kitu cha ajabu nilikuta wananchi wanaokaa lile eneo hawapati maji. Nilivyojaribu kuuliza ikaonekana kwamba maji pale yakishachotwa lazima yapelekwe Masasi kwenda kufanyiwa sasa utibabu, kuwekewa dawa ili yaweze kuwa safi kwa ajili ya matumizi ya binadamu, ndiyo baadaye sasa yaweze kusambazwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipofika pale niliagiza na sasa hivi wananchi wa maeneo yale tayari wanapata maji. Sasa sielewi hilo eneo analogumza Mheshimiwa Mbunge, linaweza likawa na tabia ya kufanana na hiyo kwamba, hapo ndipo wanapochota maji, wanaweka kwenye matenki halafu baadaye yanakwenda kwenye mtambo wa kutibu maji. Sasa, japo sijafika lakini naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hili suala nitalifuatilia na nitamjibu kabla hatujamaliza Bunge hili. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Tuendelee Waheshimiwa, Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde Mbunge wa Mtera sasa aulize swalı lake.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kwanza niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi kwa kura za kishindo jana, sitowaangusha.

Na. 117

### **Mradi wa Maji katika Jimbo la Mtera**

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE** aliuliza:-

Mradi wa Maji wa Kijiji cha Manzase ulishalipiwa nusu ya gharama za mradi na Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Nne.

(a) Je, Serikali ya Awamu ya Tano ina Mpango gani kuukamilisha ili wananchi wa Kijiji hicho wapate huduma ya maji safi na salama;

(b) Kijiji cha Chinoje kilipata Mradi wa *World Bank* na kuchimbwa visima 10 lakini maji hayakupatikana. Je, Serikali ina Mpango gani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lusinde, utaratibu unajua wa namna ya kuuliza swali, hizo salamu ungezileta wakati mwingine. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza Miradi ya Maji ya Vijiji Kumi kwa kila Halmashauri, Halmashauri ya Chamwino inatekeleza miradi kwenye vijiji saba ambapo miradi katika Vijiji vitano vya Mvumi Makulu, Itiso, Mvumi Mission, Chamuhumba na Membe imekamilika na wananchi wapatao 49,000 wanapata huduma ya maji. Mradi wa Wilunze unaendelea kutekelezwa na upo asilimia 60.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi wa maji katika Kijiji cha Manzase umefikia asilimia 40. Kazi zilizofanyika hadi sasa ni ujenzi wa vituo 11 vya kuchotea maji, ujenzi wa nyumba ya mashine na ujenzi wa tanki lenye ujazo wa lita 80,000. Gharama ya ujenzi wa mradi ni shilingi milioni 355, ambapo hadi sasa kiasi cha shilingi milioni 71 kimeshapelekwa kwenye Halmashauri hiyo kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Serikali itaendelea kupeleka fedha ili kukamilisha mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji katika Kijiji cha Chinoje ni kati ya miradi iliyokosa chanzo cha maji wakati wa utekelezaji wa awamu ya kwanza ya Program ya Maendeleo ya Maji. Utafiti wa chanzo kingine cha maji unafanyika na ujenzi wa mradi utafanyika katika mwaka wa fedha 2016/2017.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Swalii la kwanza, kwa kuwa wananchi wa Manzase wanakabiliwa na kero kubwa ya maji na Mkandarasi hayupo kwenye eneo la Site, je, Naibu Waziri yuko tayari kuongozana na mimi kufika Manzase kwenda kuonana na wananchi na kuwashakishia mwenyewe kwamba kweli mradi ule utakamilika?

Swalii la pili, kwa kuwa Mradi wa *World Bank*, maeneo mengi maji yalipochimbwa vijiji hayakupatikana na wananchi wanaendelea kukabiliwa na shida kubwa ya maji. Serikali ina mpango gani wa kukamilisha miradi ya maji au Je, wananchi waendelee kusuburi tena, hawana mpango wowote Serikali mpaka Benki ya Dunia itusaidie tena? Ahsante. (Makofii)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kijiji cha Manzase, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi ni kweli Mkandarasi alikimbia na tayari tumeshafanya ufuutiliaji ni kwa nini alikimbia, tumemwagiza katika muda wa siku kumi arudi eneo la mradi, kama hatarudi basi tumeshapanga kuchukua hatua nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi huo utakamilika kabla ya nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha tunaouanza mwezi Julai. Pia sina tatizo kwa ruhusa ya Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa sababu hapa ni Dodoma sina tatizo Mheshimiwa Mbunge, tunaweza kwenda huko tukawaambia wananchi ni lini huo mradi utakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili Mheshimiwa ameuliza kwamba kuna miradi mingi ya *World Bank* ambayo ilifanyiwa kazi, lakini kuna maeneo ambayo maji hayakupatikana. Je ni lini sasa miradi hii itakamilishwa au tusubiri tena *World bank*?

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na Program ya kwanza ya Maendeleo ya Maji ambayo ilikwisha mwezi Desemba mwaka 2015, sasa tunaingia katika program ya pili. Maeneo yote yale tulikuwa tumeyapanga kwamba tunachimba maji, lakini katika kuchimba maji hayakupatikana, maeneo hayo mengi tumeshayafanya utafiti, tumepata vyanzo vingine vya maji, kwa hiyo kuanzia bajeti ya mwaka wa fedha unaokuja 2016/2017, tutahakikisha kwamba maeneo hayo tunatekeleza hiyo miradi ili wananchi waweze kupata maji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Risala Kabongo

**MHE. RISALA S. KABONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa kuanza kunipatia maji

katika vijiji vyangu vya Udadai, Ngiresi na Sokontuu. Swalii langu ni kwamba, kumekuwa na tatizo kubwa la wizi wa maji maeneo mbalimbali nchini. Mfano, katika Jiji la Arusha asilimia 40 ya maji yanaibiwa; je, Serikali imejipangaje kukabiliana na tatizo hili kubwa la wizi wa maji. Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Serikali tayari imefanikiwa kupata fedha zaidi ya dola milioni 210 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa ajili kutekeleza mradi mkubwa wa maji katika Jiji la Arusha. Mradi huo unaanza kutekelezwa katika mwaka fedha wa 2016/2017, utakuwa ni mradi wa miaka mitatu baada ya mradi huo kukamilika, Jiji la Arusha litapata maji asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Jiji la Arusha lina upungufu mkubwa wa maji lakini juhudhi mbalimbali zinafanyika katika hiki kipindi kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge amezungumzia kuhusu upotevu wa maji, ni kweli upotevu wa maji upo kwa sababu miundombinu ambayo ipo ni ya zamani, kwa hiyo maji yanavuja na pili, hiyo element ya wizi nayo ipo. Mamlaka ya Maji ya Arusha inaendelea kufanya juhudhi kupunguza upotevu wa maji na katika mradi unaokuja iko item ya kutekeleza hiyo kuhakikisha kwamba tunapunguza upotevu wa maji na tunatarajia kwamba upotevu utapungua mpaka kufika asilimia 30.

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalii lake.

Na. 118

### **Matukio ya Kubakwa na Kulawitiwa Watoto**

**MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA** aliuliza:-

Matukio ya kubakwa na ulawiti kwa watoto nchini yamekuwa yakijirudia mara kwa mara na watuhumiwa walio wengi huachiwa au humalizana na wazazi wa waathirika kifamilia:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa kesi hiso hazimalizwi kifamilia?

(b) Je, ni mkakati gani umewekwa ili kuhakikisha kuwa watuhumiwa hao wanapopatikana na hatia wapewe adhabu kali ili iwe fundisho kwa wengine wenye nia mbaya?

(c) Je, watoto waliopatwa na matukio hayo wamewekewa mazingira gani ili kuwaondoshea msongo wa mawazo na kuendelea na elimu bila kubughudhiwa na wenzao.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Agelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b), na (c), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli matukio ya kubakwa na kulawitiwa, watoto yamekuwa yakinotoka na kuripotiwa katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Pia ni kweli kuwa baadhi ya kesi za aina hiyo zimekuwa zikimalizwa kifamilia kwa maridhiano kati ya mtuhumiwa na wazazi wa mtoto muathirika. Hivyo kuwapa shida sana Wapelelezi wa kesi hizo kupata ushahidi.

(a) Tatizo la kuficha ushahidi na kuzimaliza kesi hizo kifamillia haliwezi kumalizwa na Vyombo vya Dola vinavyofanya uchunguzi peke yake bila ushirikiano na wananchi wanaishi na watuhumiwa. Hivyo, Serikali imekuwa ikitoa elimu kwa umma kwa kuficha ushahidi na kuyamaliza matukio hayo ati kifamilia siyo kosa la jinai peke yake, bali vile vile, utaratibu huo unachochea vitendo hivyo kuendelea katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ili kuweka mazingira rafiki kwa waathirika na wananchi wenye taarifa au ushahidi wa aina hiyo, Serikali imeanzisha madawati ya jinsia katika vituo mbalimbali vya Polisi yanayopokea taarifa kutoka kwa wananchi na kuliwezesha Jeshi la Polisi kuendesha upelelezi kwa ufanisi. Pindi tukio la kubaka au kulawiti linaporipotiwa upelelezi hufanyika na mtuhumiwa hufunguliwa mashtaka mara moja. Kwa utaratibu huu Serikali inahakikisha kuwa matukio haya hayamalizwi nje ya utaratibu wa haki jinai.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kuitia Bunge lako Tukufu tumetunga sheria zenyе adhabu kali kwa watuhumiwa wa makosa hayo, wanapopatikana na hatia. Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16, imeweka adhabu ya kifungo cha maisha kwa mtu yeyote anayekutwa na hatia ya kumbaka msichana, hicho ni Kifungu cha 136(1) au miaka 14 kwa anayekutwa na hatia ya kujaribu kumbaka msichana, Kifungu cha 136(2). Pia sheria imeweka adhabu ya kifungo cha miaka 14, kwa kosa la kulawiti Kifungu cha 154.

Mkakati wa Serikali ni kuhakikisha kuwa, sheria hizi zinasimamiwa ipasavyo na kuendelea kuimarisha upelelezi na uendeshaji wa mashauri ya ubakaji na ulawiti ili kuiwezesha Mahakama kutoa adhabu stahiki pindi mtuhumiwa anapopatika na hatia.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, waathirika wa vitendo hivi viovu, hupata msongo wa mawazo na kujisikia vibaya mbele ya wenzao, hali ambayo ina athari mbaya kwenye masomo yao na makuzi ya watoto hao. Serikali imeanza utekelezaji wa mwongozo wa mwaka 2015 wa kuzuia ukatili dhidi ya watoto, mwongozo ambao unataka Walimu Washauri, wateuliwe kila shule ya Msingi na Sekondari na kupatiwa mafunzo ya ushauri nasaha.

**MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, adhabu mojawapo aliyoitaja ni kifungo cha maisha kwa wale ambao watapatikana hatia na huko gerezani tayari wameshakuwa na tabia kama hiyo, haoni kwamba kwa kuwaweka gerezani maisha wataendelea kufanya shughuli hiyo, kwa nini adhabu isiongezwe na waweze kuhasiwa ili wasirudie tena kitendo hicho?

Swali la pili, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba vitendo vya ubakaji vinajirudia mara kwa mara; Je, anaweza kunipa taarifa kwa kipindi cha miaka miwili iliyopita ni kesi ngapi zimepelekwa Mahakamani na ngapi zimetolewa hukumu. Ahsante. (Makofi)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge yeye anaona adhabu ya gereza haitoshi, hata kwenda jela maisha haitoshi ila anataka vile vile wahasiwe. Siwezi kuwa na jibu hapa kwa sababu hili ndilo Bunge linalotunga sheria za nchi, ningeomba tu Mheshimiwa Mbunge aje na hilo wazo liletwe mbele ya Bunge hapa, ni ninyi mtakaopitisha kwamba wanaume wahasiwe wanaokutwa na hilo tatizo au la, lakini siyo Serikali kuja na shauri hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalilake la pili, anataka kujua *statistics*, kujua ukubwa wa tatizo hili. Naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tatizo la kubaka na kulawiti nchi hii sasa hivi limefikia mahali pabaya kwa sababu, ukichukua takwimu za miaka mitatu au miaka minne iliyopita, tuna matukio kumi na tisa kila siku ya Mungu ya kubaka na kulawiti. Hayo matukio 19 ya kila siku ya Mungu ni yale ambayo yanaripotiwa, sasa siyo ajabu yakawa mara tatu ya hapo yale ambayo yanapita bila kuripotiwa na kupelekwa Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hili ni tatizo kubwa, Waheshimiwa Wabunge lazima tushirikiane. Kati ya mwezi Januari mpaka mwezi Machi mwaka huu tu nimepata taarifa hapa kwamba tuna mashauri 2,031, miezi

mitatu tu! Mpaka sasa naipongeza Mahakama kwamba pamoja na uchache wao wameweza kuzikamilisha kesi 111, watuhumiwa 96 wamefungwa. watuhumiwa 18 wameachiwa huru kwa kukosa ushahidi, lakini bado kesi 1,920 kwa miezi mitatu bado hazijakamilika. Hiyo ndiyo changamoto tuliyonayo ambayo naona Waheshimiwa Wabunge wote ni kazi yetu kuweza kuitatua. (Makofij)

Na 119

### **Mfuko wa Pamoja wa Sekta ya Afya (HSBF)**

**MHE. NJALU D. SILANGA** aliuliza:-

Sekta ya Afya hutenga fedha za Mfuko wa Pamoja (HSBF) kwa ajili ya kununua dawa, vifaa tiba na kadhalika:-

(a) Je, Serikali imejipanga vipi kuboresha mfumo wa manunuzi ili kupunguza mlolongo mrefu wa manunuzi uliopo sasa wa Halmashauri kutoa fedha, kisha kusubiri mpaka MSD itafute mzabuni mwingine?

(b) Mgao unaotolewa kutoka MSD kwenda vituoni ni kwa vituo vyenye fedha tu; Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa vituo vyote vinapata dawa kwa wakati ili kuhudumia wananchi wake?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijajibu swalii, naomba nitumie nafasi hii kwa heshima na taadhima kuwashukuru Wabunge wenzangu wote wa CCM kwa kunipa kura nyingi, nami nawaahidi sitowaangusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, Mbunge wa Jimbo la Itilima, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha mfumo wa ununuzi wa dawa, vifaa, vifaatiba na vitendanishi, Wizara inaomba Halmashauri kuwasilisha mapema maombi ya kununuliwa dawa na vifaa hivyo, ili MSD iweke kwenye mpango wake wa mwaka mzima wa manunuzi. Pia MSD imeingia mkataba, yaani *frame work contracts* na washitiri ili kupunguza mlolongo mrefu wa manunuzi ya dawa kwa sasa, mikataba hii, itasaidia Halmashauri kupata dawa katika muda mfupi zaidi.

Pia, MSD imeingia mkataba na washitiri wa ndani, yaani prime venders ili waweze kusambaza dawa pale ambapo zitakosekana katika maghala ya bohari ya dawa MSD. Idadi ya washitiri wa ndani kwa sasa imefikia 13 na juhudini zinafanyika kuongeza idadi hiyo ili kuimarisha utoaji wa huduma za dawa nchini. Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, pia imewasilisha mapendekezo ya kufanya mapitio ya Sheria ya Manunuvi, ili dawa ziweze kununuliwa kwa muda mfupi zaidi kuliko ilivyo hivi sasa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mgao wa dawa unaotolewa kutoka MSD kwenda vituoni, Serikali imetoe maelekezo kwamba, vituo vyote vya umma vipatiwe dawa bila kujali kama vina deni MSD. Pale Wizara inapopata mgao wa fedha kutoka Hazina madeni hayo hulipwa, pia Wizara yangu imeagiza Halmashauri kutumia vyanzo mbadala vya mapato kama vile Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) makusanyo ya papo kwa papo na fedha toka Bima ya Afya (NHIF), zitumike kununulia dawa ili kuziba pengo la bajeti toka Serikali Kuu. Fedha zingine ni za Mfuko wa Pamoja, (Health Basket Fund), ambapo asilimia 67 inatakiwa itumike katika kununulia dawa, vifaa, vifaatiba na vitendanishi. Vyanzo vyote hivyo vikitumika na kusimamiwa vizuri, vitapunguza sana pengo la bajeti kutoka Serikali Kuu.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, kwa vile, Halmashauri yangu ya Wilaya ya Itlima imeweza kulipa MSD zaidi ya milioni 120, hivi sasa tunavyozungumza vituo hivyo havijaweza kupata dawa, vituo hivyo ni Mwaswale, Nangale, Chinamili, Nkoma, Sunzura na Sawida. Je, ni lini sasa vituo hivyo vitapata dawa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante. Ni kweli tumepokea fedha za dawa kutoka Mfuko wa Pamoja kutoka kwenye vituo walivyovitaja vya Mwaswale ambapo tuna milioni 17.7, Lugulu milioni 16.2, Nyamalapa milioni 13.8, Chinamili milioni 13 na vituo vingine takribani zaidi ya shilingi milioni 50. Vituo hivi vitapata dawa kutoka kwa wale washitiri wa ndani (*prime venders*) ambao nimewazungumzia, nimesema mpaka sasa tuna Washitiri 13 na tunaendelea kufanya jitihada za kuongeza Washitiri wengine. Lengo likiwa ni kupunguza time ya Washitiri hawa ku-supply dawa kwenye vituo hivi. Washitiri tulionao kwa sasa kwa faida ya Waheshimiwa Wabunge wote ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao Astra Farmer, Jill Came, Salama Pharmacy, Anuther, Planet Farmer, Bahari Pharmacy, Samiro Pharmacy, Hashi Pharmacy, Pyramid, Mac Medics, Shukuru, Abakus na Philips. Washitiri hawa wanatusaidia kwa kiasi kikubwa kuziba pengo pale ambapo kwenye Bohari ya

Taifa ya Dawa hatuna dawa na tuna fedha kutoka Halmashauri basi Halmashauri zinapokosa dawa zinapaswa kuandikiwa kibali maalum kutoka kwenye Bohari ya Dawa ya Kanda na kwenda kununua dawa hizo kwa Washitiri hawa wa ndani ambao wana mikataba na MSD.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo likiwa ni kuhakikisha Halmashauri zetu zinanunua dawa kwa watu waliothibitishwa na dawa ambazo zina viwango vya ubora vinavyohitajika. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nchambi, swali fupi la nyongeza.

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, wabheja sana. kwa niaba ya wananchi sharp wa Jimbo Sharp, namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri, Jimbo la Kishapu limekamilisha ujenzi wa hospitali ya kisasa kabisa ya Wilaya, tena ni hospitali ya mfano na kujivunia ambayo Serikali ya Chama cha Mapinduzi, imeijenga kwa kushirikiana na wananchi wa Jimbo la Kishapu pamoja na Wawekezaji.

Kwa kuwa, hospitali hiyo ina upungufu mchache, imekamilika takribani kwa asilima 78 na upungufu huo katika swali la nyongeza hauwezi kunoga kuueleza, nimwombe Naibu Waziri, yuko tayari kufuatana na Mbunge sharp, kwenda kwa wananchi sharp, kuiona hospitali sharp, inayotoa huduma sharp sharp, ili mambo yaendelee kuwa sharp wakati wowote atakapotamka kwamba yuko tayari? Wabheja Sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu sharp!

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa majibu sharp, kwa Mbunge sharp wa wananchi sharp wa Kishapu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa na mimi ni Naibu Waziri sharp, namuahidi Mbunge sharp kwamba nitakuwa sharp, kuandamana naye ili tufanye safari ya sharp sharp, kwenda Kishapu kwa ajili ya kuwashudumia wananchi sharp wa Kishapu.

Mheshimiwa Naibu Spika, weekend ijayo baada ya hii, namuahidi Mheshimiwa Suleiman Nchambi kuandamana naye kwenda Kishapu kwenda kuitembelea hospitali hii na naomba Waheshimiwa Wabunge wengine wawe sharp kutekeleza mambo sharp sharp kwa ajili ya wananchi wao kama Mbunge wa Kishapu. (*Makofi/ Kicheko*)

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nimesimama kwa Kanuni ya 68(7), Serikali yetu imeridhia Mikataba mbalimbali ikiwemo ya Maputo Protocol, juu ya haki ya wanawake kuingia kwanye nafasi mbalimbali za uongozi. Jana wakati Mheshimiwa akichangia Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Kombani alisema kwamba wanawake wa upande wa CHADEMA tumeingia kwa sababu ya kuitwa ma-baby kwenye uongozi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wetu amefanya vizuri sana kutimiza ahadi hii hata wewe amekuchagua, kama mwanamke mahiri kuwa Mbunge na kukuteua kusimama kuwa Naibu Spika leo, kwa sababu ya saini tuliyosaini Maputo protocol, sitaki kuamini kwamba wanawake wote wanapitia mchakato wa uzinifu ili wapate uongozi. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama mama, kama mwanaharakati, mfumo dume uliojikita kwa wananchi na kwa wanasiisa, kwamba kila mwanamke ni mzinzi nataka kuipinga na nataka unipe mwongozo kama je, hii ni sahihi? Hata hivyo, tuna vyama vyetu vya Kibunge ndani ya Bunge hili, ikiwemo TWPG, leo hii mimi kama mwanachama wa chama hicho natangaza kujivua kwa sababu, lengo la chama kile ndani ya Bunge ni kutetea haki za wanawake wanaponyanyaswa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, naona huzuni Mwenyekiti na wadau wengine ambaao ni wanawake wenzetu wa chama hicho, wanashangilia udhalilishwaji usiokuwa na vidhibiti, naomba mwongozo wako juu ya suala hili na likome na huko nje wanaofikiri kila mwanamke ni mzinifu. (Makofii)

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo.

**NAIBU SPIKA.** Mheshimiwa Upendo Peneza naomba ukae, Waheshimiwa Wabunge tusikilizane, Kanuni ya 68(7)...

Mheshimiwa Esther Bulaya tafadhali, kinasema: "Hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote, ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufanuzi, kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi, kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papo hapo, au baadaye kadri atakavyoona inafaa.

Waheshimiwa Wabunge, jana nilisimama hapa niliposimama sasa hivi, baada ya yale maneno ambayo niliyatolea ufanuzi kwa maana ya kwamba jana pande zote mbili zilizoko huku Bungeni zilitumia maneno mabaya na nilitoa maelezo.

(Hapa Wabunge waliongea bila utaratibu kuonesha kutokukubaliana na Naibu Spika)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tusikilizane, nilitoa maelezo kwamba maneno yale yafutwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. Baada ya kusema hivyo tulienendelea na tukapitisha bajeti, naomba tuendelee na shughuli iliyopo mbele yetu, Mwongozo wangu ndiyo huo na kwa mujibu wa Kanuni huo ndiyo mwisho wa huo Mwongozo.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika!

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mliosimama nadhani mnatambua kwamba mnapaswa kukaa, mimi nikiwa nimesimama! Waheshimiwa mliosimama naomba mkae...

(Hapa Baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilishatolea maelezo jana, sasa hivi nimeomba mwongozo, nimetoa tena maelezo na hayo ndio maelezo yangu, tunaendelea na Bunge.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliendelea kuongea bila utaratibu)

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Taarifa Mheshimiwa!

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika

(Hapa baadhi ya wabunge waliendelea kuongea bila utaratibu)

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa, tunao wageni hapa ndani. Nitaanza kuwatangaza kwenu wageni wa Mheshimiwa Charles Mwijage, Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

**MBUNGE FULANI:** Tumuiteni baby, baby!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pauline Gekul, Mheshimiwa Sabreena Sungura, Mheshimiwa Halima Mdee naomba mkae, Mheshimiwa Lucy S. Magereli kaa chini, Mheshimiwa Kunti Majala kaa chini.

**MBUNGE FULANI:** Kaeni chini kwanza.

**NAIBU SPIKA:** Naomba mkae chini, Kanuni mnazifahamu. Mheshimiwa Mdee naomba ukae chini...

(*Hapa baadhi ya Wabunge waliendelea kuongea bila utaratibu wakiomba Mwongozo*)

**MBUNGE FULANI:** Na yeye ameletwa hapa kama baby.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Charles Mwijage wageni wake ni kama ifuatavyo:-

Dkt. Adelhem James Meru, Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda, mgeni mwengine ni Profesa Adolf Mkenda, Katibu Mkuu Biashara na Uwekezaji. Mgeni mwengine ni Injinia Joel Marongo, Naibu Katibu Mkuu Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Mheshimiwa Mwijage pia anao Wakuu wa Mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara na Viwanda, Biashara na Uwekezaji. (Makofi)

(*Hapa baadhi ya Wabunge waliendelea kuongea bila utaratibu wakionesha kutokubaliana na Kiti*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sakaya tafadhali, Mheshimiwa Peneza naomba tunyamaze jamani tusikilize. Naomba tuendelee na yaliyopo Mheshimiwa Sakaya tafadhali naomba tuendelee na yaliyopo mbele yetu.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine 12 wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kutoka taasisi za sekta binafsi zinazofanya kazi ya Wizara Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Tunao wageni wengine 51 wa Mheshimiwa Shaban Shekilindi wa Jimbo la Lushoto kutoka Chuo Cha SEKOMU kilichopo Lushoto, karibuni sana. (Makofi)

Wageni wengine ni wageni 15 wa Mheshimiwa Angeline Mabula, Mbunge wa Jimbo la Ilemela ambao ni wanachuo kutoka UDOM, karibuni sana. (Makofi)

Pia tunaye mgeni wa Mheshimiwa Hawa Mchafu Mbunge wa Viti Maalum ambaye anaitwa Mariam Msuya, nimetaarifiwa huyu ni mtoto wake. (Makofi)

Vile vile tunao wageni watatu ambao ni Wajumbe kutoka Taasisi ya PS Counseling Consultancy ya Jijini Dar es Salaam ambao ni Dkt. Tumaini S. Gurumo ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi, pia tunaye ndugu Mkumbo Mitula Mkurugenzi wa Asasi na ndugu Elinimo Mswai, Mjumbe wa Bodi, karibuni sana. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni 10 wa Mheshimiwa Tauhida Gallos, Mbunge wa Viti Maalum. Karibuni sana. (Makofi)

Pia tuna mgeni wa Mheshimiwa Kasuku Bilago, huyu ni Mbunge wa Jimbo la Buyungu na mgeni wake anaitwa Yokishani Toyi, huyo ni mpigakura wake, karibu sana. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao wanafunzi waliokuja kwa ajili ya mafunzo 41 kutoka Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, Dodoma, karibuni sana. (Makofi)

Pia tunao wanafunzi 107 na Walimu watano kutoka shule ya wasichana Msalato, Dodoma, karibuni sana. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine ni tangazo la kikao cha Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii na Mwenyekiti Mheshimiwa Peter Serukamba anaomba Wabunge hawa wakutane leo saa saba mchana, katika jengo la Utawala, chumba Na. 229 mara baada ya Bunge kuahirishwa. Kwa hiyo, Mwenyekiti anaomba Wajumbe wote wa Kamati hii mhudhurie huo mkutano.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la mwisho, mnatangaziwa kwamba kesho tarehe 7 Mei, kutakuwa na mchezo wa kirafiki wa mpira wa miguu kati ya Bunge Sports Club na Maafisa wa JWTZ, Ihumwa, kwenye uwanja wa Jamhuri saa kumi jioni, wote mnaombwa kuhudhuria. Tangazo hili limeletwa na Mwenyekiti wa Bunge Sports Club, Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangalla. (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge naomba tuendelee. (Makofi)

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba mwongozo ili tuweze kuendelea.

**NAIBU SPIKA:** tunaendelea, Katibu!

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:** Hoja za Serikali, hoja ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, kwamba Bunge sasa likubali kupitisha

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Kiti.

(*Hapa baadhi ya Wabunge waliendelea kuongea bila utaratibu wakitaka kupewa nafasi ya kuomba mwongozo*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa naomba mkae, nitatoa hiyo nafasi baadaye.

**MBUNGE FULANI:** Hakuna, we can't!

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba mkae, Waheshimiwa Wabunge naomba mkae tuendelee, Kanuni ya 72...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Wacha kutisha watu wewe!

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ya 72, Kanuni ndogo ya kwanza...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kwamba inafanya nini!

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Lusinde wewe mwanamke?

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba mkae.

**MBUNGE FULANI:** Unatumia vibaya Kanuni.

(*Hapa baadhi ya Wabunge waliendelea kuongea bila utaratibu kuonesha kutokubaliana na uamuzi wa Kiti*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba mliosimama mkae, Waheshimiwa Wabunge mliosimama naomba mkae! Waheshimiwa Wabunge mliosimama naomba mtoke nje.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, wala siyo suluhisho.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mliosimama naomba mtoke nje...

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mliosimama naomba mtoke nje, Sargent At Arms naomba Wabunge waliosimama muwatoe nje.

**NAIBU SPIKA:** Wabunge wote waliosimama Sargent At Arms naomba muwatoe nje.

**MBUNGE FULANI:** Twendeni upande wao.

**MBUNGE FULANI:** Eti wewe ni baby wa Magufuli?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Halima abaki ni mwenzetu. (*Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Watateteanaje hawa wakati hawataki wanaume!

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge naomba tuendelee, Katibu.

**MHE. PETER S. MSIGWA:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa naomba ukae tafadhali.

**MHE. PETER S. MSIGWA:** Si kanuni zinaturuhusu.

**NAIBU SPIKA:** Naomba ukae...

**MHE. PETER S. MSIGWA:** Si Kanuni ndiyo zinaturuhusu? Kwa nini unatu-intimidate,*Why are you intimidating us?*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msigwa naomba ukae, naomba ukae.

**MHE. JOHN H. WEGESA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sisi siyo wanafunzi wala wewe siyo headmaster hapo.

**MHE. PETER S. MSIGWA:** Tukifuata utaratibu hutaki sasa tufanyeje?

**MHE. JOHN H. WEGESA:** Fuata utaratibu.

**MBUNGE FULANI:** Huyu katumwa.

**NAIBU SPIKA:** Katibu tuendelee.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:** Hoja za Serikali, hoja ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, kwamba Bunge sasa likubali kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

## HOJA ZA SERIKALI

### **Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017- Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji. (Makofii)

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba yangu ni ndefu, nitaomba hotuba yangu yote iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge (Hansard).

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuwasilisha hotuba yangu, kwa ruhusa yako nitaomba nimtambue Baba Mchungaji Profesa Aba Mpesha kutoka Michigan ambaye ni mtaalam katika shughuli za biashara ndogo na viwanda vidogo na aliyefanya utafiti kuhusu zao la korosho, yupo safarini anakuja Dar es Salaam, atakuja hapa, kwa hiyo Jumuiya ya Kimataifa ipo pamoja na sisii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ambayo ilichambua bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji tarehe 13 Aprili, 2016; naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, kwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema na baraka zake na kutujalia afya njema kwa kuwa pamoja leo kutekeleza wajibu wetu kwa Taifa. Naomba aendelee kuwa nasi ili hayo tunayoyapanga yampendeze kutupa kibali chake na kuyatekeleza ili tuweze kufanikiwa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii adimu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika uchaguzi wa Oktoba 2015. Nawapongeza pia Mheshimiwa Dkt. Ally Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Mheshimiwa Balozi Seif Ally Idd kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, kwa kuteuliwa na kuthibitishwa na Bunge letu Tukufu

kuwa Waziri Mkoo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia nampongeza Mheshimiwa George Masaju kwa kuteuliwa kuwa Mwanasheria Mkoo wa Serikali. Nawapongeza pia Mawaziri, Naibu Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa au kuteuliwa kubeba dhamana ya kuwawakilisha wananchi katika Bunge hili Tukufu. Hakika Watanzania wamepata Viongozi wenye kupenda kuleta mabadiliko na matokeo stahiki kwa maendeleo na ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee napenda kukupongeza wewe binafsi na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuchaguliwa kuliongoza Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Serikali ya Awamu ya Tano. Pia niwapongeze Wenyevitii wa Kamati za Kudumu za Bunge, Katibu wa Bunge na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge la Jamhuri wa Muungano wa Tanzania na niwashukuru sana kwa ushirikiano mzuri mnaotoa kwa Wizara yetu na wadau wa sekta ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru kwa namna ya pekee kabisa Mheshimiwa Rais kwa kuniamini na kunateua kubeba dhamana hii kubwa ya kusimamia na kuendeleza viwanda, biashara, masoko, viwanda vidogo, biashara ndogo na uwekezaji nchini. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais kuwa nitaendeleza dhana ya 'Hapa Kazi Tu' kuhakikisha kuwa natimizia kiu ya Watanzania na kufanya zaidi ya yale wanayokusudia kadiri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda kupongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira chini ya Mwenyezekiti Mheshimiwa Dkt. Dalali Peter Kafumu, Mbunge wa Igunga na Makamu wake Vicky Paschal Kamata, Mbunge wa Viti Maalum na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati namna ambavyo mmepokea, kuchambua na kushauri juu ya mambo ya msingi ya bajeti ya 2016/2017 katika kuendeleza viwanda, biashara, masoko, viwanda vidogo na biashara ndogo na uwekezaji. Napenda kukuhakikishia ushauri na maelekezo ya Kamati yamezingatiwa katika kuandaa na kuboresha hotuba ninayoiwasilisha mbele ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkoo kwa hotuba yake nzuri yenye kutoa mwelekeo sahihi, dira na malengo ya utendaji wa Serikali katika kutekeleza mipango na programu za Serikali ya Awamu ya Tano, kwa mwaka 2016/2017; na kuendeleza mafanikio yaliyopatikana kwa awamu zilizopita. Aidha, nawapongeza Mawaziri ambao wamewasilisha hotuba zao za bajeti kwa mwaka 2016/2017 na kupitishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati wapiga kura wote wa Jimbo la Muleba Kaskazini kwa kuniamini, kunipa

moyo na ushirikiano mzuri ulioniwezesha kuchaguliwa kuwa Mbunge wao na pia katika kutekeleza majukumu yangu kama mwakilishi wao katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru familia yangu hususani mke wangu, watoto, ndugu na jamaa kwa sala zao na ushirikiano wao mzuri wanaoniwezesha kuwatumikia Watanzania bila kuchoka. Nawaomba tuendelee kushirikiana kwani naona tuendapo kuna mwanga na matumaini makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa uchumi wa nchi yetu na hususani maendeleo ya sekta ya viwanda, biashara, masoko, viwanda vidogo, biashara ndogo na uwekezaji unategemea sana ushirikiano wa wananchi na wadau wote wa ndani na nje ya nchi. Hivyo napenda kuwatambua na kuwashukuru Taasisi na Sekta Binafsi nchini, Waandishi na Wamiliki wa Vyombo vyta Habari, Washirika wa Maendeleo na Watanzania wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, namshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na wachapishaji wengine kwa kuchapisha machapisho mbalimbali ya Wizara yangu ambayo kwa namna ya pekee yanasaidia kuwaelimisha Watanzania juu ya dhima ya kujenga uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii ya bajeti ninayoiwasilisha ni matokeo ya uratibu na ushirikiano mzuri wa Viongozi wenzangu katika Wizara, napenda kumshukuru Katibu Mkuu Dkt. Meru, Profesa Adolf Mkenda na Joseph Marongo, Wakuu wa Idara na watu wote ambao kwa namna moja au nyingine wamesaidia katika kutekeleza kazi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwapa pole ndugu na jamaa ambao katika kipindi hiki tunapoanza Awamu ya Tano wamepata misukosuko katika maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mchango na mwelekeo wa sekta ya viwanda, biashara na uwekezaji katika kuleta mageuzi ya uchumi. Ujenzi wa uchumi wa viwanda ni vita, tena ni vita kubwa sana; mafanikio katika uchumi wa viwanda yanababisha nchi yetu kuwa Taifa lenye watu wa kipato cha kati; hii ni jamii ambayo watu wake walio wengi wanaondokana na matatizo ya ujinga, umaskini na maradhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa pili uchumi wa viwanda utaliweka Taifa letu katika kundi la Mataifa yanayozalisha bidhaa bora na zenye ushindani wa soko la Kimataifa, badala ya kuwa chanzo cha malighafi na soko la bidhaa kwa viwanda vyta Mataifa mengine. Ili kufikia azma hiyo, ushiriki na mchango wa mtu mmoja mmoja, makundi ya watu, taasisi za umma na taasisi binafsi

utahitajika katika vita hiyo, muhimu ni Watanzania kubadili mtazamo na kujenga utamaduni unaolenga kuwa na Taifa lenye uchumi wa viwanda. Hii ni pamoja na kila mmoja wetu kwa uwezo wake kulenga kuwekeza katika viwanda na kupenda kununua bidhaa zinazozalishwa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miaka ya 80 viwanda vingi vilivyokuwa vimeanzishwa chini ya Mkakati wa Taifa wa Viwanda vya Msingi (*Basic Industrial Strategy*) vikiwa vinamilikiwa na Serikali vilikufa kutokana na sababu kadhaa. Moja ya sababu hizo ni matumizi ya teknolojia duni katika uzalishaji uliosababisha kuzalisha bidhaa zisizokuwa na viwango na ubora wa chini na hivyo kushindwa kuhimili ushindani katika masoko ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia changamoto hizo Serikali ilibaini ni vema jukumu la kuendesha uchumi lipewe sekta binafsi na Serikali ikabaki na kujukumu la kuweka mazingira wezeshi na rafiki ya kufanya biashara na kuwekeza. Huo ndiyo mwelekeo katika ujenzi wa sekta ya viwanda unaohamasishwa na Serikali ya Awamu ya Tano na Wizara yangu imejjipanga vema katika kuhakikisha Watanzania wanashirikishwa ipasavyo katika kujenga uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa Sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Kwa mujibu wa takwimu za mwaka wa kizio wa 2007, mchango wa sekta ya viwanda katika pato halisi la Taifa ulikuwa asilimia 5.2 mwaka 2005 ukilinganisha na 5.6 mwaka 2004. Hivi sasa pato la Taifa linaongezeka kwa asilimia saba ukilinganisha na ukuaji wa sekta ya viwanda ya 5.2. Aidha, mchango wa sekta ya viwanda katika mauzo ya nje umefikia asilimia 23.31 mwaka 2014 ikilinganishwa na 9.31 mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya viwanda hapa nchini imeendelea kuongezeka kutoka viwanda 125 mwaka 1961 hadi kufikia viwanda 49,443 mwaka 2003. Aidha, kati ya hivyo viwanda vikubwa vinavyoajiri kuanzia watu 100 mpaka 247, viwanda vya kati vinavyoajiri watu 50 na 99 ni 150 viwanda vidogo vinavyoajiri kati ya watu watano mpaka arobaini na tisa. Kwa takwimu hizo utaona kwamba asilimia 99.19 ni viwanda vidogo sana na asilimia 1.5 ni viwanda vikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia Sera ya Ubinafsishaji iliyoanza kutekelezwa katika miaka ya 90 jumla ya viwanda 141 nchini vilirekebisha mifumo yake kuititia ubinafsishaji. Viwanda hivyo ni kutoka sekta ya viwanda, kilimo, mifugo, madini, maliasili na misitu. Ubinafsishaji ulifanyika kwa kuuza hisa, kuuza mali yote, kuingia ubia na sekta binafsi na ufilisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa viwanda vilivyo vingi kama siyo vyote mikataba ya mauzo iliendana na masharti yake makuu ambayo wamiliki

wapya, pamoja na fedha waliyotoa walitakiwa kuhakikisha viwanda hivyo vinafanya kazi kwa tija ili viweze kulipa kodi, kutoa ajira na kuzalisha bidhaa na huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lengo la Serikali ya Awamu ya Tano kuwa viwanda vyote vilivyobinafsishwa vinafanya kazi. Kati ya viwanda 106 vilivyofanyiwa tathmini viwanda 45 vinafanya kazi vizuri, viwanda 24 vinafanya kazi kwa kusuasua, 37 vimefungwa. Mpango wetu ni kuhakikisha kuwa viwanda 35 vilivyobaki vinafanyiwa tathmini haraka na kabla ya nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha unaoanzia Julai moja, hatima ya viwanda visivyofanya kazi itajulikana. Hatima ya viwanda visivyofanya kazi ni wamiliki waliopewa kutekeleza mikataba ya mauzo au wawape wengine waendeleze.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini yetu pia inaonesha mafanikio yaliyotokana na utekelezaji wa sera ya ubinafsishaji. Serikali imeondokana na mzigo mkubwa wa kutoa ruzuku ya kuendesha mashirika ya biashara yaliyokuwa chini yake. Itakumbukwa kuwa utaratibu wa ruzuku ni moja ya sababu zilizosababisha mashirika ya umma kufanya vibaya siku za nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vinavyofanya kazi vimeweza kutimiza malengo ya kutoa ajira na kuzalisha bidhaa. Hali hii inadhihirishwa na ongezeko la uzalishaji wa bidhaa kama saruji, nguo, sigara, chupa na kwa kutaja baadhi. Aidha, viwanda hivyo vimekuwa ni mionganini mwa makampuni yanayolipa kodi vizuri. Kwa mfano, mwaka 2015 Kampuni ya Bia ya TBL imelipa jumla ya shilingi bilioni 384.3 kama kodi kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo. Sekta ya viwanda vidogo na vya kati (*micro small and medium enterprises*) ina nafasi kubwa katika kuzalisha ajira nchini na kuongeza kipato kwa wananchi wa kawaida. Kulingana na utafiti wa shughuli za viwanda vidogo na biashara ndogo ambazo Profesa Aba Mpesha ambaye ni mshauri wetu amekuja kushuhudia, sekta hiyo inatoa ajira za moja kwa moja kwa Watanzania milioni 5.2 na kuchangia takriban asilimia 28 katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha kulingana na takwimu za awali za sensa ya viwanda nchini inaonesha Tanzania ina jumla ya viwanda 49,243 kama nilivyozungumza, vinavyojumuisha viwanda vidogo sana, viwanda vidogo, viwanda vya kati na viwanda vikubwa. Kupitia takwimu hizo ni dhahiri kuwa asilimia 99.15 ya viwanda vyote nchini ni viwanda vidogo sana na viwanda vya kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, taswira ya takwimu hizo inaonesha wazi kuwa maendeleo ya viwanda Tanzania, kama ilivyo katika nchi nyingine yatatokana na kuwekeza nguvu katika sekta ya viwanda vidogo sana na viwanda vidogo.

Faida ya sekta hiyo ni kuwa uanzishwaji wa viwanda aina hiyo havihitaji elimu na mtaji mkubwa na hivyo vinaweza kuanzishwa katika eneo lolote la nchi yetu.

Sekta hiyo inatoa mwanya mkubwa kwa vijana na akinamama kuanzisha viwanda na kujajiri, ambapo wasingepata fursa katika sekta nyingine zinazotoa ajira. Viwanda vidogo huongeza thamani ya mazao, hali ambayo humpatia kipato zaidi mzalishaji na kupunguza hasara baada ya mavuno (*post-harvest loss*).

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya viwanda vidogo ni shule mahsus kwa Watanzania kwa kuwa inawaandaa kuwa wamiliki wa viwanda vya kati na viwanda vikubwa hapo baadaye. Upande wa kijamii na kiuchumi pia uwepo wa viwanda sehemu zote za nchi hasa vijiji hupunguza kasi ya wananchi kuhamia mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Biashara. Mauzo katika soko la India yaliongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 1,254 mpaka kufikia Dola milioni 1,320. Ongezeko hilo lilichangiwa na uuzaji wa bidhaa mbalimbali kama karafuu, korosho, ngozi na wanyama, nazi, bidhaa jamii za kunde pamoja na samaki, pamba na nyuzi za katani. Mauzo katika soko la Japan yaliongezeka kutoka Dola 247.8 mwaka 2014 mpaka Dola 263.4 mwaka 2015 jedwali namba 10 linaleleza zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutumia vyema fursa za masoko ya kikanda mauzo ya Tanzania kwenda katika nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki yaliongezeka mwaka 2015 na kufikia Dola za Kimarekani milioni 1,062 ikilinganishwa na Dola milioni 598 mwaka 2014. Hali hiyo ilichangia Tanzania kuwa na urari chanya wa biashara katika soko hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mauzo ya Tanzania kwenda katika soko la Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Afrika Kusini (SADC) yaliongezeka mwaka 2015 na kufikia Dola za Kimarekani milioni 1,357.7 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani 1,235.9.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepanga kuboresha sekta ya *antidumping*. Maboresho hayo yataendana na mpango wa Serikali ya Awamu ya Tano ya kuwa na uchumi wa viwanda unaotumia na kuhamasisha ongezeko la thamani kwa malighafi zinazopatikana nchini. Vile vile sheria hiyo inatarajiwa kuwa madhubuti kwa kukabiliana na ushindani usio sawa. Hatuwezi kukubali sisi kuwa soko la bidhaa hafifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Uwekezaji inaendelea kutoa mchango mkubwa kutokana na wawekezaji wapya wa ndani na nje ya nchi. Tanzania imeendelea kuongoza katika kuvutia wawekezaji kutoka nje ikilinganishwa na

nchi nyingine katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kwa takriban miaka mitano mfululizo. Uwekezaji wa miradi hiyo umekuwa muhimu kwa uchumi wa nchi yetu, hasa kwa kuingiza mitaji na teknolojia mpya, mafunzo na mbinu mpya za kitaalam katika kuendesha na kusimamia miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2015 miradi 464 iliyosajiliwa ilitarajiwa kuwekeza mtaji wa kufikia Dola za Marekani milioni 5,892 na kuongeza ajira kwa Watanzania 46,250. Kutokana na uhamasishaji unaoendelea ni matarajio yetu kuwa mwaka 2016 uwekezaji utaongezeka na pia ajira zitaongezeka na hivyo kuchangia katika kukuza pato la Taifa na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwelekeo wa Sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Maendeleo endelevu ya kiuchumi yanahitaji mifumo iliyounganishwa katika kujenga uwezo wa uzalishaji wa ndani wenyewe kuunganisha juhudzi za kila sekta ya uchumi (*forward and backward linkage*) ili kumudu kiwango kikubwa cha mahitaji ya soko la ndani na ushindani wa bidhaa kutoka nje. Uwezo wa kushindana utategemea zaidi uzalishaji kwa kutumia rasilimali za ndani ya nchi zenye uwezo wa kuvutia uwekezaji makini kwa maendeleo ya biashara ya ndani. Ujenzi wa uchumi wa viwanda ni moja ya mbinu muhimu ya uhakika ya kukabiliana na changamoto ya umaskini ikiwa ni pamoja na kupunguza pengo la walionacho na wasionacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mkakati huu ukuaji wa uchumi katika takwimu utaendana na maisha bora ya wananchi. Nchi kama Malaysia, Korea Kusini, Singapore na nyinginezo ambazo watu wanazitolea mfano wakati tunapata uhuru zilikuwa zinalingana na Tanzania ziliwekeza katika maendeleo ya viwanda. Hivyo kwa kuzingatia mwelekeo huo Wizara itaendelea kuwaelimisha Watanzania waelewe na kukubali dhana ya kujenga uchumi unaoongozwa na viwanda, hii inawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia mtazamo wa msukumo wa kimaendeleo unaohitaji kuleta mageuzi ya kiuchumi Serikali itaelekeza nguvu zake katika ujenzi wa uchumi wa viwanda. Nguvu kubwa itaelekezwa katika ujenzi wa uchumi wa viwanda unaoshirikisha sekta binafsi ikiwa muhimili mkuu wa utekelezaji. Aidha, Dira ya Maendeleo 2025 itataka tuwe na uchumi wa viwanda ambayo sura na maisha ya Watanzania walio wengi yatafanana na nchi ya kipato cha kati. Kwa msingi huo, Wizara itahakikisha kuwa inasimamia ipasavyo suala la viwanda na kuleta mafanikio na haya ndiyo mambo tutakayofanya:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, kuhakikisha viwanda vyote vilivyopo vinafanya kazi kwa uwezo wake mkubwa kadri inavyowezekana. Viwanda vya Tanzania vitapewa kipaumbele katika tender na shughuli zote za ku-supply hapa nchini. Kuondoa vikwazo vyote vinavyopunguza uwezo wa

kiushindani kwa viwanda vyetu. Hapo ndipo tunapozungumza kwamba bidhaa hafifu, bidhaa ghafi tutazidhibiti kikamilifu.

Kwa kutambua kuwa Watanzania wana uwezo wa kuwekeza katika sekta ya viwanda, kwa namna ya kipekee tutahamasisha wananchi kuwekeza katika viwanda. Kwa umakini kabisa tutahimiza, kushauri na kusimamia ushiriki wa Watanzania katika sekta hiyo, kila mmoja au kundi kwa uwezo wake kuanzia ngazi ya Vijiji, Kata, Wilaya mpaka katika ngazi ya Taifa. Tunatimiza maelekezo ya Mkuu wa Nchi, tajiri namba moja, kwamba viwanda vitajengwa nchi yote; viwanda vidogo, vidogo sana, vya kati na viwanda vikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutahamasisha wawekezaji wakubwa wa ndani na nje kuwekeza katika sekta ya viwanda katika ngazi ya Kanda na Taifa. Tutapigana kufa na kupona ili tuwe na miundombinu wezeshi na miundombinu saidizi ilio tayari katika maeneo yetu. Huo ni mkakati maalum ambao unalenga kuongeza wepesi wa kuwekeza nchini. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yaliyoko chini ya Wizara yetu yanayokwamisha shughuli za uwekezaji na biashara nchini yataboreshwa. Naomba nirudie; maeneo yaliyoko chini ya Wizara ninayoiongoza yanayokwamisha shughuli za uwekezaji na biashara nchini yataboreshwa. Aidha, Wizara yangu itakuwa mboni ya Serikali kubaini Idara yoyote ya Serikali ambayo utekelezaji wake unaiweka Tanzania katika nafasi mbaya katika kuvutia wawekezaji duniani. Lengo ikiwa ni kuboresha mazingira ya uwekezaji ili Tanzania iwe kivutio kwa wawekezaji wa ndani na nje. Sasa ni zamu ya Afrika na mtu akikuuliza Afrika wala usitafune maneno, Afrika ni Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua faida ya kuwepo miundombinu wezeshi pia kwa kuzingatia mikataba ya mauzo tutahakikisha kuwa viwanda vyote vilivyobinafsishwa vinafanya kazi kwa ufanisi. Naomba nirudie, viwanda vyote vilivyobinafsishwa vitafanya kazi kwa ufanisi. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua kuwa sekta ya viwanda nchini bado ni changa Serikali italinda viwanda hivyo kuhakikisha kuwa kuna uwanja sawa wa ushindani kwa washiriki wote. Viwanda vyote vitakuwa na ushindani sawia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali katika kutekeleza mkakati wa kujenga viwanda nchini, utahimiza na kusimamia msambao wa viwanda sehemu zote za nchi (*Regional Dispersion*), naomba nirudie. Tutahakikisha viwanda vinasambaa nchi yote Tanzania nzima. Hatutakubali viwanda kuwa sehemu moja ya nchi wakati sehemu nyingine ikiwa sehemu ya kutoa nguvukazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ngazi ya Taifa tutaendeleza jitihada za kutenga na kuboresha maeneo madum ya kiuchumi ili kurahisisha uwekezaji mkubwa katika sekta ya viwanda. Hatua ya kwanza ni kuhakikisha kwamba fidia inalipwa kwa maeneo yote yaliyotengwa siku za nyuma. Hatua ya pili ni kuendeleza maeneo ambayo tuna uhakika wawekezaji watayachukua katika siku za hivi karibuni. Hatua ya tatu ni kutenga maeneo kwa kuzingatia mahitaji ya miaka ya usoni. Mipango yetu katika kutenga maeneo hayo inazingatia uzoefu wa nchi nyingine kama Vietnam ambayo sasa ina maeneo maalum ya kiuchumi 150, ukizingatia kuwa ukubwa wa nchi hiyo ni moja ya saba ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuhamasisha uwekezaji. Kama tunavyofahamu Tanzania ni moja ya maeneo yanayovutia uwekezaji kutokana na kupakana na nchi nane ambazo kati ya hizo sita ni nchi zisizo na bandari. Aidha, uwepo wa malighafi ya kutosha, sera nzuri za uwekezaji, pamoja na uhakika wa usalama wa mali za wandaowekeza nchi yetu inawavutia wawekezaji wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuwezesha uwekezaji nchini Serikali imejipanga kujenga miundombinu ya msingi kwenye maeneo ya viwanda Kibaha TAMCO kwa ajili ya wawekezaji wanaokuja haraka, lakini Zuzu kwa makusudi maalum ya kutatua tatizo la sekta ya ngozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda vidogo katika Wilaya, ni muhimu kuzingatia upatikanaji wa soko, teknolojia rafiki na malighafi zilizoko katika Wilaya hizo. Tunaamini mafanikio ya lengo hilo yatachangia kujenga ushindaji mkubwa kati ya Wilaya na Wilaya, Mkoa na Mkoa mwagine, hivyo kukuza ubunifu katika jamii. Wito wangu katika hilo ni kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Manispaa na Halmashauri zote nchini tushirikiane katika kuhamasisha ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua sana umuhimu wa upatikanaji wa teknolojia katika kuendeleza viwanda nchini, hasa kwa viwanda vidogo. Serikali itaendelea kufanya maboresho ya vituo vyatua kuendeleza na kuhaulisha teknolojia viliyoko chini ya SIDO ili viweze kutoa huduma nzuri zaidi na teknolojia bora zenye uwezo wa kushindana na zile zinazotoka nje. Vituo hivyo vitawezeshwa ili viweze kuhawilisha teknolojia zinazotoka katika taasisi za utafiti kama vile CAMATEC, TIRDO, TEMDO ambazo zote ziko chini ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Mpango wa Bajeti Mwaka 2015/2016. Nitaomba kwanza hii niiache niwaeleze kwanza malengo yangu ya mwaka 2016, nije niwaeleze tulifanya nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako. Malengo ya Mwaka 2016/2017. Katika mwaka 2016/2017, sekta ya maendeleo ya viwanda itatekeleza yafuatayo:

Kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha na kuendeleza viwanda vinavyotumia malighafi za hapa nchini na kuvutia wawekezaji kujenga viwanda vya vifungashio (*intergrated packaging industry*)

Kutekeleza miradi ya kimkakati kwa kushirikiana na sekta binafsi ambayo ni Mchuchuma na Liganga, Magadi soda ya Engaruka, viwanda vya mbolea vya kemikali na kufufua Kiwanda cha Kutengeneza Matairi cha General Tyre ya Arusha. Kuanzisha na kuboresha vituo vya uwekezaji katika viwanda vinavyozalisha ajira kwa wingi kwa kuwalenga zaidi wazawa. Naomba nirudie, kuanzisha na kuboresha vivutio vya uwekezaji katika viwanda vinavyozalisha ajira kwa wingi na kwa kuwalenga zaidi wazawa. Wazawa wamiliki viwanda wakati ni huu wa Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuendelea kubainisha maeneo ya viwanda katika mikoa yote kwa matumizi ya sasa na mbeleni na kuendeleza maeneo maalum ya uwekezaji (*EPZ na SEZ*). Kujenga kongano za viwanda (*industrial cluster*) hususan katika sekta ndogo za ngozi na bidhaa za ngozi. Dodoma ni mojawapo na nimeitaja. Nguo na mavazi katika eneo la TAMCO Kibaha. Kukusanya, kuchambua na kuandaa wajihii na takwimu za viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuhamasisha vyuo vya ufundi stadi, kuhusisha mafunzo ya ujuzi maalum wa viwanda (*Specialized industrial skill*) katika mitaala yao ili kutambua upatikanaji wa ujuzi husika. Kujenga uwezo wa taasisi za utafiti zilizo chini ya Wizara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji ili ziongeze uwezo wa mifumo yao ya uvumbuzi, uhamasishaji na usambazaji wa teknolojia (*technological transfer innovation and commercialization*) na kuhamasisha sekta binafsi kutumia teknolojia hizo. Tutatoa teknolojia hizo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kuanzisha kiwanda usianzishe kiwanda bila kuja Wizarani kwangu, kuwaliza *TIRDO*, kuwaliza *SIDO*, kuwaliza *TBS*, huduma zitatolewa bure hiyo iko chini ya mamlaka yangu. Kwa kushirikiana na Msajili wa Hazina kufanya uchambuzi wa mikataba ya viwanda vilivyobinafsishwa na hasa vile vinavyosuasua na vilivyokuwa na kuchukua hatua stahiki kwa wamiliki wa viwanda vilivyokiuka masharti ya mikataba. Nimeeleza, hatua stahiki ni kwamba ama waendeleze viwanda ama wawaachie wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuwahamasisha wananchi kuunga mkono dhima ya ujenzi wa uchumi wa viwanda. Awali nilieleza kwamba hii ni vita na kushinda vita lazima uungwe mkono na watu wote. Kazi yangu nitakayoifanya, nitazungumza sana, nitashawishi sana, nitazunguka nchi nzima kuwashawishi watu wote waelewe dhana hii ambayo uchumi unakua kwa takwimu na vile vile watu mnakuwa na nguvu kwenye mifuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanza majadiliano na taasisi maalum za Serikali kama Jeshi, Polisi na Magereza juu ya kutumia taasisi hizo kuongeza kasi ya ujenzi wa uchumi wa viwanda ifikapo mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo. Mwaka 2016/2017 sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

- (i) Kuhamasisha Serikali za Mikoa na Wilaya kutenga maeneo kwa ajili ya kuanzisha mitaa ya viwanda vidogo;
- (ii) Kuandaa mwongozo kwa ajili ya kurasimisha shughuli za kiuchumi za wajasiriamali wadogo;
- (iii) Kufanya mapitio ya Sera ya viwanda vidogo na biashara ndogo ya mwaka 2003;
- (iv) Kuwezesha upatikanaji wa mtaji wa zaidi ya shilingi bilioni 2.4 kwa wajasiriamali wadogo (*NEDF*);
- (v) Kuwezesha upatikanaji wa teknolojia kwa wajasiriamali wadogo, kufanya mageuzi (*restructuring*) SIDO ili kulenga kuboresha huduma zake kwa walengwa wote nchi nzima;
- (vi) Kuwezesha sekta za samani kutoa huduma bora na ufanisi ikijumuisha kufanya tathmini ya mahitaji halisi ya sekta hiyo. Tunalenga ifikie wakati na nitaishawishi Serikali ambayo mimi ni mjumbe wake, kwamba tusiuze magogo nje, *furniture* zote zitengenezwe hapa ili watu wa nje waje wanunue *furniture* hapa ili tutengeneze ajira; na
- (vii) Kuhamasisha na kusimamia maendeleo ya sekta ya mafuta ya mbegu hususan alizeti. Tanzania sasa hivi tunazalisha tani 120,000 za alizeti, tunataka tuzalishe tani milioni moja ikiwezekana ili tuuze alizeti nje. Tani moja ya alizeti inauzwa ghali kuliko tani ya mafuta jamii ya *petrol* ambayo huuzwa dola 880.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Biashara. Katika mwaka 2016/2017, sekta ya biashara itatekeleza yafuatayo:

- (a) Kuendelea na majadiliano ya biashara katika nchi na nchi (*bilateral*), kikanda (*regional*) na kimataifa (*multilateral*). Mmeona takwimu zetu, tumeuza bidhaa nyingi katika nchi za SADC na East Africa kuliko wakati wowote;
- (b) Kuendelea kuimarisha wepesi wa kufanya biashara;
- (c) Kuendelea na majadiliano ya kuanzishwa kwa eneo huru la biashara la nchi za Afrika;
- (d) Kukamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Biashara ya Mwaka 2013;
- (e) Kuendelea na maandalizi ya kuandika upya Sera ya *Antidumping* na *Counter fate Measures* kwa ajili ya kulinda viwanda vyetu itakapobidi. Viwanda vya Tanzania lazima vilindwe hapo mimi sitafuni maneno, siwezi kumlisha mtoto wa kware, mtoto wa kuku akafa njaa!

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Masoko; katika Mwaka 2016/2017, Sekta ya Masoko itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji chini ya Mpango wa Matokeo Makubwa (*BRN*);
- (b) Kuendelea kutafuta masoko ya bidhaa za maendeleo ndani na nje ya nchi;
- (c) Kuendeleza miundombinu ya masoko nchini;
- (d) Kuimarisha biashara ya mipakani; na
- (e) Kuwezesha vikundi vya Wakulima, Wajasiriamali, Wafanyabiashara kutangaza bidhaa na huduma za Tanzania katika masoko ya ndani, Kikanda, Kimataifa na kwa njia mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Uwekezaji; katika mwaka 2016/2017, Idara ya Uwekezaji itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kuhamasisha uwekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwekeza katika sekta mbalimbali za uchumi hapa nchini;

(b) Kwa namna ya pekee, kubuni mpango na mkakati wa kuhamasisha Watanzania kuwekeza katika sekta ya viwanda;

(c) Sekta ya uwekezaji itabuni mkakati wa kuwabembeleza, kuwashawishi na kuwaeleza kwa namna yoyote Watanzania muwekeze katika Sekta ya Viwanda;

(d) Kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji hapa nchini ili kuondoa changamoto zinazowapata wafanyabiashara na wawekezaji;

(e) Kukamilisha mapitio ya Sera ya Uwekezaji ya mwaka 1996 na Sheria ya mwaka 1997 na Kanuni zake; na

(f) Kusimamia na kuratibu shughuli za taasisi zilizoko chini ya Idara ya Uwekezaji ambayo ni Kituo cha Uwekezaji Tanzania TIC, zinazotekeleza majukumu yanayohusu uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ndiyo mipango yetu kwa mwaka 2016/2017 na kama nilivyosema kuna utekelezaji wa malengo na mipango ya Wizara yangu kwa mwaka 2015/2016, ambayo tumezungumzia kitu kilichofanyika katika mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji inakusanya mapato yake kutokana na mauzo ya nyaraka na zabuni, ada, leseni na faini za leseni. Hadi kufikia mwezi Machi, 2016, Wizara imeweza kukusanya jumla ya shilingi bilioni 8.9 ikiwa ni asilimia 74.25 ya lengo la mwaka 2015/2016 la kukusanya bilioni 12, makusanyo hayo ni asilimia 111 ya makusanyo. Makusanyo hayo....oo! samahani sentensi hiyo nimeirudia!

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi; mwaka uliopita, katika mwaka 2015/2016 Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 88 ili kutekeleza majukumu yake, kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 42 ziliwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida zikiwemo shilingi bilioni 44.8 za mishahara na Shilingi bilioni saba zilizotengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo, OC. (**Maneno haya yalifutwa na hivyo siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge**)

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ndiyo yaliyofanyika na yameelezwa vizuri, na yameorodheshwa vizuri katika kitabu changu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio ya utekelezaji kipindi kilichopita; Wizara yangu imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kuendeleza viwanda na kuvutia wawekezaji hususani viwanda vya msingi ambavyo ni kichocheo cha uanzishwaji wa viwanda vingine na viwanda vya kuongeza thamani ya mazao

ya kilimo. Katika kuongeza juhudzi za kuongeza thamani ya mazao na kuondokana na uuzaji wa mazao ghafi, Wizara imeendelea kuhamasisha wawekezaji katika sekta ya kusindika mazao ya kilimo, mmeona takwimu zetu, mauzo ya viwanda yameendelea kuongezeka siku hadi siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na TAMISEMI kwa kuunga mkono juhudzi za kuendeleza viwanda. Jitihada zao zimewezesha kuyalinda maeneo maalum kwa ajili ya viwanda chini ya mamlaka ya EPZ yaliyokwishatengwa kutoka mikoa 21. Wizara imepokea maombi maalum ya kutenga maeneo ya EPZ kwenye Mikoa mipy ya Njombe, Geita, Katavi, Simiyu na Songwe; niwahakikishie kwamba mtapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Lukuvi, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ushirikiano anaotupatia kwa kuhusisha maeneo ya viwanda katika mipango ya miji hususani katika eneo la Kigamboni. Katika eneo la Kigamboni, Mheshimiwa Lukuvi ameniita ofisini kwake akanipatia hekta 800, kazi yangu ni kuleta Wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendelezaji wa viwanda vya kimkakati; malengo ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kuwa na uchumi unaoongozwa na maendeleo ya viwanda ifikapo 2020/2025. Hivyo mipango ya Kitaifa na Kiseka inajielekeza katika kutekeleza malengo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua ya utekelezaji Wizara yangu imeshiriki katika kuibua na kutekeleza miradi ya kimkakati ambayo sekta binafsi haijavutiwa kuwekeza. Hivyo kupitia Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC), Wizara yangu imeendelea kutekeleza miradi ya kimkakati ya makaa ya mawe ya Mchuchuma na chuma cha Liganga, makaa ya mawe ya Ngaka, mradi wa magadi soda wa Engaruka, Kiwanda cha kuzalisha viuadudu kwa ajili ya kuua viluilui vya mbu unaoendelezwa kule Kibaha na tunapitia kama nilivyowaeleza mara nyingi Bungeni namna gani tuanzishe Kiwanda cha General Tyre.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa makaa ya mawe wa Mchuchuma na Liganga; Wizara yangu imewahi kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa kiasi cha tani milioni 126 za chuma na tani milioni 428 za makaa ya mawe kimepatikana katika maeneo ya mradi na miradi hiyo inaweza kutekelezwa kwa faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu za kulipa fidia wananchi walio ndani ya maeneo hayo zitafanyika baada ya kupatikana fedha kutoka kwa Makampuni ya ubia ya Tanzania na China. Majadiliano kati ya kampuni ya ubia na TANESCO kuhusu mkataba wa kuuziana umeme PPA na ujenzi wa msongo wa umeme wa kilovolti 400 kutoka Mchuchuma hadi Makambako yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa miradi ya kufua umeme wa Megawatt 600 na kiwanda cha chuma unatarajiwa kuanza mwaka 2016 na uzalishaji unategemewa kuanza mwaka 2019 mpaka 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa makaa ya mawe wa Engaruka nishaelezea, mradi wa magadi soda wa Engaruka nimeuelezea, mradi wa kiwanda cha viuadudu wa Kibaha umeshaanza majaribio utafanya kazi, nimetoa mara nyingi taarifa kuhusu *General Tyre*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Mafuta ya Mawese; NDC imeingia ubia na Kampuni ya NAVA *Balati Singapore* kwa ajili ya kuanzisha kilimo cha mashamba makubwa ya michikichi katika eneo la hekta 10,000 pamoja na kiwanda cha kuzalisha mafuta ya kula *Pam Oil* katika Kijiji cha Kimalamisale na Dutumi, Mkoani Pwani. Mradi huo utazalisha lita milioni 58 za mafuta ya kula kwa mwaka pamoja na umeme kiasi cha Megawatt 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania inatumia mafuta ya kula tani 400,000, hawa watu wa NDC wataingiza kwenye soko tani 60,000 na tutaanzia hapo kwenda kwenye mikoa mingine tukiwahimiza tujitosheleze kwa kuweza kuwa na mafuta ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la viwanda vidogo la TAMCO Kibaha; Shirika la NDC linaendeleza maeneo ya Viwanda Industrial Estate kwa ajili ya kuanzisha viwanda vipyta hasa vya kusindika mazao na kuunganisha mashine na mitambo mbalimbali. Katika miradi ya aina hii Shirika litahalalisha viwanja kwa ajili ya uanzishwaji wa viwanda katika maeneo husika. Pale Kibaha tunalenga kuweka viwanda vya nguo, viwanda vya kuunganisha magari ili wawekezaji wanapokuja waweze kufika na kuanza kazi mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya uwekezaji chini ya EPZ; katika kuhakikisha malengo ya kuendeleza viwanda nchini, maeneo ya EPZ na SEZ ni muhimu. Maeneo ya EPZ ni maalum kwa uwekezaji wa viwanda kwa ajili ya kuzalisha bidhaa na kuza nje ya nchi wakati maeneo ya SEZ bidhaa zake ni kwa ajili ya masoko ya ndani na nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara yangu kupitia mamlaka ya EPZ imeendelea kutekeleza maeneo ya SEZ na hususani eneo la Bagamoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya fedha kwa mwaka 2016/2017, Mapato ya Serikali; katika mwaka wa 2016/2017, Wizara inatarajia kukusanya maduhuli ya shilingi bilioni 20 ikilinganishwa na lengo la shilingi bilioni 12 kwa

mwaka 2015/2016 kutokana na ada za leseni, uuzaji wa nyaraka za zabuni, faini kwa kukiuka Sheria za Leseni na makusanyo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maombi ya Fedha; katika mwaka 2016/2017, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji inaomba kutengewa jumla ya shilingi bilioni 81, 871, 992, 000 ili kutekeleza majukumu ya Wizara. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 41, 871, 992, 000 sawa na asilimia 51 ya bajeti ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 40 sawa na asilimia 49 ya bajeti ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, kumbukumbu kamili katika *Hansard* ichukuliwe katika kitabu changu cha hotuba ambayo pia inapatika kwenye tovuti ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, na Watanzania wote milionisikiliza nawashukuru sana. Pacha wangu alisema kama mnataka mali mtaipata shambani. Mimi naendelea kusema ukitoka shambani pitisha bidhaa yako kiwandani ili ukifika sokoni upate mali na tija kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

**HOTUBA YA WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI MHESHIMIWA  
CHARLES J.P. MWIJAGE (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA  
MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2016/2017 KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI.**

## 1.0 UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ambayo ilichambua Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji tarehe 13 Aprili, 2016, Jijini Dar es Salaam, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mwaka 2016/2017.

2. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema na baraka zake na kwa kutujalia afya njema kuwa pamoja leo kutekeleza wajibu wetu kwa Taifa. Naomba aendelee kuwa nasi ili hayo tuliyoyapanga, yampendeze kutupa kibali chake tuyatekeleze na yafanikiwe.

3. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Nitumie fursa hii adimu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu wa Rais na Wabunge hapo Oktoba 2015. Nawapongeza pia Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Kassim M. Majaliwa (Mb.), kwa kuteuliwa na kuthibitishwa na Bunge letu Tukufu kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia nampongeza, Mheshimiwa George Mcheche Masaju, kwa kuteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Ninawapongeza pia Mawaziri, Manaibu Waziri na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa au kuteuliwa kubeba dhamana ya kuwawakilisha wananchi katika Bunge hili Tukufu. Hakika, Watanzania wamepata viongozi wenye kupenda kuleta mabadiliko na matokeo stahiki kwa maendeleo na ustawi wa Taifa.

4. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kwa namna ya pekee, napenda kukupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika na Naibu Spika kwa kuchaguliwa kuliongoza Bunge la Kumi na Moja (11) la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Awamu ya Tano ya Uongozi wa Nchi yetu. Pia nawapongeza Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge, Katibu wa Bunge na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushirikiano mzuri ambao Wizara na wadau wetu wameendelea kuupata.

5. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Namshukuru kwa namna ya pekee kabisa Mheshimiwa Rais, kwa kuniamini na kunitfea kubeba dhamana hii kubwa ya kusimamia na kuendeleza viwanda, biashara, masoko, viwanda vidogo na biashara ndogo na uwekezaji nchini. Napenda kumhakikisha Mheshimiwa Rais, kuwa nitaendeleza dhana ya HAPA KAZI TU, kuhakikisha kuwa natimiza kiu ya Watanzania na kufanya zaidi ya yale yaliyokusudiwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia.

6. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Vilevile napenda kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dkt. Dalali Peter Kafumu, Mbunge wa Igunga (CCM), na Makamu wake Mheshimiwa Vicky Passcal Kamata, Mbunge wa Viti Maalum (CCM) na Waheshimiwa Wajumbe wote kwa namna ambayo wameipokea, kuichambua na kushauri juu ya mambo ya msingi ya Bajeti ya Mwaka

2016/2017, katika kuendeleza viwanda, biashara, masoko, viwanda vidogo na biashara ndogo na uwekezaji. Napenda kukuhakikishia Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri na maelekezo ya Kamati yamezingatiwa katika kuandaa na kuboresha Hotuba ninayoiwasilisha.

7. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri yenyе kutoa mwelekeo sahihi, dira na malengo ya utendaji wa Serikali katika kutekeleza Mipango na Programu za Serikali ya Awamu ya Tano kwa Mwaka 2016/2017, na kuendeleza mafanikio yaliyopatikana kwa awamu zilizopita. Aidha, nawapongeza mawaziri ambao wamewasilisha Hotuba zao za Bajeti za Mwaka 2016/2017 na kupitishwa na Bunge lako Tukufu.

8. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Napenda kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati kabisa wapiga kura wangu wote wa Jimbo la Muleba Kaskazini kwa kuniamini, kunipa moyo na ushirikiano mzuri ulioniwezesha kuchaguliwa kuwa Mbunge wao na pia katika kutekeleza majukumu yangu kama mwakilishi wao katika Bunge hili Tukufu. Naishukuru pia familia yangu hususan mke wangu, watoto, ndugu na jamaa kwa sala zao na ushirikiano wao mzuri unaoniwezesha kuwatumikia Watanzania bila ya kuchoka. Nawaombeni tuendelee kushirikiana kwani naona tuendako kuna mwanga na matumaini makubwa zaidi.

9. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Ujenzi wa uchumi wa nchi yetu na hususan maendeleo ya sekta za viwanda, biashara, masoko, viwanda vidogo, biashara ndogo na uwekezaji unategemea sana ushirikiano wa wananchi na wadau wote wa ndani na nje ya nchi. Hivyo, napenda kuwatambua na kuwashukuru Taasisi za Sekta Binafsi za ndani na nje ya nchi, waandishi na wamiliki wa vyombo vya habari, Washirika wa Maendeleo na Watanzania wote kwa ujumla. Aidha, namshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na wachapishaji wengine kwa kuchapisha machapisho mbalimbali ya Wizara kwa wakati.

10. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Hotuba hii ya Bajeti ninayoiwasilisha ni matokeo ya uratibu na ushirikiano mzuri wa viongozi wenzangu katika Wizara. Napenda kuwapongeza Katibu Mkuu – Viwanda, Dkt. Adelhelm Meru; Katibu Mkuu-Biashara na Uwekezaji, Prof. Adolf Mkenda, Naibu Katibu Mkuu, Mhandisi Joseph Malongo; Wakuu wa Idara, Vitengo, Taasisi na watumishi wote wa Wizara. Hilo ndilo jeshi langu la wataalamu wachapa kazi, lenye ari, wanaobeba kwa dhati dhamana ya kutekeleza maamuzi mapana ya kitaifa katika sekta na ndiyo kiini cha mafanikio ya sekta hii. Kwa ujumla wanatumia ipasavyo utaalamu na ujuzi wao na hivyo kufanya kazi nzuri katika kuongoza na kusimamia utekelezaji wa majukumu ya kisekta (Jedwali Na. 1). Napenda kuwasihhi kuendelea na ari hiyo.

11. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Naomba kuwapa pole ndugu, jamaa na wananchi wote waliokumbwa na kadhia ya mafuriko na ajali zilizotokea na kusababisha majeruhi, ulemavu na uharibifu mkubwa wa mali. Mwenyezi Mungu awatie nguvu na kuwapa faraja na ahueni haraka ili warejee katika hali njema na tuendelee kulijenga Taifa.

## 2.0 MCHANGO NA MWELEKEO WA SEKTA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI KATIKA KULETA MAGEUZI YA UCHUMI

12. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Mwaka 2016/17 – 2020/21 ambao utekelezaji wake unaanza Mwaka 2016/2017, unalenga katika kujenga uchumi wa viwanda ili kuleta mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu. Mpango huo unabainisha mikakati mipya na pia kukamilisha mipango iliyotangulia ambayo haijakamilishwa ikiwemo MKUKUTA na Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano, ili hatimaye Tanzania iwe nchi ya uchumi wa kati inayoongozwa na viwanda ifikapo Mwaka 2025. Kimsingi, Sekta ya Viwanda ina umuhimu wa kipekee katika uchumi wa nchi yeyote ile hasa katika kutoa ajira nyingi na endelevu, kuzalisha na kukuza teknolojia zinazohitajika na sekta nyingine, kuchangia katika Pato la Taifa moja kwa moja na kupitia sekta mwambata pamoja na kodi itokayo kwa watu walioajiriwa. Aidha, Sekta ya Viwanda ni msingi wa maendeleo ya Sekta ya Kilimo kwa sababu kuu mbili. Kwanza inazalisha teknolojia na zana mbalimbali ambazo zinarahisisha na kuongeza tija kwa Sekta ya Kilimo. Pili, Sekta ya Viwanda inaokoa na kurefusha maisha ya malighafi kwa kuzisindika ambapo zingeweza kuharibika au kwisha muda wa matumizi yake mapema. Kadhalika, Sekta ya Viwanda inawezesha Taifa kujitegemea kiuchumi na hiyo inalipa Taifa nafasi nzuri ya kujilinda na maadui ambao hutumia uchumi kama nyenzo ya kuyumbisha mataifa mengine. Sekta hiyo pia inachocheara ukuaji wa sekta nyingine (backward and forward linkage) kwa kutoa fursa ama za kuanzisha viwanda unganishi au kutumika kama malighafi mahiri katika sekta nyingine.

13. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Ujenzi wa uchumi wa viwanda ni vita, tena vita kubwa sana. Mafanikio katika uchumi wa viwanda yatasababisha nchi yetu kuwa Taifa la watu wenyе kipato cha kati. Hii ni jamii ambayo watu wake walio wengi wameondokana na matatizo ya ujinga, umaskini na maradhi. Upande wa pili, uchumi wa viwanda utaliweka Taifa letu katika kundi la mataifa yanayozalisha bidhaa bora na zenye ushindani wa soko la kimataifa badala ya kuwa chanzo cha malighafi na soko la bidhaa kwa viwanda vya mataifa mengine. Ili kufikia azma hiyo, ushiriki na mchango wa mtu mmoja mmoja, makundi ya watu, taasisi za umma na taasisi za binafsi utahitajika katika vita hiyo. Muhimu, ni Watanzania kubadili mtazamo na kujenga utamaduni unaolenga kuwa na Taifa lenye uchumi wa viwanda. Hiyo ni pamoja na kila

mmoja wetu kwa uwezo wake kulenga kuwekeza katika viwanda na kupenda kununua bidhaa zinazozalishwa nchini.

14. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika miaka ya 1980, viwanda vingi vilivyokuwa vimeazishwa chini ya Mkakati wa Taifa wa Viwanda vya Msingi (Basic Industrialization Strategy) vikiwa vinamiliikiwa na Serikali vilikuwa kutokana na sababu kadhaa. Mojawapo ya sababu hizo ni matumizi ya teknolojia duni katika uzalishaji uliosababisha kuzalisha bidhaa zenyenye viwango na ubora wa chini na hivyo kushindwa kuhimili ushindani katika masoko ya kimataifa. Aidha, vingi ya viwanda hivyo viliendeshwa na menejimenti ambazo hazikuwa na ujzi pamoja na stadi za uendeshaji wa viwanda kwa tija na zenyenye mwelekeo wa kibiashara. Uhaba wa mafuta (global oil crisis) ulioikumba dunia uliosababisha kukosekana kwa fedha za kigeni za kuagiza vipuri na malighafi muhimu za kutumia viwandani ambazo pia zilipanda bei na hivyo kufanya viwanda kufanya kazi chini ya uwezo uliosimikwa (capacity under-utilization). Vilevile, Vita vya Kagera vya Mwaka 1978, vilisababisha rasilimali za Taifa hata zile zilizotegemewa kutumika katika uzalishaji viwandani kuelekezwa katika kukabiliana na adui.

15. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kufuatia changamoto hizo, Serikali ilibaini ni vyema jukumu la kuendesha uchumi lipewe Sekta Binafsi na Serikali ibaki na jukumu la kuweka mazingira wezeshi na rafiki ya kufanya biashara na kuwekeza. Huo ndiyo mwelekeo katika ujenzi wa Sekta ya Viwanda unaohamasishwa na Serikali ya Awamu ya Tano, na Wizara yangu imejipanga vema katika kuhakikisha Watanzania wanashirikishwa ipasavyo katika kujenga uchumi wa viwanda.

## 2.1 MCHANGO WA SEKTA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI

### 2.1.1 Sekta ya Viwanda

16. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kwa mujibu wa takwimu mpya za Mwaka wa Kizio wa 2007, mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato halisi la Taifa ulikuwa asilimia 5.2 Mwaka 2015 ukilinganishwa na kiwango cha asilimia 5.6 Mwaka 2014. Kwa kipindi cha 2005 hadi 2014, ukuaji wa Sekta ya Viwanda umekuwa ukiongezeka kutoka asilimia 9.6 Mwaka 2005 na kufikia kilele cha asilimia 11.5 Mwaka 2007 kisha kuanza kushuka hadi kufikia kiwango cha chini cha asilimia 4.1 Mwaka 2012 na kuanza kupanda tena hadi kufikia asilimia 6.8 Mwaka 2014. Hivi sasa, Pato la Taifa linaongezeka zaidi (7%) ya ukuaji wa Sekta ya Viwanda (5.2%). Pamoja na ukuaji wa Sekta ya Viwanda kuwa wa kupanda na kushuka, mchango wake katika Pato la Taifa kwa wastani umekuwa ukiongezeka ijapokuwa katika kiwango kidogo (increasing at decreasing rate). Aidha, mchango wa Sekta ya Viwanda katika mauzo ya nje umefikia asilimia 23.31 Mwaka 2014 ikilinganishwa na asilimia 9.31 Mwaka 2005 (Jedwali Na 2).

17. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Idadi ya viwanda hapa nchini imeendelea kuongezeka kutoka viwanda 125 Mwaka 1961 (wakati wa uhuru) hadi kufikia viwanda 49,243 Mwaka 2013. Kasi kubwa ya kuongezeka viwanda imekuwa kati ya Mwaka 2006 hadi 2013 ambapo vimeongezeka kutoka viwanda 5,153 Mwaka 2005 hadi viwanda 49,243 Mwaka 2013.

Aidha, kati ya hivyo, viwanda vikubwa vinavyoajiri kuanzia watu 100 ni 247, viwanda vya kati vinavyoajiri kati ya watu 50 na 99 ni 170, viwanda vidogo vinavyoajiri kati ya watu watano na 49 ni 6,907 na vile viwanda vidogo sana vinavyoajiri chini ya watu watano ni 41,919. Hiyo inadhihirisha kuwa, jithada za Serikali zinazoendelea kuelekezwa katika kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara na kuendeleza viwanda vidogo, zitasaidia wananchi walio wengi zaidi kupata ajira, kuongeza kipato na kupunguza umasikini. Vilevile, jithada za uhamasishaji zinazoendelea kufanywa na Serikali kwa kushirikiana na SIDO, TIC, NDC na EPZA ikiwemo uanzishwaji wa viwanda vipyta na kuongeza uwezo wa uzalishaji (capacity utilization) kwa viwanda vinavyozalisha chini ya uwezo uliosimikwa (installed capacity) zitaongeza uzalishaji na idadi ya viwanda (Jedwali Na.3 & 4).

18. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Viwanda vimeendelea kuwa chanzo cha ajira hususan kwa vijana na wanawake ambapo jumla ya ajira 264,223 zimepatikana hadi kufikia Mwaka 2015. Ajira hizo ambazo ziko mikoa yote nchini zimegawanyika kutokana na ukubwa wa kiwanda kama ilivyoanishwa katika Jedwali Na 5. Aidha, uzalishaji viwandani kwa baadhi ya bidhaa muhimu umeendelea kuongezeka katika kipindi cha miaka tisa kuanzia Mwaka 2006 hadi 2015 kama inavyoonekana katika Jedwali Na 6. Pamoja na kukua kwa sekta ya uzalishaji viwandani, viwanda vya hapa nchini havijaweza kuzalisha hadi kufikia kiwango cha uwezo uliosimikwa (installed capacity). Takwimu kutoka Ofisi ya Takwimu ya Taifa zinaonesha kuwa wastani wa uzalishaji viwandani ni asilimia 50 ya uwezo wake kwa mwaka.

### **Viwanda Vilivyobinafsishwa**

19. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kufuatia sera ya ubinafsishaji iliyoanza kutekelezwa katika miaka ya 1990, jumla ya viwanda 141 nchini vilirekebisha mifumo yake kuptitia ubinafsishaji. Viwanda hivyo ni kutoka sekta za viwanda, kilimo, mifugo, madini, maliasili na misitu. Ubinafsishaji ulifanyika kwa kuuza hisa, kuuza mali yote, kuingia ubia na Sekta Binafsi, na ufilisi (Jedwali Na 7). Kwa viwanda vilivyo vingi kama si vyote, mikataba ya mauzo iliendana na masharti yake makuu matatu ambapo wamiliki wapya pamoja na fedha waliyotoa walitakiwa kuhakikisha viwanda hivyo vinafanya kazi kwa tija ili viweze kulipa kodi, kutoa ajira na kuzalisha bidhaa na huduma.

20. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Ni lengo la Serikali ya Awamu ya Tano kuona kuwa viwanda vyote vilivyobinafsishwa vinafanya kazi. Viongozi Wakuu wa Nchi wamekuwa wakisitisiza utekelezaji wa lengo hilo na Wizara yetu kwa kushirikiana na Msajili wa Hazina tunafuatilia jukumu hilo siku kwa siku. Kati ya viwanda 106 vilivyofanyiwa tathmini, viwanda 45 vinafanya kazi vizuri, 24 vinafanya kazi kwa kusuasua na 37 vimefungwa. Mpango wetu ni kuhakikisha kuwa viwanda 35 vilivyobaki vinafanyiwa tathmini haraka na kabla ya nusu ya kwanza ya Mwaka wa Fedha unaoanza Julai 1, 2016, hatima ya viwanda visivyofanya kazi itajulikana. Hatima ya viwanda visivyofanya kazi ni kwa wamiliki waliopewa kutekeleza mikataba ya mauzo au kupewa wawekezaji wapya ili waviendeshe.

21. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Tathmini yetu pia inaonesha mafanikio yaliyotokana na utekelezaji wa Sera ya Ubinafsishaji. Serikali imeondokana na mzigo mkubwa wa kutoa ruzuku ya kuendesha mashirika ya biashara yaliyokuwa chini yake. Itakumbukwa kuwa utaratibu wa ruzuku ni moja ya sababu zilizosababisha mashirika ya umma kufanya vibaya siku za nyuma. Viwanda vinavyofanya kazi vimeweza kutimiza malengo ya kutoa ajira na kuzalisha bidhaa. Hali hii inadhihirishwa na ongezeko la uzalishaji wa vinywaji, saruji, nguo, sigara, chupa kwa kutaja baadhi. Aidha, viwanda hivyo vimekuwa miongoni mwa makampuni yanayolipa kodi vizuri. Kwa mfano, Mwaka 2015, TBL imelipa jumla ya shilingi bilioni 384.3 kama kodi kwa Serikali.

## 2.1.2 Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo

22. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Sekta ya Viwanda Vidogo na vya Kati (Micro, Small and Medium Enterprises- SMEs) ina nafasi kubwa katika kuzalisha ajira nchini na kuongeza kipato cha wananchi wa kawaida. Kulingana na utafiti wa shughuli za Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ya Mwaka 2012, Sekta hiyo inatoa ajira za moja kwa moja kwa Watanzania milioni 5.2 na kuchangia takribani asilimia 28 katika Pato la Taifa. Aidha, kulingana na takwimu za awali za Sensa ya Viwanda nchini, inaonesha kuwa, Tanzania ina jumla ya viwanda 49,243 vinavyojumuisha viwanda vidogo sana (85.13%), viwanda vidogo (14.02%), viwanda vya kati (0.35%) na viwanda vikubwa (0.5%). Kupitia takwimu hizo, ni dhahiri kuwa asilimia 99.15 ya viwanda vyote nchini ni viwanda vidogo sana na viwanda vidogo.

23. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Taswira ya takwimu hizo, inaonesha wazi kuwa maendeleo ya viwanda Tanzania kama ilivyo katika nchi nyingine yatatokana na kuweka nguvu katika sekta ya viwanda vidogo sana na viwanda vidogo. Faida za sekta hiyo ni kuwa, uanzishwaji wa viwanda vya aina hiyo hauhitaji elimu na mtaji mkubwa na hivyo vinaweza kuanzishwa katika eneo lolote la nchi yetu. Sekta hiyo inatoa mwanya mkubwa kwa vijana na wanawake kuanzisha viwanda na kujajiri ambapo wasingepata fursa katika sekta nyingine zinazotoa ajira. Viwanda vidogo huongeza thamani ya mazao, hali ambayo humpatia

kipato zaidi mzalishaji na kupunguza hasara baada ya mavuno. Sekta ya Viwanda Vidogo ni shule mahsus kwa Watanzania kwa kuwa inawaandaa kuwa wamiliki wa viwanda vya kati na viwanda vikubwa hapo baadae. Upande wa kijamii na kiuchumi pia, uwepo wa viwanda sehemu zote za nchi na hasa vijijiini hupunguza kasi ya wananchi kuhamia mijini.

### 2.1.3 Sekta ya Biashara

24. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wizara imeendelea na jitihada za kupanua wigo wa fursa za masoko yenye masharti nafuu kuitia majadiliano ya kibiashara baina ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa. Jitihada hizo zinaenda sambamba na kuhamasisha Sekta Binafsi nchini kuchangamkia fursa hizo. Pato la Taifa kwa shughuli za biashara ambazo inahusisha mauzo na manunuzi ya bidhaa na huduma kwa bei za soko liliongezeka kutoka Shilingi bilioni 32.6 mwaka 2014 hadi Shilingi bilioni 36.34 kwa mwaka 2015. Baadhi ya shughuli za kibiashara zilizochangia ongezeko hilo ni pamoja na malazi na huduma, habari na mawasiliano, upangishaji nyumba, sanaa na burudani (*Jedwali Na. 8*).

25. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Mauzo ya bidhaa kwenye baadhi ya nchi zinazotoa masoko ya upendeleo yalikuwa kama ifuatavyo: mauzo ya Tanzania kwenye soko la China yalipungua kutoka Dola za Marekani milioni 683.9 Mwaka 2014 hadi Dola za Marekani milioni 645.9 Mwaka 2015. Wakati manunuzi ya Tanzania kutoka China yalikuwa Dola za Marekani milioni 2147.6 Mwaka 2015 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 1571.1 Mwaka 2014. Mauzo katika Soko la India yaliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 1,254 .5 Mwaka 2014 hadi Dola za Marekani milioni 1,320.3 Mwaka 2015. Ongezeko hilo lilichangiwa na uuzaji wa bidhaa mbalimbali kama; karafuu, korosho, ngozi za wanyama, nazi, bidhaa za jamii ya kunde pamoja na samaki, pamba na nyuzi za katani. Kwa Mwaka 2015, manunuzi ya Tanzania kutoka India yalipungua kutoka Dola za Marekani milioni 1848.6 Mwaka 2014 hadi Dola za Marekani milioni 1,458.3 mwaka 2015. Hali hiyo ilisababishwa na kupungua kwa kiwango cha uingizaji wa bidhaa kama vile vyuma, vitu vya plastiki, bidhaa za kemikali, tumbaku, nafaka na chai (*Jedwali Na. 9*). Mauzo katika soko la Japani yaliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 247.8 Mwaka 2014 hadi Dola za Marekani milioni 263.4 milioni Mwaka 2015. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni pamoja na vito vya thamani (precious metal ores), kahawa, samaki, nyama, mafuta ya mbegu, chai, wanyama hai, matunda na pamba. Mwaka 2015, manunuzi ya bidhaa kutoka Japani yalikuwa na thamani ya jumla ya Dola za Marekani milioni 458.6 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 559.3 mwaka 2014, sawa na upungufu wa aslimia 18. Aidha, kwa ujumla kuongezeka kwa mauzo ya Tanzania katika masoko hayo, mbali na mambo mengine, kumechangiwa kwa kiasi kikubwa na jitihada mbalimbali zinazoendelea nchini za kuimarisha Sekta ya Viwanda na hamasa ya wananchi kuanza kutumia bidhaa zinazozalishwa nchini (*Jedwali Na. 10*).

26. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika kutumia vema fursa za masoko ya kikanda, mauzo ya Tanzania kwenda katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki yaliongezeka Mwaka 2015 na kufikia Dola za Marekani milioni 1,062.4 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 598.1 Mwaka 2014. Hali hiyo ilichangia Tanzania kuwa na urari chanya wa biashara katika soko hilo. Bidhaa za Tanzania zilizouzwa kwa wingi katika soko hilo ni pamoja na; mboga mboga, chai, matunda, magunia, mifuko ya plastiki, wanyama hai, viazi, samaki, udongo asilia, kahawa, mahindi, mchele, unga wa nafaka, karanga, mawese, ufuta, pamba na makaa ya mawe. Kwa upande mwingine manunuzi ya Tanzania kutoka nchi za Jumuiya hiyo yalipungua kutoka Dola za Marekani milioni 706.4 Mwaka 2014 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 322.8 Mwaka 2015. Upungufu huo umechangiwa na kuimarika kwa uzalishaji wa ndani uliosababisha kupungua kwa kasi ya uagizaji wa bidhaa kama vile sabuni, vifaa vya plastiki, mafuta ya kupikia, sukari, nyama, wanyama hai, vinywaji na bidhaa za mifugo (Jedwali Na. 11).

27. **Mheshimiwa Naibu Spika**, mauzo ya Tanzania kwenda katika soko la nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), yaliongezeka Mwaka 2015 na kufikia Dola za Marekani milioni 1,357.7 ikilingwanishwa na Dola za Marekani milioni 1,235.9 Mwaka 2014. Bidhaa zilizouzwa katika soko hilo ni pamoja na dhahabu, chai, mazao jamii ya kunde, tumbaku, ngano, ngozi, pamba, matunda ya juisi, mawese, mbolea, vipuri vya magari na samaki. Aidha, manunuzi ya Tanzania kutoka katika soko hilo yalipungua kutoka Dola za Marekani milioni 773 mwaka 2014 mpaka Dola za Marekani milioni 771.2 Mwaka 2015. Hali hiyo ilitokana na kupungua kwa uagizaji wa bidhaa kama vile chuma, vipuri vya magari, madini na vinywaji (Jedwali Na. 12).

28. **Mheshimiwa Spika**, Katika kuongeza fursa masoko na kurahisisha ufanyaji biashara, Wizara inakamilisha Mkakati wa Kitaifa wa kukuza mauzo ya Tanzania katika soko la Marekani kuititia mpango wa AGOA. Hadi sasa kuititia Mpango huo mauzo ya viwanda viwili vya Tanzania (Tooku Garments Ltd na Mazava Fabrics Ltd) vinavyouza nguo kuititia Mpango wa AGOA yamefikia jumla ya Dola za Kimarekani milioni 25 na vimetoa ajira 4,000 nchini. Ni matarajio yetu kuwa Mkakati huo utakapoanza kutumika utakuwa chachu ya kuongezeka kwa ajira na mauzo ya Tanzania katika soko la Marekani kwa kipindi cha nyongeza cha mpango huo (AGOA Extension and Enhancement Act (2015) (Jedwali Na. 13).

29. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Serikali imepanga kuboresha Sheria ya Anti Dumping (2004). Maboresho hayo yataendana na mpango wa Serikali ya Awamu ya Tano ya kuwa na uchumi wa viwanda unaotumia na kuhamasisha uongezaji thamani wa malighafi zinazopatikana nchini. Vile vile, Sheria hiyo inatarajiwa kuwa madhubuti katika kukabiliana na ushindani usio wa haki katika soko la ndani. Pia, Wizara inakamilisha Waraka ili kuiomba Serikali kuridhia

Mkataba wa Urahisishaji Biashara chini ya Shirika la Biashara Duniani. Mchakato huo unaenda sambamba na zoezi la kuunda Kamati ya Kitaifa itakayosimamia utekelezaji wa Mkataba huo. Tayari Wizara imekwishatoa maelekezo kwa wizara na taasisi husika kuhusu uundwaji wa Kamati hiyo. ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa matakwa ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mshariki. Aidha, Wizara imekamilisha rasimu ya mwisho ya Mkakati wa Kitaifa wa kuondoa Vikwazo Visivyo vya Kiushuru. Ni matumaini yetu kuwa juhudhi zote hizo zitasaidia kwa kiasi kikubwa wepesi wa kufanya biashara nchini, kikanda na kimataifa.

**30. *Mheshimiwa Naibu Spika*,** Katika kukuza dhana ya diplomasia ya kiuchumi na biashara kimataifa, Wizara imekuwa ikishiriki katika mikutano ya majadiliano ya kibiashara katika ngazi za kikanda na kimataifa. Kupitia majadiliano hayo, Wizara imeendelea kutetea na kulinda maslahi mapana ya Taifa na makundi maalum kama vile Afrika (African Group), Nchi Changa (Least Developed Countries-LDCs), G77+China n.k.

Kwa fursa ya kipekee napenda kumpongeza Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuteuliwa tena kwa kipindi cha mwaka mmoja kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, Tanzania imeteuliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa kundi la G77+China katika Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo (UNCTAD); na pia kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Haki Miliki na Ubunifu chini ya Shirika la Biashara la Dunia (WTO). Uteuzi huo ni ishara tosha kuwa ushiriki wetu katika majadiliano hayo una tija sio tu kwa Taifa bali hata kwa nchi na makundi mengine yenye maslahi yanayofanana na ya kwetu.

#### **2.1.4 Sekta ya Masoko**

**31. *Mheshimiwa Naibu Spika*,** Bei ya mazao makuu ya chakula kama vile mahindi, maharage, mchele, ngano, uwele, ulezi, na mtama kwa msimu wa 2015/2016 zimeongezeka kwa viwango tofauti ikilinganishwa na msimu wa 2014/2015. Kwa mfano, wastani wa bei ya mahindi kwa gunia la kilo 100 ilipanda kutoka Shilingi 41,760 Mwaka 2014/2015 na hadi Shilingi 61,245 Mwaka 2015/2016 sawa na ongezeko la asilimia 46.66. Bei ya gunia la maharage la kilo 100 ilipanda kutoka Shilingi 146,350 Mwaka 2014/2015 hadi Shilingi 166,061 Mwaka 2015/2016 sawa na ongezeko la asilimia 13.47. Bei ya mazao mengine ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 14. Kupanda huko kwa bei ya mazao makuu ya chakula kumetokana na kushuka kwa ugavi (supply) na pia Serikali kuendelea kutekeleza sera ya kuruhusu uuzaji wa mazao makuu ya chakula nchi jirani bila vikwazo na hivyo wakulima kuuza kwenye masoko yenye bei nzuri zaidi.

**32. *Mheshimiwa Naibu Spika*,** Katika Mwaka 2015/2016, kumekuwa na ongezeko dogo la bei ya mifugo hususan ng'ombe, mbuzi na kondoo. Wastani

wa bei ya jumla ya ng'ombe (majike na madume) kwa daraja la pili iliongezeka kutoka wastani wa shilingi 1,063,897 Mwaka 2015, hadi Shilingi 1,105,321 mwezi Machi, 2016 sawa na ongezeko la asilimia 3.89. Bei ya ng'ombe (majike na madume) daraja la tatu ilipanda kutoka Shilingi 784,609 Mwaka 2015 hadi shilingi 802,756 mwezi Machi, 2016, sawa na ongezeko la asilimia 2.31. Bei ya mifugo mingine ni kama ilivyoonekana katika Jedwali Na. 15. Kupanda kwa bei hizo kumechangiwa na ongezeko la ubora wa mifugo na ongezeko la mahitaji.

### **2.1.5 Sekta ya Uwekezaji**

33. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Sekta ya Uwekezaji imeendelea kutoa mchango mkubwa kutokana na wawekezaji wapya wa ndani na nje ya nchi. Tanzania imeendelea kuongoza katika kuvutia wawekezaji kutoka nje ikilinganishwa na nchi nyingine katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa takriban miaka mitano mfululizo. Uwekezaji wa miradi hiyo umekuwa wa muhimu kwa uchumi wa nchi yetu hasa kwa kuwa umeingiza mitaji, teknolojia mpya na mafunzo ya mbinu mpya za kitaalamu katika kuendesha na kusimamia miradi. Mwaka 2015, miradi 466 iliyosajiliwa ilitarajiwa kuwekeza mtaji wa kufikia Dola za Marekani milioni 5,892 na kutoa ajira kwa Watanzania 46,250. Kutokana na uhamasishaji unaoendelea, ni mategemeo yetu kuwa mwaka 2016, uwekezaji utaongezeka na pia ajira zitaongezeka na hivyo kuchangia katika kukuza Pato la Taifa na kupunguza umaskini.

## **2.2 MWELEKEO WA SEKTA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI**

34. **Mheshimiwa Naibu Spika**; Maendeleo endelevu ya kiuchumi yanahitaji mifumo ilioimashwa katika kujenga uwezo wa uzalishaji wa ndani wenye kuunganisha juhudhi ya kila sekta ya uchumi (forward and backward linkages) kumudu kwa kiwango kikubwa mahitaji ya soko la ndani na ushindani wa bidhaa kutoka nje. Uwezo wa kushindana utategemea zaidi uzalishaji kwa kutumia rasilimali za ndani ya nchi zenye uwezo wa kuvutia uwekezaji makini kwa maendeleo ya biashara ya ndani. Ujenzi wa uchumi wa viwanda ni moja ya mbinu muhimu na ya uhakika ya kukabiliana na changamoto ya umasikini ikiwa ni pamoja na kupunguza pengo la walionacho na wasio nacho. Hivyo, uwepo wa Sekta ya Viwanda iliyojijenga na kuimariika una umuhimu mkubwa katika kuweka chachu ya maendeleo ya sekta nyingine. Ni dhahiri kuwa, utashi wa Serikali ya Awamu ya Tano wa kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi unaoongozwa na viwanda kama inavyoelekezwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 ni mtazamo sahihi na wenye mwelekeo muafaka.

35. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kwa misingi hiyo, na kutokana na umuhimu huo, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji inatekeleza jukumu la kuongeza mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa na kuongeza ajira kwa umma hususan kwa vijana na wanawake. Wizara yangu, imeandaa

mpango kazi wa kutekeleza malengo hayo katika kipindi cha miaka mitano (2015 - 2020) kwa kuhusisha sekta zote za uchumi. Mpango huo unakusudia kuendeleza viwanda vinavyotumia malighafi za ndani hususan kwenye sekta za kilimo na maliasili; viwanda vinavyozingatia fursa za kijiografia; viwanda vinavyotumia nguvu kazi zaidi (kuzalisha ajira); viwanda vinavyoendana na ukuaji wa miji; viwanda vitakavyozalisha bidhaa kukidhi mazingira ya biashara na kuwekeza zaidi kwenye rasilimali watu; na viwanda vinavyozaa viwanda vingine. Viwanda vinavyolengwa ni vya mbolea na kemikali zitokanazo na mafuta jamii ya petroli au gesi asilia, chuma (iron & steel), nguo na mavazi, *light industries*, utalii na usindikaji mazao ikiwemo mafuta ya kula, ubanguaji wa korosho, matunda, maziwa na bidhaa zitokanazo na maziwa na bidhaa zitokanazo na ngozi.

36. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Nchi kama Malaysia, Korea Kusini, Singapore na nyiningezo ambazo uchumi wake ulikuwa unalingana na Tanzania wakati tunapata uhuru, ziliwekeza katika maendeleo ya viwanda. Hivyo, kwa kuzingatia mwelekeo huo, Wizara itaendelea kuwaelimisha Watanzania waelewe na kukubali dhana ya kujenga uchumi unaoongozwa na viwanda. Hii inazingatia ukweli kwamba uwekezaji katika viwanda, pamoja na kupanua wigo wa kodi, utaongeza ajira kwa Watanzania na kuchangia katika Pato la Taifa. Tunapozungumzia kujenga viwanda tunatambua wazi jukumu hilo ni la Sekta Binafsi kwa kampuni moja kuwekeza yenye au kuingia ubia na kampuni nyininge. Jukumu kuu na la msingi la Serikali ni kuhakikisha kuwa nchi inakuwa salama na pia inajenga mazingira wezeshi kwa Sekta Binafsi kuzalisha na kufanya biashara. Hivyo, Wizara yangu itaendelea kuhamasisha Sekta Binafsi ya Watanzania na wageni kuwekeza kwenye Sekta ya Viwanda Vidogo, vya Katiba na Vikubwa. Aidha, Wizara itawezesha upatikanaji wa maeneo ya kujenga viwanda na kutoa ushauri kuhusu upatikanaji wa mitaji na teknolojia za kisasa. Kwa ujumla, Wizara yangu itabeba jukumu la kuibua wana viwanda, kuwakuza na kuwaendeleza.

37. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kwa mujibu wa Mwongozo wa Uainishaji wa Shughuli za Kiuchumi wa Kimataifa (International Standards of Industrial Classification - ISIC), Sekta ya Viwanda inahusisha shughuli kuu tano, ambazo ni Uzalishaji Viwandani (Manufacturing); Uchimbaji Madini na Kokoto (Mining and Quarrying); Ujenzi (Construction); Uzalishaji na Usambazaji wa Umeme, Gesi, Mvuke na Hali Joto (Production and Distribution of Electricity, Gas, Steam and Air Conditioning Supply) na Shughuli za Kusafisha na Kusambaza Maji (Sewerage, Waste Management and Remediation Activities). Takwimu zilizopo kwa mujibu wa Sensa ya Mwaka 2013, zinaonesha kuwa Tanzania ina jumla ya viwanda 49,243 vikiwemo vikubwa, vya kati na vidogo vinavyohusika na shughuli za uzalishaji viwandani, uchimbaji madini, uzalishaji na usambazaji wa umeme, gesi na maji, na usafishajji na usambazaji wa maji. Kati ya viwanda

hivyo, viwanda 48,474 (sawa na asilimia 98.4) vinahusika na shughuli za uzalishaji viwandani (manufacturing).

38. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kwa mujibu wa takwimu hizo, Tanzania ina idadi kubwa ya viwanda ambavyo vingi vyake ni viwanda vidogo sana na viwanda vidogo. Viwanda hivyo ni muhimu kwani huchangia kwa kiwango kikubwa muunganiko wa shughuli za kiuchumi za uzalishaji katika hatua za awali (primary production) na utoaji mahitaji na huduma ya bidhaa. Mbali ya kuajiri watu moja kwa moja, viwanda ni kichocheo muhimu cha ajira katika sekta nyiningine za uchumi. Kwa mfano, kiwanda cha nguo mbali ya kuajiri wafanyakazi, pia huwezesha ajira za wazalishaji wa pamba, watoa huduma za usafirishaji, wabebaji mizigo na sekta ya huduma kama vile mabenki. Kimsingi, kuendelezwa kwa viwanda ni chachu muhimu katika kutuletea maendeleo makubwa na endelevu yenye kuongeza kipato na kupunguza umaskini nchini kwa kiwango kikubwa.

39. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kwa kuzingatia mtazamo na msukumo wa kimaendeleo unaohitaji kuleta mageuzi ya kiuchumi nchini, Serikali itaelekeza nguvu zake katika ujenzi wa uchumi wa viwanda. Nguvu kubwa itaelekezwa katika ujenzi wa uchumi wa viwanda unaoshirikisha sekta binafsi ikiwa mhimili mkuu wa utekelezaji. Aidha, Dira ya Maendeleo ya 2025 inatutaka tuwe nchi ya uchumi wa viwanda ambapo sura na maisha ya Watanzania walio wengi yatafanana na nchi ya kipato cha kati. Kwa msingi huo, Wizara itahakikisha kuwa inasimamia ipasavyo suala la viwanda na kuleta mafanikio yaliyokusudiwa kwa kufanya yafuatayo:

- i) Kuhakikisha viwanda vilivyopo vinafanya kazi kwa uwezo mkubwa kadri iwezekanavyo. Hii ni kwa kudhibiti bidhaa toka nje zinazoingia bila ushindani ulio sawa. Kuendeleza jitihada za kupatikana nishati ya kutosha na inayoaminika wakati wote. Kutoa nafasi ya soko kwa bidhaa zinazozalishwa na viwanda ambavyo vimesajiliwa kwenye soko la hisa la Dar es Salaam, viwanda ambavyo Serikali au Taasisi zake zina hisa na vile vinavyoajiri watu wengi;
- ii) Kuondoa vikwazo vinavyopunguza uwezo wa kiushindani kwa viwanda vyetu. Upatikanaji wa mbegu za alizeti zinazotoa mazao mengi kwa ekari na mafuta mengi kwa kilo ni moja ya eneo lilitolengwa. Uhimizaji wa uwepo wa mashamba kiini (nucleus farm) ni mbinu itakayosaidia viwanda vya Juice na maziwa kuwa endelevu;
- iii) Kwa kutambua kuwa Watanzania wana uwezo wa kuwekeza katika Sekta ya Viwanda, kwa namna ya kipekee kuhamasisha wananchi kuwekeza katika viwanda. Kwa umakini kabisa tutahimiza, kushauri na kusimamia ushiriki wa watanzania katika sekta hiyo kila mmoja/kundi kwa uwezo wake kuanzia ngazi ya vijiji, kata, wilaya mpaka taifa;

- iv) Tutahamasisha wawekezaji wakubwa wa ndani na nje ya nchi kuwekeza katika Sekta ya Viwanda katika ngazi ya kanda na taifa, na tutapigana kufa na kupona ili tuwe na miundombinu wezeshi na saidizi iliyotayari katika maeneo hayo. Huo ni mkakati maalum ambao unalenga kuongeza wepesi wa kuwekeza nchini;
- v) Maeneo yaliyoko chini ya wizara yetu yanayokwamisha shughuli za uwekezaji na biashara nchini yataboreshwa. Aidha, tutakuwa mboni ya Serikali kubaini Idara na Taasisi za Serikali ambazo utekelezaji wake unaiweka Tanzania katika nafasi mbaya katika kuvutia wawekezaji duniani. Lengo likiwa ni kubaresha mazingira ya uwekezaji ili Tanzania iwe kivutio kwa wawekezaji wa ndani na nje; na
- vi) Kwa kutambua faida ya kuwepo miundombinu wezeshi lakini pia kwa kuzingatia mikataba ya mauzo, tutahakikisha kuwa viwanda vyote vilivyobinafsishwa vinafanyakazi kwa ufanisi.

40. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Tunapoelekeza nguvu zaidi katika ujenzi wa uchumi wa viwanda tunatambua kabisa Sekta ya Viwanda nchini bado ni changa na inahitaji kulindwa. Serikali italinda viwanda hivyo kwa kuhakikisha kwamba kuna uwanja sawa wa ushindani kwa washiriki wote. Kuhusu bidhaa zinazotoka nje kama nilivyoeleza hapo juu, tutahakikisha kuwa bidhaa zinazokidhi ubora tu ndizo zinaruhusiwa kuingia nchini mwetu. Aidha, bidhaa zote zinazoingizwa nchini zitatozwa ushuru na kodi stahiki. Itakapobidi, tutaweka viwango vya ushuru ambavyo vitachochea matumizi ya malighafi zinazopatikana nchini na kuzuia bidhaa zinazozalishwa kwa ruzuku nchi za nje. Kwa namna ya kipekee, tutadhibiti bidhaa zinazoingia kwa njia ya magendo kwani pamoja na kuathiri ukuaij wa viwanda, ni chanzo cha upotevu wa mapato ya Serikali na huhatarisha afya za walaji.

41. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wizara itaendelea kuwahamasisha Watanzania kutumia ulinzi wa viwanda, biashara na masoko tunaoupara kwa mujibu wa makubaliano yaliyopo kuzalisha bidhaa shindani katika masoko ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, SADC, COMESA, CFTA na kuwasihii wazalishaji wa Tanzania wajifunge kibwebwe kusimama imara na siyo kutegemea ulinzi usiokoma (avoid protection for permanent infancy). Ni muhimu kutambua kuwa Sekta ya Viwanda tunayoilenga ni ile itakayozalisha bidhaa na huduma kukidhi mahitaji ya soko la ndani na wakati huo huo ikilenga soko la nje (import substitution plus export promotion). Ujumbe kwa wanaviwanda kote nchini; mnapozalisha bidhaa na huduma kwa ajili ya soko la ndani, muwaone wateja wenu kama wateja wa soko la kimataifa.

42. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Mpango wa Serikali katika kutekeleza mkakati wa kujenga viwanda nchini utahimiza na kusimamia msambao wa viwanda

katika sehemu zote za nchi (regional dispersion). Kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri Mkuu katika Hotuba yake ya Bajeti (2016/2017), Mamlaka za Mikoa na Wilaya zimeelekezwa kutenga maeneo kwa shughuli za viwanda na biashara. Chini ya utaratibu huo, Mamlaka za Mikoa zitawajibika kutenga maeneo; Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji itawajibika kutoa ushauri wa kitaalam; na Wizara na Taasisi zinazohusika na ujenzi wa miundombinu wezeshi zitawajibika kuhakikisha maeneo hayo yanapatiwa huduma hizo muhimu. Jambo la kuzingatia ni kwamba maeneo ya ngazi za vijiji, kata, tarafa na wilaya gharama zake zitabebwa na Serikali ya Mitaa.

43. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika ngazi ya kitaifa, tutaendeleza jitihada za kutenga na kuboresha maeneo madlum ya kiuchumi ili kurahisisha uwekezaji mkubwa katika Sekta ya Viwanda. Hatua ya kwanza ni kuhakikisha kwamba fidia inalipwa kwa maeneo yaliyotengwa siku za nyuma. Hatua ya pili ni kuendeleza maeneo ambayo tuna uhakika wawekezaji watayachukua katika siku za hivi karibuni. Hatua ya tatu ni kutenga maeneo kwa kuzingatia mahitaji ya miaka ya usoni. Mipango yetu katika kutenga maeneo hayo inazingatia uzoefu wa nchi nyingine kama Vietnam ambayo sasa inayo maeneo maalum ya kiuchumi 150 ukizingatia kuwa ukubwa wa nchi hiyo ni 1/7 ya eneo la nchi yetu.

44. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika kufanikisha hayo yote, tutajenga na kuimarisha Sekta Binafsi ili ikue na kuweza kuakisi matashi ya kisera na malengo ya kitaifa. Hivyo, sambamba na haki zinazotolewa, Sekta Binafsi ina wajibu wa kutekeleza majukumu ambayo yana tija na kuweza kuendeshwa kibiashara ikiwemo kulipa kodi na ada stahiki za Serikali. Kwa upande wa wawekezaji kutoka nje ni jukumu na wajibu wao kuhakikisha kuwa wanazingatia mikataba na masharti ya uwekezaji ikiwemo kuwajibika kulipa kodi na ada stahiki kwa Serikali, kulipia michango ya wajibu kwa nchi, kujenga mahusiano mema katika maeneo ya uwekezaji na kutoa fursa ya matumizi ya rasilimali za ndani (fedha, wafanyakazi, malighafi na huduma) yaani kuzingatia matakwa ya Local Content.

### Kuhamasisha Uwekezaji

45. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kama tunavyofahamu Tanzania ni moja ya maeneo yanayovutia uwekezaji kutokana na kupakana na nchi nane ambapo kati ya hizo sita ni nchi zisizo na bandari. Aidha, uwepo wa malighafi za kutosha, sera nzuri za uwekezaji pamoja na uhakika wa usalama wa mali zilizowekezwa nchini vinawavutia wawekezaji kuwekeza hapa nchini. Kuanzia mwezi Novemba 2015 hadi sasa wawekezaji 32 wameonesha nia ya kuwekeza kufuatia uhamasishaji uliofanywa na Wizara na Taasisi zake za uwekezaji (TIC na EPZA) katika mikoa mbalimbali nchini. Majina ya makampuni hayo yako katika Jedwali Na. 16 (a), (b), na (c). Aidha, katika juhudu hizo, Wizara imefanya

mazungumzo na wawekezaji kutoka China, Lianfa (Africa) Industrial Park project, ECO Source Limited kutoka Bangladesh na Ridham Texport Private Limited kutoka India na makampuni yanayokusudia kujenga viwanda vya kuunganisha magari.

46. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kwa mujibu wa *World Investment Report* 2015, Tanzania imekuwa chaguo namba moja kwa wawekezaji katika Kanda ya Afrika Mashariki (Tanzania is a preferred destination for industrial investment in the region). Hali hiyo ni matokeo ya uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji. Takwimu za jarida maridadi la *The Economist Pocket World in Figures* 2015 zinaonesha kuwa Tanzania ni nchi ya 17 duniani katika kasi ya ukuaji wa viwanda. Kwa kutambua hilo, Wizara yangu itaendeleza jitihada za kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara ili kuzidi kuvutia wawekezaji wapya wengi zaidi na kulinda waliopo.

47. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika kuwezesha uwekezaji nchini, Serikali imejipanga kujenga miundombinu ya msingi kwenye maeneo ya viwanda ya TAMCO – Kibaha na Zuzu - Dodoma. Wizara yangu itashirikiana na Wizara nyingine na Taasisi za Serikali ili kufanya kazi changamoto zinazokabili Sekta ya Viwanda ili kwa pamoja tuweze kuvutia wawekezaji na hatimaye kuleta maendeleo endelevu ya viwanda. Serikali inaelekeza jitihada kubwa kutokana na kutambua umuhimu na faida za uwekezaji unaofanywa na wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Uwekezaji umewezesha kuvutia mitaji ya kuchochea uzalishaji; kuongeza mapato ya serikali yanayotokana na ulipaji kodi; kutoa ajira zenye staha kwa Watanzania; na kuchangia shughuli za kuiendeleza jamii ya Watanzania.

### **Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo**

48. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika Sekta ya Viwanda Vidogo, Serikali imedhamiria kuendelea kuhamasisha Watanzania wote kuanzisha viwanda vidogo na vile vile kuhakikisha kuwa vile vidogo vilivyoanzishwa vinakuwa vya kati na vya kati vinakuwa vikubwa. Dhamira hiyo itatimia kwa kuwa Serikali imekuja na mikakati tofauti yenye lengo la kutoa huduma bora zinazokidhi mahitaji ya viwanda vidogo. Katika kuendeleza viwanda vidogo, Serikali itaendeleza maeneo ya viwanda vidogo yanayomilikiwa na SIDO. Maeneo hayo yamekuwa msaada mkubwa hasa baada ya kuanzisha utaratibu ambao hutambua ubunifu wa mjasiriamali na kumlea mpaka kufikia kampuni inayosimama yenye na kuhimili ushindani katika soko. Wito wangu kwa Watanzania na hasa vijana wanaohitimu vyuo changamkia fursa hiyo ili muweze kujajiri, kuajiri vijana wenzeni na kujenga uchumi wa Taifa letu.

49. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda vidogo katika wilaya, ni muhimu kuzingatia upatikanaji wa soko, teknolojia rafiki

na malighafi zilizoko katika wilaya hizo. Tunaamini mafanikio ya lengo hilo yatachangia kujenga ushindani mkubwa kati ya wilaya na wilaya au mkoa na mkoa na hivyo kukuza ubunifu katika jamii. Wito wangu katika hilo ni kuwaomba waheshimiwa wabunge, wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa manispaa na halmashauri zote nchini tushirikiane katika kuhamasisha ujenzi wa uchumi wa viwanda. Wizara kupitia taasisi zake hususan SIDO tutatoa utaalamu unaohitajika. Tukiweza kutumia sehemu kubwa ya rasilimali fedha zilizotengwa kwa ajili na vijana na wanawake kupitia Halmashauri za Wilaya na sehemu ya shilingi milioni 50 za kila kijiji, ujenzi wa uchumi wa viwanda utakwenda kwa kasi.

50. **Mheshimiwa Naibu Spika,** Serikali inatambua sana umuhimu wa upatikanaji wa teknolojia katika kuendeleza viwanda nchini hasa kwa viwanda vidogo. Serikali itaendelea kufanya maboresho ya vituo vyta kuendeleza na kuhawilisha teknolojia vilivyoko SIDO ili viweze kutoa huduma nzuri zaidi na teknolojia bora zenye uwezo wa kushindana na zile zinazokua kutoka nje. Vile vile, vituo hivyo vitawezeshwa ili viweze kuhawilisha teknolojia zinazotoka katika taasisi za utafiti kama vile CAMARTEC, TIRDO na TEMDO. Aidha, kwa kuzingatia umuhimu wa matokeo ya matumizi ya TEHAMA katika kurahisisha mawasiliano, kukusanya na kuchambua taarifa, Serikali itakamilisha ujengaji wa mtandao utakao ratibu Sekta ya Viwanda na Biashara Ndogo chini ya SIDO ili kufanya kazi kwa ufanisi. Pia, nchi za, China, Brazil, India, Indonesia, Japan, Korea Kusini, Malaysia, Afrika ya Kusini na Vietnam kwa kutaja baadhi, ujenzi wa Sekta ya Viwanda umetegemea sana ujenzi wa viwanda vidogo na viwanda vyta kati. Serikali kwa kutambua mafanikio waliyoyapata wenzetu tutahimiza taasisi zetu na sekta binafsi kufanya kazi kwa karibu na nchi hizo kwa lengo la kujifunza kutoka kwao.

### 3.0 UTEKELEZAJI WA MIPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2015/2016

51. **Mheshimiwa Naibu Spika,** Utekelezaji wa mipango ninaouwasilisha ni mwendelezo wa kazi na mafanikio yaliyopatikana katika awamu zilizotangulia za uongozi wa nchi yetu. Mipango hiyo imeweka misingi imara ya kuchochea maendeleo endelevu ya sekta za viwanda, biashara, masoko, viwanda vidogo & biashara ndogo na uwekezaji.

#### 3.1 MALENGO NA MIPANGO YA MWAKA 2015/2016

52. **Mheshimiwa Naibu Spika,** Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji katika mwaka 2015/2016 imetekeliza majukumu yake kwa kuzingatia Mpango Mkakati wa Wizara wa miaka mitano, yaani 2011/2012 – 2015/2016 na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Aidha, Wizara imekuwa ikitekeleza Malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015 na yale yaliyoendelezwa katika Ilani ya mwaka 2010. Kwa kuzingatia miongozo hiyo ya kisera na kimkakati, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji katika kipindi cha Mwaka 2015/2016, iliweka

msukumo mkubwa katika kuimarisha uzalishaji na tija katika viwanda viliyyopo; kuhimiza ujenzi wa viwanda vipyta ili kuongeza uwezo wa uzalishaji na michepua ya bidhaa; kuhimiza mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi; kushirikiana na Sekta Binafsi katika uanzishaji na uendelezaji viwanda vya msingi na vya kimkakati kupitia taasisi zake za NDC na EPZA; kuendeleza na kuimarisha taasisi za utafiti na maendeleo ya viwanda; uboreshaji wa mazingira ya kufanya biashara, uwekezaji na uzalishaji; na kuendeleza taaluma na weledi wa watumishi wake ili kutoa huduma bora zaidi kwa wadau. Madhumuni ya hatua zote hizo ilikuwa ni kuchangia katika uboreshaji wa urchumi wa Taifa ili kujenga Taifa linalojitegemea na linaloongozwa na urchumi wa viwanda ifikapo mwaka 2025.

### 3.1.1 Mapato

53. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwezeshaji inakusanya mapato yake kutokana na mauzo ya nyaraka za zabuni, ada za leseni na faini za leseni. Hadi kufikia mwezi Machi 2016, Wizara imeweza kukusanya jumla ya Shs. 8,910,259,698.65 ikiwa ni asilimia 74.25 ya lengo la Mwaka 2015/16 la kukusanya Shs.12,000,014,000. Makusanyo hayo ni asilimia 111.76 ya makusanyo yote ya mwaka 2014/2015 ambayo yalikuwa Shs.7,972,578,142.77. Kuongezeka huko kwa mapato kwa mwaka 2015/2016 kunatokana na sababu zifuatazo:-

- i) Jitihada za Wizara kuwaelimisha wafanyabiashara juu ya umuhimu wa kulipia leseni kwa ajili ya biashara zao;
- ii) Wizara kuweza kufanya ukaguzi wa leseni kwa mikoa miwili ya mkoa wa Dar es Salaam na Arusha. Ukaguzi huo ulisaidia kugundua wafanyabiashara wengi ambao walikuwa wanafanya biashara bila kuwa na leseni au kuwa na leseni zisizolingana na biashara wanazozifanya;
- iii) Wafanyabiashara wengi ambao walikuwa hawalipi kodi kwa miaka iliyopita walijitokeza na kulipia adhabu za ada za leseni na kulipia ada ya mwaka ya leseni; na
- iv) Taasisi za umma ambazo zilikuwa hazilipii leseni walikumbushwa na hivyo kulipia leseni hizo.

Ni matumaini yangu Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba kiasi kilichobakia cha makusanyo ya Shilingi 3,089,754,301.40, kitakusanya kabla ya kufikia mwisho wa mwaka 2015/2016.

### 3.1.2 Matumizi

54. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika Mwaka 2015/2016, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ilitengewa jumla ya shilingi 87,470,349,000 ili kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, shilingi 52,082,968,000 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, zikiwemo shilingi 44,810,316,000 za Mishahara (PE), na shilingi 7,272,652,000 zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC). Shilingi 4,800,000,000 zilitokana na makusanyo ya ndani ya Wizara (Retention) na Shilingi 2,472,652,000 kutoka Hazina.

55. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika Shilingi 44,810,316,000 zilizotengwa kwa ajili ya mishahara (PE), shilingi 4,726,832,000 zilitengwa kwa ajili ya Mishahara ya Wizara na Shilingi 40,083,484,000 zilitengwa kwa ajili ya Mishahara ya Taasisi. Aidha, kati ya fedha za Matumizi Mengineyo ya Shilingi 7,272,652,000, Shilingi 6,234,887,000 (86%) ni kwa ajili ya Wizara na Shilingi 1,037,765,000 (14%) ni kwa ajili ya Taasisi zake. Vivyo hivyo, Wizara ilitengewa Shilingi 35,387,381,000 za Matumizi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi 26,588,200,000 ni fedha za ndani na Shilingi 8,799,181,000 ni fedha za nje. Hadi kufikia mwezi Machi, 2016, Wizara ilikuwa imepokea Shilingi 29,752,487,320 sawa na asilimia 34 ya fedha zilizotengwa kwa Wizara na Mashirika kwa mwaka 2015/2016. Kati ya fedha hizo, Shilingi 28,150,375,658 ni za Matumizi ya Kawaida na Shilingi 1,602,111,662 ni za Matumizi ya Maendeleo.

#### **Matumizi ya Fedha za Kawaida na Matumizi ya Fedha za Maendeleo**

56. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Hadi kufikia mwezi Machi, 2016, fedha za Matumizi ya Kawaida Shilingi 28,150,375,658 zilizopokelewa kutoka Hazina, Shilingi 24,769,189,947 ni kwa ajili ya mishahara (PE) na Shilingi 3,381,185,711 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC). Katika fedha za matumizi mengineyo (OC) za Shilingi 3,381,185,711, Shilingi 2,082,908,934 zilitokana na makusanyo ya ndani na Shilingi 1,298,276,777 zilitoka Hazina. Kwa upande wa matumizi ya fedha za maendeleo, Shilingi 1,602,111,662 zilipokelewa kutoka Hazina ikiwa ni fedha za nje.

### 3.2 MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI

#### 3.2.1 Sekta ya Viwanda

57. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wizara yangu imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kuendeleza viwanda na kuvutia uwekezaji hususan katika viwanda vya msingi ambavyo ni kichocheo cha uanzishwaji wa viwanda vingine na viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo. Katika kuongeza juhudzi za kuongeza thamani ya mazao na kuondokana na uuzaaji wa

mazao ghafi, Wizara imeendelea kuhamasisha uwekezaji katika sekta za kusindika mazao ya kilimo.

58. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Napenda kuwashukuru Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na TAMISEMI kwa kuunga mkono juhudzi za kuendeleza viwanda. Jitihada zao zimewezesha kuyalinda maeneo ya Maeneo Maalum kwa ajili ya viwanda chini ya Mamlaka ya EPZ yaliyokwisha tengwa katika mikoa 21. Wizara imepeleka maombi maalum ya kutenga maeneo ya EPZ kwenye mikoa mipya ya Njombe, Geita, Katavi, Simiyu na Songwe. Ni matarajio yetu kuwa mikoa hiyo itatenga maeneo kwa ajili ya kuendeleza viwanda katika maeneo yao.

59. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mhe. William Lukuvi, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ushirikiano anaotupatia kwa kuhusisha maeneo ya viwanda katika mipango miji hususan katika eneo la Kigamboni kulikotengwa zaidi ya hekta 800 kwa ajili ya uwekezaji wa Viwanda bila fidia yoyote. Ninaomba ushirikiano huo uendelee kwa wizara na Halmashauri mbalimbali kutenga maeneo ya viwanda katika mipango miji ya mikoa mingine.

### **Uendelezaji wa Viwanda vya Kimkakati**

60. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Malengo ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kuwa na uchumi unaoongozwa na maendeleo ya viwanda ifikapo mwaka 2025. Hivyo, mipango ya kitaifa na kisekta inajielekeza katika kutekeleza malengo hayo. Katika hatua ya utekelezaji, Wizara yangu imeshiriki katika kuibua na kutekeleza miradi ya kimkakati ambayo sekta binafsi haijavutiwa kuwekeza. Hivyo, kupitia Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) Wizara yangu imeendelea kutekeleza miradi ya kimkakati ya Makaa ya Mawe wa Mchuchuma na chuma cha Liganga, makaa ya mawe Ngaka, mradi wa magadi-soda wa Engaruka, kiwanda cha kuzalisha viuadudu kwa ajili ya kuua viluwiluwi vya mbu wanaoeneza malaria Kibaha na Kiwanda cha Kutengeneza Matairi cha General Tyre Arusha.

### **Mradi wa Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma cha Liganga**

61. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wizara yangu imewahi kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa kiasi cha tani milioni 126 za chuma na tani milioni 428 za makaa ya mawe kimepatikana katika maeneo ya mradi na miradi hiyo inaweza kutekelezwa kwa faida. Aidha, ujenzi wa barabara kutoka Itoni (Njombe) kuelekea maeneo ya miradi kwa kiwango cha changarawe ulikuwa umekamilika. Taratibu za kulipa fidia wananchi walio ndani ya maeneo ya miradi utafanyika baada ya kupatikana fedha kutoka kwa kampuni ya ubia ya Tanzania China International Mineral Resources Ltd. Majadiliano kati ya

Kampuni ya Ubia na TANESCO kuhusu Mkataba wa kuuziana umeme (PPA) na ujenzi wa msongo wa umeme wa kilovoti 400 kutoka Mchuchuma hadi Makambako yanaendelea. Ujenzi wa miradi ya kufua umeme Megawatt 600 na kiwanda cha chuma unatarajiwa kuanza mwaka huu 2016 na uzalishaji mnamo 2019/2020.

### **Mradi wa Makaa ya Mawe ya Ngaka Kusini-Ruvuma**

62. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kampuni ya TANCOAL Energy Ltd ambayo ni ya Ubia kati ya NDC na Intra-Energy Corporation ya Australia imeendelea kuzalisha makaa ya mawe katika mradi wa makaa ya mawe ya Ngaka. Tangu uzalishaji uanze Julai, 2011 hadi Februari, 2016 Kampuni ya TANCOAL imeweza kuzalisha jumla ya tani 858,645 na kuza jumla ya tani 779,623 ndani na nje ya Tanzania. Nchi zinazonunua makaa ya mawe kutoka mradi huu ni pamoja na Malawi, Kenya, Uganda, Zambia na Rwanda. Aidha, viwanda vya hapa nchini viliviyowahi kutumia makaa ya mawe ya mradi huu ni pamoja na viwanda vya saruji Tanga, Mbeya, Lake na Dangote, Tanzania Gypsum Ltd Mufindi Paper Mills na Simba Lime. Hata hivyo, ni viwanda viwili vya saruji vya Mbeya na Lake vinaendelea kununua wakati viwanda vingine vinaagiza kutoka nje na wengine kuwa na migodi yao.

63. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Uwezo wa TANCOAL kwa sasa ni kuzalisha kati ya tani 50,000 hadi 85,000 za makaa ya mawe kwa mwezi kulingana na mahitaji ya soko. Kwa kawaida viwanda vinavyohitaji makaa ya mawe vinatoa "order" ya kuzalishiwa makaa hayo. Kulingana na uwezo wa mgodi, uzalishaji unaweza kufikia tani milioni 1.5 kwa mwaka iwapo ujenzi wa kituo cha umeme utakamilika. Ujenzi wa kituo cha kufua umeme unasubiri ujenzi wa Msongo wa Umeme wa Kilovoti 220 kutoka Makambako hadi Songea na kukamilika kwa majadiliano ya Mkataba wa kununua umeme kati ya NDC na TANESCO.

### **Mradi wa Magadi-Soda wa Engaruka**

64. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kutokana na changamoto kubwa ya mazingira katika eneo la Ziwa Natron, NDC imekuwa ikielekeza nguvu zake katika kuendeleza mradi wa magadi katika Bonde la Engaruka liliopo Wilaya ya Monduli, Mkoa wa Arusha. Mradi huu kwa sasa unaendelezwa na Serikali kupitia NDC ambapo mbia anatafutwa ili kushirikiana na Serikali kujenga na kukiendesha kiwanda cha magadi. Kwa sasa NDC inaendelea kukamilisha tafiti za msingi za Techno-economic Study na tafiti za mazingira. Tafiti hizo zitawezesha kujua gharama ya uwekezaji katika mradi kutumika katika majadiliano na mbia atakayejitokeza kuhusu mgawanyo wa hisa.

65. **Mheshimiwa Naibu Spika**, NDC imekwishaainisha eneo la ardhi linalohitajika kwa ajili ya mradi na maombi rasmi ya kumilikishwa ardhi

yamewasilishwa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli na kukubaliwa. Maandalizi ya kufanya upimaji na kazi ya utafiti wa maji safi kwa ajili ya matumizi ya kiwanda na usanifu wa miundombinu husika inaendelea. NDC inaendelea kumtafuta mbia watakayeshirikiana kujenga kiwanda hicho.

### **Mradi wa Kiwanda cha Viuatilifu katika eneo la TAMCO-Kibaha**

66. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika harakati za kutokomeza ugonjwa wa malaria nchini, Wizara kuititia NDC imekamilisha ujenzi wa Kiwanda cha Kuzalisha Viuadudu (Biolarvicides) vya kuua viluwiluvi vya mbu wanaoeneza malaria katika eneo la TAMCO-Kibaha Mkoa wa Pwani. Kiwanda hicho kilizinduliwa na Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Awamu ya Nne Nchini kwa ushirikiano na Mhe. Hailemariam Desalgne, Waziri Mkuu wa Ethiopia tarehe 2 Julai 2015 wakati majoribio ya mitambo yakiwa yanaendelea. Mpaka sasa kiwanda kimeajiri wafanyakazi 143 ambaao wamefanyiwa mafunzo yanayotakiwa. Uzalishaji wa majoribio umeanza mwezi Machi, 2016 wakati taratibu za kupata fedha za kuanza uzalishaji kamili zinakamilishwa. Aidha, makubaliano na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuhusu ununuzi wa dawa hiyo yamefikiwa na utekelezaji wake utafanyika mara baada uzalishaji kamili kuanza. Uuzaji wa viuadudu hivyo nje ya nchi unategemea kuliingizia Taifa fedha za kigeni zipatazo Dola za Kimarekani milioni 48.6 kwa mwaka.

### **Kiwanda cha Kutengeneza Matairi cha General Tyre (EA) Arusha**

67. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kiwanda cha Kutengeneza Matairi cha General Tyre Arusha kilisimamisha shughuli zake mwaka 2009 kutokana na Serikali kukosa fedha kwa ajili ya kukiendesha. Wakati huo huo aliyejewa mbia mwenza (Kampuni ya Continental AG) hakuwa tayari kuendelea kuwekeza katika kiwanda hiki. Dhamira ya Serikali hivi sasa ni kuona kiwanda hicho kinaanza kuzalisha matairi mapema iwezekanavyo. Hili linadhihirishwa wazi katika Mpango wa Serikali wa Miaka Mitano 2016/17-2020/21, na tumeponga kuanza utekelezaji mwaka wa fedha unaoanza Julai, 2016. Serikali tayari imenunua asilimia 26 ya hisa zilizokuwa zinamiliwi na mbia mwenza na hivyo kukifanya kiwanda hicho kumiliwi na Serikali kwa asilimia 100. Vile vile, Serikali imeamua kuweka dhamana ya kusimamia na kuendesa kiwanda hicho chini ya NDC na Tangazo la Serikali (GN) juu ya uamuzi huo litatolewa wakati wowote.

68. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Mradi wa Kiwanda cha Kutengeneza Matairi Arusha una maslahi mengi kwa Taifa kuanzia wakulima wa mpira, wafanyakazi kiwandani na maduka ya bidhaa hiyo, usalama kwa vyombo vya usafiri vitumiavyo matairi, kodi kwa mamlaka mbalimbali na kuokoa fedha za kigeni zinazotumika kuagiza tairi nje ya nchi. Ufufuaji wa kiwanda hicho utaenda

sambamba na upanuaji wa mashamba ya Kihuhwi (Muheza) na Kalunga (Kilombero) ili kuongeza uzalishaji wa mpira kwa ajili ya kiwanda. Kwa kuzingatia umuhimu wa mradi huo, Wizara imeiagiza NDC kuandaa andiko la kitaalamu ambalo pamoja na mambo mengine litatakiwa kujibu masuala ya kiuchumi, kiufundi na kijamii na lazima lizingatie maoni ya wadau wa sekta husika. Hatua hiyo inaenda sambamba na kuendelea kufanya utafiti wa kina kubaini ghamama za uwekezaji mpya na teknolojia ya kisasa ya kuzalisha matairi yatakayokidhi mahitaji na kuhimili ushindani katika soko la ndani na nje. Mradi huo ambao ni kielelezo tunataka ujiendeshe kwa kuwa na menejimenti huru yenye watu wenye weledi katika biashara ya matairi na bila kutegemea ruzuku ya Serikali.

### **Programu ya Kilimo kwa Ajili ya Mali Ghafi za Viwandani**

69. **Mheshimiwa Naibu Spika**, NDC inaendeleza miradi ya kilimo cha mashamba makubwa ya kibiashara kwa kushirikiana na sekta binafsi. Katika programu hiyo, Shirika linaanzisha mradi husika kwa kutafuta ardhi kwa ajili ya kilimo, kufanya upembusi yakinifu, kisha kuvutia wawekezaji watakaowekeza kwenye kilimo cha mazao yaliyobainishwa na kujenga viwanda vya kuongeza thamani ya mazao hayo. Kila mradi unasihamiwa na kampuni inayoanzishwa kwa ubia kati ya NDC na mwekezaji. Shirika pia linashirikisha wakulima wadogo katika utekelezaji wa miradi hiyo kwa utaratibu wa kilimo cha mkataba ambapo mwekezaji anawajibika kuwawezesha kwa kuwapa huduma za ughani (extension services) ili waweze kuzalisha malighafi za viwanda zenyе ubora na kwa wingi unaotakiwa na kisha kuiuzia kampuni ya ubia. Lengo kubwa la miradi hiyo ni kuzalisha mazao ya kilimo na kuongeza thamani kabla ya kuuzwa katika masoko ya ndani na nje. Moja ya miradi inayoendelezwa na Shirika chini ya utaratibu huo ni kilimo cha michikichi Mkoa wa Pwani.

### **Kilimo cha Michikichi na Kiwanda cha Mafuta ya kula**

70. **Mheshimiwa Naibu Spika**, NDC imeingia ubia na kampuni ya Nava Bharat Singapore (NBV) kwa ajili ya kuanzisha kilimo cha mashamba makubwa ya michikichi katika eneo la hekta 10,000 pamoja na kiwanda cha kuzalisha mafuta ya kula (Palm Oil) katika Kijiji cha Kimala Misale na Dutumi Mkoani Pwani. Mradi huo utazalisha lita milioni 58 za mafuta ya kula kwa mwaka, pamoja na umeme kiasi cha Megawati 10 kwa ajili ya mradi, na kuuza ziada kwenye Gridi ya Taifa. Mradi huo utagharimu Dola za Kimarekani zipatazo Millioni 111 na mapato yanayotarajiwa ni Dola za Kimarekani Milioni 51.7 kwa mwaka. Mradi pia utatoa ajira za moja kwa moja zipatazo 1,000 na nyininge zisizo za moja kwa moja zipatazo 4,000 pamoja na kuhusisha wakulima wadogo kwa utaratibu wa kilimo cha mkataba. NDC wanakamilisha taratibu za kumilikishwa ardhi kwa ajili ya mradi kiasi cha Hekta 4,000 katika Kijiji cha Kimala Misale. Utekelezaji utaanza mara moja baada ya kupata ardhi hiyo iliyombwa

na kukamilisha utafiti wa mazingira. Taratibu za kupata ardhi iliyokusudiwa kutoka kijiji cha Kimala Misale Wilayani Kisarawe (Hekta 4,000) na Dutumi Wilayani Kibaha (Hekta 6,000) zinaendelea kwa kufuatilia uhaulishaji ardhi kutoka ardhi ya kijiji kwenda ardhi ya jumla (general land) ili kuruhusu Kampuni Tanzu kupewa Hati ya Matumizi (Derivative Title).

### **Uendelezaji wa Mashamba ya Mpira**

71. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Shirika lilikabidhiwa mashamba ya mpira yaliyoko Kihuhwi – Wilayani Muheza, Mkoani Tanga na Kalunga Wilayani Kilombero – mkoani Morogoro mwezi Aprili 2009 kwa ajili ya kuyaendeleza kwa kushirikiana na sekta binafsi. Mashamba hayo yana jumla ya hekta 1,539 ambapo hekta 510 tu ndizo zilizoendelezwa kwa ajili ya kuzalisha mpira. Kwa kuwa mashamba hayo yalikuwa katika hali duni wakati wa kukabidhiwa, NDC iliweka utaratibu wa kuvuna na kuza mpira ulioko shambani, kuboresha miundombinu ya uzalishaji wa mpira na kuyaendeleza mashamba husika. Kwa sasa upandaji wa miti mipya ya mpira katika maeneo ya mashamba ambayo hayajapandwa umekwishaanza na unaendelea vizuri. Hadi sasa NDC imekwishapanda miche mipya katika eneo la wazi la Hekta 211 katika shamba la mpira Kalunga Wilayani Kilombero. Aidha, kazi ya kuanzisha vitalu vya miche ya mpira katika shamba la Kihuhwi – Muheza itaanza mwezi Julai 2016. Uzalishaji wa mpira utakapoanza mashamba hayo yanatarajiwa kutoa ajira za moja kwa moja zipatazo 350.

### **Mradi wa Kasi Mpya wa kuzalisha Chuma Ghafi**

72. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Mradi huo unatekelezwa na Kampuni ya Maganga Matitu Resource Development Ltd (MMRDL) ambayo ni ya Ubia kati ya NDC kwa niaba ya Serikali na Kampuni ya MM Steel Resources Public Limited Company (MMSR PLC) ya Tanzania. Kazi za uchorongaji wa chuma katika eneo la Maganga Matitu na makaa ya mawe katika eneo la Katewaka ili kubaini wingi wa madini husika zimekamilika. Taarifa ya Joint Ore Resources Commission (JORC) katika eneo la Maganga Matitu zinaonesha kuwepo kwa tani milioni 39.8 za chuma. Hata hivyo, kiwango hicho kinaweza kuongezeka kufuatia tafiti zaidi zilizofanyika hivi karibuni. Aidha, katika eneo la Katewaka taarifa za awali zinaonesha kuwepo kwa tani milioni 81.65 za makaa ya mawe. Taarifa ya mwisho ya kamisheni itakayojumuisha chuma cha Maganga Matitu na makaa ya mawe ya Katewaka inakamilishwa. Taarifa hiyo ni muhimu ili kuainisha maeneo ya uchimbaji, kuandaa Mpango wa Uchimbaji (Mining Plan) na hivyo kuomba Leseni za Uchimbaji wa Madini (Mining Licenses).

73. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kazi za utafiti wa sampuli za chuma na makaa ya mawe ili kubaini ubora wake kwa kiwango kinachokubalika kimataifa zimekamilika. Mtiririko (Process Flow Sheet) wa namna ya kuzalisha chuma ghafi

(sponge iron) kwa kutumia chuma cha Maganga Matitu na makaa ya mawe ya Katewaka umekwishaandaliwa. "Process Flow Sheet" ni muhimu katika kuandaa usanifu wa kiwanda cha kuzalisha chuma ghafi. Aidha, kampuni iko katika maandalizi ya kufanya utafiti wa mazingira na uthaminishaji wa mali za wananchi waliomo ndani ya maeneo ya mradi ili kuwafidia. Aidha, Kampuni ya Maganga Matitu Resource Development Ltd iko mbioni kuandaa Bankable Feasibility Study (BFS) Report itakayozivutia taasisi za fedha kutoa mkopo wa ujenzi.

### Eneo la Viwanda - Kibaha TAMCO Industrial Parks

74. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Shirika la NDC, linaendeleza Maeneo ya Viwanda (Industrial Estates) kwa ajili ya kuanzisha viwanda vipyta hasa vya kusindika mazao na kuunganisha mashine na mitambo mbalimbali. Katika miradi ya aina hii, Shirika linatayarisha viwanja kwa ajili ya uanzishwaji wa viwanda katika maeneo husika na kujenga miundombinu inayohitajika kwa ajili ya wawekezaji. Moja ya maeneo hayo ni eneo la viwanda la TAMCO lilitoko Kibaha mkoani Pwani, ambapo NDC inamiliki eneo la viwanda lenye ukubwa wa hekta 94. Eneo hilo ambalo ni nje ya liliojengwa Kiwanda cha Viuadudu limegawanywa katika viwanja kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vipyta. Wawekezaji mbalimbali wamejitokeza kuwekeza katika eneo hilo ambapo kampuni nne zimeshaingia mkataba wa upangaji (land lease) na NDC. Wawekezaji wengine amba mojatiliano yanaendelea ni pamoja na TATA Holding Ltd ya India ambayo inatazamiwa kuanzisha kiwanda cha kuunganisha magari, Kampuni ya LIANFAS ya China na VANITY FAIR ya Marekani kwa ajili ya kuwekeza katika viwanda vya nguo na mavazi, na kampuni ya EDOSAMA kwa ajili ya kuanzisha kiwanda cha samani zitokanazo na mba. Hata hivyo, wawekezaji wengi huhitaji eneo lenye miundombinu iliyo tayari tofauti na hali ya eneo ilivyo kwa sasa. Ujenzi wa miundombinu ya msingi (barabara za ndani, umeme, maji) katika eneo hilo unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2016/2017.

### NDC na Ushirikishaji wa Wananchi

75. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Shirika linashirikisha Wananchi katika fursa za utekelezaji wa miradi mbalimbali kupitia Programu Shirikishi ya Participatory Appraisal of Competitive Advantage (PACA). Shirika liliendelea kufuatilia utekelezaji wa matokeo ya programu hii shirikishi ya PACA iliyoanzishwa ili kuwashirikisha wananchi wa Ludewa katika kuibua na pia kuwaandaa waweze kuchangamkia fursa zitokanazo na miradi mikubwa ya Mchuchuma na Liganga. Mchakato wa kutengeneza maandiko ya mwanzo ya miradi na fursa zilizoainishwa na wananchi wawakilishi katika shughuli za kiuchumi na huduma ulikamilika. Aidha, juhudhi za kuwajengea uwezo wa kuendesha miradi na kuchangamkia fursa hizo, ikiwa ni pamoja na kuanzisha mahusiano ya kibiashara kati yao na walaji au wawekezaji zimefanyika na zinaendelea.

Mpango huo utatekelezwa katika maeneo mengine ya miradi ya NDC, ikiwa ni pamoja na Engaruka (Monduli) na Kimala Misale (Kisarawe).

### **Maeneo ya Uwekezaji chini ya EPZA**

76. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika kuhakikisha malengo ya kuendeleza viwanda nchini, maeneo ya EPZ na SEZ ni muhimu. Maeneo ya EPZ ni maalum kwa uwekezaji wa viwanda kwa ajili ya kuzalisha bidhaa za kuuza nje ya nchi wakati maeneo ya SEZ bidhaa zake ni kwa ajili ya soko la ndani na nje. Tangu uanzishwaji wa maeneo haya mwaka 2006 hadi mwaka 2015, jumla ya makampuni 140 yanayotoa ajira kwa wafanyakazi 36,227 yamesajiliwa na EPZA. Kati ya makampuni hayo, makampuni 61 sawa na asilimia 44 yapo ndani ya maeneo ya viwanda ya EPZA (Industrial Parks) na 79 sawa na asilimia 56 yamejenga viwanda nje ya maeneo ya viwanda yanayomilikiwa na EPZA. Jumla ya mtaji uliowekezwa katika maeneo hayo hadi mwaka 2015 ni Dola za kimarekani Bilioni 1.306. Aidha, mauzo ya nje yameongezeka kutoka Dola za Kimarekani Milioni 28 mwaka 2007 hadi Dola Bilioni 1.124 mwaka 2015.

77. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Mamlaka ya EPZ imeanzisha Kituo cha Huduma cha Pamoja (One Stop Service Centre) katika Ofisi za Mamlaka ya EPZ zilizopo ndani ya eneo maalum la uwekezaji la Benjamin William Mkapa Mabibo. Kituo hicho cha huduma kinaundwa na maafisa wa Serikali toka taasisi za TRA, Ofisi ya Waziri Mkuu inayoshughulikia Kazi na Ajira na Idara ya Uhamiaji. Maafisa hawa wanashirikiana na maafisa wa Mamlaka ya EPZ kutoa huduma mbalimbali kwa wawekezaji kama vile leseni, vibali vya kufanya kazi, vibali vya kuishi na kutoa vibali vya misamaha ya kodi na, kutatua matatizo mbalimbali ya wawekezaji kwa ujumla wake. Wizara yangu inaendelea kukiimarisha kituo hicho ili kurahisisha huduma kwa wawekezaji.

78. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika Mwaka 2015/2016, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya EPZ imeendelea kuendeleza maeneo ya uwekezaji katika baadhi ya mikoa yalikotengwa. Katika eneo la SEZ – Bagamoyo, uzinduzi wa ujenzi wa eneo la Bandari pamoja na eneo la viwanda ulifanyika tarehe 16 Oktoba, 2015 ambapo Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete Rais mstaafu wa awamu ya nne aliweka jiwe la msingi na kushuhudia utiaji saini wa makubaliano ya msingi ya uendelezaji wa bandari (Heads of Agreement). Katika kuendeleza eneo hili, kipaumbele ni ujenzi wa mradi wa bandari ya Bagamoyo kwa kuwa utachangia katika maendeleo ya eneo hilo maalumu la kiuchumi (Bagamoyo SEZ) hususan eneo la viwanda.

79. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika eneo la Mradi wa Kurasini Logistic Centre, Wizara yangu imekamilisha malipo ya fidia kwa wananchi ambao walikuwa wakiidai Serikali mwezi Aprili, 2016. Kwa sasa mipango inakamilishwa kwa ajili ya kulisafisha eneo na kuandaa michoro kwa ajili ya miundombinu

muhimu. Aidha, EPZA wanakamilisha mipango ya kutafuta fedha kwa ajili ya kulipia fidia maeneo yaliyobakia na kuweka miundombinu muhimu. Upatikanaji wa miundombinu katika maeneo hayo kutasaidia nchi yetu kuweza kushindana na nchi nyingine za Afrika kama Ethiopia na Kenya ambao wameendeleza maeneo yao ya uwekezaji kwa kujenga "Industrial Parks"

### **Mpango wa Kuhamasisha Biashara - India na Nchi za Afrika (SITA)**

80. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Tanzania ni moja ya nchi zinazofaidika na utekelezaji wa "Programu ya Support India's Trade and Investment for Africa" (SITA) inayohamasisha biashara na uwekezaji kati ya India na nchi za Afrika kwa lengo kuhamasisha biashara. Programu hiyo inasimamiwa na Kituo cha Biashara cha Umoja wa Mataifa (International Trade Centre (ITC) na kufadhiliwa na Serikali ya Uingereza. Katika kufanikisha kutumia fursa za biashara kati ya Afrika na India, Tanzania ilichagua kuandaa mikakati mitatu ya Pamba-Nguo hadi Mavazi (Cotton to Cloth), Ngozi (leather) na Mafuta ya Alizeti (Sunflower) na Muongozo (Roadmap) za zao la Mikunde (Pulses). Uchaguzi wa maeneo haya ulizingatia zaidi idadi ya ajira zitakazozalishwa katika mnyororo wote wa thamani wa mazao hayo (value chain) na kuongeza thamani ya mazao ya kilimo. Mikakati hiyo na mwongozo imekamilika na kuzinduliwa tarehe 2 Mei, 2016. Utekelezaji wa mikakati hiyo utaanza Mwaka 2016/2017.

### **Uwekezaji na Uzalishaji katika Viwanda mbalimbali**

#### **Viwanda vya Saruji**

81. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Hadi kufikia mwezi Desemba mwaka 2015, jumla ya viwanda nane vya saruji vilikuwa vikifanya kazi. Viwanda hivi vyote vilikuwa na uwezo uliosimikwa wa kuzalisha Tani Milioni 8.7 ukilinganisha na mahitaji halisi ya nchi ya takribani Tani milioni 4.3 kwa mwaka. Viwanda vingine vipya vilivyoanza uzalishaji wa saruji ni pamoja na Moshi Cement, Arusha Cement (Zaidi cement) na Fortune (Diamond cement). Pamoja na kufikia mahitaji ya saruji nchini, wawekezaji mbalimbali wameendelea kujitokeza na baadhi ya viwanda vinategemea kuongeza uzalishaji kwa kupanua viwanda vyao. Mfano, Kiwanda cha Saruji cha Mbeya kinatarajiwa kuongeza uzalishaji kutoka tani 400,000 hadi tani 1,100,000 za saruji kwa mwaka. Aidha, Kampuni ya Hengya Cement kutoka nchini China inategemea kujenga kiwanda chenye uwezo wa kuzalisha tani 2,500,000 za saruji kwa mwaka mkoani Tanga. Ongezeko hilo litaleta mchango mkubwa katika Sekta ya Ujenzi ambayo imezidi kukua kwa kasi hapa nchini na kuongeza fedha za kigeni kwa kuza saruji ya ziada.

## Sekta Ndogo ya Ngozi

82. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kwa kuzingatia wingi wa mifugo ambayo Tanzania inayo na kiasi kikubwa cha jozi 42 milioni za viatu zinazoingizwa kutoka nje kwa mwaka, Wizara yangu inatoa umuhimu mkubwa wa kuendeleza uzalishaji na kuwekeza zaidi katika sekta ya ngozi. Lengo ni kuongeza bidhaa za ngozi na idadi ya viwanda vya kusindika ngozi mpaka hatua ya “wet blue” ambavyo ni vinane kwa sasa. Hatua hii itasaidia kuepuka kuharibika kwa ngozi ghafi.

83. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika Mwaka 2015/2016, Wizara imekamilisha kufanya mapitio ya Mkakati wa Kuongeza Thamani zao la Ngozi ambao utakuwa ni mbadala wa Mkakati Uunganishi wa Kufufua na Kuendeleza Sekta ya Viwanda vya Ngozi nchini ambao muda wake wa utekelezaji umemalizika mwaka 2012. Kupitia mkakati huu, wizara kwa kushirikiana na wadau wengine itahamasisha uanzishwaji wa viwanda vinavyoboresha ngozi kutoka katika hatua ya wet blue kwa kulenga matumizi ya mtu wa mwisho (crust). Hatua hii itahamasisha uwekezaji katika viwanda vya kutengeneza viatu na bidhaa nydingine za ngozi hapa nchini.

84. **Mheshimiwa Naibu Spika**, ili kufanikisha viwanda vya ndani kuweza kuhimili ushindani katika soko, ninapenda nitoe shukurani zangu za dhati kwa wakuu wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mapendekezo yao ya kuacha utegemezi wa kutumia viatu vya mitumba na kuhamasisha uzalishaji ndani ya nchi wanachama. Ni mategemeo yangu kuwa hatua hii itatekelezwa kwa kadri tunavyoongeza uzalishaji wa kutosheleza soko la Jumuiya. Aidha, vizuizi vya kiushuru viendelee kwa kuzingatia upatikanaji wa bidhaa zilizozalishwa nchini katika soko la ndani. Vile vile, ninahimiza taasisi zinazosimamia majeshi, wanafunzi, sekta ya afya na kilimo na wananchi kwa ujumla kupenda kununua na kutumia bidhaa zenye ubora zilizozalishwa ndani ili kuwahakikishia wazalishaji uwepo wa soko. Mamlaka husika zitaendelea kusimamia viwango na ubora ili kumlinda mlaji.

85. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wizara inamiliki eneo la hekta 107 katika eneo la Zuzu mkoani Dodoma mahususi kwa ajili ya uanzishwaji wa kijiji cha viwanda vya ngozi na bidhaa za ngozi. Eneo hilo litatumwa na wawekezaji wadogo wadogo (wajasiriamali) watakaotumia ngozi kutengeneza bidhaa mbalimbali za ngozi. Uendelezaji wa eneo hilo unategemewa kuanza Mwaka 2016/2017 kwa kuweka miundombinu muhimu ikiwa ni pamoja na barabara, umeme na maji. Aidha, tathmini ya Kiwanda cha Ngozi cha Mwanza ambayo niliisimamia mimi mwenyewe ilibaini kuwa kama Taifa lazima jitihada zote zifanyike ili miundombinu ile itumike kwa kusindika ngozi.

## Viwanda vya Nguo na Mavazi

86. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Sekta ya Nguo na Mavazi ni sekta ambayo hutumia nguvu kazi kubwa katika uzalishaji. Hivyo, uendelezaji wa sekta hiyo yenye kuajiri watu wengi unapewa kipaumbele cha juu kwa kuzingatia mchango wake katika kufikia malengo ya kuongeza ajira hapa nchini. Aidha, uendelezaji wa sekta hiyo utakuwa na manufaa kwa Sekta ya Kilimo kwa kutoa fursa ya soko la uhakika na hivyo kuhamasisha uzalishaji zaidi. Kwa kuzingatia umuhimu wake, Wizara yangu kupitia Program ya SITA imekamilisha maandalizi ya Mkakati wa Uongezaji thamani zao la pamba na nguo nchini (Cotton to Cloth Value Chain Strategy). Mkakati huo unajumuisha mnyororo wote wa thamani kutoka uzalishaji wa pamba hadi utengenezaji wa mavazi. Uzinduzi wa Mkakati huo umefanyika tarehe 2 Mei, 2016 na utekelezaji unaanza mwaka 2016/2017. Sambamba na mkakati huo, Wizara inatafakari wazo la kushauri Serikali ambapo wanafunzi wa shule na vyuo watatakiwa kuvala fulana maalum (t-shirt) na fulana nadhifu (polo t-shirt), kaptula/suruali na sketi ambazo vitambaa vyake vimezalishwa na viwanda vilivyoko nchini mwetu. Inakadiriwa kuwa chini ya utaratibu huo ajira za watu 25,000 zitapatikana na matumizi ya pamba izalishwayo nchini itaongezeka kwa asilimia 17 kutoka uzalishaji wa sasa.

87. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wizara yangu imehamasisha wawekezaji kwa kuandaa vivutio mbalimbali na kuviveka katika tovuti ya TDU ([www.tdu.or.tz](http://www.tdu.or.tz)). Wawekezaji mbalimbali wakiwemo VF Corp kutoka USA, Jiangsun Lianfa kutoka China na Echo Sourcing kutoka Uingereza na Bangladesh wameonesha nia ya kuja kuwekeza nchini. Mazungumzo na wawekezaji hao yanaendelea. Aidha, baadhi ya wawekezaji wa viwanda vya mavazi vinavyoendelea kuzalisha hapa nchini wanategemea kupanua viwanda vyao kwa kuongeza uzalishaji na ajira. Mfano, kiwanda cha Mazava Fabric and Production EA Ltd kinategemea kupanuliwa na kuongeza ajira kutoka wafanyakazi 2,600 wa sasa hadi 6,000 Mwaka 2017. Vile vile, Kiwanda cha mavazi cha Touk Tanzania Ltd kinategemea kupanuliwa na kuongeza ajira kutoka 1,600 wa sasa hadi 3,000 Mwaka 2017.

88. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Ili kuimarisha umoja kwa ajili ya kubadilishana uzoefu, Wizara yangu kwa kushirikiana na Kitengo cha Maendeleo ya Sekta ya Nguo na Mavazi (Textile Development Unit – TDU) imeweza usajili wa Chama cha Wazalishaji wa Nguo na Mavazi (TEGAMAT). Chama hiki kinachohusisha wadau katika mnyororo wote wa thamani ya nguo na mavazi wakiwemo washona nguo, wenye viwanda vya nguo na mavazi, watengenezaji batiki na vikoi, n.k kimekuwa mbadala wa chama cha TEXTMAT ambacho kilikuwa kinajumuisha wenye viwanda vya nguo na mavazi pekee. Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka nyingine itaendelea kuwalinda wazalishaji wa nguo na mavazi kwa kuhakikisha bidhaa za nguo zinazoingia nchini zinalipa kodi stahiki na hivyo kuweka mazingira sawa ya ushindani katika soko.

## Sensa ya Viwanda

89. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha taarifa ya Sensa ya Viwanda. Taarifa hiyo itawezesha Serikali kutunga sera na kufanya maamuzi sahihi yanayozingatia hali halisi ya viwanda vilivyopo na namna ya kuzitafutia suluhu changamoto zilizopo.

## Uzalishaji unaozingatia Kanuni za Mazingira

90. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Utunzaji, uhifadhi na kulinda mazingira katika shughuli zote za uzalishaji viwandani ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya kuendeleza viwanda nchini. Katika kutekeleza hilo, Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Mamlaka ya Usalama mahali pa Kazi OSHA na Ofisi ya Makamu wa Rais - Idara ya mazingira, imeendelea kuhamasisha na kusimamia miongozo inayohusu kuhifadhi na kulinda mazingira katika shughuli zote za uzalishaji viwandani. Aidha, Wizara imeendelea kuhamasisha Sekta Binafsi kutumia mitambo ya kisasa na rafiki kwa mazingira kwenye mlolongo wa uzalishaji.

## Kufanya tathmini ya Maendeleo ya Viwanda

91. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wizara iliweka malengo ya kufanya tathmini ya maendeleo ya viwanda ili kubaini changamoto zinazoikabili sekta ndogo ya viwanda ambapo jumla ya mikutano 13 ya kisekta imefanyika. Masuala mbalimbali ya kisera na ya kiutendaji ikiwemo migogoro mbalimbali na kupokea mapendekezo ya kurahisisha ufanyaji biashara yalijadiliwa. Aidha, Wizara ilifanya ziara katika viwanda vilivyopo mkoani Dar es Salaam, Arusha, Iringa, Shinyanga, Morogoro, Kilimanjaro, Tabora, Tanga, Mbeya, Mtwara, Pwani, Dodoma, Mwanza na Kagera kwa nia ya kuangalia utendaji kazi na uzalishaji katika viwanda hivyo. Changamoto zilizoainishwa na kutolewa taarifa ziliwasilishwa kwenye mamlaka husika kwa ajili ya kufanyiwa kazi. Pia, changamoto zinazohusu masuala ya kiushuru zinaendelea kujadiliwa katika kamati maalum inayohusisha Serikali na Sekta Binafsi kwa lengo la kukubaliana kabla ya Serikali kutoa maamuzi yanayozingatia kuwalinda wawekezaji kwa kuzingatia sheria zilizopo.

## Uendelezaji Viwanda kupitia Utafiti na Teknolojia

92. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Utafiti na Teknolojia ni eneo muhimu katika kuendeleza viwanda nchini. Tafiti hizo husaidia kubuni teknolojia mpya na rahisi zinazotumika katika uzalishaji wenyewe ubora unaokidhi masharti ya soko la ndani na nje. Kwa misingi hiyo, taasisi za utafiti na teknolojia za TIRDO, TEMDO na CAMARTEC zimekeleza yafuatayo katika Mwaka 2015/2016:-

## Taasisi ya Utafiti na Maendeleo ya Viwanda (TIRDO)

93. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika Mwaka 2015/2016, TIRDO imeendelea na taratibu za kukamilisha usimikaji wa mtambo wa kurejesha taka za ngozi. Mara baada ya kukamilika usimikaji, TIRDO itaanza kutoa mafunzo kwa Sekta ya Ngozi kuhusu uhifadhi na urejeshaji (recycling) wa taka za ngozi kwa kuziongezea thamani na kuhifadhi mazingira. Mafunzo ya kuwajengea uwezo wataalam yamefanyika kwa afisa mtafiti mmoja na mafundi mchundo wawili kwa lengo la kuijandaa kuendesha mafunzo mara baada ya kusimika mtambo.

94. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika juhudi za kuisaidia CAMARTEC kutengeneza teknolojia mpya za kilimo, TIRDO kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya SARI mkoani Arusha kimefanya majaribio ya mashine za kupandia mazao na kutoa mafunzo kwa wakulima juu ya dhana nzima ya kilimo hifadhi katika mikoa ya Arusha na Manyara. Vile vile, TIRDO kwa kushirikiana na Taasisi ya AWF iliyopo Mkoani Arusha na wadau wengine imeweza kutengeneza mashine 14 za kutengeneza matofali ya udongo saruji kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu na kutoa mafunzo kwa wanakikundi zaidi ya 30 juu ya matumizi ya mashine hizo.

95. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika juhudi za kuimarisha upatikanaji wa nishati vijiji, TIRDO kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro kipo katika utekelezaji wa ujenzi wa mitambo mikubwa 4 ya biogesi (65m<sup>3</sup>) katika Shule ya Sekondari Visitation Sanya Juu na Gereza la Karanga Mkoani Kilimanjaro. Vile vile, kituo kupitia mradi wake wa "Tanzania Domestic Biogas Programme (TDBP)" unaofadhiliwa na "Africa Biogas Partnership Programme (ABPP)" kupitia Shirika lisilo la Kiserikali la HIVOS la Uhulanzi kimeweza kujenga mitambo midogo 1,790 kwa matumizi ya kaya katika mikoa mbalimbali hapa nchini. Aidha, Kituo kimeweza kutoa mafunzo kwa takribani mafundi 200 kwa ajili ya ujenzi wa mitambo hiyo na kusajili Kampuni 65 za ujenzi wa mitambo ya biogesi kwa mfumo wa "SME". Kampuni hizo zimeajiri vijana zaidi ya 300.

96. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kwa mwaka 2015/2016, Taasisi ya TEMDO ikishirikiana na Wakala wa Kusambaza Umeme Vijiji (REA) iliendelea na utekelezaji wa mradi wa kufunga mtambo wa kisasa unaozalisha umeme utokanao na jua pamoja na upepo katika kituo cha Olduvai Gorge-Ngorongoro. Aidha, TEMDO katika jitihada za kutoa mchango katika Sekta ya Afya na Utunzaji wa Mazingira, iliendelea kuboresha kiteketezi cha taka za hospitali na kufunga kiteketezi cha aina hiyo kwenye hospitali za rufaa za Bombo, Morogoro na hospitali ya taifa ya magonjwa ya kuambukiza ya Kibong'oto. Ubunifu na uendelezaji wa kiteketezi maalum (sanitary pad burner) umekamilika na majaribio yanaendelea. Vile vile uendelezaji na uhamasishaji wa utengenezaji kibiashara wa mtambo wa kuzalisha nishati itokanayo na mabaki ya mimea kupitia wajasiriamali watengenezaji unaendelea.

### 3.2.2 Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo

97. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wizara katika juhudzi zake za kuboresha mazingira ya biashara hususan katika Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo, iliendelea kuhamasisha mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kutenga maeneo maalum kwa ajili ya kuanzisha mitaa ya viwanda na sehemu muafaka za masoko kwa ajili ya wajasiriamali wadogo wakiwemo machinga na Mama Lishe. Hatua hii inalenga kuondoa kero za muda mrefu kwa kundi hili sambamba na kuwafikishia huduma muhimu kwa pamoja. Aidha, itasaidia kuwarasimisha wajasiriamali wengi ambao hawako rasmi kwa kukosa sehemu za kufanya kazi. Hadi sasa, tayari baadhi ya Halmashauri zimeanza kutenga maeneo maalum ya wajasiriamali wadogo wadogo ikiwemo Mikoa ya Arusha, Geita, Mbeya na Mwanza. Aidha, Mkoa wa Dar es Salaam umeanza kuainisha maeneo kwa ajili hiyo. Vilevile, Wizara ilielekeza mikoa mipy ya Geita na Katavi kutenga maeneo kwa ajili ya kujenga Mitaa ya SIDO na tayari agizo hilo limetekelezwa na mikoa husika.

98. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wizara pia iliendelea kurahisisha upatikanaji wa huduma za usajili wa biashara kupitia mtandao (Online Registration) na upatikanaji wa Leseni za Biashara kwa Wajasiriamali Wadogo na wa Kati ili kusaidia urasimishaji wa Kundi hili. Mfumo huo pia unaruhusu malipo kufanyika kwa njia ya simu za mikononi na hivyo kupunguza gharama za biashara. Aidha, Uendelezaji na uhawilishaji wa teknolojia ni muhimu katika kuwezesha viwanda vidogo kupata na kutumia teknolojia. Katika kipindi cha 2014/2015, Wizara kupitia vituo vya uendelezaji na uhawilishaji teknolojia vya SIDO imewezesha upatikanaji na usambazaji jumla ya teknolojia mpya 416 zilizosaidia katika uanzishaji na uimarishaji miradi 2,210 ya wazalishaji kote nchini. Teknolojia hizo zimelenga katika kuongeza thamani mazao mbalimbali kama vile korosho, mihogo na alizeti. Aidha, programu ya atamizi inayolea ubunifu kwa wajasiriamali wadogo imeendelea na jumla ya wabunifu 58 wako katika programu ya atamizi katika vituo mbalimbali vya SIDO nchini.

99. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika kuendeleza viwanda vidogo na biashara ndogo vijijini, Serikali ilianzisha mradi wa Uendelezaji wa Ujasiriamali Vijijini (MUVI) unaoteklezwa na SIDO ikishirikiana na sekta binafsi ambao umeweza kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda vidogo na biashara ndogo kwa kuboresha mnyororo wa thamani wa mazao ya muhogo, mahindi, mpunga, alizeti, nyanya, serena, ufuta, matunda, maharage na mifugo katika wilaya 19 nchini. Hadi sasa familia 92,910 ambazo ni asilimia 82 ya lengo, zimefikiwa na kutoa ajira mpya zipatazo 13,026 ambazo ni asilimia 85 ya lengo. Pia miradi mbalimbali 15,580 ambayo ni asilimia 89 ya lengo imeweza kuzalishwa na kuimarishwa.

Sambamba na mafanikio hayo, uzalishaji wa wakulima 69,929 ambao ni asilimia 89 ya wanaohudumiwa na mradi umeongezeka kutokana na washiriki kujifunza mbinu bora za kilimo, biashara, uongezaji thamani katika mazao na upatikanaji wa masoko ya uhakika. Ingawaje shughuli za mradi huo zinakamilika Septemba 2016, mradi umejenga uwezo kwa SIDO na wazalishaji washiriki kutekeleza maendeleo ya viwanda vidogo katika wilaya kwa kufuata mlolongo wa thamani.

100. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika kipindi cha Mwaka 2015/2016, Wizara imeendelea kuratibu na kushiriki maadhisho na maonesho mbalimbali yanayowahusisha wajasiriamali kwa lengo la kuwapatia masoko ya bidhaa zao ndani na nje ya nchi, ikiwemo Maonesho ya SIDO kikanda, Sabasaba, Nanenane, Jua Kali na Expo Milan. Ushiriki katika maonesho hayo kuliwawezesha kutangaza bidhaa zao na kujifunza mbinu bora za kuzalisha bidhaa ili kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje. Katika kipindi cha mwaka 2015/2016, jumla ya wajasiriamali 2,950 walishiriki maonesho matano ya bidhaa yaliyoandalila na SIDO.

101. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika kutatua changamoto ya mitaji kwa wajasiriamali wadogo na wa kati, katika kipindi cha Mwaka 2015/2016, Wizara kupitia SIDO ilitoa jumla ya mikopo 6,254 yenye thamani ya Shilingi bilioni 7.16 ilitolewa na kuzalisha ajira 11,810. Asilimia 50 ya mikopo hiyo ilitolewa kwa akina mama na asilimia 39 ilitolewa kwa miradi ya vijijini. Aidha, kati ya mikopo hiyo, Shilingi bilioni 3.1 zilitoka Mfuko wa Taifa wa Uendelezaji Ujasiriamali (National Enterpreneurship Development Fund – NEDF). Vile vile, katika kipindi hicho cha Mwaka 2015/2016, Mfuko wa Dhamana ya Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo na wa Kati (SME Credit Guarantee Scheme) ambao ulioanzishwa kwa kushirikiana na Serikali ya Japan na Benki ya CRDB, katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2015, ulipokea zaidi ya maombi 38 yenye mahitaji ya jumla ya Shilingi 839,000,000.00 yaliyowasilishwa Benki ya CRDB na jumla ya shilingi 110,000,000 zimekwishatolewa mpaka sasa.

102. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wizara imekamilisha maandalizi ya awali ya kurejea Sera ya Maendeleo ya Biashara Ndogo na Viwanda Vidogo ya mwaka 2003, ikiwa ni pamoja na kukutana na wadau kuainisha maeneo muhimu yatakayotakiwa kufanyiwa uchambuzi yakinifu. Aidha, Wizara imeanisha mahitaji ya bajeti kwa ajili ya kutekeleza baadhi ya kazi za marejeo ya sera hiyo na imeandaa andiko na kuliwasilisha kwa Wadau wa Maendeleo ili kupata fedha za kufanya kazi hiyo. Tunakusudia kuimarisha na kuipa mwelekeo mpya SIDO ili iwe mamlaka kamili itayoweza kuhudumia biashara na viwanda vidogo sana, vidogo na vya kati kwa kutekeleza mambo yafuatayo:-kurejea upya majukumu ya SIDO; kuandaa Muundo mpya wa taasisi hiyo; na kuifanyia maboresho Sheria ya uundwaji wa SIDO Na. 28 ya mwaka 1973. Katika kutekeleza hayo, Wizara kwa sasa imeanza maandalizi ya awali ya mkakati huo

kwa kufanya tathmini ya kubainisha mahitaji yatakayotoa mwelekeo wa hatua za kufuatwa katika kutekeleza azma hiyo.

103. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ni msingi muhimu katika kujenga viwanda vya kati na viwanda vikubwa nchini. Naomba nitoe mfano wa Kampuni moja ya Mwanza Quality Wine ambayo ilianza biashara ikiwa na wazo la kutengeneza mvinyo wa ndizi mwaka 2007 baada ya kupata mafunzo na mkopo kutoka SIDO wa Shillingi 500,000. Kampuni hiyo kwa sasa ina mtaji wa shilingi bilioni moja na imetoa ajira za kudumu kwa watu 24 na inaendelea kupanuka. Mfano mwagine kutoka huko huko Mwanza ni Kampuni ya Chobo Investment Ltd inayomilikiwa na wajasiriamali vijana wa Kitanzania. Kampuni hiyo imeweza kujenga mtandao wa wafugaji wa ng'ombe, mbuzi na kondoo na inayo machinjio ya kisasa yenye uwezo wa kuchinja ng'ombe 600 kwa masaa nane. Fundisho hapa ni kuwa waasisi wa kampuni hiyo walanza kwa kumiliki bucha zinazoendeshwa chini ya miti kukua taratibu mpaka kufikia hatua hiyo. Wito wangu kwa Bunge Tukufu na Watanzania wote kwa ujumla ni kufutilia mifano hiyo yenye mafanikio ikiwa ni pamoja na kutembelea vituo vya SIDO wakati tunapoingia rasmi katika ujenzi wa uchumi wa viwanda.

### 3.2.3 Sekta ya Biashara na Masoko

#### Ukuzaji na Uendelezaji Mauzo Nje

**Kuwezesha vikundi vya wakulima, wajasiriamali na wafanyabiashara kutangaza bidhaa na huduma za Tanzania katika masoko ya ndani, Kikanda na Kimataifa**

104. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Sekta Binafsi kuitia Kampuni ya GS1 National (Tz) Ltd imeendelea kuhamasisha wafanyabiashara kutumia alama za mistari (bar codes) kutambulisha bidhaa wanazozalisha ili kukuza mauzo ndani na nje ya nchi. Hadi kufikia mwezi Machi, 2016, jumla ya bidhaa 10,600 na Kampuni 820 zimetumia alama za mistari zinazoitambulisha Tanzania ambapo asilimia 51 ya makampuni hayo yapo Dar es Salaam. Ili kukuza matumizi ya alama za mistari kwa bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya ndani, Shirika la Viwango (TBS) limeingia makubaliano na Kampuni ya GS1 National (Tz) Ltd ili wenye viwanda vinavyopata alama ya ubora wa TBS vitumie alama za mistari zinazoonyesha kuwa bidhaa hizo zimezalishwa Tanzania.

105. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade), Vituo vya Biashara London na Dubai, katika Mwaka 2015/2016 imetekeliza mambo yafuatayo:

- i) Imeandaa mwongozo 'Charter for Cross Border Trade' na kutoa mafunzo mbalimbali ya kuwajengea uwezo wafanyabiashara wanawake katika mipaka ya Kabanga, Rusumo, Manyovu, Mtukula, Sirali, Holili, Horohoro, Tunduma, Kasumulo na Namanga ili waweze kuendesha biashara ya mpakani kwa ufanisi zaidi;
- ii) Iliandaa Maonesho ya 39 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (39th DITF), ambayo hutoa fursa kwa wakulima, wajasiriamali na wafanyabiashara kutangaza bidhaa zao Kitaifa na Kikanda;
- iii) Imeendelea kuratibu ushiriki wa wajasiriamali wa Tanzania katika maonesho ya biashara ya kimataifa katika nchi za nje kama ifuatavyo:
  - Maonesho ya Tisa ya Chakula na Huduma yaliyofanyika Mascat Oman kuanzia tarehe 9 -11 Septemba, 2015. Kupitia maonesho hayo soko kwa mazao ya kilimo na mifugo kama vile nyama, korosho, mahindi ya njano, mboga mboga lilipatikana;
  - Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Uganda (KITF 2015) yaliyofanyika kuanzia tarehe 2-11 Oktoba, 2015: Katika maonesho hayo wafanyabiashara walifanya mauzo ya papo kwa papo ya Shilingi za Tanzania 6,969,969.96. Vilevile, wajasiriamali wamepokea oda yenye thamani ya Shilingi za Tanzania 3,315,151; na
  - Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Nairobi (NITF 2015) yaliyofanyika kuanzia tarehe 28 Septemba, - Oktoba, 2015: Katika maonesho hayo wafanyabiashara walifanya mauzo ya papo kwa papo ya Shilingi za Tanzania 11,000,000 na kupokea oda ya bidhaa za thamani ya ya Shilingi za Tanzania 8,000,000.
- iv) Tanzania ilishiriki maonesho makubwa ya Dunia (Expo 2015 MILAN) yaliyofanyika mijini Milan kuanzia tarehe 01 Mei, 2015 na hadi tarehe 31 Oktoba, 2015, nchini Italia. Aidha, makampuni 17 ya Wajasirimali yalishiriki na kutumia fursa hiyo kutangaza na kuuza bidhaa zao kwenye soko hilo; na
- v) TanTrade pia iliendelea kuratibu mikutano ya ana kwa ana baina ya wazalishaji na wanunuza na kuwaunganisha wafanyabiashara wa Tanzania katika nchi 70 kupitia Kituo cha Trade Point Dar es Salaam kinachopata taarifa kutoka World Trade Point Federation na kuwapatia taarifa za kibiashara (mahitaji ya soko, bei za bidhaa na ushindani wa soko) kwa wafanyabiashara, watafiti, wanafunzi na wadau wengine wa biashara.

106. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kwa upande wa AGOA, Wizara ilishiriki katika Kongamano la AGOA liliyofanyika mijini Librevile, Gabon mwezi Agosti, 2015

likijumuisha nchi zote zilizo chini ya Jangwa la Sahara pamoja na Marekani kwa lengo la kujadili fursa zilizopo chini ya mpango wa AGOA na changamoto zinazokwamisha utekelezaji wake. Kupitia kongamano hilo, Serikali ya Marekani imeidhinisha awamu nyininge ya mpango wa AGOA kwa kipindi kingine cha miaka kumi (10) kuanzia tarehe 30 Septemba, 2015 hadi 30 Septemba, 2025 ambapo nchi zilizopo chini ya Jangwa la Sahara zitaendelea kunufaika na mpango huo wa kuza bidhaa zake kwenye soko la Marekani Bila Ushuru na Bila Kikomo (Duty Free Quota Free).

### **Majadiliano ya kikanda**

107. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Tanzania imeendelea kushiriki kikamilifu kwenye majadiliano ya Biashara ya kikanda ikiwa ni pamoja na EAC, SADC, Eneo Huru la Biashara la Utatu (COMESA- EAC - SADC Tripartite FTA), AGOA, EAC – EU EPA na Eneo Huru la Biashara la Afrika. Kutokana na majadiliano ya kikanda Tanzania imeweza kuvutia wawekezaji wa ndani na nje katika sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na biashara ya huduma na zile za bidhaa. Katika majadiliano ya kikanda Tanzania imeweza kufaidika na miradi mikubwa ya kikanda ikiwa ni pamoja na ujenzi wa vituo 15 vya pamoja vya kiforodha (OSBP) vilivyopo katika mipaka ya nchi wanachama wa Jumuiya na ujenzi wa barabara ya Arusha – Holili/Taveta – Voi yenye urefu wa kilometra 234.3 ambayo ilizinduliwa na marais wa Jumuiya ya Afrika Mashariki chini ya Uenyekiti wa Mhe. Dkt. John P. J. Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnamo tarehe 3 Machi, 2016, Arusha, Tanzania ambapo barabara hiyo itasaidia kufungua fursa mbalimbali za maendeleo katika eneo la Afrika Mashariki.

108. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Tanzania pamoja na Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki imeendelea kutekeleza Itifaki ya Umoja wa Forodha kwa kuruhusu bidhaa kutoka nchi wanachama kuingia nchini bila kutozwa Ushuru wa Forodha. Ili kuboresha mazingira ya biashara nchini tumefanikiwa kutoa nyaraka za Uasili wa Bidhaa (Certificate of Origin) kwa njia ya mtandao ambapo mfanyabiashara halazimiki kusafiri kutafuta Ofisi husika. Kupitia majadiliano ya kimataifa, katika Mwaka 2015/2016, Wizara imeendelea kushiriki kikamilifu kwenye majadiliano ya biashara ya kimataifa kwa lengo la kuhakikisha kuwa tunaendelea kufaidika kikamilifu pamoja na kuimarisha ushiriki wetu kwenye biashara ya kimataifa.

109. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Aidha, Wizara ilishiriki kikamilifu kwenye Mkutano wa Kumi (10) wa Mawaziri wa Biashara wa Shirika la Biashara la Dunia (WTO) uliofanyika mjini Nairobi, Kenya kuanzia tarehe 15 hadi 19 Desemba, 2015. Mkutano wa Mawaziri wa Biashara, ndicho chombo kikuu cha maamuzi katika Shirika la Biashara Duniani. Mkutano huo wa Kumi wa Mawaziri wa Biashara wa Nairobi, ulifanya maamuzi muhimu yenye manufaa kwa nchi ambayo ni pamoja na:-

- i) Maamuzi ya uondoshwaji ruzuku ya mauzo nje kwa bidhaa za kilimo ambayo yatasaidia kupunguza madhara yaliyoanza kujitokeza ya kufurika kwa bidhaa za kilimo zenyenye bei rahisi nchini;
- ii) Kufikiwa kwa makubaliano ya kulegeza na kurahisisha Vigezo vya Uasili wa Bidhaa (Rules of Origin) katika masoko ya upendeleo. Uamuzi huo utaiwezesha nchi kuweza kutumia kikamilifu fursa zitokanazo na masoko ya upendeleo (DFQF);
- iii) Maamuzi yanayohusu pamba kwa kuondolewa kwa ruzuku ya mauzo nje na kuruhusu soko la pamba kuwa Bila Ushuru na Bila Ukomo (DFQF) ambapo nchi itanufaika kwa kuwepo ushindani halali katika soko na kupatikana kwa masoko;
- iv) Maamuzi ya kuendelea na utaratibu wa Serikali kuhifadhi chakula kwenye maghalia kwa lengo la usalama wa chakula kwa nchi zinazoendelea na masikini, bila kujali kupitiliza kikomo kilichokubalika katika Mkataba wa Kilimo chini ya Shirika la Biashara Duniani mpaka suluhisho la kudumu litakapopatikana Mwaka 2017; na
- v) Uharakishwaji wa kupata Mfumo Maalumu wa Kujihami (Special Safeguard Mechanism - SSM) katika kulinda soko la ndani kwa bidhaa za kilimo kwa nchi zinazoendelea na masikini.

110. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Napenda pia kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa tarehe 14 Machi, 2016, Tanzania iliridhia Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba wa Shirika la Biashara Duniani wa masuala ya Haki Miliki na Ubunifu (WTO TRIPS AGREEMENT). Marekebisho hayo yanakusudiwa kuruhusu nchi masikini na nchi zinazoendelea kuweza kuzalisha madawa yenye Haki Miliki (Generic drugs) kwa ajili ya magonjwa kama vile HIV, Kifua Kikuu n.k. Marekebisho ya Mkataba huo yatakuwa rasmi baada ya Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba huo kuridhiwa na theluthi mbili ya wanachama wa Shirika la Biashara Duniani.

Pia Tanzania pamoja na nchi zingine wanachama wa Shirika la Biashara Duniani zinaendelea na mchakato wa uridhiwaji wa Mkataba wa Shirika la Biashara Duniani wa Kurahisisha Biashara (Trade Facilitation Agreement). Mkataba wa Kurahisisha Biashara ulipitishwa mwezi Desemba 2013 wakati wa Mkutano wa Tisa wa Mawaziri wa Shirika la Biashara Duniani uliofanyika Bali, Indonesia. Tanzania kwa upande wake tayari imeshawasilisha Maeneo ya Kundi A (category A Measures) ambayo itayatekeleza punde Mkataba utakapo anza kutumika rasmi. Tunategemea Mkataba huu utasaidia kwa kiasi kikubwa

kurahisisha shughuli za biashara na hivyo kuweza kunufaika zaidi na biashara ya kimataifa. Mkataba huo utaanza kutumika rasmi baada ya kuridhiwa na theluthi mbili ya wanachama wa Shirika la Biashara Duniani.

Aidha, makubaliano mengine yalizilenga moja kwa moja nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania. Makubaliano hayo ni pamoja na; Vigezo vya Uasili wa Bidhaa (Rules of Origin) katika masoko ya upendeleo. Nchi wanachama zinazotoa masoko ya upendeleo kwa mara ya kwanza zitatakiwa kulegeza Vigezo vya Uasili wa bidhaa zinazotoka nchi changa na Utekelezaji wa Maamuzi ya Upendeleo Maalum kwa Biashara ya Huduma. Mawaziri wameongeza muda wa ukomo wa utaratibu huo kutoka 2027 mpaka 2030 kutokana na kuchelewa kuanza kutekeleza utaratibu huo kwa miaka mitatu tangu kutolewa.

### **Kukuza Mauzo Nje**

#### **Kituo cha Biashara cha Tanzania Dubai (TTC-DUBAI)**

111. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kituo kwa kushirikiana na Tanzania Mineral Audit Agency na Arusha Gem Show kinaendelea na maandalizi ya kuwa na Wiki ya Tanzania itakayofanyika Mwezi Aprili, 2016 kwa uenyeji wa Dubai Multi Commodity Center, ambapo mauzo ya madini mbalimbali kutoka Tanzania yatafanyika kwenye eneo la kuoneshea la DMCC, Dubai. Mazungumzo baina ya EPZA, baadhi ya wawekezaji kutoka SEZ ya Mtwara, Uongozi wa JAFZA na Khalifa Industrial Park KIZAD yanaendelea kuhusu mashirikiano ya kuendesha Free Zones.

#### **Kituo cha Biashara cha Tanzania London (LTC)**

112. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kituo, kwa kushirikiana na Ubalozi, kiliandaa Mkutano wa Wafanyabiashara wa Kitanzania na Mtaalam wa masuala ya biashara anayesimamia utekelezaji wa Programu ya Kimataifa (ITC) kwa lengo la kuangalia namna Watanzania walioko nje ya nchi (Diaspora business community) wanavyoweza kuchangia maendeleo ya Taifa. Kituo pia kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii na Bodi ya Utalii (TTB), kilifanikisha ushiriki wa Tanzania katika Maonesho ya Kimataifa ya Utalii Duniani, yajulikanayo kama World Travel Market (WTM 2014). Kituo vilevile kiliweza kuratibu ushiriki wa Maonesho ya Utalii yanayofanyika nchini Uingereza kama yale ya Manchester na London. Aidha, Kituo kiliiwakilisha nchi kwenye mikutano ya mashirika ya kimataifa ambayo Tanzania ni nchi mwanachama, ikiwemo Shirika la Kimataifa la Kahawa Duniani (International Coffee Organisation – ICO), Shirika la Kimataifa la Sukari – ISO, Shirika la Katani – LSA, na Shirika la

Kimataifa la Taaluma ya Kilimo - CABI. Hatua hiyo iliwezesha maslahi ya Taifa kulindwa na pia kupunguza ghamama za ushiriki.

113. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, imeanzisha utaratibu wa kurahisisha ufanyaji biashara mipakani (Simplified Trade Regime) kwa wajasiriamali wadogo wenyewe bidhaa za thamani isiyozidi Dola za Marekani 2,000 kutumia Cheti Rahisi cha Uasili wa Bidhaa (Simplified Certificate of Rule of Origin). Utaratibu huo umeanza kutumika kwa mipaka ya Nchi Wanachama wa Jumuia ya Afrika Mashariki. Aidha, katika mpaka wa Tunduma/Nakonde tayari wadau wa Tanzania na Zambia wameainisha aina ya mazao na bidhaa zitakazoingia katika utaratibu huo. Rasimu ya makubaliano ya kutekeleza utaratibu huo imeandaliwa.

114. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wizara imeendelea na kukamilisha taratibu za ujenzi wa masoko ya kimkakati katika maeneo ya Segera mkoani Tanga na Makambako Mkoani Njombe, ambapo masoko hayo yote yako katika hatua za mwisho za kulipa fidia kwa wananchi waliopisha ujenzi wa masoko hayo. Kwa upande wa Soko la Makambako, tathmini ya pili imefanyika Mwezi Septemba, 2015, na kuitishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali. Wizara imetenga fedha hizo katika bajeti yake ya 2016/2017. Benki ya Rasilimali (TIB) imeonesha nia ya dhati ya kuwekeza katika mradi huo na inaendelea kushauriana na Halmashauri ya Mji wa Makambako ili kukamilisha Andiko la Mradi (Business Plan) na kuliwasilisha TIB kwa ajili ya hatua zaidi. Aidha, katika kufanikisha ujenzi wa masoko hayo, Wizara imeendelea kutoa ushauri wa kiutaalamu juu ya aina ya miundombinu inayohitajika, kuratibu shughuli zinazofanywa na wadau katika ujenzi wa soko na kuzunganisha Halmashauri na vyanzo vya fedha ili kufanikisha ujenzi huo.

115. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wizara imeendelea kukusanya, kuchambua, kuhifadhi na kusambaza kwa wadau taarifa za masoko kutoka katika masoko 113 ya mazao ya chakula na minada 53 ya mifugo nchini. Taarifa hizo husambazwa kwa wadau kuitia magazeti mbalimbali, ujumbe wa simu za kiganjani na tovuti ya LINKS ambayo ni [www.lmistz.net](http://www.lmistz.net) ambayo hutangaza taarifa za masoko ya mifugo. Vilevile, Wizara imeendelea kuboresha mifumo ya taarifa za masoko ili kuhakikisha wazalishaji wengi hapa nchini wanapata taarifa na fursa za masoko zilizopo kwa wakati. Kwa upande wa taarifa za mazao ya matunda na mbogamboga, Wizara kwa kushirikiana na TAHA imeandaa mfumo wa kutoa taarifa za masoko ya mazao hayo kuitia simu za viganjani ili kuyaunganisha na soko la hoteli za kitalii nchini.

#### Kuendelea kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji chini ya BRN

116. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wizara imeendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji chini ya Mpango wa Matokeo Makubwa sasa – BRN kwa kurazinisha sheria zinazokinzana baada ya kuunda Kamati ya kufanya mapitio

ya Sheria za udhibiti (Regulatory Licensing Reform Committee) ili kuondoa changamoto ya mwingiliano wa kisheria kati ya taasisi moja na nyingine, jambo ambalo litapunguza gharama ya kufanya biashara nchini. Vilevile, Wizara imeendelea kurahisisha shughuli za usajili wa majina ya Biashara kwa kutumia mifumo ya kieletroniki kupitia tovuti ya <https://ors.brela.go.tz/login>. Mfumo huo sasa unafanyakazi na wateja wanajasili majina ya Biashara. Aidha, mfumo wa kuandikisha makampuni kwa njia ya kieletroniki, design ya mfumo huo ilikamilika, zabuni ya kumpata mshauri mwelekezi wa kuweka mfumo huo ilitangazwa Novemba 2015, na kufunguliwa Januari, 2016. Hatua inayofuata ni BRELA kufanya tathmini ya zabuni hizo ili kumpata mshauri mwelekezi mwenye sifa.

117. **Mheshimiwa Naibu Spika**, uanzishwaji wa Dirisha la Taarifa za Biashara (National Business Portal- NBP) ambalo litakuwa na taarifa zote muhimu zinazohusu masuala ya biashara na kuwezesha utoaji wa Leseni za Kundi A kwa njia ya mtandao unaendelea chini ya Mradi wa *Regional Communication Infrastructure Proramme-RCIP*. Wizara imempata mkandarasi (contractor) atakayeweka mfumo wa taarifa za biashara na tayari ameanza kazi na mfumo huo unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2016. Mahitaji ya Mfumo yamekusanywa, prototype imekamilika na hivi sasa mkandarasi anaendelea na kufanya design.

118. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wizara imeendelea kuboresha mifumo ya ukaguzi wa mazingira ya biashara (Reform Compliance Enforcement System) kwa kuhakikisha kuwa kila Wizara na Taasisi zinaweka katika tovuti zao sera, sheria, kanuni, ada, taratibu za ukaguzi na adhabu kwa wadau ili kujua masharti yanayotakiwa kutimizwa wakati wa kuomba na kufanya aina fulani ya biashara. Jambo hilo litamwezesha mfanyabiashara kujua mahali ambapo anapaswa kuwasilisha maombi yake, hatua zinazopaswa kufuatwa ili kukamilisha ombi lake, kiwango cha ada au gharama anazopaswa kulipa, utaratibu unaotumika kukagua biashara, adhabu inayotolewa kwa kutokuftuata taratibu husika na kuwa na kibali husika. Katika kufanikisha zoezi hilo, baadhi ya Wizara na Taasisi zimeweka taarifa hizo, kwa mfano, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuu; Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

### **Mfumo wa Stakabadhi za Ghala**

119. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika kuimarisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala na kuanzisha Mfumo wa Soko la Bidhaa (Commodity Exchange), Wizara imeendelea kushughulikia changamoto zinazokabili matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa kufanya marekebisho ya Sheria Namba 10 ya mwaka 2005 ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala na kupitishwa na Bunge mwezi Machi mwaka 2015. Marekebisho hayo yatawezesha pia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kutumika katika Soko la

Mazao na Bidhaa ambalo sheria yake (Commodity Exchange Act. No. 15 of 2015) ilipitishwa mwezi Juni, 2015. Mfumo huo wa soko ulizinduliwa tarehe 30 Oktoba, 2015. Maandalizi yanaendelea na tayari jengo la ofisi na jukwaa la mauzo (trading platform) limekwishapatikana.

Aidha, mafunzo kwa waendesa masoko (market intermediaries) yamefanyika na elimu kwa umma imeanza kutolewa katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Dodoma, Singida, Manyara na Morogoro. Pia, maandalizi ya Mpango wa Biashara (Business Plan) yapo katika hatua za mwisho. Mfumo wa Soko la Mazao na Bidhaa utaanza na zao la korosho na kufuatiwa na mazao ya kahawa, mahindi, mpunga/mchele, alizeti, ufuta na mbaazi.

### **3.2.4 Utekelezaji wa Taasisi chini ya Wizara**

#### **Shirika la Viwango Tanzania (TBS)**

120. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kwa kipindi cha miezi tisa ya mwanzo wa Mwaka 2015/2016, jumla ya vyeti vya ubora wa bidhaa zitokazo nje ya nchi (Certificates of Conformity - CoCs) 21,749 vimetolewa, sawa na 68% ya matarajio ya kutoa jumla ya vyeti vya ubora 32,000 kwa Mwaka 2015/16 ikilinganishwa na vyeti 28,891 vilivyotolewa Mwaka 2014/2015. TBS imekuwa ikishirikiana na mashirika mengine ya Serikali katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Na. 2 ya mwaka 2009. Kwa mfano, TBS inashirikiana kwa karibu sana na SIDO kuhakikisha wajasiri amali wadogo wanazalisha bidhaa bora kukidhi ushindani wa kibiashara katika soko la ndani na nje ya nchi. SIDO inawajengea utaalamu wa kiteknolojia, kuwasaidia kwa miundombinu ya uzalishaji na kuwatambulisha rasmi kwa TBS ili kupewa leseni ya kutumia nembo ya ubora ya TBS. Huduma hiyo inatolewa kwa gharama ya Serikali bila mjasiri amali kuchangia chochote mara tu anapoanza kujengewa uwezo.

121. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Vilevile, TBS inashirikiana na mashirika na taasisi kama CAMARTEC, NIT, TCRA katika kufanya shughuli za kuandaa Viwango na ukaguzi wa zana za kilimo na magari yaliyotumika ambayo hayakukaguliwa huko yanakotoka; na halikadhalika, TBS imekuwa ikishirikiana na Jeshi la Polisi na taasisi nyingine za Serikali kama TFDA, TRA, FCC, GCLA, EWURA katika kufanya ukaguzi wa kushtukiza sokoni ili kuhakikisha kuwa bidhaa hafifu, zilizo chini ya viwango na ambazo si salama kwa afya au matumizi ya mlaji zinaondolewa sokoni.

122. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kwa kipindi cha miezi tisa ya mwanzo ya Mwaka 2015/2016, jumla ya leseni 131 za nembo ya ubora ya TBS zimetolewa ambayo ni sawa na asilimia 65 ya lengo la kutoa leseni 200 hadi kufikia mwezi Juni, 2016. Miiongoni mwa leseni hizo, leseni 23 zilitolewa kwa wajasiri amali wadogo kwa bidhaa za asali, maji, mafuta ya alizeti, mvinyo, siagi ya karanga,

jemu, mafuta ya kujipaka, sabuni ya maji na sabuni ya kuogea. Aidha, katika kipindi cha Julai 2015 hadi Machi 2016, jumla ya sampuli 4,792 zilipimwa katika maabara mbalimbali za Shirika kwa lengo la kuhakiki ubora wake, hii ni sawa na 68.5% ya lengo la kupima sampuli 7,000 kwa mwaka. Aidha, kwa kupitia msaada wa Jumuiya ya Ulaya (EDF), Shirika limenunua mitambo miwili ambayo ni Gas Chromatography – Mass Spectrometer (GC- MS) kwa ajili ya kupima mabaki ya viwatilifu (pesticides residues) katika bidhaa za vyakula na vinywaji na Inductive Coupled Plasma – Mass Spectrometer (ICP-MS) inayotumika kupima uchafu wa madini aina ya chuma (metal contaminants) katika bidhaa mbalimbali.

123. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016, jumla ya sampuli 4,888 zilifanyiwa ugezi. Hiyo ni sawa na 69.8% ya lengo la kufanya ugezi wa mitambo 7,000 kwa kipindi cha mwaka mzima wa 2015/2016. Shirika pia limekamilisha viwango 53 katika kilimo, chakula, uhandisi na viwango vya vifungashio mbalimbali ambavyo ni sawa na 26.5% ya lengo la kutayarisha viwango 200 kwa mwaka. Shirika pia liliendelea kusimamia viwango vya kitaifa kwa kutumia mifumo iliyopo ya kuhakiki ubora (Certification Schemes) kwa kutumia maabara zake zikiwemo za ugezi, kemia, chakula, na nguo ambazo zina sifa za umahiri. Vilevile, Shirika limefanyiwa tathmini ya awali (pre-assessment) katika maabara za Uhandisi ili kujua mapungufu yaliyopo yaweze kufanyiwa marekebisho kabla ya ukaguzi rasmi. Sambamba na hilo Maabara ya Kemia imefanyiwa tathmini ya awali kwa nia ya kutanua wigo wa umahiri katika upimaji wa mbolea na mafuta.

124. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Shirika la Viwango Tanzania (TBS) limenunua vifaa mbalimbali vya kupimia lami na zege la lami (Asphalt and Bitumen Testing Equipment) na vifaa vya kupimia mabomba ya plastiki kwa ajili ya kusafirishia maji safi na maji taka (UPVC na HDPE) ambavyo vimewekwa katika maabara ya Uhandisi (ujenzi) iliyopo katika ofisi za TBS makao makuu. Ufungaji wa vifaa hivyo umekamilika na kazi ya upimaji imekwishaanza baada ya kuwapatia mafunzo ya awali wataalamu wa maabara hiyo. Aidha, Shirika limeendelea kutoa mafunzo kwa Wajasiriamali nchini kwa kutumia fedha za ndani na msaada wa mfuko wa Maendeleo wa Ulaya (EDF). Kwa kipindi cha miezi tisa ya Julai, 2015, mpaka Machi, 2016, mafunzo yalitolewa kwa wajasiriamali wadogo pamoja na wadau mbalimbali wapatao 837 wa sekta ndogo za chai, viungo, mbogamboga na matunda. Wajasiriamli hao walitoka katika mikoa ya Morogoro, Arusha, Tanga, Njombe na Dar es Salaam. Aidha, mafunzo hayo ambayo yaliwalenga zaidi wajasiriamali wadogo yalilenga zaidi dhana nzima ya kuzingatia mifumo bora ya kusimamia na kuzalisha bidhaa zenye ubora ili waweze kupata masoko ya bidhaa zao.

125. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2015 hadi Machi, 2016, jumla ya vyeti vya ukaguzi wa magari 24,930 vimekwishatolewa.

Kiasi hicho cha vyeti ni sawa na asilimia 54.2 ya matarajio ya kufikisha jumla ya vyeti 46,000 hadi kufikia mwezi Juni, 2016. Aidha, katika kuimarisha usimamizi wa ubora wa bidhaa zinazoingizwa nchini, Shirika limefungua ofisi katika mipaka ya Rusumo, Kabanga, Kasumulo, Mtukula, Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA) na Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA). Ufunguzi wa ofisi ya mpaka wa Tunduma umepangwa kufanyika kabla ya mwisho wa mwaka 2015/2016.

Pia, shirika limeimarisha vituo vilivyokuwepo kwa kuongeza watumishi kutoka mmoja hadi wawili kwa kila kituo. Vilevile, Shirika limepanga kufungua ofisi kabla ya mwisho wa Mwezi Juni, 2016 katika mkoa wa Mbeya utakaohudumia mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na Mkoa wa Arusha utakaohudumia Kanda ya Kaskazini kwa nia ya kusogeza karibu huduma za Shirika kwa wananchi. Pamoja na hatua hizo, Shirika limepanga kujenga jengo la kisasa la maabara ambalo litagharimu takriban Shilingi 15 bilioni. Shirika liko katika hatua za mwisho za kumpata mzabuni kwa ajili ya ujenzi wa maabara hiyo. Ujenzi unategemewa kuanza pindi taratibu za uzabuni zitakapokamilika.

### **Chama cha Hakimiliki Tanzania (COSOTA)**

126. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Utaratibu wa urasimishaji wa kazi za filamu na muziki unasimamiwa kwa ushirikiano wa Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji na Wizara ya Habari Utamaduni, Michezo na Wasanii. Kwa kupitia taasisi zake (Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Chama cha Hakimiliki na Hakishiriki Tanzania (COSOTA), Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) na Bodi ya Filamu imeandaa utaratibu wa pamoja wa kurasimisha kazi za filamu kwa wamiliki wa kazi za filamu na muziki au waliopewa mamlaka ya kuzalisha na kusambaza kazi za filamu na muziki zenyet stempu za TRA baada ya kupata uthibitisho toka taasisi zilizotajwa hapo juu. Matumizi ya Stempu yanarasimisha uuzwaji wa CD, DVD na kanda ili kukusanya kodi, kuzuia na kupunguza uharamia wa kazi za sanaa. Matumizi ya stempu pia husaidia katika kutofautisha kazi zilizo halali na zile zisizo halali. Kwa kipindi chote toka urasimishwaji wa kazi za sanaa kuanza, CDs na DVDs zilizokamatwa hadi mwezi Desemba, 2015 ni kazi 30,984 (kazi za ndani) na 66,150 (kazi za nje ya nchi).

127. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika kipindi cha robo tatu cha Mwaka 2015/2016, jumla ya stempu 30,730,000 zimetolewa, kati ya hizo 24,110,000 ni za filamu za ndani wakati stempu 6,620,000 ni za muziki wa ndani. Idadi ya stempu kwa Mwaka 2015/2016 inaonesha kuwa kubwa zaidi ukilinganisha na mwaka wa fedha uliopita, hivyo muamko wa matumizi ya stempu katika kazi za sanaa inaonesha kuongezeka. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na COSOTA, imekusanya maoni kutoka kwa wadau mbalimbali kuhusu marekebisho ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7/1999 ambayo yapo katika hatua za kuwasilishwa kwenye Baraza la Mawaziri kwa maamuzi.

128. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika Mwaka 2015/16, COSOTA imesajili wanachama (Kampuni, Vikundi na watu binafsi) wapatao 283 na kusajili kazi 1,586. Aidha, jumla ya hati ya uthibitisho wa kazi (clearance certificate) 356 zilitolewa. Vilevile, hadi kufikia Desemba, 2015, COSOTA imekusanya mirabaha na kutoa leseni kwa matumizi ya maonesho kwa umma na utangazaji kama ifuatavyo: Jumla ya Sh. 96,000,000 zimekusanya na mawakala na wafanyakazi wa COSOTA kutoka katika maeneo yanayotumia kazi za muziki na filamu kwa maonesho ya umma na kutoka kwa baadhi ya Mashirika ya utangazaji. Katika makusanyo hayo, asilimia 70 hugawanywa kwa wasanii, asilimia kumi hutumika kwa uendeshaji wa shughuli za COSOTA na asilimia ishirini hutumika kuwalipa mawakala wa COSOTA.

129. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wizara kupitia COSOTA imeendelea kusuluuhisha migogoro ya hakimiliki na hakishiriki. Migogoro saba kati ya migogoro 18 imeshughulikiwa kwa Mwaka 2015/16. Kesi zilizokuwepo za masuala ya hakimiliki zinazosimamiwa na COSOTA ni mbili ambazo zinaendelea kwenye mahakama ya Kariakoo, Ilala na Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Dar es Salaam. Kesi nyingine za hakimiliki na hakishiriki za jinai na za madai zilizofunguliwa na Jamhuri au wadau wenyewe zinaendelea katika mahakama mbalimbali ndani na nje ya Dar es Salaam. Kwa kipindi cha 2015/2016, Wizara kupitia COSOTA imefanya ukaguzi wa kazi za sanaa zinazolindwa na Sheria ya hakimiliki na hakishiriki katika mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Lindi na Mtwara.

### **Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (TanTrade)**

130. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wizara kwa kushirikiana na TanTrade ilifanya utafiti katika Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Mwanza ili kutambua fursa na changamoto katika kuendeleza sekta ya ngozi. Utafiti ulibaini kuwepo kwa upungufu katika kusimamia ufugaji na uchunaji wa ngozi kwani ng'ombe wengi wanawekewa alama za moto ili kuepusha wizi na wachunaji wengi hawana utaalamu wa uchunaji bora wa ngozi ambapo hutoboa ngozi wakati wa kuchuna.

131. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kufuatia utafiti huo, yaliandaliwa mafunzo maalum ya uchunaji ngozi za ng'ombe na mbuzi kwa wachunaji 60 wa Machinjio ya Vingunguti na Ukonga Dar-es-Salaam. Mafunzo haya yalifanyika Vingunguti kuanzia tarehe 12 – 14 Aprili, 2016, ambapo Wataalamu kutoka Chuo cha Teknolojia Dar-es-Salaam Kampasi ya Mwanza waliratibu mafunzo hayo. Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa kushirikiana na TanTrade na SIDO pia iliandaa mafunzo maalum ya awali ya utengenezaji wa viatu na bidhaa za ngozi yaliyofanyika kuanzia tarehe 18 – 22 Aprili, 2016, katika Chuo cha Teknolojia cha Dar-es-Salaam, Kampasi ya Mwanza na kushirikisha Washiriki

41 kutoka Mikoa ya Kanda ya Ziwa ya Mwanza, Geita, Simiyu, Kagera, Shinyanga na Mara. Katika muda wa siku tano, washiriki walijifunza utengenezaji wa pateni za viatu, ukataji wa ngozi, ushonaji pamoja na umalizajji wa viatu na bidhaa nyingine za ngozi. Mafunzo hayo yatafanyika nchi nzima na umeandaliwa mfumo wa kuwafuatilia washiriki ambapo watakuwa wakikutanishwa kila baada ya miezi mitatu ili kuelezea mafanikio na changamoto zinazowakabili ziweze kufanyiwa kazi kwa pamoja na kupiga hatua nyingine ya maendeleo.

132. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ikishirikiana na TanTrade na Taasisi ya Muungano wa Vikundi vya Wazalishaji Wadogo Tanzania (MVIWATA) iliandaa mafunzo kwa Wakulima wa bidhaa za viungo (spices) wapatao 94 kutoka tarafa ya Mkuyuni na Matombo Wilayani Morogoro Vijijiini. Mafunzo haya yalilenga kuwafundisha Wakulima kuhusu kilimo biashara, mkakati wa kuendeleza kilimo biashara, usimamizi wa mnyororo wa ugavi, usimamizi wa biashara na mpango na uratibu wa kuuza nje ya nchi (Export Plan). Mafunzo hayo yatafanywa kwa wakulima wa bidhaa za viungo nchi nzima ili kuwawezesha kuzalisha bidhaa bora kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi.

133. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ikishirikiana na TanTrade chini ya ufadhili wa Taasisi ya Biashara ya Kimataifa (ITC) Geneva iliratibu msafara wa wafanyabiashara wa viungo kutoka Zanzibar na Tanzania Bara kwenda Dubai, Muungano wa Falme za Kiarabu ambapo pia ulitembelea Maonesho ya chakula ya dunia yaitwayo Gulf Food 2016. Katika msafara huu, Wafanyabiashara wa Tanzania waliweza kupata oda ya tani 24 za karafuu zenye thamani ya Sh. 432,000,000. Aidha, wafanyabishara wa Dubai walifanya maulizo ya bidhaa nyingine za Tanzania zikiwemo kungumanga, mchaichai na asali ambapo majadiliano yanaendelea ili kufikia muafaka wa bei na taratibu nyingine za biashara.

### Bodi ya Leseni za Maghala (TWLB)

134. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa kushirikiana na Bodi ya Leseni za Ghala imefanya marekebisho ya Sheria ya Stakabadhi za Ghala Na. 10 ya Mwaka 2005 ili kuimarisha usimamizi wa mfumo huo wa soko. Pamoja na marekebisho ya sheria, kanuni mpya za Sheria ya Mfumo zimeandaliwa ili kufanikisha utekekezaji wa Sheria hii iliyofanyiwa mapitio. Bodi imeendelea na utekelezaji wa majukumu yake na jumla ya Leseni zipatazo 13 za Waendeshaji Ghala na 16 za Ghala katika msimu wa 2015/2016 kwenye mazao ya korosho na kahawa zilitolewa. Bodi ilifanya ukaguzi katika ghala zilizotumika kuhifadhi mazao ya wakulima na kuchukua hatua stahiki dhidi ya upotevu wa mazao ya wakulima uliobainika katika ghala. Pia Bodi kwa kushirikiana na Tume ya Ushirika imejenga na kuimarisha mahusiano na Mrajis

wa Ushirika na kufanikiwa kuondoa migongano ya kisheria na ukiritimba wa ushiriki katika mfumo. Aidha, Bodi ya Leseni kwa kushirikiana na Bodi ya Korosho na Kahawa zimeanzisha ushirikiano mzuri wa kuhakikisha wanatoa miongozo ya utekelezaji kazi katika mfumo wa Stakabadhi kwa kila msimu kutegemeana na uhitaji.

135. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Bodi ya Leseni imeendelea kukutana na Taasisi za Fedha kwa lengo la kuzishawishi ili kuendelea kutoa mikopo nafuu kwa wakulima wanaotumia Mfumo. Aidha, Benki zilizowakopesha wakulima katika msimu wa 2015/2016 zinajumuisha NMB PLC Ltd, CRDB PLC Ltd, Kilimanjaro Cooperative Bank na Bank of Africa (BOA). Pia Bodi imeendelea kuwashirikisha na kuwaelimisha wadau kuhusu utaratibu wa kuomba leseni na faida za kutumia mfumo wa stakabadhi za ghala. Vilevile, Bodi ilitoa elimu kwa wadau kwa kushirikiana na wadau wengine kama ANSAF pamoja na kikundi cha wakulima cha AMSHA kilichoshiriki katika kipindi cha Redio Mashujaa Mjini Lindi kuelezea maana ya mfumo, mafanikio na changamoto zake. Bodi ilianda mafunzo kwa Waendesha Ghala ambapo jumla ya washiriki 58 walishiriki na kufundishwa mambo mbalimbali yahusuyo sheria, kanuni na utaratibu mzima wa kupokea na kutunza mazao katika ghala. Washiriki hao walitoka sekta ndogo ya korosho na kahawa. Wote walifuzu na kupata vyeti vya ushiriki.

136. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wataalamu wa Bodi walitembelea Mikoa ya Lindi na Mtwara na kufanya ukaguzi katika ghala zote zenyet lese ni wakati msimu unaendelea ili kuwaelimisha wafanyakazi wa ghala katika suala zima la utaratibu mpya wa kupanga mazao katika ghala kwa lengo la kuongeza ufanisi. Aidha, Bodi iliendelea kutoa mafunzo kwa watumiaji wa mifumo ya kielektroniki katika Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ili kurahisisha utendaji kazi. Mfano ni mfumo wa kielektroniki unaohusisha takwimu za mapokezi na utoaji wa mazao ghalani. Vilevile, Bodi imetengeneza mfumo wa kielektroniki wa kupokea taarifa za takwimu za mapokezi na utoaji wa mazao ghalani kwa wakati. Mfumo huo umeanza kutumika kwa majaribio katika msimu wa 2015/2016 kwenye zao la korosho. Pia, Bodi kwa kushirikiana na taasisi ya NRI katika Chuo Kikuu cha Greenwich kilichoko Uingereza imetengeneza Mfumo wa Kielektroniki wa ukaguzi wa ghala. Mfumo huo unajulikana kama Warehouse Inspection Reporting System na umeshaanza kutumika katika ukaguzi wa ghala msimu wa 2015/2016 na kuonesha mafanikio makubwa.

### Tume ya Ushindani (FCC)

137. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika Mwaka 2015/2016, Tume ya Ushindani imefanya mapitio ya Sera ya Bima, 2015 na Sera ya Taasisi za Mikopo 2015 na kutoa maoni kwa wahusika. Jumla ya mikataba 22 ya miungano ya makampuni imefanyiwa mapitio ili kubaini kama inaweza kufifisha ushindani kwa soko na uchumi kwa ujumla. Matarajio ni kuitia mikataba 31 kwa kipindi cha Mwaka

2015/16. Aidha, jumla ya malalamiko 24 yamefanyiwa uchunguzi, kati ya hayo malalamiko saba yametolewa uamuzi wa mwisho na malalamiko 17 uchunguzi unaendelea.

138. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Malalamiko 24 ya walaji yamepokelewa, na malalamiko 19 yametatuliwa kwa mlaji kurudishiwa fedha, kupatiwa bidhaa nyingine au kutengenezewa bidhaa. Malalamiko 5 yako kwenye majadiliano. Kazi ya kupokea na kutatua malalamiko ya mlaji ni endelevu. Kuhusu uondoaji wa mikataba inayomkandamiza mlaji anaponunua bidhaa au huduma (standard form consumer contracts), kanuni ziko tayari na zimeshawekwa kwenye tovuti ya tume na notisi imeshatolewa kwa zoezi la kuwasilisha mikataba hiyo kwa uhakiki tangu Januari, 2016. Kesi moja inayohusu kuondolewa/kutengenezwa kwa bidhaa isiyo salama sokoni inayohusu magari aina ya Range Rover na Range Rover Sport (zilizokuwa na hitilafu) uchunguzi wa awali pamoja na uandaaji wa notisi vimekamilika. Aidha, uchunguzi katika Kampuni ya Toyota na Nissan kuhusu ubovu (uliokwishagundulika kimataifa) unaoweza kuhatarisha maisha ya mtumiaji utaendelea. Kuhusu uandaaji wa Sera ya Taifa ya Kumlinda Mlaji, hadidu za rejea zilishakamilishwa na taratibu za kumtafuta mtaalamu mwelekezi zinaendelea. Vile vile marekebisho ya Sheria ya Ushindani yataendelea. Kazi ya uandaaji wa *English Popural Version of Standard Form Consumer Contract Regulation* umekwishakamilika na tayari imewekwa katika tovuti ya Tume ya Ushindani. Kazi ya uandaaji wa *Guidelines on Consumer Dispute Handling* umekwishakamilika, inasubiri marekebisho ya Sheria ya Ushindani kuhusu mamlaka ya Tume katika kushughulikia kwa ukamilifu masuala ya kumlinda mlaji.

139. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Zoezi la ukaguzi bandarini na bandari kavu (ICDs) Dar es Salaam liliwezesha kukamatwa kwa makontena 46 yaliyokuwa na bidhaa bandia. Wahusika walichukuliwa hatua kulingana na Sheria ya Alama za Bidhaa (merchandise Mark Act, 1963) kama ilivyorekebishwa. Tume ilifanya kaguzi 12 za kushtukiza (counterfeit raids) katika mikoa ya Arusha, Mwanza, Kilimanjaro, Shinyanga na Dar es Salaam ambapo watuhumiwa 29 walikamatwa na bidhaa bandia kinyume na Sheria ya Alama za Bidhaa kama ilivyorekebishwa. Bidhaa zilizokamatwa ni pamoja na nyembe aina ya supermax, viatu aina ya timberland, konyagi, kiwi, dawa ya wadudu aina ya Baygon na simu aina ya NOKIA na TECNO.

140. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Tume ya ushindani kwa kushirikiana na mtaalamu mwelekezi imeandaa matangazo mafupi yanaylorushwa katika luninga na kutangazwa katika radio kuhusiana na bidhaa bandia na mikataba ya mlaji inayoandaliwa na mzalishaji au mtoa huduma. Lengo ni kuelimisha umma kuhusiana na udhibiti wa bidhaa bandia na utetezi wa mlaji. Tume imeshiriki katika maonesho ya SabaSaba na NaneNane ambapo iliweza kutoa elimu na vipeperushi kuhusiana na bidhaa bandia, utetezi wa mlaji na masuala

ya ushindani kwa umma. Vilevile, Tume iliweza kuzungumza na vyombo vyahabari kuhusiana na mafanikio ya tume katika kipindi cha miaka nane ya uwepo wake. Tume iliendesha semina kwa ajili ya wadau wa elimu tarehe 29/11/2015 kwa lengo la kuelimisha na kuhamasisha uanzishwaji wa mitaala ya somo la elimu kwa mlaji na masuala ya bidhaa bandia kwa ajili ya shule za msingi na sekondari. Katika semina hiyo, ilikubalika kuwa, muongozo wa kuanzisha elimu kwa mlaji katika mitaaala ya elimu ya msingi na sekondari uanze haraka iwezekanavyo. Tume imeshaanza mazungumzo na Taasisi ya Elimu Tanzania kuhusiana na kuandaa muongozo huo. Zoezi la utoaji elimu kwa wadau mbalimbali litaendelea. Vilevile, Tume inajipanga kuandaa mpango Mkakati wa Elimu wa miaka mitatu ambao utaainisha makundi mbalimbali katika jamii na jinsi makundi hayo yatakavyofikiwa.

### Baraza la Ushindani (FCT)

141. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika Mwaka 2015/2016, Baraza limeendelea kusikiliza kesi za rufaa zinazotokana na mchakato wa udhibiti wa ushindani katika soko la sekta za nishati na madini, usafirishaji na biashara. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2015 hadi Januari 30, 2016 Baraza lilikuwa na jumla ya kesi 29 yakiwemo maombi tisa ya rufaa na kumi ya *bill of cost*. Kati ya kesi zilizokuwepo 13 ni mpya na 16 ni za zamani. Aidha, katika kipindi husika Baraza lilitolea maamuzi jumla ya kesi 9 ikiwemo 1 mpya na 8 za zamani. Baraza linaendelea kushughulikia kesi 20 ambazo zipo katika hatua mbalimbali za maamuzi ikiwemo majadiliano yanayopelekea maamuzi, usikilizwaji, maamuzi na hatua stahiki.

142. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Baraza limeendelea kuwawezesha watumishi na wajumbe wa Baraza kupata mafunzo yanayohusu ushindani na udhibiti wa soko katika nyanja zinazohusiana na Baraza. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2015 hadi Januari 30, 2016, Jumla ya watendaji wanenye na wajumbe wa Baraza wawili waliwezesha kupata mafunzo hayo. Aidha, Baraza limeendelea kujitangaza kupitia maonesho ya kitaifa na kimataifa kwa kuhudhuria katika maonesho ya SabaSaba na NaneNane yaliyofanyika katika Jiji la Dar es Salaam na Mkoa wa Lindi. Kupitia maonesho hayo, wadau mbalimbali walifahamishwa juu ya utendaji kazi na umuhimu wa Baraza kwa njia mbalimbali zikiwemo machapisho ya vijitabu, majarida pamoja na mazungumzo.

### Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA)

143. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika kipindi cha Mwaka 2015/2016, Wizara kwa kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imeweka mifumo ya kiteknolojia itakayowawezesha wadau kupata taarifa na huduma kwenye mifumo ya kompyuta na kusajili kwa njia ya mtandao. Wakala katika kuboresha utoaji wa huduma zake imejenga Mfumo wa Usajili wa Majina ya Biashara (Online Business Names Registration System-OBRS) uliozinduliwa rasmi tarehe

2/10/2015. Mfumo huo unawawezesha wateja kuomba na kupidishiwa majina ya Usajili, kulipa ada na kupata taarifa za majalada kwa njia ya Mtandao. Pia Wakala kwa sasa inaendelea kutoa elimu kwa wadau na imeweke dawati maalumu la elimu kwa wadau.

144. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wakala imetangaza zabuni ya kutengeneza mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao ambayo imefunguliwa tarehe 8/1/2016. Mradi huo kwa awamu ya kwanza unategemewa kukamilika Desemba 2016 na utawezesha kufanya usajili wote wa Makampuni, Leseni za Viwanda, Alama za Biashara na huduma na kutoa Hataza kwa njia ya mtandao. Aidha, shughuli zote za wakala zitaweza kuwa katika mifumo ya kielectroniki ili kuwezesha shughuli za usajili kwa mtandao ziweze kufanyika. Mradi huo pia unategemewa kuunganishwa na masijala nyingine zinazotegemeana kama vile TIC, TRA, NIDA na RITA. Tovuti ya Wakala ([www.brela.go.tz](http://www.brela.go.tz)) imeboreshwa sambamba na kuelimisha wadau ili kuweza kwenda sambamba na teknolojia ya sasa, kuweza kutoa huduma ya usajili kwa mtandao na kuwa rafiki kwa watumiaji. Taratibu za usajili pamoja na ada zote zimebekwa kwenye tovuti zikiwemo fomu zote za usajili, Katiba Mfano kwa wateja wanaotaka kusajili kampuni, Vigezo vya kutumia kuangalia majina yanayofaa na yasiyofaa, na pia majina na simu za Wakuu wote wa Idara na Vitengo ili kuweza kutoa maelezo na msaada kwa wadau wakati wowote.

145. **Mheshimiwa Naibu Spika**, BRELA imeboresha mifumo ya uwekaji na utunzaji wa masijala tano za kisheria zinazosimamiwa na Wakala ili kuweza kushabihiana na mifumo ya kiteknolojia na hatimaye kurahisisha utoaji huduma. Wakala imeboresha mifumo ya usajili na utunzaji wa masijala kwa kuweka mifumo ya kielectroniki saidizi kwa ajili ya kutunza masijala na usajili wa Majina ya Biashara ambao mifumo hiyo imetuwezesha kusajili jina la biashara ndani ya masaa nane tu badala ya siku tatu za awali. Wakala imeboresha masijala tano za kisheria na vitendea kazi kwa kuweka taarifa za masijala kwenye mifumo ya kiteknolojia hivyo kuweza kupata taarifa za majalada kwa urahisi, kununua vitendea kazi vyote vinavyohitajika kama kompyuta, mashubaka kwa ajili ya masijala zote tano, ili kuweza kutekeleza kazi za Wakala kwa wakati, ufanisi na kwa ubora. Wakala imeanzisha kitengo chenye wataalam wa kusimamia na kutunza masijala na kumbukumbu za wakala chini ya Ofisi ya Mtendaji Mkuu. Wakala pia imeendelea kufanya mapitio ya sheria zake ili kuweza kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia katika kutoa huduma ambapo sheria hizo zipo katika hatua mbalimbali za kufanyiwa mabadiliko.

146. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wakala iliweza kupata eneo kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la ofisi zake. Michoro ya jengo iko tayari, mkandarasi alikwishapatikana na sasa Wakala iko kwenye taratibu za kupata fedha za kuwezesha ujenzi wa Jengo hilo. Ofisi hizo zitakapokamilika zitaiwezesha BRELA

kupunguza gharama za kulipia pango la ofisi. Hatua hiyo itasaidia pia kuweka mifumo ya kielektroniki itakayorahisisha usajili wa biashara.

147. **Mheshimiwa Naibu Spika**, BRELA imechukua hatua za makusudi na kufanya kampeni katika mikoa mbalimbali nchini ili kutoa elimu juu ya huduma zinazotolewa na Wakala na pia, kuhamasisha wafanyabiashara wakubwa na wadogo kufanya usajili wa majina ya biashara hapo walipo kwa njia ya mtandao. Wakala imetoea elimu kwa umma Kanda ya Kusini katika mikoa ya Mbeya, Njombe, Ruvuma na pia elimu ya usajili kwa mtandao imetolewa katika Kanda ya Kaskazini kwa kuwahuishaa maafisa biashara na maafisa wa TCCIA. Pamoja na hiyo, Wakala imeweke dawati maalum kwa ajili ya mafunzo kwa wateja juu ya usajili kwa mtandao. Aidha, Wakala inaendelea kutoa elimu kwa wadau kuhusu usajili kwa njia ya mtandao hususan kwa maafisa wa TCCIA na maofisa biashara wilayani na mikoani.

148. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wakala imeendelea kushirikiana na ARIPO na WIPO katika kutekeleza majukumu yake na pia kuendeleza mahusiano na mashirikiano mazuri na taasisi mbalimbali katika kutoa huduma, zikiwemo TRA, TCCIA n.k. Aidha, tangu Julai, 2015 hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2016, Wakala imesajili Makampuni 6,600, Majina ya Biashara 8,028, Alama za Biashara na Huduma 2,956, Hataza 17 na imetoea Leseni za Viwanda 99.

### **Wakala wa Vipimo (WMA)**

149. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wakala wa Vipimo imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kuimarisha usimamizi wa matumizi ya vipimo vilivyo sahihi nchini ambapo hadi kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2015/2016 vipimo 518,893 vilihakikiwa; vipimo 16,912 vilirekebishwa; vipimo 2,538 vilikatazwa kutumika kwenye biashara; na matenki 4,925 yakiwemo fuel storage tank –(FST), Bulk Storage Tank – (BST) na Vehicle Storage Tank – (VST) yalipimwa. Wakala pia imeimarisha ukaguzi wa bidhaa zote zilizofungashwa katika mipaka.

150. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wakala iliendelea kutoa elimu kwa wananchi kupitia Maonesho ya Sabasaba na Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika kitaifa mkoani Lindi. Aidha, Wakala kupitia vyombo mbalimbali vya habari kama vile luninga, redio na mitandao ya kijamii imeendelea kutoa mafunzo kuhusu ufungashaji, matumizi ya vipimo katika ununuvi na uuzaji wa zao la pamba; mitungi ya gesi zitumikazo majumbani; matumizi ya mizani katika maduka ya nyama; vituo vya mafuta na utambuzi wa ujazo sahihi wa malori ya mchanga katika masoko ya Mabibo, Tandale, Kariakoo, Buguruni na Singida mwezi Agosti, 2015. Wakala imefanya zoezi la sensa ya vipimo katika Mkoa wa Ilala na hivyo kuwezesha kukamilika kwa kazidata ya vipimo katika mkoa huo. Aidha, sensa hiyo imekwishafanyika katika mikoa ya Mbeya, Rukwa, Katavi na Kinondoni.

151. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wakala imeandaa miongozo ya usimamiaji na uhakiki wa vipimo vya mafuta (operation and test manuals) utakaosaidia upimaji wa mafuta kabla ya kusafirishwa kuja nchini. Maboresho ya fomu ya utendaji kazi yamefanyika kulingana na maboresho ya mfumo mpya. Aidha, Wakala kwa kushirikiana na wadau imepitia rasimu ya kanuni za upimaji mafuta na gesi asilia (bulk edible oil, petroleum products and natural gas measurements regulations 2015). Aidha, Wakala imeendelea na ujenzi wa kituo cha kupimia ujazo wa malori ya mafuta cha Misugusugu Mkoani Pwani ambao unatarajija kukamilika katika robo ya kwanza ya 2016/2017.

### **Kituo cha Uwekezaji Tanzania**

#### **Usajili, Umiliki na Mgawanyo wa Miradi ya Uwekezaji**

152. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika kipindi cha Julai 2015 hadi Machi 2016, Kituo kilifanikiwa kusajili jumla ya miradi 271 yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 4,478.81. Miradi hiyo ilitarajiwa kutoa ajira mpya zipatazo 34,609. Sekta iliyoongoza kwa idadi ya usajili wa miradi ni uzalishaji/usindikaji viwandani, ikifuatiwa na Sekta ya Utalii, Usafirishaji na Majengo ya Biashara. Sekta zinazotarajiwa kutoa ajira kwa wingi zaidi ni Sekta ya Uzalishaji viwandani, Sekta ya Kilimo, Sekta ya Majengo ya Biashara ikifuatiwa na Sekta ya Utalii. Aidha, uchambuzi wa takwimu unaonesha katika kipindi cha Julai 2015 hadi Machi, 2016, Watanzania waliongoza kwa usajili wa miradi mingi ipatayo 117, sawa na 43% ya miradi yote, wakati miradi ya wageni ikiwa ni 109 sawa na 40% na iliyobaki ambayo ni miradi 45 sawa na 17% ilimilikiwa kwa ubia kati ya Watanzania na wageni. Katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 Mkoa wa Dar es Salaam uliendelea kuongoza kwa kusajili miradi mingi kwa kuwa na miradi 125 kati ya miradi 271 sawa na 46% ya miradi yote iliandikishwa. Mkoa wa Pwani ulifuatia kwa kusajili miradi 30 ya miradi yote sawa na 11%, kisha Arusha miradi 27 sawa na 10%, Mwanza miradi 19 sawa na 7%, na Mikoa iliyobaki kila mmoja ilisajili chini ya miradi 10.

### **Huduma kwa Wawekezaji**

153. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016, Kituo kimeendelea kufanya kazi kwa Mfumo wake wa Mahali Pamoja pa Kuhudumia Wawekezaji (One Stop Centre), na pia kufanya maboresho ya mfumo huo. Pia, Kituo kiliendelea kuboresha huduma zake kwa kuanza utekelezaji wa kuanzisha mtandao wa *Tanzania Investment Window (TIW)* ili kuongeza kasi katika kuwashudumia wawekezaji. Baada ya kukamilika kwa mradi huo, huduma nyingine zote zikiwepo za uhamiaji, vibali vya kazi, ardhi, kufungua kampuni n.k zinatolewa ndani ya TIC kwa mfumo wa mtandao. Katika kutoa huduma hizo, Kitengo cha Usajili wa Makampuni, kilishughulikia jumla ya maombi yapatayo 583. Kati ya hayo, makampuni 86 yalisajiliwa na

Iesen 12 za uanzishwaji viwanda zilitolewa. Kitengo cha Leseni za Biashara kilifanikiwa kushughulikia maombi yapatayo 255 ambapo Iesen za biashara 93 zilitolewa. Kitengo cha Kazi kilifanikiwa kutoa jumla ya vibali 3,126 vya daraja A kwa ajili ya wenyе hisa na daraja B kwa ajili ya wafanyakazi. Kitengo cha TRA kilifanikiwa kuhudumia jumla ya wateja 1,371 mpaka Desemba, 2015 kwa kuwasaidia kupata huduma kama vile, misamaha ya kodi, usajili wa mlipa kodi na VAT na masuala mbalimbali yahusuyo kodi kwa ujumla.

Aidha, Kitengo cha ardhi kiliendelea kutoa huduma za ushauri kwa wawekezaji katika masuala mbalimbali ya ardhi pamoja na kuainisha maeneo yenye ardhi kwa ajili ya uwekezaji katika maeneo mbalimbali ya Tanzania. Kitengo cha Ardhi kilifanikiwa kushughulikia jumla ya masuala mbalimbali yapatayo 573 ya ardhi, hati zisizo asili (Derivative title) 59 zilipokelewa na kushughulikiwa na jumla ya hati 10 zisizo asili zimekamilika na kukabidhiwa wawekezaji mpaka Desemba, 2015.

### **Ufuatiliaji wa Miradi ya Uwekezaji**

154. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kuanzia mwezi Mei, 2015 Kituo kimeanzisha mpango maalum wa kufuatilia kwa karibu wawekezaji ili kujua changamoto zinazowakabili na kuwa karibu nao. Kupitia mpango huo imetengenezwa database maalum inayokusanya taarifa na takwimu muhimu za wawekezaji na kufuatilia changamoto zao kwa lengo la kuwa na mahusiano ya karibu na wawekezaji. Kwa kuanzia, mpango huo umelenga sekta ya uzalishaji. Tangu kuanza kwa mpango huo, jumla ya miradi 117 iliyaojiri zaidi ya watu 50 iliweza kutembelewa.

### **Ardhi kwa ajili ya Uwekezaji**

155. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 Kituo cha uwekezaji kiliandaa andiko kwa ajili ya kuiwezesha Serikali kuliweka Shamba la Mkulazi lenye hekta 63,227 katika Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano kuanzia Julai, 2016. Lengo ni kuhakikisha shamba hilo linawekewa miundombinu stahiki ikiwepo barabara, umeme, maji, bomba la gesi na kuunganishwa na reli ili kuanzisha agriculture city/industrial park ili eneo hilo litumike katika kutekeleza Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda. Inatarajiwa miundombinu ya nje ya shamba itajengwa na Serikali wakati miundombinu ya ndani ya shamba itajengwa na wawekezaji binafsi. Kituo kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kupitia mpango wa BRN, kiliainisha maeneo kwa ajili uwekezaji katika kilimo. Jumla ya mashamba 25 yamefanyiwa kazi na yapo katika hatua mbalimbali. Aidha, Shamba la Lukuliro Rufiji limeshapata hati na mwekezaji kupewa Hati isiyo asili.

## **Elimu kuhusu Uwekezaji**

156. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kituo kiliimarisha idara inayohusika na utoaji elimu kwa umma ili kuelimisha jamii kuhusu faida na kuvutia uwekezaji. Mkakati huo unalenga kuongeza ushirikiano kutoka katika makundi mbalimbali ya jamii ili kuondoa dhana hasi kuhusu uwekezaji zinazotokana na uelewa duni juu ya manufaa ya uwekezaji. Pia, Kituo kililenga katika kuelimisha wawekezaji wa ndani kujisajili na Kituo ili kupatiwa huduma mbalimbali zinazotolewa Kituoni kwa wawekezaji wote. Kituo kimeandaa Mkakati wa Mahusiano na Elimu kwa Umma na pia katika kutekeleza mkakati huo, Kituo kimeandaa documentary ambayo imeoneshwa kwenye vyombo mbalimbali vyahabari kuonesha uwekezaji wa aina mbalimbali na faida zake kwa jamii.

## **Ofisi za Kanda za Kituo cha Uwekezaji**

157. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kwa kupitia Ofisi tatu za kanda za Mwanza, Mbeya na Moshi, Kituo kimetekeleza jukumu la kutoa elimu kwa wafanyakazi wa Serikali na wawekezaji wa ndani waliopo katika mikoa mbalimbali kuhusu uwekezaji na huduma zinazotolewa na Kituo. Pia ofisi za Kanda zimeshirikiana na viongozi wa mikoa husika katika kutafuta na kutenga ardhi kwa ajili ya uwekezaji kwenye mikoa hiyo. Katika Mwaka 2016/2017, Kituo kimepanga kuboresha ofisi zake za Kanda hasa katika eneo la wafanyakazi ili kiweze kutekeleza jukumu la kuhamasisha uwekezaji wa ndani, kutoa elimu kwa wajasiriamali, kutafuta maeneo ya uwekezaji mikoani, kutoa huduma kwa miradi ya uwekezaji iliyopo Aftercare Services na pia kufuatilia na kutathmini miradi ya uwekezaji iliyopo katika mikoa hiyo.

## **Uhamasishaji Uwekezaji**

158. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kituo kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa iliratibu ushiriki katika makongamano ya uwekezaji katika nchi za Misri na Kenya. Makongamano hayo yalihudhuriwa na zaidi ya wafanyabiashara 200 kutoka nchi mbalimbali. Ushiriki wetu katika makongamano hayo ulitupa fursa kutoa taarifa mbalimbali zenye lengo la kuhamasisha uwekezaji nchini ikiwamo mada juu ya hali ya uchumi, fursa za uwekezaji zinazopatikana nchini, mazingira ya uwekezaji na vivutio vinavyotolewa kwa wawekezaji. Makongamano hayo yalitoa nafasi ya kufanyika kwa mikutano baina ya wafanyabiashara na kati ya wafanyabiashara na Serikali.

159. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kituo cha Uwekezaji kilishiriki katika maandalizi ya ushiriki wa Tanzania katika makongamano ya uwekezaji, mikutano na kupokea ujumbe wa wafanyabiashara kutoka nchi mbalimbali zikiwamo Misri, China, Nigeria, Japan, Oman, Urusi, Uturuki, Jordan, Singapore, India na

Vietnam. Shughuli mbalimbali za kuhamasisha uwekezaji wa ndani ya nchi zilihusisha zaidi ya washiriki 700 wengi wao wakiwa ni wafanyabiashara. Makongamano hayo yalihusisha washiriki kutoka taasisi za umma na binafsi na yalilenga kukutana na wafanyabiashara na kuwapatia taarifa muhimu kuhusu masuala ya uwekezaji na pia kuwawezesha kuzitambua na kuchangamkia fursa za uwekezaji katika sekta mbalimbali hapa nchini.

160. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kituo cha uwekezaji kwa kushirikiana na ofisi za wakuu wa mikoa kimeweza kuandaa makongamano ya uwekezaji yaliyohudhuriwa na watu zaidi ya 3000 kwenye mikoa mbalimbali nchini. Makongamano hayo yaliandaliwa katika ngazi ya Kanda, Mkoa na Wilaya. Katika Kanda ya Nyanda za juu Kusini inayojumuisha mikoa ya Mbeya, Iringa, Njombe, Kigoma, Rukwa na Katavi, makongamano yalisfanyika katika mikoa ya Mbeya na Kigoma. Kituo pia kwa kushirikiana na uongozi wa wilaya kiliandaa kongamano la uhamasishaji wa uwekezaji liliofanyika katika Wilaya ya Bunda (Bunda Investment Forum).

161. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Pamoja na makongamano hayo, Kituo kwa kushirikiana na taasisi za Serikali na za watu binafsi kama vile mabenki, TRA n.k kiliandaa semina zilizoshirikisha wawekezaji na wajasiriamali wa nje na ndani. Lengo kuu la makongamano na semina hizo ilikuwa kutoa elimu kuhusiana na kazi za kituo na faida zake, elimu kuhusiana na maswala ya uwekezaji, namna serikali inavyoweza kuwasaidia katika uanzishaji wa kampuni, unafuu wa kodi ambao Serikali itawapa kupitia Kituo cha Uwekezaji na pia kuwahamasisha wananchi na hasa wazawa kutumia fursa za uwekezaji zilizopo katika maeneo yao kama vile kilimo, madini, utalii, misitu na kadhalika ili kukuza kipato chao na kuondokana na umasikini.

162. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kituo kimekuwa kikishiriki kila mwaka katika maonesho mbalimbali ya kitaifa kama vile Sabasaba, Wiki ya Utumishi wa Umma na Nanenane ikiwa na lengo kuu la kutoa elimu kwa umma kuhusu huduma zitolewazo na kituo, faida za kituo kwa mwekezaji hasa mzawa, kutoa elimu ya uwekezaji, fursa za uwekezaji zilizopo katika maeneo husika na vivutio vitolewavyo na kituo kwa wawekezaji. Ushiriki wa Kituo umekuwa na faida kubwa kwani wananchi wengi waliweza kutembelea banda la Kituo na kupata elimu hiyo.

### **Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE)**

163. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) kwa Mwaka 2015/2016 kimetekeleza yafuatayo:-

- i) Chuo kimekamilisha taratibu za uanzishaji wa Shahada ya Uzamili kwenye TEHAMA (ICT for Development and IT Project Management) kwa kushirikiana na

Chuo Kikuu cha Stockholm - Sweden. Vile vile, Chuo kipo kwenye hatua za uanzishwaji wa Shahada ya Uzamili kwenye uendeshaji wa biashara ya mafuta na gesi kwa kushirikiana na Maastricht School of Management ya Uhlanzi. Aidha, Chuo kinaendelea kuimarisha uwezo wa wahadhiri wake ambapo jumla ya wahadhiri 37 wapo kwenye mafunzo ya muda mrefu, kati yao 19 wapo kwenye mafunzo ya shahada ya uzamivu (PhD degree) na 18 wapo kwenye mafunzo ya shahada ya uzamili (Masters degree).

- ii) Vilevile, chuo kimeandaa Mpango Kamambe (Master Plan) wa kiwanja cha Kiseke cha Kampasi ya Mwanza na kiwanja cha Medeli-Dodoma. Ukarabati mkubwa wa jengo la utawala (Block A) na uboreshaji wa hema ya muda ya mihadhara kwa kampasi ya Dar es salaam unaendelea. Pia, uboreshaji mkubwa umefanyika katika kampasi ya Dodoma ikiwa ni pamoja na; Ukarabati wa jengo la cafeteria; jengo moja la hosteli kuwa ofisi ya wahadhiri; ofisi sita za wahadhiri kuwa madarasa mawili na ukarabati wa jengo la nyumba mbili za wafanyakazi kuwa maktaba unaendelea.
- iii) Katika kuongeza uwezo wake wa kutoa elimu ya biashara, Chuo kimenuna eneo lenye ukubwa wa ekari 54.9 kwa ajili ya ujenzi wa Kampasi katika eneo la Iganzo mkoani Mbeya kwa gharama ya Shilingi 271 milioni. Mchakato wa kuandaa Mpango Kamambe (Master Plan) wa eneo la Iganzo unaendelea na tayari Chuo kimetangaza zabuni kwa ajili ya kumpata mtaalamu (consultant) ili aweze kuandaaa mpango huo.

### **Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO)**

164. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika mwaka 2015/2016, Serikali kupitia SIDO imehamasisha Serikali za Mitaa nchi nzima kutenga maeneo ya kongano; imeandaa Mkakati wa Taifa wa Kuendeleza Kongano; na kutayarisha Mipango ya Biashara ya maeneo ambayo tayari yametengwa kama vile Kizota Dodoma. Aidha, kwa kupitia ufadhili wa UNIDO, SIDO imeweza kuimarisha kongano ya ubanguaji wa korosho iliyopo katika Mtaa wa Viwanda wa SIDO Mkoani Mtwara.

165. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Mpango wa viatamizi hutumika kuwalea wajasiriamali wenyе ubunifu wa teknolojia, mawazo na bidhaa mpya kwa kuwajengea miundo mbinu ya kisasa na kuwapatia ushauri ili waweze kukuza ubunifu wao na hatimaye kunufaisha jamii kubwa. Katika Mwaka 2015/2016, mambo yafuatayo yameteklezwa:-

- i. Mafunzo ya watoa huduma kwenye miradi ya kiatamizi yaliyotolewa na Wataalamu kutoka Serikali ya Finland;

- ii. Kufanyika kwa makubaliano ya ufadhilli na Serikali ya India kupitia Shirika la Viwanda Vidogo la India wenyewe lengo la kuboresha program ya kiatamizi Dar es Salaam; na
- iii. Kufanyika kwa makubaliano na baadhi ya taasisi za elimu ya juu ili kushirkiana katika utekelezaji kwa kuwasaidia wahitimu wenyewe vipaji vya ubunifu.

166. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Ili kuimarisha mfumo wa ufuatuliaji wa shughuli za Shirika mambo yafuatayo yametekelizwa:-

- i) Mfumo wa TEHAMA wa kusimamia taarifa za shirika (Management Information System) umetengenezwa;
- ii) Mfumo wa kusimamia mfuko wa kuendeleza wajasiriamali na mahesabu ya shirika (Loan Performer ) umeimarishwa.
- iii) Mfumo wa kuratibu utendaji wa vituo vya kuendeleza teknolojia (Technology Centres) umetengenezwa; na
- iv) Utengenezaji wa SIDO Web Portal.

167. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Serikali kupitia SIDO imeendelea kutambua umuhimu wa kupeleka huduma kwa wananchi mahali walipo, hilo hufanywa kwa kutoa huduma zinazowawezesha kuanzisha miradi yao ya uzalishaji na kutoa huduma vijijini. Utekelezaji wa huduma hiyo umekuwa ukifanywa kupitia Mkakati wa Wilaya Moja Bidhaa Moja (ODOP). Utoaji wa huduma katika maeneo yote unazingatia kumjengea msingi na uwezo mjasiriamali mdogo wa kuzalisha bidhaa kutohana na malighafi zilizopo katika kuchangia maendeleo ya viwanda vidogo vijijini. Huduma zilizotolewa ziliwezesha uanzishwaji wa viwanda vidogo 127 na kutengeneza ajira zipatazo 1,334 katika wilaya mbalimbali nchini.

168. **Mheshimiwa Naibu Spika**, SIDO inamiliki vituo vya maendeleo ya teknolojia saba katika mikoa ya Arusha, Kigoma, Kilimanjaro, Iringa, Mbeya, Lindi na Shinyanga. Vituo hivyo vinajihusisha na uendelezaji wa teknolojia na utengenezaji wa mashine/vifaa na kutoa huduma za kiufundi kwa wajasiriamali wadogo na kati wa mjini na vijijini. Vituo vimeweza kuzalisha aina 185 ya teknolojia. Vituo hivyo vimejengewa uwezo ufuataao ili viweze kuimarika na kutoa huduma bora:-

- i. Kujenga uwezo wa mifumo ya TEHAMA ya vituo hivyo kwa kutengeneza 'ICT software';
- ii. Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa vituo hivyo; na

iii. Kupeleka wataalamu wa kuvifanyia tathmini na ushauri wa jinsi ya kuviboresha kwa kushirikiana na Taasisi ya CESO ya Canada.

169. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Teknolojia ni msingi mkuu katika kuanzisha miradi ya uzalishaji hasa viwanda vidogo na vya kati. Matumizi ya teknolojia sahihi, licha ya kuongeza ufanisi huleta tija na kuhakikisha bidhaa zinakuwa na viwango vinavyotakiwa. Msingi wa utoaji huduma katika eneo hili, ni kuboresha na kuendeleza teknolojia za ndani na nje ili ziwe na tija na ufanisi na matumizi yake yaenee na kuwanufaisha wananchi wengi. Kwa Mwaka 2015/2016, jumla ya mashine mpya 185 zilitambuliwa/zilizalishwa na kusambazwa. Mashine na zana hizo ziliwezesha kuanzishwa na kuimarisha shughuli za miradi 212 ya uzalishaji kote nchini. Maeneo ya teknolojia hizo ni ubanguaji wa korosho, usindikaji wa mihogo, ukamuaji wa mafuta ya mawese, usindikaji wa vyakula, upunguzaji wa matumizi ya miti na mazao yake kama nishati na ufungashaji wa vyakula vilivyosindikwa. Teknolojia nyingine ni za utengenezaji wa vifaa vya ujenzi hasa matofali, utengenezaji wa chokaa na chaki, ukamuaji mafuta ya kula kutokana na michikichi, utengenezaji wa sabuni na usindikaji ngozi kwa kutumia njia za asili. Teknolojia hizo zimesaidia kuimarisha na kuongeza ubora wa bidhaa za wajasiriamali.

170. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wajasiriamali wenyе ubunifu wa teknolojia na mawazo ya bidhaa mpya husaidiwa kuendelezwa kwa kupatiwa huduma mbalimbali kama vile maeneo ya kufanya kazi, ushauri wa kiufundi na mitaji ili wakue na kufikia viwango vya kujitegemea. Katika kipindi 2015/2016, jumla ya teknolojia na mawazo ya bidhaa mpya nane yalihudumiwa. Miiongoni mwa teknolojia hizo zilihusu utengenezaji wa sabuni, uyeyushaji wa vyuma ili kupata vipuri vya aina mbalimbali, usindikaji vyakula, uchakataji na utengenezaji wa bidhaa za ngozi na utengenezaji wa zana za kilimo.

171. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Ili kuweza kuongeza uwezo wa uzalishaji, SIDO imeweza kutoa mafunzo ya ujasiriamali, uongozi wa biashara na usindikaji kwa wajasiriamali wanaofanya shughuli zao katika kongano mbalimbali na wale wanaotarajia kutumia kongano. Pia, wamepewa huduma ya kuimarisha na kuthibitisha ubora wa bidhaa wanazozalisha kwa kuunganishwa na taasisi husika kama vile TFDA, TBS na GS1 National (Tz). Aidha, wajasiriamali hao waliweza kutafutiwa vifungashio vyenye ubora unaotakiwa ikiwa ni pamoja na kusaidiwa kutafutiwa masoko ya bidhaa zao. Aidha, Shirika kwa kushirikiana na vyuo mbalimbali linakusudia kuwezesha ubunifu na utengenezaji wa bidhaa mpya kupitia programu ya wahitimu wa vyuo. Lengo la programu ni kuwalea na kuwakuza wahitimu wa vyuo wenyе vipaji maalumu ili waweze kukua, kujitegemea na kuchangia katika maendeleo ya taifa. Hadi hivi sasa makubaliano yameshafanyika na vyuo vya VETA, UDSM na SUA ili wahitimu wake waweze kusaidiwa.

172. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Uhawilishaji wa teknolojia ni nguzo muhimu katika kukuza maarifa na upatikanaji wa teknolojia kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Teknolojia kutoka ndani na nje ya nchi zilihawilishwa ili kutumika kwa wajasiriamali wa mijini na vijiji. Mkazo mkubwa ulikuwa ni kwenye teknolojia zinazoongeza thamani katika mazao ya kilimo, mifugo, madini, uvuvi na utunzaji wa mazingira. Katika kipindi hiki, tumehamasisha wajasiriamali kushiriki katika kazi ya uhawilishaji wa teknolojia; tumehawilisha jumla ya teknolojia 39 kwa wajasiriamali wadogo na kuandaa maonesho mawili ya teknolojia.

173. **Mheshimiwa Naibu Spika**, SIDO imeendelea kusimamia Mradi wa MUVI na kazi za uendelezaji wa mnyororo wa thamani kwa mazao mbalimbali zimeendelea kufanyika na hadi sasa jumla ya kaya 186,797 na wananchi 866,587 wamefikiwa na huduma za mradi huo katika wilaya 19 za mikoa 6 inayoshiriki. Aidha, huduma za utoaji wa mikopo kupitia Mfuko wa NEDF iliendelea, na katika kipindi hiki jumla ya mikopo 2,740 yenye thamani ya shilingi bilioni 3.602 ilitolewa. Mikopo iliyotolewa iliwezesha upatikanaji wa ajira 7,131.

### 3.2.5 Maendeleo ya Rasilimali Watu na Utoaji wa Huduma

#### Kada Kiutumishi

174. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wizara ina jumla ya Watumishi 260 wa kada mbalimbali. Kati ya hao 105 ni wanawake ambaeo ni sawa na asilimia 40 na 155 ni wanaume ambaeo ni sawa na asilimia 60. Kwa Mwaka 2015/2016, Wizara imewathibitisha kazini watumishi 58 na kuwathibitisha katika vyeo watumishi 43 ambaeo wameonesha utendaji mzuri katika kazi zao na kuwapandisha vyeo watumishi 21 kwa kuzingatia miundo ya kada zao na matokeo ya utendaji kazi wao kupitia OPRAS.

#### Mafunzo

175. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Mwaka 2015/2016, Wizara iliandaa mpango wa mafunzo wa muda wa mwaka mmoja ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake. Katika utekelezaji wa mpango huo, Wizara imewajengea uwezo jumla ya watumishi 31 kwa kuwapeleka mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ndani na nje ya nchi. Aidha, Watumishi sita walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi ishirini na tano walihudhuria mafunzo ya muda mfupi katika fani za uhazili, usimamizi wa fedha, biashara, Shahada ya uzamili ya Uongozi na Utawala na mafunzo ya udereva.

## MWAMTUKA (OPRAS)

176. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika kutekeleza Programu ya Kuboresha Utumishi wa Umma na kuimarisha utendaji unaojali matokeo na kuimarisha uwajibikaji katika Utumishi wa Umma, kwa mwaka 2015/2016 watumishi 256 kati ya 260 wamesaini mikataba ya kazi na wasimamizi wao kwa mfumo wa wazi wa Mapitio ya Tathmini ya Utendaji Kazi (OPRAS) na kufanya mapitio ya nusu mwaka mwezi Desemba, 2015. Aidha, watumishi wanne ambao hawajasaini mikataba wapo mafunzoni. Inatarajiwa kufikia mwisho wa mwezi Juni, 2016 kila mtumishi atafanyiwa tathmini ya utendaji wake wa kazi kwa kipindi cha mwaka mzima kwa kutumia utaratibu huo wa MWAMTUKA.

### Michezo na Afya za Watumishi

177. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kwa Mwaka 2015/2016, Wizara imefanikiwa kushiriki katika Bonanza lililodhaminiwa na TANTRADE kwa lengo la kujenga afya za Watumishi, kushirikiana na kufahamiana.

### Usimamizi wa Mapato na Matumizi

178. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kuhusu usimamizi wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali, Wizara yangu imeendelea kuhakikisha wanaopaswa kulipa ada ya leseni wanalipa wanafanya hivyo. Wizara kwa kutumia kitengo cha Ufuatiliaji na Uperembaji (M & E Section) na maafisa biashara walio katika Halmashauri zote nchini wameendelea kufanya ukaguzi kuhakikisha kila mfanyakia biashara anayestahili kulipia ada ya leseni analipa na hatua za kisheria zinachukuliwa kwa mfanyakia biashara yejote anayepatikana akifanya biashara bila kuwa na leseni stahili na zoezi hilo ni endelevu.

179. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kuhusu matumizi, Wizara inaendelea kuhakikisha matumizi yanafanya kulingana na Kanuni, Taratibu na Sheria za fedha za Serikali. Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kimeendelea kuimarishwa na kimeweza kutoa mchango mkubwa wa kusimamia matumizi mazuri ya fedha za Serikali, aidha Wahasibu wamepata nafasi ya kupata mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ili kuwaongezea uwezo wa kufanya kazi zao kitaalaumu zaidi kwa kufuata Kanuni, taratibu na sheria za fedha za Serikali. Pia Kamati ya Ukaguzi wa Hesabu (Audit Committee) imeimarishwa na inapitia taarifa zinazotolewa na Mkaguzi Mkuu wa Ndani kila robo mwaka na kutoa maagizo mbalimbali. Utendaji huu wa Kamati ya Ukaguzi wa Hesabu umeongeza nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali katika Wizara yangu.

## Usimamizi wa Ununuzi

180. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wizara imeendelea kusimamia shughuli za ununuzi kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi Na.7 ya mwaka 2011 na kanuni zake za mwaka 2013, GN 446. Sheria hiyo kwa sasa ipo kwenye marekebisho chini ya Tume ya kurekebisha Sheria kwa madhumuni ya kubainisha upungufu katika utekelezaji wa sheria hiyo pamoja na madhara ya upungufu huo kwa Serikali na taasisi zake.

181. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika kutekeleza majukumu yanayohusu Usimamizi wa Ununuzi, Wizara kuitia Kitengo chake cha Ununuzi kimeteketeza majukumu yafuatayo;

- i) Kufanya manunuvi ya jumla ya Sh. 245,139,796 hadi robo ya pili ya mwaka ambapo Sh.110,837,888 zilitumika kununua bidhaa na Sh.134,301,912 zilitumika kununua huduma mbalimbali;
- ii) Kufanya vikao vya Bodi ya Zabuni vipatavyo vitano (5) na kufanikisha upatikanaji wa ridhaa ya Bodi katika mambo yanayohusu Ununuzi Wizarani na kuwezesha upatikanaji wa thamani ya fedha kwenye bidhaa na huduma zilizonunuliwa;
- iii) Kununua na kugawa bidhaa na huduma mbali mbali kwa mujibu wa Mpango wa Ununuzi wa Mwaka 2015/2016 ambapo taarifa za Ununuzi za mwezi na robo za mwaka ziliandaliwa na kuwasilishwa kwenye Taasisi ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA); na
- iv) Kuhakiki mali za Wizara (Physical Verification and stock taking) kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na kufanikisha uboreshaji wa daftari la Mali za Wizara (Updating Asset Register) kwa mujibu wa Sheria ya Fedha Na. 6 ya Mwaka na Kanuni zake, GN.132 2001iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2004.

## Masuala ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)

182. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wizara imeendelea kusimamia matumizi bora na sahihi ya vifaa na mifumo ya TEHAMA kwa watumishi ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na utoaji huduma kwa wadau wa ndani na wa nje. Katika Mwaka 2015/2016, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Wakala wa Serikali Mtandao ilipata kibali kutoka Benki ya Dunia na kumruhusu mtaalamu mwelekezi kuanza kazi ya utengenezaji wa Mfumo na Mtandao wa Tovuti ya Biashara ya Kitaifa (National Business Portal). Kazi ya utengenezaji wa mfumo inaendelea. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Chuo cha Utumishi wa Umma (Tanzania Public Service College) imekamilisha usimikwaji wa Mfumo wa Ufutiliaji wa Majalada (Computerized File Tracking

System) ambapo mafunzo juu ya matumizi ya Mfumo huu yameanza katika ngazi ya Menejimenti na yanaendelea kutolewa kwa watumishi. Aidha, Wizara imeboresha tovuti yake kulingana na mwongozo uliotolewa na Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma (Technical Standards and Guidelines for Government Websites – 2014) ili kutimiza mahitaji ya Serikali na wadau wote.

## HUDUMA ZA SHERIA

183. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika kutekeleza majukumu yanayohusu usimamizi wa sheria, Wizara kuitia Kitengo chake cha Sheria kimeteketeza majukumu yafuatayo;

- i) Wizara kwa kushirikiana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanya marekebisho ya Sheria ya Stakabadhi ya Ghala na imeandaa Kanuni ya Stakabadhi ya Ghala na Kanuni ya "Communication to the Public" inayosimamiwa na COSOTA kwa ajili ya kulinda wasanii;
- ii) Imeandaa "The Prescribed National Standards Notices" pamoja na Matamko matatu ya Kiwango (three Declaration on Standards za - TBS) kwa ajili ya kuweka viwango kwenye bidhaa zinazoingia nchini;
- iii) Imefanya mapitio ya Mikataba 44 ya Viwanda vilivyo binafishwa na kutoa ushauri wa kisheria;
- iv) Imeandaa Mikataba ya watoa huduma wote kwa Wizara; na
- v) Imeandaa "Mechantile Mark Act, Task Force for Fair Competition Commission" kwa ajili ya kumshauri Mtendaji Mkuu wa Ushindani kwenye kuteketeza bidhaa bandia.

## Mambo Mtambuka

### Kushughulikia Malalamiko

184. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika Mwaka 2015/2016, Wizara imeunda Dawati la kushughulikia malalamiko na kero za wadau wa nje. Dawati limeweka utaratibu wa kupokea, kukusanya, kufuafilia na kutafuta ufumbuzi wa malalamiko na kero na kuwasilisha taarifa kwenye Menejimenti ya Wizara. Aidha, umewekwa muda maalum wa wiki moja kushughulikia malalamiko na kero na kutoa mrejesho kwa wadau ndani ya muda maalumu.

## Kupambana na Rushwa

185. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kwa Mwaka 2015/2016 Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa kupambana na Rushwa kwa kuhakikisha kuwa Sheria, Kanuni na Taratibu zinazotoa miongozo ya utoaji huduma bora na uwajibikaji katika utumishi wa Umma zinafuatwa. Pia, Wizara imeendelea kuboresha huduma mbalimbali zinazotolewa kwa wateja wa ndani na nje baada ya kupatiwa mafunzo ya elimu ya huduma kwa mteja.

## Usimamizi wa Mazingira

186. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kwa Mwaka 2015/2016 Wizara kupitia vikao vya kisekta imeendelea kuhamasisha wenyewe viwanda kusimamia na kutekeleza miongozo inayohusu kuhifadhi na kulinda mazingira katika shughuli zote za uzalishaji viwandani. Aidha, Wizara imeendelea kuhamasisha sekta Binafsi kutumia mitambo ya kisasa na rafiki kwa mazingira kwenye mlolongo wa uzalishaji (cleaner production) ambapo kiwanda kinatakiwa kutumia mitambo itakayozuia utoaji na umwagaji wa taka ovyo kabla ya kuanza na hata baada ya kukamilisha uzalishaji. Mfano viwanda vya saruji vinatoa vumbi jembamba wakati wa uzalishaji, ili kuzuia hali hiyo hutumia mitambo inayoitwa electrostatic precipitator ambayo ndani yake kuna majimaji yanayofyonza vumbi hilo kabla halijaachiliwa hewani. Vile vile, Wizara kwa kushirikiana na NEMC imeweza kufanya ukaguzi wa viwanda kwa lengo la kuwashauri juu ya utunzaji bora wa mazingira.

## Mapambano ya UKIMWI

187. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kwa mujibu wa Mwongozo wa Serikali, kupitia Waraka Na. 1 wa mwaka 2006 unaohusu utoaji huduma kwa watumishi wanaoishi na Virusi vya VVU na UKIMWI, kwa Mwaka 2015/2016 Wizara imeendelea kutoa huduma ya lishe, usafiri na virutubisho kwa watumishi wake wanne waliojiweka wazi na wanaoishi na VVU na UKIMWI. Huduma hii hutolewa kwa ajili ya kuboresha afya zao ili waweze kuchangia katika ujenzi wa Taifa. Pia, Watumishi wameendelea kusitizwa kupima afya zao kwa hiari na kujikinga na maambukizi mapya.

## JINSIA

188. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wizara kwa Mwaka 2015/2016 iliendelea kutoa elimu ya dhana ya jinsia kwa wadau wa sekta hususan Maafisa Biashara mikoani na maafisa wanaoshughulikia masuala ya wanawake mipakani. Pia iliendelea kutatua kero za wanawake wafanyabiashara kwa kuanzisha Dawati la kushughulikia masuala ya jinsia kwenye mipaka ya Tanzania na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

189. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wizara kwa kushirikiana na UN WOMEN imeandaa mfumo wa upatikanaji wa taarifa za utekelezaji zinazozingatia jinsia. Mfumo huo umeandaliwa na timu ya wataalam 15 kutoka Idara/Taasisi chini ya Wizara wanaohusika na masuala ya Jinsia. Aidha, maafisa wa M&E/waratibu wa Madawati 70 kutoka Wizara na Taasisi walijengewa uwezo wa ukusanyaji wa taarifa zinazozingatia jinsia kwa kutumia mfumo huo ambao unatarajiwa kuanza kutumika 2016/2017.

190. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wizara kwa kushirikiana na UN WOMEN wamefanya uchambuzi wa kijinsia kwa Sera mpya ya Biashara (National Trade policy) inayoandaliwa. Masuala muhimu yanayotiliwa mkazo katika Sera mpya ya Biashara (NTP) ni pamoja na kuhakikisha kuwa itawezesha ukuaji wa maslahi ya wanawake wafanyakazi na kuwezesha wanawake katika viwanda vidogo na biashara vidogo. Pia, Wizara imeandaa mafunzo maalum kwa ajili ya Maafisa Biashara wa Mikoa kuhusu Jinsia, upangaji wa bajeti inayozingatia jinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi tarehe 23-27 Novemba, 2015 iliyofanyika mkoani Dodoma. Jumla ya Maafisa Biashara wa Mikoa 26 ya Tanzania bara walishiriki. Aidha, washiriki walitakiwa kuandaa Mipango kazi ya kuwawezesha Wanawake kiuchumi katika mikoa wanayotoka kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

191. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Vilevile, Wizara inaratibu uanzishwaji wa Dawati la Kijinsia (Gender Help Desk) kwenye mipaka ili kuwasaidia wanawake wanaofanya biashara ya kimataifa. Mwongozo kwa ajili ya uanzishwaji wa Dawati la Kijinsia umeandaliwa na mafunzo kwa ajili ya kujengea uwezo maafisa wa Kamati ya Pamoja Mipakani yalifanyika 4-5 Februari, 2016 mkoani Dodoma. Jumla ya maafisa 35 kutoka mipaka ya Kabanga, Mutukula, Sirari na Namanga na Holili walinufaika. Mafunzo yalihuisha kanuni za Masuala ya Jinsia na wajibu wa maafisa katika uendeshaji wa madawati ya Kijinsia yaliyoanzishwa na Miongozo mbalimbali ya biashara za mipakani.

## 4.0 MALENGO YA MWAKA 2016/2017

### 4.1 IDARA ZA KISEKTA

#### 4.1.1 Sekta ya Viwanda

192. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika mwaka 2016/2017 Sekta ya Maendeleo ya Viwanda itatekeleza yafuatayo:-

- i) Kuhamasisha Sekta Binafsi kuanzisha na kuendeleza viwanda vinavyotumia malighafi za hapa nchini na kuvutia wawekezaji kujenga viwanda vya vifungashio (intergrated packaging industry);

- ii) Kutekeleza Miradi ya Kimkakati kwa kushirikisha Sekta Binafsi ambayo ni Mchuchuma na Liganga, Magadi Soda-Engaruka, Viwanda vya mbolea na kemikali na kufufua Kiwanda cha Kutengeneza Matairi cha General Tyre East Africa Ltd;
- iii) Kuanzisha na kuboresha vivutio vya uwekezaji katika viwanda vinavyozalisha ajira kwa wingi (Light Manufacturing) kwa kuwalenga zaidi wazawa;
- iv) Kuendelea kubainisha maeneo ya viwanda katika mikoa yote kwa matumizi ya sasa na mbeleni na kuendeleza maeneo Maalumu ya Uwekezaji (EPZ & SEZ);
- v) Kujenga Kongano za Viwanda (Industrial Clusters) hususan katika sekta ndogo za ngozi na bidhaa za ngozi (Dodoma) na nguo na mavazi katika eneo la TAMCO Kibaha;
- vi) Kukusanya, kuchambua na kuandaa wajih (profile) na takwimu za viwanda; Kuhamasisha vyuo vya ufundi stadi kuhusisha mafunzo ya ujuzi maalum wa viwanda (specialised industrial skills) katika mitaala yao ili kutatua upatikanaji wa ujuzi husika; Kujenga uwezo wa Taasisi za utafiti zilizo chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ili ziongeze uwezo wa mifumo yao ya uvumbuzi, uhamishaji na usambazaji wa teknolojia (technology tranfer, innovation and commercialization) na kuhamasisha Sekta Binafsi kuzitumia;
- vii) Kwa kushirikiana na Msajili wa Hazina kufanya uchambuzi wa mikabata ya viwanda vilivyobinafsishwa hasa vile vinavyosuasua na vilivyokufa na kuchukua hatua stahiki kwa wamiliki wa viwanda vilivyokiuka masharti ya mikabata ya mauzo;
- viii) Kuhamasisha wananchi kuunga mkono dhima ya ujenzi wa uchumi wa viwanda; na
- ix) Kuanza majadiliano na taasisi maalum za Serikali kama Jeshi, Polisi na Magereza juu ya kutumia taasisi hizo kuongeza kasi ya ujenzi wa uchumi wa viwanda 2017/2018.

#### **4.1.2 Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo**

193. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika Mwaka 2016/2017, Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo imepanga kutekeleza malengo yafuatayo;

- i) Kuhamasisha Serikali za Mikoa na Wilaya kutenga maeneo kwa ajili ya kuanzisha mitaa ya viwanda vidogo nchini;
- ii) Kuandaa muongozo kwa ajili ya kurasimisha shughuli za kiuchumi za wajasiriamali wadogo nchini;

- iii) Kufanya mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ya Mwaka 2003;
- iv) Kuwezesha upatikanaji wa mtaji wa ziada wa Shilingi 2,400,000,000 kwa wajasiriamali wadogo – NEDF;
- v) Kuwezesha upatikanaji wa teknolojia kwa wajasiriamali wadogo;
- vi) Kuifanya mageuzi (restructuring) SIDO kwa lengo la kuboresha huduma zake kwa walengwa;
- vii) Kuwezesha Sekta ya Samani kutoa huduma bora na ufanisi ikijumuisha kufanya tathmini ya mahitaji halisi ya sekta hiyo; na
- viii) Kuhamasisha na kusimamia maendeleo ya sekta ya mafuta ya mbegu hususan alizeti.

#### 4.1.3 Sekta ya Biashara

194. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika Mwaka 2016/2017 Sekta ya Biashara itatekeleza yafuatayo:-

- i) Kuendeleza majadiliano ya kibashara kati ya Nchi na Nchi (Bilateral), Kikanda (Regional) na Kimataifa (Multilateral) kwa ajili ya kupanua wigo wa fursa za masoko na biashara ili kuvutia uwekezaji;
- ii) Kuendelea kuimarisha wepesi wa kufanya biashara kwa kusimamia na kuratibu shughuli za Kamati za Kitaifa za Kuondoa Vikwazo vya Biashara Visivyokuwa vya Kiushuru (Non Tariff Barriers), Sheria za Afya ya Binadamu, Wanyama na Mimea (Sanitary and Phytosanitary Measures), Vikwazo vya Biashara vya Kiufundi (Technical Barrier to Trade) na Uwezeshaji wa Biashara (Trade Facilitation);
- iii) Kuendelea na maandalizi ya kutekeleza Mkataba wa Urahisishaji wa Biashara (Trade facilitation) chini ya Shirika la Biashara la Dunia (WTO);
- iv) Kuendelea na majadiliano ya kuanzishwa kwa Eneo Huru la Biashara la nchi za Afrika (Continental Free Trade Area) na Mikakati ya Kukuza Biashara mionganoni mwa Nchi Wanachama wa Afrika (Boosting Intra African Trade);
- v) Kukamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Biashara ya 2003; na
- vi) Kuendelea na maandalizi ya kuandika upya Sheria ya Anti Dumping and Counterfeit Measures kwa ajili ya kulinda viwanda vyetu pale itakapobidi.

#### 4.1.4 Sekta ya Masoko

195. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika Mwaka 2016/2017 Sekta ya Masoko itatekeleza yafuatayo:-

- i) Kuendelea kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji chini ya Mpango wa Matokeo Makubwa sasa – BRN;
- ii) Kuendelea kutafuta masoko ya bidhaa za mazao ndani na nje ya nchi;
- iii) Kuimarisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi Ghalani;
- iv) Kuendeleza Miundombinu ya Masoko nchini;
- v) Kuimarisha biashara za mipakani;
- vi) Kuwezesha vikundi vya wakulima, wajasiriamali na wafanyabiashara kutangaza bidhaa na huduma za Tanzania katika masoko ya Ndani, Kikanda na Kimataifa kwa njia mbalimbali ikiwemo maonesho ya Kibiashara Kitaifa, Kikanda na Kimataifa;
- vii) Kuimarisha Mfumo wa ukusanyaaji wa taarifa za Masoko;
- viii) Kufanya tafiti mbalimbali kuhusu masoko ya Mazao na Bidhaa;
- ix) Kuandaa Sera ya Taifa ya Kumlinda Mlaji (National Consumer Protection Policy);
- x) Kuandaa Sera ya Taifa ya Viwango (National Standard Policy);
- xi) Kukamilisha Sera na Mkakati wa Miliki Bunifu;
- xii) Kukamilisha Marekebisho ya Sheria ya Haki Miliki na Haki Shiriki ya Mwaka 1999; na
- xiii) Kukamilisha Marekebisho ya Sheria ya Vipimo.

#### 4.1.5 Sekta ya Uwekezaji

196. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika Mwaka 2016/2017, Idara ya Uwekezaji itatekeleza yafuatayo:-

- i) Kuhamasisha uwekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwekeza katika sekta mbalimbali za uchumi hapa nchini;

- ii) Kwa namna ya kipekee kubuni mpango na mkakati wa kuhamasisha Watanzania kuwekeza katika Sekta ya Viwanda;
- iii) Kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji hapa nchini ili kuondoa changamoto zinazowapata wafanyabiashara na wawekezaji;
- iv) Kukamilisha mapitio ya Sera ya Uwekezaji ya Mwaka 1996, Sheria yake ya mwaka 1997 na Kanuni zake;
- v) Kusimamia na kuratibu shughuli za Taasisi zilizopo chini ya Idara ya Uwekezaji ambazo ni Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) zinazotekeleza majukumu yanayohusu Uwekezaji nchini; na,
- vi) Kuratibu tafiti mbalimbali kuhusu uwekezaji.

## 4.2 TAASISI CHINI YA WIZARA

### Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO)

**Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika Mwaka 2016/2017, Wizara kupitia Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO) itatekeleza yafuatayo:-

- i) Kuendelea kutoa ushauri wa kitaalam na kiufundi kwa Benki ya TIB Development kweneo maeneo yote yanayohusu viwanda na sekta zinazoibukia za mafuta na gesi;
- ii) Kuendelea kutoa huduma za kitaalamu viwandani zenyelengo la kuongeza uzalishaji wa bidhaa bora bila kuchafua mazingira pia zinazolenga matumizi bora ya nishati;
- iii) Kuanzisha na kuhakiki maabara ya makaa ya mawe, mafuta na gesi itakayokuwa na viwango vya kimataifa na kuweza kutoa huduma bora kwa wazalishaji viwandani;
- iv) Kuendelea na mchakato wa kufanya utafiti na kutoa mafunzo kwa wadau mbalimbali wa Sekta ya Ngozi jinsi ya kupunguza uharibifu wa mazingira kwa kuhifadhi na kurejesha taka za ngozi ili kutengeneza bidhaa kama 'Leather boards';
- v) Kuendelea na kukamilisha mchakato wa kuhakiki na kuboresha maabara ya mazingira, kemia na ya vifaa vya kihandisi ili ziweze kufikia viwango vya kimataifa na kuweza kutoa huduma bora kwa wazalishaji viwandani;
- vi) Kuanzisha na kuhakiki maabara ya vipimo vya chuma kigumu (Iron and Steel metallurgy laboratory);

- vii) Kuwapa mafunzo wafanyakazi kumi kwenye 'ISO' (Specific professional skills development);
- viii) Kufanya matengenezo ya vifaa vya maabara ya mazingira, chakula na kemia;
- ix) Kutafiti vigezo vya uzalishaji wa chuma cha pua (steel bar production parameter) katika viwanda/mashine za kawaida za chuma (conventional rolling mill);
- x) Kuendelea kukamilisha mchakato wa kurejea Sheria ya Bunge Na. 5 ya mwaka 1979 ilioanzisha TIRDO; na
- xi) Kuendelea kutekeleza Mfumo wa Ufuatiliaji wa Mazao (traceability) kwa kutumia teknohamma na pia kusaidia utendaji wa kampuni ya GS1 National (Tz) Ltd kama mshauri wa kiufundi.

### **Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo (TEMDO)**

197. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kwa Mwaka 2016/2017, Taasisi ya Uhandisi na Usanifu wa Mitambo (TEMDO) itatekeleza yafuatayo:-

- i) Kubuni teknolojia mbalimbali zitakazowezesha uanzishwaji wa viwanda vidogo na vya kati kwa kutumia malighafi za nchini. Teknolojia hizo ni pamoja na: kutengeneza vifaa na vipuri vya pikipiki nchini na kutengeneza bidhaa mbalimbali kutokana na taka za mijini;
- ii) Kubuni na kuendeleza teknolojia zinazolinda mazingira, afya na kuendeleza nishati mbadala ikiwa ni pamoja na: mtambo wa kusafisha na kurejesha maji taka, jokofu litakalotumika kuhifadhi bidhaa mbalimbali; mtambo wa kuzalisha umeme kwa njia ya maji na mabaki ya mimea;
- iii) Kuendeleza na kuhamasisha mitambo ya kusindika mafuta ya kula (alizeti na mengineyo) pamoja na kukausha mazao mbalimbali ya kilimo kwa lengo la kuanzishwa kwa viwanda vidogo na vya kati;
- iv) Kuboresha miundombinu ya kiatamizi cha teknolojia na biashara na kutoa huduma kwa wajasiriamali watengenezaji wa mashine na vifaa kwa matumizi ya viwanda vidogo na vya kati; na,
- v) Kutangaza shughuli za taasisi kupitia vyombo vya habari na kushiriki kwenye maonesho ya kibashara ili kutangaza teknolojia zinazoendelezwa na Taasisi.

### **Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijiini (CAMARTEC)**

198. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kwa Mwaka 2016/2017, Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijiini (CAMARTEC) kitatekeleza yafuatayo:-

- i) Kuandaa kanuni mbalimbali zitakazowezesha utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya kituo;
- ii) Kutengeneza mashine maalumu kwa ajili ya kuandaa matofali yatakayotumika katika kueneza ujenzi wa nyumba za gharama nafuu nchini;
- iii) Kusambaza teknolojia zilizohakikiwa pamoja na kutoa mafunzo kupitia vikundi mbalimbali katika jamii;
- iv) Kuendeleza ujenzi wa mitambo ya biogas ambayo ni nishati rafiki kwa mazingira kwa ajili ya kuzalisha umeme, gesi ya kupikia kwa ngazi ya kaya na familia;
- v) Kubuni, kuendeleza, kutengeneza na kusambaza teknolojia mbalimbali zilizo rafiki na nafuu kwa ajili ya uboreshaji wa shughuli za kilimo na ufundi vijijiini;
- vi) Kutafuta maeneo kwa ajili ya kufanya majoribio ya zana za kilimo ili kubaini ubora wake kabla ya kusambazwa kwa watumiaji; na
- vii) Kutoa mafunzo kwa vikundi vitakavyosaidia ujenzi, uenezaji na usambazaji wa mitambo ya biogas kwa ngazi ya kaya kupitia Mradi wa Tanzania Domestic Biogas Programme (TDBP) kitaendelea. Aidha, Kituo kitatoa elimu juu ya matumizi ya mbolea hai (bioslury) katika kuongeza tija na uzalishaji kwenye kilimo.

### **Chama cha Hakimiliki Tanzania (COSOTA)**

199. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika Mwaka 2016/2017, COSOTA itatekeleza yafuatayo:-

- i) Kuimarisha shughuli za makusanyo ya mirabaha kutoka kwenye mashirika ya habari na utangazaji (redio na televisheni);
- ii) Kutoa elimu kwa wananchi na wadau wa sanaa kuhusiana na mambo ya Hakimiliki na Hakishiriki;
- iii) Kufanya ukaguzi wa kazi zinazolindwa na Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki (anti piracy raids);
- iv) Kushughulikia migogoro na kesi za Hakimiliki na Hakishiriki;

- v) Kushughulikia marekebisho ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7/1999 na Kanuni za Leseni na kanuni nyingine zinazohusiana na Hakimiliki;
- vi) Kuendelea kukusanya na kugawa mirabaha kwa wasanii; na
- vii) Kuendelea kusajili wanachama (wasanii) na kazi zao.

### **Bodi ya Leseni za Maghala (TWLB)**

200. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika Mwaka 2016/2017, Bodi ya Leseni za Maghala Tanzania itatekeleza yafuatayo:-

- i) Kuboresha mfumo wa utoaji leseni, na kupanua wigo wa mikopo kwa wakulima wa vijiji kwa lengo la kuongeza ufanisi katika biashara ya mazao ya kilimo;
- ii) Kuendelea kushirikiana na wadau zikiwemo taasisi za elimu ya juu kutoa mafunzo yanayohusu Mfumo wa Stakabadhi;
- iii) Kufanya utafiti kuhusu mazao yanayotumia mfumo ili kuwawezesha wadau kuwa na uelewa mpana kuhusu mazao na Mfumo kwa ujumla;
- iv) Kujenga uwezo wa wafanyakazi wa Bodi kutumia Mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa kununua vifaa na kuanzisha mifumo wa kielektroniki kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji, utunzaji na usambazaji wa taarifa za mfumo kwa wadau pamoja na kuwaelimisha wadau jinsi ya kutumia mifumo hiyo;
- v) Kuanzisha ofisi katika mikoa ya Mtwara na Lindi;
- vi) Kuendelea kutoa elimu ya Mfumo kwa wadau wote kwa kuandaa semina na makongamano, kushiriki katika vipindi vyta redio na televisheni, kusambaza vipeperushi na kuwatembelea wadau na kusikiliza maoni, ushauri na malalamiko yao kuhusu mfumo;
- vii) Kujenga uwezo kwa watendaji wa Bodi ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi;
- viii) Kuomba na kufuutilia ajira mpya za wafanyakazi wa Bodi ili kujaza ikama ya Bodi; na
- ix) Kuendelea kutafuta na kuboresha vyanzo vyta ndani vyta mapato ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Bodi.

### **Baraza la Ushindani (FCT)**

201. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Baraza La Ushindani (FCT) katika Mwaka 2016/2017 litatekeleza mambo yafuatayo:-

- i) Kusikiliza na kutoa maamuzi ya kesi za rufaa zinazotokana na mchakato wa udhibiti na ushindani wa kibiashara nchini;
- ii) Kuongeza uwezo wa Baraza katika kushughulikia kesi zinazohusu masuala ya ushindani wa kibiashara kwa kuwaongezea ujuzi wajumbe wa Baraza, Watumishi wa Baraza sambamba na maboresho katika mifumo ya utendaji kazi wa Baraza;
- iii) Kuendelea kutoa elimu kwa umma juu ya kazi za Baraza, umuhimu katika uchumi pamoja na namna ya kuwasilisha rufaa katika Baraza; na
- iv) Kuendelea kushughulikia masuala mtambuka ikiwa ni pamoja na utawala bora na mapambano dhidi ya UKIMWI na virusi vya UKIMWI.

### **Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA)**

202. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Malengo ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) kwa kipindi cha Mwaka 2016/2017 ni kama yafuatayo:-

- i) Kuendelea kuweka na kuboresha mifumo ya kiteknolojia itakayowawezesha wadau kupata taarifa na huduma kwenye mifumo ya kompyuta na kuwawezesha wateja kusajili kwa njia ya mtandao;
- ii) Kuendelea kufanya marejeo ya sheria zinazosimamiwa na Wakala ili ziweze kwenda na wakati;
- iii) Kuendelea kuelimisha umma kuhusu shughuli za Wakala na jinsi taarifa zinavyotolewa kwa njia ya mtandao na umuhimu wa kusajili biashara;
- iv) Kuendeleza watumishi na kuweka mazingira mazuri ya utendaji kazi ili kuongeza tija na uwajibikaji;
- v) Kuendeleza mahusiano na mashirika ya kimataifa ambayo Tanzania ni mwanachama;
- vi) Kuanza kwa ujenzi wa Jengo la BRELA kwa ajili ya Ofisi na Masijala;
- vii) Kuendeleza na kuimarisha ushirikiano na taasisi mbalimbali za Serikali na binafsi ambazo ni wadau wa Wakala;

- viii) Kutafuta rasilimali fedha kwa ajili ya kugharimia shughuli za maendeleo za Wakala; na,
- ix) Kufanya utambuzi wa viwanda vyote nchini vilivyo katika maeneo na visivyo kuwa katika maeneo ya viwanda na pia vilivyo na visivyo na leseni.

### **Wakala wa Vipimo (WMA)**

203. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Malengo ya Wakala wa Vipimo kwa Mwaka 2016/2017 ni yafuatayo:-

- i) Kukagua na kusimamia matumizi ya vipimo rasmi;
- ii) Kushirikiana na wadau kufanikisha kutungwa kwa Sheria Mpya ya Vipimo;
- iii) Kuhamasisha matumizi ya TEHAMA katika kutekeleza majukumu ya Wakala;
- iv) Kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi sahihi ya vipimo;
- v) Kuanzisha kazidata ya vipimo itakayotumiwa wakati tunapopanga na kufanya makadirio ya mapato ya Wakala;
- vi) Kukamilisha ujenzi wa jengo la upimaji wa matenki ya mafuta eneo la Misugusugu, Kibaha na ofisi ya Wakala Mkoani Kilimanjaro;
- vii) Kufanya maboresho ya Ofisi za Wakala wa Vipimo;
- viii) Kununua vitendea kazi yakiwemo magari na mitambo (verification trucks);
- ix) Kuanzisha na kutekeleza Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini (M&E system) ili kuimarisha utunzaji wa takwimu mbalimbali; na
- x) Kuongeza Idadi ya Watumishi.

### **Baraza la Taifa la Utetezi wa Mlaji (NCAC).**

204. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika kipindi cha Mwaka 2016/2017, Baraza la Taifa la Utetezi wa Mlaji (NCAC) litatekeleza yafuatayo:

- i) Kuwatetea walaji dhidi ya ushindani usio wa haki;
- ii) Kufanya marekebisho Sheria ya Ushindani ili kuimarisha utetezi wa haki za walaji; na

iii) Kushirikiana na wadau kuandaa Sera ya Taifa ya Kumlinda Mlaji.

### **Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Kuzalisha Bidhaa za Kuza nje (EPZA)**

205. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kwa Mwaka 2016/2017, Wizara kupitia Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Kuzalisha Bidhaa za Kuza Nje (EPZA) itatekeleza yafuatayo:-

#### **Bagamoyo SEZ**

- i) Kufanya usanifu wa kina wa ujenzi wa miundombinu ya ndani (barabara), katika eneo la awamu ya kwanza ya eneo la mradi;
- ii) Kuboresha makazi holela ya maeneo ya makazi ya Mlingotini, Kiromo na Zinga;
- iii) Kuendelea kufanya tafiti na ufuatiliaji wa kutathmini utendaji wa Mamlaka ya EPZ katika kufikia malengo yake;
- iv) Kuwezesha ujenzi na usambazaji wa miundombinu ya nje, umeme na maji kufikia eneo la mradi;
- v) Kumalizia kulipa fidia katika eneo lilihofanyiwa uthamini lenye ukubwa wa hekari 5,743;
- vi) Kuwezesha ujenzi wa makazi mapya katika eneo la Zinga kwa waliopisha Mradi wa Eneo la Viwanda (Port side Industrial Zone);
- vii) Kupima viwanja na kuchora ramani pamoja na gharama za usajili wa Hati Miliki katika eneo la awamu ya 1 na 2B la eneo la mradi wa viwanda; na
- viii) Kuendelea kuutangaza mradi kitaifa na kimataifa na kuendeleza shughuli zote za maendeleo ya mradi.

#### **Kurasini Logistic Centre**

- i) Kubomoa, kusafisha eneo na kujenga uzio kuzunguka eneo la mradi;
- ii) Kuandaa michoro itakayoonesha jinsi eneo litakavyokuwa ikiwemo matumizi; na
- iii) Kutafuta mwekezaji mahiri ili ajenge miundombinu na kuvutia wawekezaji.

#### **Maeneo Mengine**

- (i) Kumalizia fidia katika maeneo ya mradi yaliyofanyiwa uthamini ya Tanga, Bunda, Kigoma, Ruvuma na Manyoni SEZ;

- (ii) Kufanya Upembuzi Yakinifu na Mpango Kamambe katika miradi ya Mtwara, Tanga, Manyoni, Bunda na Ruvuma SEZ;
- (iii) Kufanya Usanifu wa Kina wa ujenzi wa miundombinu ya ndani katika maeneo ya mradi ya Tanga na Ruvuma;
- (iv) Kupima viwanja na ghamama za usajili wa Hati Miliki katika maeneo ya miradi ya Tanga, Kigoma, Manyoni, Bunda na Ruvuma; na
- (v) Kuendelea kutangaza miradi kitaifa na kimataifa na kuendeleza shughuli zote za maaendeleo ya miradi ya Tanga na Ruvuma.

### **Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC)**

206. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kwa mwaka 2016/2017, Wizara kuitia Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) itatekeleza yafuatayo:-

- i) Kuendeleza utekelezaji wa miradi unganishi ya makaa ya mawe ya Mchuchuma na Chuma cha Liganga - Ludewa;
- ii) Kuendeleza utekelezaji wa Mradi wa Kuzalisha Chuma Ghafi -(Ludewa);
- iii) Kukamilisha majaribio na kuanza uzalishaji katika Kiwanda cha Kuzalisha Viuadudu (biolarvicides) kwa ajili ya kuua viluwiluvi kwenye mazalia ya mbu wa malaria (TAMCO, Kibaha);
- iv) Kutekeleza Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa kutumia makaa ya mawe ya Ngaka (Mbinga, Ruvuma);
- v) Kufanya uchambuzi yakinifu kwa ajili ya kubainisha ghamama na teknolojia muafaka kwa ajili ya Kiwanda cha Kutengeneza Matairi cha General Tyre, Arusha;
- vi) Kukamilisha upembuzi yakinifu na kumpata mbia wa kujenga Kiwanda cha Kuzalisha Magadi Soda (Engaruka, Arusha);
- vii) Kuendeleza Mashamba ya Mpira ya Kalunga (Morogoro) na Kihuhwi (Tanga);
- viii) Kuhaulisha matumizi ya ardhi kutoka ardhi ya kijiji kwenda uwekezaji na kuanza utekelezaji wa Mradi wa Kilimo cha Michikichi na Kiwanda cha Kuzalisha Mafuta ya Mawese (Kisarawe, Pwani). Aidha, kuhamasisha mikoa ya Mbeya na Kigoma kuwekeza katika miradi ya michikichi;
- ix) Kujenga miundombinu muhimu katika eneo la viwanda TAMCO (Kibaha) na kupima viwanja katika eneo la KMTC na Kange;

- x) Kujenga uwezo wa wananchi wa maeneo husika ili wafaidike na miradi inayotekelawa na NDC;
- xi) Kuratibu uendelezaji wa Kanda za Maendeleo za Mtwara, Tanga, Kati na Uhuru;
- xii) Kufanya tafiti yakinifu na kuanzisha miradi mipya ya viwanda vitokanavyo na rasilimali asilia kama vile gesi, madini, kilimo na mifugo;
- xiii) Kutafuta fedha za kutekeleza mradi wa kuzalisha umeme wa upepo katika Mkoa wa Singida; na
- xiv) Kuanzisha kiwanda cha kuchimba na kusaga mawe magumu kwa ajili ya utengenezaji wa nguzo za umeme na mataruma ya reli.

### **Shirika la Viwango la Taifa (TBS)**

207. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika Mwaka 2016/2017, Wizara kupitia Shirika la Viwango la Taifa (TBS) itatekeleza yafuatayo:-

- i) Kuendeleza utaratibu wa kupima ubora wa bidhaa zote mahali zinapotoka kabla ya kuingia nchini (Pre-shipment Verification of Conformity to Standards – PVoC);
- ii) Kushirikiana kwa karibu na vyombo vingine vya Serikali kama Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA), Mkemia Mkuu wa Serikali, Mamlaka ya Udhifikasi wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Tume ya Ushindani (FCC) na Mamlaka ya udhifikasi wa Huduma za Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA), ili kuhakikisha kuwa bidhaa zinazoingia nchini ni zenyе ubora unackubalika;
- iii) Kuongeza idadi ya leseni za ubora kutoka leseni 200 zinazotarajiwa kwa Mwaka 2015/2016 na kufikia leseni 220 katika Mwaka 2016/2017;
- iv) Kuongezeka idadi ya upimaji sampuli kutoka 7,000 kwa mwaka hadi kufikia 7,500 katika Mwaka 2016/2017;
- v) Kuongezeka idadi ya vyeti vya ugezi kutoka 7,000 kwa mwaka hadi kufikia 7,500 kwa Mwaka 2016/2017;
- vi) Kutayarisha viwango vya kitaifa 220 vikiwemo viwango vya Sekta ya Huduma;

- vii) Kuendelea na juhudzi za kuhakikisha kwamba maabara zote za Shirika zinapata vyeti vya umahiri (laboratory accreditation) ili kuongeza kukubalika kwa bidhaa nyingi za Tanzania katika soko la ndani na la kimataifa;
- viii) Kuendelea kutoa mafunzo kwa wajasiriamali nchini kote kuhusu viwango vya udhibiti wa ubora wa bidhaa na kuongeza utoaji vyeti vya ubora wa bidhaa;
- ix) Kuendelea kuimarisha utaratibu wa kukagua ubora wa bidhaa ukiwemo ukaguzi wa magari kabla ya kuingia nchini;
- x) Kufungua ofisi mpya tatu za mipakani katika mikoa ya Kigoma, Rukwa na Mtwara;
- xi) Kufungua ofisi mpya katika mikoa ya Mwanza itakayohudumia mikoa ya Kanda ya Ziwa, Dodoma kwa mikoa ya Kanda ya Kati na Mtwara kwa mikoa ya Kusini; na
- xii) Kuanza ujenzi wa jengo la maabara ya kisasa na upanuzi wa miundombinu ya maabara.

### **Tume ya Ushindani (FCC)**

208. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika Mwaka 2016/2017, Wizara kupitia Tume ya Ushindani (FCC) itatekeleza yafuatayo:-

- i) Kulinda na kuendeleza ushindani katika soko;
- ii) Kumlinda na kumtetea mlaji;
- iii) Kupambana na kudhibiti bidhaa bandia na kutoa elimu ya bidhaa bandia kwa mlaji;
- iv) Kufanya tafiti mbalimbali juu ya masuala ya ushindani; na
- v) Kuongeza vyanzo vya mapato na kusimamia Sheria ya Matumizi kama ilivyopitishwa (sound financial acquisition and utilization).

### **Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC)**

209. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika kipindi cha Mwaka 2016/2017, Wizara kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania itatekeleza yafuatayo:-

- i) Kufanya utafiti wa uwekezaji wa kimataifa (Foreign Direct Investment – FDI) na faida za uwekezaji;

- ii) Kuanzisha Kitengo cha Ufuatiliaji na Uperembaji (M&E) kwa lengo la kuhakiki miradi iliyoandikishwa TIC;
- iii) Kufanya warsha za kisekta kuboresha uwekezaji na kutatua changamoto zao;
- iv) Kuhudumia wawekezaji kwa kuboresha huduma za One Stop Shop na kuwezesha usajili kwa njia ya mtandao;
- v) Kuwasaidia wawekezaji kupata vibali na hati mbalimbali za kisheria ili waweze kuwekeza hapa nchini;
- vi) Kuandaa na kusambaza taarifa sahihi kwa wawekezaji kuhusu fursa za uwekezaji pamoja na upatikanaji wa mitaji ya wabia;
- vii) Kutafuta maeneo yenyе ardhi inayofaa kuwekeza kwa kulenga mahitaji ya wawekezaji;
- viii) Kuwasaidia wajasiriamali wadogo na wa kati kuibua fursa za uwekezaji kwa lengo la kukuza biashara zao na kuongeza kipato;
- ix) Kuwahamasisha wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza kwenye sekta muhimu zitakazokuza uchumi kwa haraka hasa viwanda; na
- x) Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Kituo ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

### **Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE)**

210. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika Mwaka 2016/2017, Wizara kuitia Chuo Cha Elimu ya Biashara (CBE) itatekeleza yafuatayo:-

- i) Kujenga uwezo (capacity building) wa wahadhiri kuitia mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi ya shahada za uzamili na uzamivu;
- ii) Kuboresha miundombinu ya Kampasi ya Dar es Salaam na Dodoma;
- iii) Kuandaa Mpango Kamambe (Master Plan) kwa Kampasi ya Mbeya;
- iv) Kuanzisha kozi mpya za shahada ya uzamili (master degree) katika masomo ya biashara; na
- v) Kuongeza urefu wa jengo la mgahawa kwa ajili ya kupata kumbi za mihadhara na maktaba kwa Kampasi ya Dar es Salaam.

### **Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO)**

211. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika Mwaka 2016/2017, Wizara kupitia Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) itatekeleza malengo yafuatayo:-

- i) Kuendelea kuboresha huduma ya maeneo ya kufanya kazi kwa kujenga miundombinu ya mitaa ya viwanda vidogo katika mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Morogoro na Mwanza;
- ii) Kujenga uwezo wa vituo vyta kuendeleza na kuhawilisha teknolojia na kuhakikisha vinatengeneza bidhaa bora na zenye uwezo wa kushindana;
- iii) Kutoa ushauri na mafunzo katika suala la teknolojia hasa katika kubuni, kuchagua, kununua, kutengeneza, kuuza na kuboresha;
- iv) Kutoa ushauri na mafunzo katika mambo ya rasilimali fedha hasa katika upatikanaji wake, udhibiti na uwekaji wa kumbukumbu;
- v) Kutoa mafunzo ya ujasiriamali, usimamizi wa biashara na kuongeza thamani malighafi zilizoko katika wilaya zote nchini;
- vi) Kukusanya na kutoa taarifa za masoko kwa wajasiriamali ikiwa ni pamoja na kuwaunganisha wajasiriamali wadogo na wakubwa;
- vii) Kujenga uwezo wa wajasiriamali kupata na kutumia taarifa za masoko kupitia TEHAMA; na
- viii) Kuboresha programu ya viatamizi (incubators) na kongano (cluster) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kama vile sekta binafsi, wanataluma na taasisi za ufundi.

### **Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE)**

212. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika Mwaka 2016/2017, Wizara kupitia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) itatekeleza yafuatayo:-

- i. Kutoa mafunzo ya kuchuna ngozi kwa kushirikiana na Taasisi ya Teknolojia ya Dar-es-Salaam, Kampasi ya Mwanza kwa wachunaji 500 katika Mikoa ya Tanzania Bara na Zanzibar ili kupata ngozi bora kwa ajili ya viwanda vyta ndani na nje ya nchi;
- ii. Kutoa mafunzo ya kutengeneza viatu na bidhaa za ngozi kwa wajasiriamali 100 wa Kanda ya Kati yatakayofanyika katika Chuo cha Ngozi cha SIDO kilichopo

Dodoma. Vilevile, mafunzo yatasolewa kwa wajasiriamali 100 wa Kanda ya Kaskazini yatakayofanyika katika Taasisi ya Teknolojia, Kampasi ya Arusha. Mafunzo hayo yanatarajia kuwawezesha washiriki kupata utaalamu wa kutengeneza bidhaa za ngozi, kuzalisha ajira na kuongeza kipato na kukuza uchumi wa nchi kwa ujumla;

- iii. Kutoa mafunzo ya ufugaji bora wa nyuki kwa ajili ya kuzalisha asali bora kwa wafuga nyuki 450 wa Mikoa ya Singida, Tabora na Shinyanga. Mafunzo hayo yatafanyika katika Kituo cha Kuchakata Asali kilichopo Mjini Singida kwa ushirikiano na Taasisi ya Singida Youth Entrepreneurs and Consultants Cooperative Society kinachoundwa na vijana wahitimu wa vyuo vikuu vya hapa nchini;
- iv. Kuwawezesha wazalishaji 200 wa ufuta wa mikoa ya Lindi na Mtwara kupata mbegu bora ya ufuta itakayowezesha kuongeza uzalishaji kwa ajili ya soko la ndani na la nje. Mafunzo ya kilimo bora cha ufuta yatasolewa kwa wakulima kwa kushirikiana na Taasisi ya AMSHA yenyewe wanachama wapatao 5,000 waliopo katika mikoa hiyo miwili;
- v. Kutoa mafunzo ya rajamu (branding) na mitindo (design) kwa watengeneza Vikapu vya "MASASI" 100 vinavyotengenezwa katika Kijiji cha Nangomba, Wilaya ya Masasi Mkoa wa Mtwara na baadaye kuwawezesha kuuza bidhaa zao katika soko la ndani na lile la Afrika Mashariki (EAC);
- vi. Kuwakesha wenye viwanda vidogo vya ngozi 60, wazalishaji wa asali 80 na wazalishaji wa vikapu 40 kushiriki Maonesho ya 41 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam 2016 na kuwakutanisha na wanunuzi wa bidhaa hizo kutoka ndani na nje ya nchi;
- vii. Kutoa mafunzo maalum ya ubora wa pilipili manga, mdalasini, tangawizi na karafuu kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kwa wakulima 300 wa Morogoro Vijijini, Muheza na Same na kuwawezesha kukutana na wanunuzi wa ndani na nje ya nchi;
- viii. Kuratibu na kudhibiti uendeshaji wa Maonesho ya Kimataifa nchini kwa mujibu wa sheria; na,
- ix. Kuimarisha uwezo wa Mamlaka kutoa huduma bora na kuijendesha.

#### 4.3 MAENDELEO YA RASILIMALI WATU NA UTOAJI WA HUDUMA

213. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika Mwaka 2016/2017, Wizara kuitia Idara ya Utawala na Maendeleo ya Rasilimali Watu itatekeleza yafuatayo:

- i) Kuajiri watumishi wapya 12 wa kada mbalimbali ili kuziwezesha Idara na Vitengo kupata rasilimali watu ya kutosha ili kutoa huduma inayotarajiwa. Aidha, watumishi 88 wanatarajia kupandishwa vyeo. Wizara inatarajia kujenga uwezo kwa rasilimali watu kwa kuwapeleka mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika vyuo mbalimbali ili kuboresha utendaji wao wa kazi pamoja na kuwawezesha kukidhi mahitaji ya kimuundo katika kada mbalimbali.
- ii) Katika Mfumo wa Wazi wa Mapitio ya Tathmini ya Utendaji Kazi (MWATUKA au OPRAS), Wizara itatekeleza yafuatayo;
  - Kutoa mafunzo kwa watumishi wapya watakaoajiriwa kuhusu namna ya ujazaji wa fomu za OPRAS;
  - Kuhakikisha kuwa watumishi wote wanasaini mikataba yao ya kazi kwa wakati;
  - Kufanya mapitio ya nusu mwaka; na
  - Kufanya tathmini ya utendaji kazi wa watumishi wa mwaka mzima kwa wakati.
- iii) Kuendelea kuratibu na kusimamia masuala yote ya uendeshaji wa shughuli za Wizara;
- iv) Kutoa huduma stahiki kwa viongozi na watumishi wa Wizara kwa kuzingatia Taratibu, Miongozo, Kanuni na Sheria za Utumishi wa Umma; na
- v) Kuwa na program mbalimbali za michezo kwa lengo la kujenga afya za watumishi, kushirikiana na kufahamiana.

#### 4.4 MAMBO MTAMBUKA

##### Kudhibiti Rushwa

214. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kwa Mwaka 2016/2017, Wizara itaendelea na jitihada za kupambana na kudhibiti rushwa kwa watumishi wake kwa kuweka mikakati mbalimbali na kutoa mafunzo ya sheria mbalimbali za kazi, kanuni na taratibu zinazotoa miongozo ya utoaji wa huduma bora na uwajibikaji katika Utumishi wa Umma na kuhakikisha kuwa zinafuatwa. Aidha, Wizara itahakikisha kuwa inawachukulia hatua za kinidhamu watumishi amba o watabainika kujihuisha na vitendo vya rushwa. Pia, Wizara itaendelea kutoa mafunzo ya Elimu ya Huduma kwa Mteja kwa watumishi ili kuwapatia mbinu za utoaji huduma kwa wateja wake wa ndani na nje ya Wizara.

## Mazingira

215. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Mojawapo ya malengo madhubuti ya Mwaka 2016/2017 katika Sekta ya Viwanda ni kuongeza jitihada katika kuhamasisha, kuhifadhi na kulinda mazingira katika shughuli zote za uzalishaji viwandani. Wizara itaendelea kutekeleza mikakati inayohusu utunzaji wa mazingira na program ya utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi na Utunzaji wa Mazingira Viwandani. Aidha, Wizara itahakikisha inaongeza uelewa kwa wenye viwanda juu ya matumizi ya mitambo ya kisasa katika uzalishaji ili kupunguza utiririshaji wa maji taka hususan yale yaliyo na kemikali hasa katika uchafuzi wa vyanzo vya maji na kupunguza uzalishaji wa taka ngumu. Viwanda vya sekta zifuatazo vitasimamiwa kwa ukaribu zaidi: Sekta ya Ngozi (viwanda vya ngozi); Sekta ya Nguo (viwanda vya nguo); Sekta ya Plastiki (viwanda vya plastiki); Sekta ya Chuma (viwanda vya chuma); Sekta ya Mafuta ya Kula (viwanda vya mafuta ya chakula na sabuni); na Sekta ya Karatasi (viwanda vya karatasi na vifungashio).

## Kupambana na UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza

216. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Kwa mujibu wa Waraka wa Utumishi Na.2 wa Mwaka 2004 kuhusu Kudhibiti Virusi vya UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza Mahali pa Kazi katika Utumishi wa Umma, Wizara itaendelea na jitihada za kupambana na janga hilo kwa kuhakikisha kuwa watumishi waliojiweka wazi na wanaoishi na virusi vya UKIMWI wanapatiwa huduma ya virutubisho, usafiri na lishe ili kuboresha afya zao. Wizara pia, itaendelea kutoa mafunzo ya kujikinga dhidi ya maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI na kuhamasisha upimaji wa afya za watumishi kwa hiari. Zoezi hilo litatekelezwa kwa kutoa mafunzo kwa waelimisha rika ili waweze kupata mbinu mpya za kuwaelimisha watumishi wenzao pamoja na familia zao.

## Masuala ya Jinsia

217. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika Mwaka 2016/2017, Wizara kupitia Dawati la Jinsia itatekeleza yafuatayo:

- i) Kuhuisha suala la uzingatiwaji wa usawa wa kijinsia kwenye uandaaji wa Sera ya Taifa ya Local Content na Sera mpya ya SME;
- ii) Kufuatilia upatikanaji wa huduma za kifedha na zisizo za kifedha (BDS) ili kuwezesha wanawake na wanaume wajasiriamali kufaidika na fursa za masoko na manunuza ya umma;
- iii) Kufuatilia upatikanaji na uendelezaji wa maeneo kwa ajili ya kongano nane na kuwezesha wanawake wajasiriamali kushiriki kwa wingi kwenye umiliki wa kongano na kufaidika na fursa zilizoko kwenye shughuli za minyororo ya thamani

ya bidhaa zitakazozalishwa kwenye kongano hizo katika mikoa ya Shinyanga (mchele na ngozi), Pwani (samani), Singida (alizeti), Dodoma (karanga), Mbeya (mchele), Njombe (maziwa) na Morogoro (sukari); na

- iv) Kuendelea kuimarisha Madawati ya Jinsia (Gender Help Desk) ya biashara mpakani kwa kutoa elimu ya jinsia kwa wadau katika Sekta ya Biashara, Viwanda na Uwekezaji hususan maafisa biashara walioko wilayani na mikoani.

### **USIMAMIZI WA MAPATO NA MATUMIZI**

218. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wizara yangu itahakikisha kwamba, kila anayestahili kulipa ada ya leseni anafanya hivyo, lli kuhakikisha kila anayefanya biashara anakuwa na leseni halali inayolingana na biashara anayoifanya, maafisa biashara wa Wizara na kitengo cha Ufutiliaji na Uperembaji (M & E Section) wakishirikiana na maafisa biashara walio katika Halmashauri na Manispaa zote nchini watafanya ukaguzi wa mlango kwa mlango wa kila mfanyabiashara na kuchukua hatua za kisheria kwa mfanyabiashara yejote atakayepatikana akifanya biashara bila leseni au leseni stahili.

219. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Wizara itahakikisha inafanya matumizi kulingana na kanuni, taratibu na sheria za fedha za Serikali. Matumizi yote yatafanyika kulingana na mpangilio wa bajeti ya Wizara (objective, targets and activities). Wizara katika kuhakikisha hilo linafanikiwa, itaendelea kuimarisha Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani ili waweze kuhakikisha taratibu zote za fedha zinafuatwa na malipo yanafanyika kulingana na vipaumbele vilivyowekwa kwenye bajeti ya Wizara. Aidha, wahasibu wataendelea kupewa mafunzo ili kupanua taaluma zao na kuweza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Pia, tutafanya mafunzo ya muda mfupi kazini juu ya sheria, taratibu na kanuni za fedha na manunuvi ya umma kwa Wahasibu, Maafisa Ugavi, Wakuu wa Idara na Vitengo, Wakurugenzi na Wahasibu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara. Lengo ni kuwapa mwangaza wa kuzijua sheria, taratibu na kanuni za msingi juu ya usimamizi wa fedha za Serikali. Mtumishi atakayefanya kinyume, sheria itachukua mkondo wake.

## **5.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2016/2017**

### **Mapato ya Serikali**

220. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika Mwaka 2016/2017, Wizara inatarajia kukusanya maduhuli ya Shilingi 20,000,000,000 ikilinganishwa na lengo la Shilingi 12,000,014,000 kwa mwaka 2015/2016 kutokana na ada za leseni, uuzaji wa nyaraka za zabuni, faini kwa kukiuka Sheria ya Leseni na makusanyo mengineyo.

## Maombi ya Fedha

221. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Katika Mwaka 2016/2017, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji inaomba kutengewa jumla ya Shilingi 81,871,992,000 ili kutekeleza majukumu ya Wizara. Kati ya fedha hizo, Shilingi 41,871,992,000, sawa na asilimia 51 ya bajeti ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 40,000,000,000, sawa na asilimia 49 ya bajeti ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Katika bajeti ya Shilingi 41,871,992,000 iliyotengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, Shilingi 36,566,995,000 ni kwa ajili ya Mishahara (PE) na Shilingi 5,304,997,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Aidha, Shilingi 40,000,000,000 zilizotengwa kwa ajili ya Maendeleo zote ni fedha za ndani.

## Fedha za Maendeleo za Ndani

222. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Miradi itakayotekeliza kwa fedha za ndani ni pamoja na miradi ya Kimkakati na ile ya Matokeo Makubwa Sasa (BRN). Miradi ya kimkakati iliyopangwa kutekelezwa ni pamoja na Mchuchuma na Liganga ambayo imetengewa Shilingi 10,000,000,000 kwa ajili ya kuchangia katika ulipaji wa fidia, kufanya uthamini wa eneo la kuhamishia wananchi wanaopisha eneo la mradi, kuwajengea makazi mapya na kusimamia utekelezaji wa kampuni ya ubia. Mradi wa Magadi Soda-Engaruka/Ziwa Natron umetengewa Shilingi 1,700,000,000 kwa ajili ya kukamilisha tafiti za teknolojia na kiuchumi, vyanzo vya maji, kufanya uthamini wa ardhi na mali, na kulipa fidia kwa wanaopisha mradi.

223. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Miradi mingine ni ya Kiwanda cha Matairi cha General Tyre - Arusha na kuendeleza mashamba ya mpira ambapo Shilingi 150,000,000 zimetengwa kwa ajili ya kuandaa andiko la mradi, kuendeleza mashamba ya mpira na kutafuta mbia mpya. Mradi wa Eneo la Viwanda la TAMCO Kibaha umetengewa Shilingi 9,000,000,000 kwa ajili ya kujenga miundombinu ya msingi ya viwanda (umeme, maji na barabara); na Mradi wa kuendeleza Kongano za Viwanda (Industrial Clusters) umetengewa Shilingi 1,000,000,000, kwa ajili ya kujenga miundombinu ya msingi ya Kongano la Sekta Ndogo ya Ngozi (Leather Value Addition Cluster) Mkoani Dodoma. Mradi wa Kuendeleza Soko la Kimkakati la Makambako umetengewa Shilingi 3,478,000,000 kwa ajili ya kulipia fidia ya ardhi.

224. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Vilevile, miradi ya kuendeleza ujasiriamali, imetengewa Shilingi 6,050,000,000 kwa ajili ya kuendeleza maeneo ya viwanda vidogo – (SIDO Industrial Estates) kwa mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Mbeya, na Mwanza; na Shilingi 2,400,000,000 zimetengwa kwa ajili ya kutunisha mtaji wa Mfuko wa NEDF hususan kuongeza wigo wa mikopo ya uzalishaji kwenye viwanda vidogo. Aidha, Mradi wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo (Agricultural Sector Development Programme - ASDP) umetengewa Shilingi

3,262,000,000, kwa ajili ya kuongeza thamani mazao ya kilimo hasa katika kuainisha na kubainisha teknolojia muafaka za uongezaji thamani mazao ya kilimo, kuzisambaza na kuwaelimisha wajasiriamali namna ya kutumia; Kutoa elimu ya matumizi ya vipimo sahihi, upangaji wa madaraja ya mazao ya kilimo, ufungashaji, umuhimu wa kuhifadhi mazao kwenye maghala, usindikaji wa mazao na matumizi ya nembo za mstari; na Kuimarisha Mifumo ya Taarifa za Masoko na kununua vitendea kazi vya wakusanya taarifa za masoko.

225. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Vilevile, jumla ya Shilingi bilioni 1.5 zimetengwa kwa ajili ya miradi ya tafiti katika Sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. TIRDO imetengewa Shilingi 500,000,000, kwa ajili ya kuendelea na uhakiki (accreditation) wa maabara ya mazingira na kurejesha taka za ngozi ili kupunguza uharibifu wa mazingira; Shilingi 500,000,000 zimetengwa kwa ajili ya CAMARTEC ili kubuni na kutengeneza teknolojia ya mashine za kufunga majani kwa ajili ya malisho ya mifugo; na Shilingi 500,000,000, zimetengwa kwa ajili ya TEMDO ili kubuni na kuendeleza mtambo wa kutengeneza umeme kutokana na nguvu ya maji - Micro-hydro power/electric generating system.

226. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Vilevile Shilingi 600,000,000, zimetengwa kwa ajili ya Mradi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (BEST) inayohusisha kutoa leseni kwa njia ya mtandao; Kurekebisha Sheria ya Leseni ya Mwaka 1972; Kuandaa Kanuni za Sheria ya Leseni itakayorekebishwa; na Kukamilisha na kuzindua "Tanzania Business Licensing Portal" ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa muhimu kwa wafanyabiashara na kupunguza muda wa usajili wa biashara. Aidha, Mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi (institutional support) za Tantrade, COSOTA na CBE, umetengewa Shilingi 100,000,000 kwa ajili ya mchango wa Serikali katika kuboresha miundombinu ya Uwanja wa Maonesho ya Biashara wa Mwl. J. K. Nyerere (Tantrade) hususan kuandaa Mpango Kamambe (Master Plan), upembuzi yakinifu na kuandaa Mpango wa Biashara (Business Plan). Shilingi 100,000,000, zimetengwa kwa ajili ya mchango wa Serikali wa kununua gari la ofisi ya COSOTA, na Shilingi 100,000,000, zimetengwa kwa ajili ya mchango wa ujenzi wa jengo la maktaba na madarasa (CBE) katika Kampasi ya Dar es Salaam.

227. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Shilingi 560,000,000 zimetengwa wa ajili ya kutoa mchango wa Serikali katika miradi ya wafadhili (counterpart fund) inayoendelea kutekelezwa chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Miradi hiyo ni pamoja na Muunganisho wa Ujasiliamali Vijijini (MUVI), Gender Mainstreaming, KAIZEN Program, UNIDO, Kuimarisha Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi Ghalani na Trade Mainstreaming.

## 6.0 HITIMISHO

228. **Mheshimiwa Naibu Spika**, naomba nichukua fursa hii kuwashukuru tena Watanzania wote na hasa Wazalendo wa Nchi hii kwa kuendelea kutuunga mkono katika jitihada zetu za kuendeleza Sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Katika kipindi kilicho mbele yetu, tutaendeleza jitihada za kujenga na kuimarisha misingi thabiti ya kujenga uchumi unaoongozwa na viwanda kama ilivyobainishwa katika DIRA 2025. Ni jukumu kubwa na nyeti ambalo linapaswa kuendelea kuungwa mkono na wapenda maendeleo wote na hasa Watanzania na wazalendo wote. Tunahitaji kila Mtanzania popote alipo kutimiza wajibu wake kwa kujituma, kubadilisha mtizamo na kuwa mstari wa mbele kulinda na kutetea jitihada za kuendeleza viwanda, biashara na uwekezaji kwa maslahi ya nchi yetu. Inawezekana, tutimize wajibu wetu.

229. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara [www.mit.go.tz](http://www.mit.go.tz).

230. **Mheshimiwa Naibu Spika**, naomba kutoa hoja.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tutamsikia Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira.

**TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA KUHUSU  
UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI,  
FUNGU 44 KWA MWAKA 2015/2016 NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO  
YA MAPATO NA MATUMIZI YA MWAKA WA FEDHA 2016/2017  
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**MHE. VICK P. KAMATA- MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA,  
BIASHARA NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda nimshukuru Mungu kwa baraka nyingi amazonijalia katika maisha yangu, zinazoniwezesha leo hii niendelee kuwa na afya njema hata niweze kusimama mahali hapa na kuwasilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda nimshukuru sana mume wangu mpenzi kwa Support kubwa anayonipa na utulivu mkubwa unaonifanya niendelee kufanya kazi zangu hapa Bungeni. Sipendi kuwasahau wanawake wote wa Geita walionichagua kwa kura nyingi sana na kunituma niwawakilishe tena kwa miaka mingine mitano. Nawashukuru sana watoto wangu kwa Sala na moyo wanaonitia hadi naendelea kuwa mtu wa furaha na amani kama nilivyo sasa. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Bunge

ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Fungu 44 kwa mwaka wa 2015/2016 na makadirio ya Bajeti ya mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, wakati wa kampeni na baada ya kuingia madarakani amekuwa akielezea azma ya Serikali yake ya kufufua na kuanzisha viwanda vingi nchini ili kuifanya nchi yetu iwe nchi ya uchumi wa viwanda. Kauli ya Mheshimiwa Rais ni ahadi kwa wananchi inayopaswa kutekelezwa pia ni agizo kwa mamlaka husika linalohitaji kutekelezwa. Dhamana ya utekelezaji wa agizo hili uko chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa fasili ya 7(d) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, inazipa Kamati za Kisekta jukumu la kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara husika. Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira imepewa jukumu la kusimamia Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Hii inamaanisha kuwa Kamati imekasimiwa na Bunge jukumu la kusimamia utekelezaji na ahadi za kuelekea kwenye nchi yetu yenye uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, naomba kukushukuru kwa kututeua kuwa Wajumbe wa Kamati hii. Tuliahidi Bunge lako Tukufu kwamba tutatekeleza majukumu yetu kwa weledi na juhudhi kubwa ili kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza azma yake ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa viwanda na hivyo kuinua hali ya hadhi ya uchumi wetu kwa manufaa ya wananchi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijadili na hatimaye kuishauri Wizara ipasavyo. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1), Kamati ilifanya ziara katika baadhi ya miradi iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2015/2016, kwa lengo la kuona hali halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo. Vile vile kwa mujibu wa Kanuni ya 98(2), Kamati ilikutana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ili kupokea taarifa za utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na kuchambua na kujadili maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii inalenga kuliomba Bunge lako Tukufu kuidhinisha maombi ya fedha kwa ajili ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, lakini pia kutoa mapendekezo kwa Bunge lako Tukufu kuhusu masuala kadhaa ambayo Kamati inaamini ni muhimu yakifanyiwa kazi ili kuiwezesha Tanzania kuwa nchi ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016; Kamati ilikutana na uongozi wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, makusanyo ya maduhuli; katika mwaka wa fedha wa 2015/2016, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ilipanga kukusanya jumla ya shilingi bilioni 12 kutokana na uuzaaji wa ada za leseni, nyaraka za zabuni pamoja na faini na makusanyo mengine. Hadi kufikia Machi, 2016 makusanyo yalikuwa yamefikia shilingi bilioni 8.9, Kamati inaipongeza Wizara kwa kufikia lengo hilo la ukusanyaji maduhuli kwa asilimia 74 hadi robo ya tatu ya mwaka wa fedha. Ni matumaini ya Kamati ifikapo Juni, 2016 robo ya mwisho ya asilimia 26, itakamilika na kukusanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina; katika mwaka wa fedha wa 2015/2016, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 87.47, kati ya fedha hizo shilingi bilioni 52.08 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 35.38 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Machi, 2016 Wizara ilikuwa imepokea shilingi bilioni 29.75 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Wizara na taasisi zilizo chini yake. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 34 tu ya fedha zilizotengwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016 kwa ajili ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya fedha hizo, zilizopokelewa ni shilingi bilioni 28.15 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na kati ya hizo shilingi bilioni 24.76 ni mishahara na shilingi bilioni 3.38 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) na shilingi bilioni 1.6 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2016 kati ya shilingi bilioni 35.38 zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 1.6 tu ndizo zilizopokelewa na Wizara. Kiasi hiki ni asilimia tano tu ya fedha zote zilizotengwa, fedha hizi zote ni sehemu ya bajeti ya fedha za nje peke yake. Kwa kuzingatia takwimu hizo ni dhahiri kwamba miradi mingi ya maendeleo iliyopangwa kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha haitatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaunga mkono dhamira ya Serikali ya kuifanya nchi yetu kuwa nchi ya uchumi wa viwanda ifikapo mwaka 2025, lakini hairidhishwi na kasi ya utekelezaji wa dhima hii. Hali hii ikiendelea itakuwa vigumu lengo la Tanzania kuwa nchi ya viwanda ifikapo mwaka 2025 kutimia, iwapo Serikali itaendelea kuchelewesha utekelezaji wa miradi ambayo ina mchango mkubwa sana katika Sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa 2015/2016; Kamati ilifanya ziara katika baadhi ya miradi ya maendeleo na kujionea hali halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji Fungu 44 iliidhinishiwa shilingi 2,150, 000,000 kwa ajili ya utekelezaji mradi namba 12,10 unajulikana kama NDC Revival of General Tyre, ambao ni mradi wa ukarabati na ufufuaji Kiwanda cha Matairi cha General Tyre kilichopo katika Mji wa Arusha, ambacho kilisimamisha uzalishaji wake tangu mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu ulipangwa kutekelezwa chini ya Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) ambapo mpaka sasa ukarabati wa majengo na mfumo wa umeme wa kiwanda kwa awamu ya kwanza na ya pili vimekwishakamilika. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya mradi huu kwa mwaka wa fedha 2015/2016 zilikuwa ni kwa ajili ya kukamilisha awamu ya tatu ya ukarabati wa mfumo wa umeme na mitambo ya uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kusikitisha ni kwamba licha ya mradi huu kutengewa fedha katika bajeti ya mwaka 2015/2016, lakini hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2016 mradi huu ulikuwa haujapelekewa fedha, jambo lililosababisha mradi huu kutokutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuchelewa kutekelezwa kwa mradi huu kumesababisha ongezeko kwa gharama za ufufuaji wa kiwanda kutoka bilioni 45 mwaka 2015/2016 mpaka kufikia bilioni 60 mwaka wa fedha 2016/2017. Fedha hiyo itahitajika kwa ajili ya kukamilisha ukarabati wa awamu ya tatu na kufanya majoribio ya uzalishaji kabla ya kuanza uzalishaji kamili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashangazwa na hatua ya Serikali kutenga fedha za tathmini katika mwaka wa fedha 2016/2017, wakati tathmini hiyo ilikwishafanywa na kukamilika. Kwa mujibu wa tathmini hiyo gharama ilikuwa ni shilingi bilioni 45 kwa mwaka wa fedha 2015/2016 kwa lengo la kufufua mitambo na mifumo ya umeme na kufanya uzalishaji wa majoribio.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inahoji kwa nini Serikali ifanye tena tathmini. Maeleo yaliyotolewa ni kuwa tathmini iliyofanywa awali haikufanywa kwa weledi hivyo Serikali inahitaji kufanya tathmini kwa mara nyingine na itafanywa na wataalam wenye weledi tena wenye tasnia ya matairi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati haioni nia ya dhati ya Serikali katika kufufua kiwanda hiki. Juhudi zilizofanyika kufufua kiwanda hiki hadi sasa hazitoshi kwani mitambo iliyopo imechoka na hata kama ikifanyiwa ukarabati haitaweza kuzalisha kwa uwezo unaostahili. Kamati inapendekeza Serikali itathmini upya

na kwa kina mwelekeo wa ufufuaji wa kiwanda hiki ili jje na mpango wenye tija. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilitembelea mradi wa viuadudu, mradi huu unamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100 chini ya Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) ambapo ujenzi wa kiwanda umekamilika. Uzalishaji ulipaswa kuanza Agosti 2015, lakini kazi ya majaribio ilisimama kutokana na kampuni iliyopewa kazi kukumbwa na uhaba wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipokea maelezo kuhusu faida za mradi huu pindi utakapokamilika kuwa ni kuzalisha viuadudu vitakavyoua viluilui vya mbu na kuipunguzia Serikali yetu mzigo mkubwa wa kununua madawa ya kuzuia malaria. Mradi huu pia utazalisha viuadudu vya ziada kwa ajili ya kuuza nje hivyo kuipatia Serikali yetu fedha za kigeni. Kiwanda hiki pia kitasaidia kuleta ajira kwa wananchi wa Kibaha na Tanzania kwa ujumla. Kamati inashauri Serikali kufanya jitihada na kuhakikisha kuwa fedha zinapatikana ili kukamilisha mradi huu muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipata fursa ya kutembelea Taasisi ya TIRDO chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Taasisi ya TIRDO inahusika na tafiti mbalimbali za viwanda na ina umuhimu wa kipekee katika kipindi hiki tunapoelekea kwenye Tanzania ya Viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na umuhimu wa taasisi hii ya TIRDO, Serikali haitoi ruzuku ya kutosha, kiasi kinachotolewa kimekuwa kikipungua mwaka hadi mwaka. Aidha, hakuna sheria yoyote inayoelekeza viwanda kutumia huduma ya TIRDO, hivyo imeifanya TIRDO ikose uhalali wa kufanya kazi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi inakumbana na changamoto kubwa ya uchakavu wa maabara na vifaa vya kitaalam vinavyotumika kufanya tafiti, hali hii huifanya TIRDO kutokuwa na uwezo wa kutimiza majukumu yake ya msingi. Kamati inatambua mchango mkubwa wa taasisi hii na inaishauri sana Serikali kuongeza ruzuku kwa taasisi hii ili ipate uwezo wa kutoa huduma nzuri kutimiza azma ya Taifa ya kufufua na kujenga viwanda nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilipata fursa ya kutembelea eneo la uzalishaji wa bidhaa kwa ajili ya kuuza nje, (Benjamin Mkapa Export Processing Zone) Mabibo, Dar es Salaam. Kamati ilijionea namna maeneo hayo yanavyoendeshwa, Kamati inaipongeza sana Serikali kwa juhudhi inazozifanya, bado kuna changamoto ya malipo ya fidia kwa wenyewe maeneo yaliyochukuliwa na Serikali. Kamati inaishauri Serikali kulipa fidia ya ardhi iliyotwaliwa kwa ajili ya uwekezaji huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilitembelea karakana ya viwanda vidogovidogo (*SIDO*) ili kupokea taarifa ya maendeleo ya viwanda vidogo nchini. Taasisi ya *SIDO* inatoa ushauri na huduma katika nyanja za ufundi, uongozi, uchumi na masoko pamoja na kuangalia ubora wa bidhaa na teknolojia, lakini pia *SIDO* inatoa mikopo kwa wajasiriamali na kuanzisha miradi ya viwanda vidogovidogo vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mchango huu mzuri sana na mkubwa wa *SIDO* kwa maendeleo ya uchumi wa nchi yetu, bado taasisi hii inakumbana na changamoto kadhaa zinazosababisha kukwama kwa utekelezaji wa majukumu yake. Changamoto hizo ni pamoja na uhaba wa fedha, kwani wakati mahitaji ya *SIDO* yakiendelea kuongezeka Serikali imekuwa ikiendelea kupunguza bajeti yake hivyo kuathiri kabisa utendaji wa *SIDO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati inashauri kwamba ili kuepuka ongezeko la gharama za utekelezaji wa miradi, miradi yote iliyotengewa fedha ipelekewe fedha kwa wakati kwa mwaka husika kwani ucheleweshaji unasababisha uchelewaji wa mradi. Aidha, ucheleweshaji huo unasababisha ongezeko la gharama katika mwaka wa fedha unaofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016. Wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Kamati ilitoa ushauri kwenye maeneo mbalimbali. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali imejitahidi kuzingatia ushauri wa Kamati japo kuna maeneo ambayo Serikali haikutekeleza ipasavyo kama inavyoainishwa kwenye taarifa ambayo Waheshimiwa Wabunge mnayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji inatarajia kukusanya shilingi bilioni 20 kutokana na ada za leseni, nyaraka na zabuni, faini kutokana na kukiukwa kwa sheria za leseni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji imetengewa jumla ya shilingi bilioni 95.69 kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Wizara. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 53.53 sawa na asilimia 56 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 42.15, sawa na asilimia 44 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Bajeti hii imeongezeka kwa asilimia 16 ikilinganishwa na bajeti inayotekeliza hivi sasa, yaani ya mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali itoe fedha zitakazoidhinishwa na Bunge kwa wakati. Kamati inaamini kwamba katika kufanya hivyo itaharakisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii katika kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Kamati inaamini kuwa Serikali inayo nia ya dhati ya kuikwamua nchi yetu kiuchumi kupitia Sera ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Kamati inaona kuwa upo umuhimu mkubwa wa kuhuisha sera, sheria na mikakati mbalimbali ya viwanda na biashara ili kuongeza tija katika maendeleo ya Sekta ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na sera na mikakati mingi ya kufufua viwanda kwa miaka mingi. Hali halisi ya viwanda mpaka sasa siyo ya kuridhisha hivyo ni lazima Serikali iangalie upya mikakati yake kwa makini, sababu za kutokufanikiwa katika mikakati hiyo mpaka sasa, hatua hii naamini kabisa itaisadia Serikali kupanga mikakati mipyä itakayoitoa nchi ilipo sasa na kusonga mbele zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi kubwa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ni kuratibu na kuweka mazingira wezeshi kwa wananchi na wawekezaji kuweka fedha zao kwa namna mbalimbali ili wao wapate faida na Serikali iweze kupata mapato na wananchi waweze kupata ajira. Kwa uelewa huu, kazi kubwa ya Wizara na Serikali kwa ujumla ni kuweka mazingira rafiki na wezeshi kwa wananchi, Kamati inaishauri Serikali iweke msukumo kwenye kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapongeza mipango mizuri ya Serikali ya kuendeleza sekta ya viwanda na ni wakati sasa wa kuweka mipango hiyo katika vitendo ili kuweza kufikia malengo ya kuifanya Tanzania kuwa nchi yenye uchumi wa kati ifikapo mwaka 2020/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapendekeza jitihada za pekee zielekezwe katika viwanda vinavyotumia malighafi za hapa nchini, kwa kuwa viwanda hivi vina mchango mkubwa zaidi katika kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja. Viwanda hivyo ni pamoja na miradi ya chuma ya Liganga, makaa ya mawe ya Mchuchuma ambayo ni miradi ya kipaumbele kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017-2020/2021) kwa ajili ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda. Kamati inaishauri Serikali kutekeleza miradi hii kwa haraka ili kuchochaea kukua kwa viwanda hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali na mamlaka zake zipunguze utitiri wa ushuru na tozo mbalimbali zinazoambatana na mazao ya kilimo, ikiwa ni pamoja na kuziondoa zile zisizo za lazima. Hatua hii itawapunguzia wakulima

gharama za uzalishaji na itatoa unafuu wa bei ya malighafi kwenye viwanda na kuongeza ushindani wa bei ikilinganishwa na bidhaa za nje. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ishirikiane na Wizara ya Kilimo na Mifugo kuhakikisha kuwa wakulima na wafugaji wanapatiwa utaalam bora ili kukidhi ubora unaotakiwa wa mazao ya mifugo na kilimo yanayohitajika viwandani kwa ajili ya uuzaji wa bidhaa bora zitakazoweza kukidhi ushindani katika soko la nje na soko la ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuweka kipaumbele katika kuweka mazingira wezeshi kwa viwanda vinavyoajiri watu wengi. Hatua hii itasaidia sana katika kupunguza tatizo la ajira nchini na kutoa fursa kwa watu wengi kujajiri, mfano, viwanda vya nguo vinavyotumia pamba, viwanda vya korosho, kahawa na mbegu za mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatakiwa kuhakikisha viwanda vya ndani vinapatiwa mazingira safi ya ushindani, suala hili liende sambamba na kuhakikisha kuwa bidhaa zinazozalishwa na viwanda vyetu vya hapa nchini zinapewa unafuu wa kodi ukilinganisha na bidhaa zinazotoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa viwanda ambavyo Serikali ina hisa chache, Kamati inapendekeza kwamba Serikali iongeze hisa zake ili kuvimiliki, hatua hii itasaidia kulinda maslahi ya Serikali na wafanyakazi. Kama ilivyofanya katika kiwanda cha General Tyre, TANELEC, Urafiki na viwanda vinginevyo.

Mheshimiwa Niabu Spika, Kamati inatambua kuwa Serikali inao mpango wa kuanzisha viwanda vipyta, hivyo Kamati inaipongeza sana Serikali kwa hatua hii. Ili uanzishwaji wa viwanda hivi uwe na tija ni lazima uzingatie maeneo maalum ya kijigrafia pamoja na upatikanaji wa malighafi. Kwa mfano viwanda vya kutengeneza bidhaa zinazotokana na mifugo vipelekwe maeneo yenye mifugo, mfano, maeneo ya Kanda ya Ziwa na Arusha. Viwanda vya Nguo vipelekwe maeneo yanayolima pamba, Viwanda vya Korosho vipelekwe maeneo ya Kusini na Pwani wanakolima korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi vipelekwe katika maeneo ya uvuvi, vile vile Serikali itoe upendeleo maalum kwa wawekezaji walio tayari kuwekeza katika maeneo haya niliyoyataja. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapendekeza Serikali itenye fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) kwa taasisi za udhibiti. Hatua hii itasaidia taasisi hizi kujikita katika majukumu yake ya msingi badala ya kujiielekeza zaidi kwenye ukusanyaji wa tozo mbalimbali kama inavyofanya hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Biashara. Kamati imebaini kuwa zipo changamoto kadhaa zinazoikabili Sekta ya Biashara kwa ujumla wake. Changamoto hizo hufanya ghamara ya uendeshaji biashara kuwa ya juu sana. Katika eneo hili Kamati ilikuwa na maoni yafuatayo:-

- 1) Katika uingizaji wa bidhaa kutoka nje Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya ucheleweshwaji wa kutoa mizigo bandarini. Kwa kuwa ucheleweshwaji huo unaongeza ghamara za biashara, Kamati inashauri Serikali kuona umuhimu wa kupunguza urasimu na hivyo kupunguza muda wa kutoa mizigo bandarini. Hatua hii itaongeza ufanisi wa bandari lakini pia itaongeza ari ya watumiaji wa bandari. (Makofii)
- 2) Kamati inaona kwamba kuna umuhimu wa mamlaka za udhibiti na ukaguzi zinazofanya kazi zinazofanana, zishirikiane ili kupunguza urasimu na ghamara. Kwa mfano, baadhi ya kazi zinazofanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Viwango yaani TBS na Mamlaka ya Udhibiti wa Dawa na Lishe TFDA zinazofanana. Aidha, udhibiti unaofanywa na OSHA unazofanana na Jeshi la Zimamoto, hivyo ni bora Serikali ikaunganisha huduma hizi ili kupunguza kero kwa watumiaji.
- 3) Kwa kuwa, kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wafanyabiashara wengi hapa nchi kuongezeka kwa bei ya bidhaa (*uplifting*), Kamati inashauri Serikali kuangalia upya vigezo vinavyotumika. Unakuja na gari yako, umenunua milioni tano, ukifika pale unaambiwa thamani ya hii gari milioni 200, inashangaza sana! (Makofii)
- 4) Nchi yetu ni mwanachama wa Jumuiya kadhaa za Kikanda na Kimataifa zenyetengo la kufungua fursa za kibashara. Katika mipango tunayojipangia kuelekea Tanzania ya viwanda, ni vema mamlaka husika zikajipanga vema kutumia fursa hizi za kibashara kwa kuwatafutia masoko wazalishaji wa bidhaa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Uwekezaji. Kamati inapongeza hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali katika kuchochea uwekezaji nchini ikiwa ni pamoja na juhudhi za kutenga maeneo maalum ya uwekezaji nchini chini ya mamlaka ya EPZA.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendeleza Sekta ya Viwanda, suala la kutenga maeneo maalum kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda nchini, lipewe umuhimu wa pekee na Kamati inashauri Serikali kushirikiana na mikoa pamoja na Halmashauri zote kutenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda nchini. Maeneo yatakayotengwa yawekewe utaratibu wa kuandaa miundombinu kama umeme, barabara, reli, maji na mawasiliano. Katika kufanya hivyo itavutia wawekezaji wa ndani na wawekezaji wa nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jithada kadhaa zinazofanywa na Serikali katika kuchochaea uwekezaji, hatua ya kufutwa kwa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwa bidhaa za nje (*deemed capital goods*) kulikofanyika katika Sheria Mpya ya VAT ya Mwaka 2014 kumekuwa ni changamoto kubwa kwa wawekezaji. Kodi hii imefanya gharama ya uwekezaji kuongezeka, hali hii imesababisha wawekezaji wengi kwa mfano watafutaji wa madini, watafutaji wa gesi, kuiona Tanzania siyo rafiki wa kuwekeza na kuamua kwenda kuwekeza katika nchi nyingine, mfano, Msumbiji, Angola na Kenya. Kamati inaishauri Serikali ipitie upya sheria hii ili kuhamasisha tena uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Ununuzi (*Public Procurement Act*) nayo ni tatizo kubwa katika kuhamasisha na kukuza viwanda nchini. Sheria huelekeza ununuzi wa bidhaa na huduma kwa bei nafuu (*lowest bidder*) na kusababisha ununuzi wa huduma za bidhaa hafifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii imesababisha taasisi za Serikali kama TANESCO kulazimika kununua bidhaa kama *transformer* zenye ubora wa chini kutoka nje na kuacha bidhaa zenye ubora mzuri kutoka viwanda vya ndani kwa mfano Tanelec, kiwanda kinachozalisha *transformer* zenye ubora nchini, lakini hakipati soko kutokana na Sheria hii ya Manunu.

Kamati inaishauri sana na inaisihi Serikali kuwa sheria hii ifanyiwe marekebisho ili masuala mengine kama ubora wa huduma viwe ni vigezo vya lazima, pia marekebisho haya yatoe kipaumbele maalum kwa wazalishaji wa ndani. Hatua hii itasaidia katika kulinda viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Kamati inaamini kuwa Tanzania ya viwanda inawezekana, Kamati inaishauri Serikali itekeleze Sera ya Viwanda kwa kuboresha viwanda vilivyopo na kuweka mazingira bora ya uanzishwaji wa viwanda vipyta. Pia Kamati inashauri kuwa mazingira ya ufanisi ya kibashara yaboreshewe kwa kuondoa changamoto zilizopo na kuhamasisha wawekezaji wa ndani na wawekezaji wa nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa Charles Mwijage, Katibu Mkuu Dkt. Meru na Profesa Adolf Mkenda pamoja na Wataalam wote wa Wizara ya Viwanda na Uwekezaji, kwa kuwa tayari kutoa ufanuzi na kupokea maoni na ushauri wa Kamati wakati wote wa majadiliano haya. Ni matarajio ya Kamati hii kwamba ushirikiano huu utaendelea katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda nitaomba taarifa yangu yote iingie kwenye Hansard.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya jumla ya shilingi 95,534,825,495 Fungu 44 kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017 ambapo shilingi 53,534,825,495 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 42,159,950,000 kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (Makofij)

**TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA KUHUSU  
UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI,  
FUNGU 44 KWA MWAKA 2015/2016 NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO  
YA MAPATO NA MATUMIZI YA MWAKA WA FEDHA 2016/2017  
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI:**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Fungu 44 kwa mwaka 2015/2016 na Makadirio ya Bajeti ya mwaka 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. John Pombe Joseph Magufuli wakati wa Kampeni na baada ya kuingia madarakani, amekuwa akielezea azma ya Serikali yake ya kufufua na kuanzisha viwanda vingi nchini ili kuifanya nchi yetu iwe nchi ya Uchumi wa Viwanda. Kauli ya Mheshimiwa Rais ni ahadi kwa wananchi inayopashwa kutekelezwa, lakini pia ni agizo kwa mamlaka husika linalohitaji kutekelezwa. Dhamana ya utekelezaji wa agizo hili iko chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa fasili ya 7(d) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 inazipa Kamati za Kisekta Jukumu la Kusimamia utekelezaji wa Majukumu ya Wizara husika. Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira imepewa jukumu la Kusimamia Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Hii inamaanisha kuwa, Kamati imekasimiwa na Bunge jukumu la kusimamia utekelezaji wa ahadi ya kuelekea kwenye nchi yenye Uchumi wa Viwanda.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa niaba ya wajumbe wa Kamati, naomba kukushukuru sana kwa kututeua kuwa wajumbe wa Kamati hii. Tunaliahidhi Bunge lako kwamba tutakeleza majukumu yetu kwa weledi na juhudhi kubwa ili kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza azma yake ya kuifanya Tanzania kuwa

nchi ya uchumi wa Viwanda, na hivyo kuinua hali na hadhi ya uchumi wetu kwa manufaa ya wananchi wote.

**Mheshimiwa Spika**, Katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilipata fursa ya kujifunza kuhusu majukumu, mafanikio na changamoto za utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Aidha, Kamati ilipitia Sera, Sheria na Mikakati mbalimbali inayosimamiwa na kutekelezwa na Wizara hii. Kamati pia ilipokea na kujadili taarifa mbalimbali za Wizara pamoja na baadhi ya Taasisi zilizo chini yake.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijadili na hatimaye kuishauri Wizara ipasavyo. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1), Kamati ilifanya ziara katika baadhi ya miradi iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2015/2016 kwa lengo la kuona hali halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo. Vilevile, kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2), Kamati ilikutana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ili kupokea taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na kuchambua na kujadili maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inalenga kuliomba Bunge lako tukufu kuidhinisha maombi ya Fedha kwa ajili ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, lakini pia kutoa mapendekezo kwa Bunge lako tukufu kuhusu masuala kadhaa ambayo Kamati inaamini ni muhimu yakafanyiwa kazi ili kuwezesha Tanzania kuwa nchi ya Viwanda.

## **2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 NA MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017.**

### **2.1 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana na uongozi wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji na kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa Fedha 2015/2016.

#### **2.1.1 Makusanyo ya Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ilipanga kukusanya jumla ya Shilingi Bilioni **12** kutohana na uuzaaji na ada za leseni, nyaraka za zabuni, faini na makusanyo mengine. Hadi kufikia Machi, 2016 makusanyo yalikuwa yamefikia Shilingi **8,910,207,736.69** Kamati inaipongeza Wizara kwa kufikia lengo ukusanyaji maduhuli kwa asilimia **74** hadi robo ya tatu ya mwaka wa fedha. Ni matumaini ya Kamati ifikapo June, 2016 robo ya mwisho asilimia 26 itakamilika kukusanya.

## 2.1.2 Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina.

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji ilitengewa jumla ya shilingi **87,470,349,000** kati ya fedha hizo shilingi **52,082,968,000** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi **35,387,381,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Machi, 2016, Wizara ilikuwa imepokea Shillingi **29,752,487,320** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara na taasisi zilizopo chini yake, kiasi hiki ni sawa na asilimia **34** tu ya fedha zilizotengwa katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016 kwa Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika**, kati ya fedha zote zilizopokelewa Shilingi **28,150,375,658** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na kati ya hizo Shilingi **24,769,189,947** ni mishahara, Shilingi **3,381,185,711** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) na Shilingi **1,602,111,662** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia mwezi Machi, 2016, kati ya Shilingi **35,387,381,000** zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni Shilingi **1,602,111,662** ndizo zilikuwa zimepokelewa na Wizara, kiasi hiki ni asilimia **5** tu ya fedha zote zilizotengwa. Fedha hizi zote ni sehemu ya bajeti ya fedha za nje tu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati hairidhishwi na namna Serikali inavyotoa fedha za Bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Wizara. Aidha kwa kuzingatia takwimu hizi ni dhahiri kwamba miradi mingi ya maendeleo iliyopangwa kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha haitatekelezwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaunga mkono dhamira ya Serikali ya kuifanya nchi yetu kuwa nchi ya Uchumi wa Viwanda ifikapo 2025 lakini hairidhishwi na kasi ya utekelezaji wa azma hii. Hali hii ikiendelea itakuwa vigumu lengo la Tanzania kuwa nchi ya Viwanda ifikapo 2025 kutimia, iwapo Serikali itaendelea kuchelewasha utekelezaji wa miradi ambayo inamchangio mkubwa katika sekta hii.

## 2.2 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGWEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ziara katika baadhi ya miradi ya maendeleo na kujionea hali halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo, Katika mwaka wa fedha wa 2015/2016, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji Fungu **44** iliidhinishiwa shilingi **2,150,000,000** kwa ajili ya kutekeleza mradi namba 1210 unaojulikana kama NDC-Revive of General Tyre ambao ni mradi wa ukarabati

na ufufuaji kiwanda cha Matairi cha General Tyre kilichopo katika mji wa Arusha ambacho kilisimamisha uzalishaji wake tangu mwaka 2009.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu ulipangwa kutekelezwa chini ya Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) ambapo mpaka sasa ukarabati wa majengo na mfumo wa umeme wa kiwanda kwa awamu ya kwanza na ya pili umekwishakamilika. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya Mradi huu kwa mwaka wa fedha 2015/16 zilikuwa ni kwa ajili ya kukamilisha awamu ya tatu ya ukarabati wa mfumo wa umeme na mitambo ya uzalishaji.

**Mheshimiwa Spika**, jambo la kusikitisha ni kwamba licha ya mradi huu kutengewa fedha katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016, lakini hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2016 mradi huu ulikuwa haujapelekewa fedha jambo lililosababisha mradi huu kutokutekelezwa.

**Mheshimiwa Spika**, kuchelewa kutekelezwa kwa mradi huu kumesababisha kuongezeka kwa gharama za ufufuji wa kiwanda kutoka **Bilioni 45** mwaka wa fedha 2015/2016 mpaka **Bilioni 60** mwaka wa fedha 2016/2017. Fedha hiyo itahitajika kwa ajili kukamilisha ukarabati wa awamu ya tatu na kufanya majaribio ya uzalishaji kabla ya kuanza uzalishaji kamili.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashangazwa na hatua ya Serikali kutenga fedha za tathimini katika mwaka wa fedha 2016/2017, wakati tathimini hiyo ilkwishafanywa nakukamilika. Kwa mujibu wa tathimini hiyo gharama ilikuwa ni Shilingi bilioni 45 kwa mwaka wa fedha 2015/2016, kawa ajili ya mitambo, mifumo ya umeme na kufanya uzalishaji wa majaribio.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilihoji kwanini Serikali inafanya tena tathmini. Maelezo yaliyotolewa kuwa tathimini iliyofanywa awali haikufanywa kwa weledi hivyo Serikali inahitaji kufanya tathimini kwa mara nyingine na itafanywa na wataalamu wenye weledi kwenye tasnia ya matairi.

**Mheshimiwa Spika**, hali ya utekelezaji wa mradi huu sio ya kuridhisha. Kamati haioni nia ya dhati ya Serikali katika kufufua kiwanda hiki. Juhudi zilizofanyika za kufufua kiwanda hicho hadi sasa hazitoshi kwani mitambo iliyopo imechoka na hata kama itafanyiwa ukarabati haitaweza kuzalisha kwa uwezo unaostahiki.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilitembelea Mradi wa Viuadudu, Mradi ambao unamillikiwa na Serikali kwa asilimia 100 chini ya Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) ambapo ujenzi wa kiwanda umekamilika. Uzalishaji ulipaswa kuanza Agosti 2015, lakini kazi ya majaribio ilisimama kutokana na kampuni iliyopewa kazi kukumbwa na uhaba wa fedha.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea maelezo kuhusu faida za mradi huu pindi utakapokamilika kuwa ni, kuzalisha viuadudu vitakavyoua viluilui vya mbu na kuipunguzia serikali mzigo wa kununua madawa ya malaria. Pia mradi huu utazalisha viuadudu vya ziada kwa ajili ya kuuza nje ya nchi hivyo kuipatia Serikali fedha za kigeni. Kiwanda hiki pia kitasaidia kuleta ajira kwa wananchi wa kibaha na Tanzania kwa ujumla. Kamati inashauri serikali kufanya jitihada na kuhakikisha kuwa fedha zinapatikana ili kukamilisha mradi huu na kuanza uzalishaji.

**Mheshimiwa spika**, Kamati ilipata fursa ya kutembelea taasisi ya TIRDO chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Taasisi ya TIRDO inahusika na tafiti mbalimbali za Viwanda na una umuhimu wa kipekee katika kipindi hiki tunapo elekea kwenye Tanzania ya Viwanda.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na umuhimu wa taasisi ya TIRDO Serikali haitoe ruzuka ya kutosha. Kiasi kinachotolewa kimekuwa kikipungua mwaka hadi mwaka. Aidha, hakuna sharia yoyote inayoelekeza Viwanda kutumia huduma ya TIRDO hivyo kuifanya taasisi hii kukosa uhalali wa kufanya kazi hizo.

#### **FEDHA ZILIZOTOLEWA NA SERIKALI KWA MIAKA MITATU KUANZIA 2012/2013-2015/2016**

**Mheshimiwa spika**, iligundulika hakuna sheria inayoelekeza Viwanda kutumia huduma ya TIRDO hali ambayo hupelekea Viwanda vitokavyo nje kutaka kufanyiwa tafiti na mashirika yanayotambulika kimataifa ambayo yapo nje hivyo TIRDO kukosa uhalali wa kufanya kazi hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha taasisi inakumbana na changamoto kubwa ya uchakavu wa maabara na vifaa vya kitaalamu vinavyotumika kufanya tafiti. Hali hii huifanya TIRDO kutokuwa na uwezo wa kutimiza majukumu yake ya msingi. Kamati imetambua mchango mkubwa wa taasisi hii na inaishauri Serikali kuongeza ruzuku kwa taasisi, ili ipate uwezo wa kutoa huduma nzuri katika kutimiza azma ya Taifa ya kufufua na kujenga Viwanda nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilipata fursa ya kutembelea Eneo la Uzalishaji wa bidhaa kwa ajili ya kuuza nje (Benjamin Mkapa Export Processing Zone) Mabibo Dar es salaam, ili kujionea namna maeneo haya yanavyoendeshwa. Kamati inaipongeza Serikali kwa juhudhi inazozifanya, lakini bado kuna changamoto ya malipo ya fidia kwa wenyewe maeneo yanayochukuliwa na Serikali. Kamati inaishauri Serikali kulipa fidia ya ardhi inayotwaliwa kwa ajili ya uwekezaji kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, kamati pia ilitembelea karakana ya Viwanda Vidogo Vidogo (SIDO) ili kupokea taarifa ya maendeleo ya viwanda vidogo nchini. Taasisi ya SIDO inatoa ushauri na huduma katika Nyanja za ufundi, uongozi, uchumi na masoko, pamoja na kuangalia ubora wa bidhaa na teknolojia. SIDO pia inatoa mikopo kwa wajasiriamali na kanzisha miradi ya Viwanda vidogo vidogo vijiji.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mchango huu mkubwa wa SIDO kwa maendeleo ya uchumi wa nchi bado taasisi hii inakumbana na chambamoto kadhaa ambazo zinakwamisha utekelezaji wa majukumu yake.. Changamoto hizo ni pamoja na uhaba wa fedha, kwani wakati mahitaji ya SIDO yakiendelea kuongezeka Serikali imeendelea kupunguza Bajeti yake hivyo kuathiri kabisa utendeji.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo kamati inashauri kwamba ili kuepuka ongezeko la gharama za utekelezaji wa miradi, miradi yote inayotengewa fedha ipelekewe fedha kwa mwaka wa fedha husika, kwani ucheleweshaji unasababisha kuchelewa utekelezaji wa miradi. Aidha ucheleweshaji huo unasababisha ongezeko la gharama katika mwaka wa fedha unaofuata.

### **3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KAMATI KUHUSU BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2015/2016**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Kamati ilitoa ushauri kwenye maeneo mbalimbali. Naomba kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imejitahidi kuzingatia ushauri wa kamati japo kuwa kuna maeneo ambayo serikali haikuyatekeleza ipasavyo kama inavyoainishwa kwenye taarifa hii;

i) **Serikali ihakikishe inalipa fidia katika maeneo yote yaliyofanyiwa tathmini yaliyopo chini ya EPZ na SEZ kufikia mwaka wa fedha 2015/2016 yenye gharama ya kufikia shilingi billion 60.** Maeleo yaliyotolewa na Wizara ni kuwa hadi kufikia Machi 2016 ni shilingi **3,048,904,930** tu ambazo zilikuwa zimetolewa na serikali kwa ajili ya ulipaji wa fidia. Fedha hizo zilitumika kulipa fidia katika maeneo ya mradi wa Tanzania China Logistics Centre. Kamati haikuridhishwa na juhudhi hizi za serikali katika kutekeleza agizo hili. Kuchelewa kulipa fidia ya shilingi **bilioni 60** imesabisha kuongezeka kwa fidia hiyo kufikia shilingi **Bilioni 190.9.**

ii) **Serikali iongeze jitihada za kufufua kiwanda cha General Tyre (EA) Ltd ikiwemo ukamilishaji wa ukarabati wa umeme wa awamu ya tatu na ukarabati wa mitambo na majaribio ya uzalishaji wa matairi ufanyike mapema.**

Mradi huu ilitengewa fedha lakini hadi kufikia Machi, 2016 ulikuwa haujapatiwa fedha. Kamati ilifanikiwa kutembelea mradi huu na kujionea utekelezaji hafifu.

**iii) Miradi inayosimamiwa na Shirika la Maendeleo la Taifa NDC ya makaa ya mawe ya Mchuchuma na chuma cha Liganga, mradi wa kuzalisha umeme wa Ngaka, mradi wa viuadudu na mradi wa uchimbaji magadi (Soda-Ash)-Ziwa Natron isimamiwe na kuratibiwa vizuri ili ikamilike kwa wakati uliopangwa.** Kamati inaendelea kusitiza kwa kuwa miradi hii ni ya muda mrefu na ni miradi muhimu katika kuchochea mageuzi ya Viwanda nchini. Kamati inashauri Serikali iongeze kasi ya utekelezaji wa miradi hii.

**iv) TIC iweka masharti kwa wawekezaji wanapokuja nchini kuwekeza kwa ubia pamoja na wazawa ili tuweze kunufaika katika miradi hiyo kuliko kuwauzia maeneo na wakiondoka nchini nchi inabaki haina kitu.** kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhimiza ushirikishwaji wa wazawa, ili kuwapatia ujuzi na teknolojia. Hatua hii itasaidia pindi muwekezaji anapoondoka nchini teknolijia na ujuzi itabaki kwa wazawa.

#### **4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017**

##### **4.1 Uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/2017**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji inatarajia kukusanya shilingi bilioni **20** kutoptana na ada za leseni, nyaraka za zabuni na faini kwa kukiuka Sheria ya Leseni.

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji imetengewa jumla ya shilingi **95,694,775,495** kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali ya Wizara. Kati ya fedha hizo shilingi **53,534,825,495** sawa na asilimia **56** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shillingi **42,159,950,000** sawa na asilimia **44** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Bajeti hii imeongezeka kwa asilimia 16 ikilinganishwa na bajeti inayotekelwa hivi sasa. Tunaipongeza sana Serikali kwa kuongeza Bajeti ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali itoe fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa wakati. Kamati inaamini kwamba katika kufanya hivyo itarahisisha utakelezaji wa Majukumu ya Wizara katika kutekeleza miradi ya maendeleo.

## 5.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaamini kuwa Serikali inayo nia ya dhati ya kuikwamua nchi yetu kiuchumi kuititia Sera ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Kamati inaona kuwa upo umuhimu mkubwa wa kuhuisha Sera, Sheria na Mikakati mbalimbali ya Viwanda na Biashara ili kuongeza tija katika maendeleo ya sekta za Viwanda na Biashara.

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo na Sera na Mikakati mingi ya kufufua Viwanda kwa miaka mingi. Hali halisi ya viwanda mpaka sasa si ya kuridhisha. Hivyo ni lazima Serikali iangalie upya mikakati yake kwa makini, sababu za kutofanikiwa katika mikakati hiyo mpaka sasa. Hatua hii itaisaidia Serikali kupanga mikakati mipyta itakayotoa nchi ilipokuwa sasa na kusonga mbele.

**Mheshimiwa Spika**, Kazi kubwa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ni kuratibu na kuweka mazingira wezeshi kwa wananchi na wawekezaji kuwekeza fedha zao kwa namna mbalimbali ili wao wapate faida, Serikali ipate mapato na wananchi wapate ajira. Kwa uelewa huu, kazi kubwa ya Wizara na Serikali kwa ujumla ni Kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji nchini. Kamati inaishauri serikali iweke msukumo mpya kwenye kuweka mazingira wezeshi (-VAT)

### 5.1 Sekta ya Viwanda

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza mipango mizuri ya Serikali ya kuendeleza sekta ya viwanda. Ni wakati sasa wa kuweka mipango hiyo katika vitendo ili kuweza kufikia malengo ya kuifanya Tanzania kuwa nchi yenye uchumi wa Kati ifikapo mwaka 2025.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapendekeza jitihada za pekee zielekezwe katika viwanda vinavyotumia malighafi za hapa nchini kwa kuwa Viwanda hivi vina mchango mkubwa zaidi katika kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja. Viwanda hivyo ni pamoja na miradi ya chuma Liganga na makaa ya mawe Mchuchuma ambayo ni miradi ya kipaumbele kwenye Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano 2016/2017-2020/2021 kwa ajili ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya Viwanda. Kamati inashauri Serikali kutekeleza miradi hii kwa haraka ili kuchochea kukua kwa viwanda nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali na mamlaka zake zipunguze utitiri wa ushuru na tozo mbalimbali zinazoambatana na mazao ya kilimo, ikiwa ni pamoja na kuziondoa zile zisizo za lazima. Hatua hii itawapunguzia wakulima gharama za uzalishaji, kutoa unafuu wa bei ya malighafi kwa wenye viwanda na kuongeza ushindani wa bei ikilinganishwa na bidhaa za nje.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ishirikiane na Wizara ya Kilimo na mifugo kuhakikisha kuwa wakulima na wafugaji wanapatiwa utaalamu bora ili kukidhi ubora unaotakiwa wa mazao ya mifugo na kilimo yanayohitajika viwandani kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa bora zianazoweza kukidhi ushindani katika soko la ndani na nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuweka kipaumbele katika kuweka mazingira wezesi kwa viwanda vinavyoajiri watu wengi. Hatua hii itasaidia sana katika kupunguza tatizo la ajira nchini nakutoa fursa kwa watu wengi kujajiri. Mfano viwanda vya nguo vinavyotumia Pamba, Viwanda vya Koroso, kahawa na mbegu za mafuta.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali inatakiwa kuhakikisha Viwanda vya ndani vinapatiwa mazingira safi ya ushindani. Suala hili liende sambamba na kuhakikisha kuwa bidhaa zinazozalishwa na viwanda vyetu vya hapa nchini zinapewa unafuu wa kodi ukilinganisha na bidhaa zinazotoka nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa viwanda ambavyo Serikali ina hisa chache, Kamati inapendekeza kwamba Serikali iongeze hisa zake ili kuvimiliki. Hatua hii itasaidia kulinda maslahi ya Serikali na wafanyakazi. Kama ilivyofanya kwa kiwanda cha General Tyre, Viwanda hivyo ni kama Tanelec, Urafiki na vinginevyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kuwa Serikali inao mpango wa kuanzisha Viwanda vipyta. Kamati inapongeza Serikali kwa hatua hii. Ili uanzishwaji wa Viwanda hivi uwe na tija ni lazima uzingatie maeneo maalum ya kijigrafia na upatikanaji wa malighafi. Kwa mfano viwanda vya kutengeneza bidhaa zitokanavyo na mifugo vipelekwe maeneo yenye mifugo mingi mfano maendeo ya kanda ya ziwa na Arusha. Viwanda vya nguo vipelekwe maeneo yanayolima pamba, Viwanda vya korosho vipelekwe maeneo ya kusini na pwani. Aidha viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi vipelekwe katika maeneo ya Uvumi. Vilevile serikali itoe upendeleo maalumu kwa wawekezaji walio tayari kuwekeza katika maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapendekeza serikali itengete fedha kwa ajili matumizi mengineyo (OC) kwa taasisi za udhibiti. Hatua hii itasaidia taasisi hizi kujikita katika majukumu yake ya msingi badala ya kujielekeza zaidi kwenye ukusanyaji wa tozo mbalimbali.

## 5.2 Sekta ya Biashara

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa zipo changamoto kadhaa zinazoikabili sekta ya biashara kwa ujumla wake. Changamoto hizo hufanya

gharama ya uendeshaji biashara kuwa juu. Katika eneo hili kamati ilikuwa na maoni yafuatayo:-

- i) **Mheshimiwa spika**, katika uingizaji wa bidhaa kutoka nje, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya ucheleweshwaji wa kutoa mizigo bandarini, kwa kuwa ucheleweshaji huu unaongeza gharama za biashara, Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kupunguza urasimu na hivyo kupunguza muda wa kutoa mizigo bandarini. Hatua hii itaongeza ufanisi wa Bandari lakini pia itaongeza ari ya watumiaji wa bandari.
- ii) **Mheshimiwa spika**, Kamati inaona kwamba kuna umuhimu wa Mamlaka za udhibiti na ukaguzi zinazofanya kazi zinazo fanana zishirikiane ili kupunguza urasimu na gharama. Kwa mfano baadhi ya kazi zinazofanya na Mamlaka ya Udhibiti wa Viwango (TBS) na Mamlaka ya Udhibiti wa Dawa na Lishe (TFDA) zinafanana. Aidha udhibiti unaofanywa na OSHA unafanana na jeshi la zimamoto ni vema Serikali ikaunganisha huduma hizi.
- iii) **Mheshimiwa spika**, kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wafanyabiashara wengi nchini kuhusu kuongeza bei ya bidhaa (Uplifting). Kamati inaishauri Serikali kuangalia upya vigezo vinavyotumika.
- iv) **Mheshimiwa spika**, Nchi yetu ni mwanachama wa Jumuiya kadhaa za kikanda na Kimataifa zenyе lengo la kufungua fursa za kibiashara. Katika mipango tunayojipangia kuelekea Tanzania ya Viwanda, ni vyema mamlaka husika zikajipanga vyema kutumia fursa hizi za kibiashara kwa kuwatafutia masoko wazalishaji wa bidhaa mbalimbali.
- v) **Mheshimiwa spika**, Kamati imebaini kuwa baadhi ya wazalishaji wa hapa nchini, wanalazimika kuagiza malighafi kutoka nje ya nchi kwa sababu ya unafuu wa gharama za malighafi hizo ikilinganishwa na zile zinazopatikana hapa nchini. Ughali wa malighafi za hapa nchini unatokana na sababu mbalimbali, ikiwemo gharama za uzalishaji na kodi zinazotozwa kwa uzalishaji huo. Kwa mfano, Kamati ilibaini kuwa, zao la Shayiri, linatozwa kodi asilimia **15**, Shayiri hii ikichakatwa kuwa Kimea (Malt) ambayo ni malighafi inayotumika kuzalisha bia. Shayiri hii inatozwa ushuru wa bidhaa wa asilimia **40** zaidi. Malt inayoagizwa kutoka nje hutozwa ushuru wa bidhaa wa asilimia **40**, hivyo kuifanya bei yake kwa nafuu ikilinganishwa na shayiri inayozalishwa hapa nchini. Viwanda vya chuma na misumari vinaagiza chuma kutoka nje wakati malighafi ya chuma ipo Tanzania, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha utekelezaji wa mradi wa chuma wa Liganga na ili malighafi hii ipatikane hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, kamati inashauri kupunguza kodi kwa mazao ya kilimo na mifugo pia kupunguza kodi za bidhaaa za kilimo ambazo zimechakatwa

kwa ajili ya matumizi ya viwanda. Kwa mfano pamba, shayiri, korosho, kahawa, ngozi, mbegu za mafuta.

### 5.3 Sekta ya Uwekezaji

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali katika kuchochaea uwekezaji nchini. Ikiwa ni pamoja na juhudzi za kutenga maeneo maalumu ya uwekezaji chini ya mamlaka ya EPZA.

**Mheshimiwa Spika**, Katika kuendeleza sekta ya Viwanda, suala la kutenga maeneo maalum kwa ajili ya uwekezaji wa Viwanda nchini lipewe umuhmu wa pekee. Kamati inaishauri Serikali kushirikiana na Mikoa pamoja na Halmashauri zote kutenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji wa Viwanda nchini. Maeneo yatakayotengwa yawekewe utaratibu wa kuandaa miundombinu kama umeme, barabara, reli, maji na mawasiliano. Katika kufanya hivyo itavutia wa uwekezaji nchini na hatimaye kuvutia wawekezaji wengi wa ndani na nje.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na jitihada kadhaa zinazofanywa na Serikali katika kuchochaea uwekezaji, hatua ya kufutwa kwa msamaha wa kodi ya Ongezeko la Thamani kwa bidhaa za mtaji (*Deemed Capital Goods*) kulikofanyika katika Sheria Mpya ya VAT ya mwaka 2014, kumekuwa ni changamoto kubwa kwa wawekezaji. Kodi hii imefanya gharama ya uwekezaji kuongezeka. Hali hii imesababisha wawekezaji kwa mfano watafutaji wa madini, mafuta na gesi kuiona Tanzania siyo rafiki wa uwekezaji na kuamua kwenda nchi nyingine kama Msumbiji, Angola na Kenya. Kamati inashauri Serikali iipitie upya sheria hii ili kuhamasisha tena uwekezaji nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Ununuzi (Public Procurement Act) nayo ni tatizo kubwa katika kuhamasisha na kukuza Viwanda nchini. Sheria hii huelekeza ununuzu wa bidhaa na huduma kwa bei nafuu (Lowest Bidder) na kusababisha ununuzu wa huduma na bidhaa hafifu. Sheria hii pia inasababisha taasisi za Serikali kama TANESCO kulazimika kununua bidhaa kama Transfoma zenye ubora wa chini kutoka nje na kacha bidhaa zenye ubora mzuri kutoka Viwanda vya ndani. Kwa mfano TANALEC kiwanda kinachozalisha Transfoma zenye ubora hapa nchini lakini hakipati soko kutokana na sheria ya manunuzi. Kamati inashauri kuwa sheria hii ifanyiwe marekebisho ili masuala mengine kama ubora wa huduma viwe ni vigezo vya lazima, pia marekebisho hayo yatoe kipaumbele maalumu kwa wazalishaji wa ndani. Hatua hii itasaidia katika kulinda viwanda vya ndani.

### 6.0 HITIMISHO:

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaamini kuwa TANZANIA YA VIWANDA inawezekana na Kamati inaishauri Serikali itekeleze Sera ya Viwanda kwa

kuboresha Viwanda vilivyopo na kuweka mazingira bora ya uanzishaji wa viwanda vipyä. Pia Kamati inashauri kuwa kuboresha mazingira ya ufanisi wa biashara yaboreshwa kwa kuondoa changamoto zilizopo na kuhamasisha uwelekezaji wa ndani na nje.

**Mhesimiwa Spika**, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji Mhe. Charles Mwijage (Mb), Makatibu Wakuu, Dr. Adelhelm Meru na Prof. Adolph Mkenda, pamoja na wataalamu wote wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa kuwa tayari kutoa ufanuzi na kupokea maoni na ushauri wa Wajumbe wa Kamati yangu wakati wote wa mjadala wa makadirio haya. Ni matarajio ya Kamati kuwa ushirikiano huu utaendelea katika mwaka ujao wa Fedha.

**Mhesimiwa Spika**, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ambao wameweza kutoa maoni, michango na mawazo yao mbalimbali katika kuboresha makadirio haya ili hatimaye yaletwe mbele ya Bunge hili tukufu. Orodha yao ni kama inavyosomeka hapa chini.

1. Mhe Dkt Dalaly P. Kafumu, Mb	Mwenyekiti
2. Mhe. Vicky P. Kamata, Mb	M/Mwenyekiti
3. Mhe. Salim H. Turky, Mb	Mjumbe
4. Mhe. Kalanga J. Laizer, Mb	Mjumbe
5. Mhe. Stanslaus H. Nyongo, Mb	Mjumbe
6. Mhe. Khatib S. Ally, Mb	Mjumbe
7. Mhe. Tauhida C. Gallos, Mb	Mjumbe
8. Mhe. Munira M. Khatibu, Mb	Mjumbe
9. Mhe. Anthony C. Komu, Mb	Mjumbe
10. Mhe. Godbless J. Lema, Mb	Mjumbe
11. Mhe. Dkt. Mary G. Mwanjelwa, Mb	Mjumbe
12. Mhe. Lameck O. Airo, Mb	Mjumbe
13. Mhe. Hawa S. Mwaifunga, Mb	Mjumbe
14. Mhe. Bal. Dkt Diodorus B. Kamala, Mb	Mjumbe
15. Mhe. Jesca D. Kishoa, Mb	Mjumbe
16. Mhe. Mbarouk S. Ali, Mb	Mjumbe
17. Mhe. Mussa R. Sima, Mb	Mjumbe
18. Mhe. Anatropia L. Theonest, Mb	Mjumbe
19. Mhe. Faida M. Bakar, Mb	Mjumbe
20. Mhe. Sylvestry F. koka, Mb	Mjumbe
21. Mhe. Gimbi D. Massaba, Mb	Mjumbe
22. Mhe. Martha M. Mlata, Mb	Mjumbe
23. Mhe. Joyce J. Mukya, Mb	Mjumbe
24. Mhe. Raphael Masunga Chegeni, Mb	Mjumbe
25. Mhe. Ibrahimu H. Mohamed Raza, Mb	Mjumbe
26. Mhe. Suleiman Ahmed Sadick, Mb	Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, naomba nikushukuru sana wewe mwenyewe binafsi na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kutupatia maelekezo mbalimbali kwa Kamati yetu ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati. Aidha, napenda pia kumshukuru na kumpongeza Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah, Makatibu wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira Bi. Zainab Mkamba, Bw. Wilfred Magova na msaidizi wa Kamati Bi. Paulina Mavunde kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fungu 44, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ambayo ni shilingi **53,534,825,495** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **42,159,950,000** kwa ajili matumizi ya maendeleo, Jumla ya shilingi **95,534,825,495**.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu, (Mb)

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA**

Mei, 2016

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira. Sasa tutamsikia Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI  
MHESHIMIWA ANTHONY CALIST KOMU (MB) KWA WIZARA YA VIWANDA  
BIASHARA NA UWEKEZAJI KUHUSU MAPITIO YA UTEKELEZAJI KWA  
MWAKA WA FEDHA 2015/2016 NA MAKADIRIO YA MAPATO  
NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17  
KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI**

**MHE. ANTHONY C. KOMU - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kutoa maoni ya Kambi Rasmi Bungeni juu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu mapitio ya utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017 chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuweza kusimama mbele ya ukumbi huu nikiwa mwenye afya njema. Naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuweza kutoa maoni haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru pia Mheshimiwa Freeman Mboge, Mbunge wa Hai na Kiongozi wa Kambi ya Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa imani yake kwangu na kunipa jukumu la kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Wizara hii nyeti ambayo imebeba dhana nzima ya Awamu ya Pili ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ya kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu (*nurturing industrialization for economic transformation and human development*).

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Moshi Vijijiini kwa imani yao kwangu na niahidi kwamba nitawawakilisha vizuri na kwa umakini mkubwa. Aidha, niwashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote hasa Wajumbe wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa ushirikiano mzuri katika kuhakikisha Bunge linatimiza majukumu yake ya Kikatiba. Mwisho lakini si kwa umuhimu ni kwa familia yangu ambayo imekuwa msaada mkubwa sana katika kutekeleza majukumu yangu. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niingie kwenye Wizara yenyewe. Kwanza ni ukosefu wa umakini na uongo wa Serikali kwa Bunge. Ukitabu cha fedha zilizopangwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa mwaka 2016/2017, Volume IV, utaona kuwa mradi wa kufufua Kiwanda cha General Tyre, Kasma 1210 zimetengwa shilingi milioni 150 tu kwa ajili ya mradi huo. Ukitabu randama ya Wizara ya Viwanda na Biashara, General Tyre, kasma 1210, ukurasa wa 148 imetengwa shilingi milioni 500 kwa ajili ya kufufua kiwanda hicho. Ila ukisoma mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ambao ultolewa na Wizara ya Fedha utaona kuwa General Tyre kwa mwaka huu wa fedha zimetengwa shilingi bilioni mbili fedha za ndani kwa ajili ya kufufua kiwanda hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ni hiyo hiyo ukitizama Mradi wa Magadi Soda katika Bonde la Engaruka, Arusha, takwimu zipo tofauti na hazifanani na hii inaleta hofu hapa kuwa Bunge linapitisha nini haswa? Ukitabu randama ukurasa wa 147 Kasma ya 1122, zimetengwa shilingi bilioni 1.7 kwa ajili ya mradi huu. Ukitabu Mpango wa Maendeleo wa 2016/2017 katika ukurasa wa 38, unasema zimetengwa shilingi milioni 700 tu kwa ajili ya mradi huu. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwenendo huu wa takwimu zisizofanana ambazo zote zinazungumzia mradi mmoja maana yake ni kuwa Serikali hii imekosa uratibu (*coordination*) na hivyo kila Wizara huja na vitu vyake na takwimu zake kama ilivyobainika hapo juu. Hali hii italiwia vigumu Bunge kupitisha bajeti hii kwani kwenye Kamati tulijadili miradi iliyokuwa kwenye

randama na fedha zilizombwa. Bunge lako lilishapitisha Mpango wa Maendeleo na viwango vya fedha zilizombwa kwa ajili ya kutekeleza mpango na leo tunajadili bajeti ya Wizara na tutapitisha vifungu vilivyoko kwenye Vitabu vya Matumizi na kile cha Maendeleo (*Volume IV*). Huu ni sawa na mchezo wa kuigiza. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kupata majibu ya kina kabla ya kupidishwa kwa bajeti hii ni Mheshimiwa Waziri wa Fedha anafanya uhuni wa kiasi hiki kwa kulidanganya Bunge? Kwani Wizara ya Fedha ndiyo wanaotoa viwango vya mwisho vya malipo kwa matumizi ya kawaida na kwa miradi ya maendeleo (*ceilings*) au ni Waziri wa Viwanda na Biashara na Uwekezaji? (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kuelewa takwimu zilizopitishwa na Kamati kwa miradi husika kwa makubaliano na Serikali inakuwaje zinakuwa tofauti na takwimu zinazopitishwa na Kamati ya Bunge Zima? Hapa ndipo uhuni na utapeli wanaofanyiwa Wabunge na Serikali yao. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inawaasa Waheshimiwa Wabunge kuwa makini kwa kuoanisha takwimu za fedha zilizopo kwenye randama na zile zilizotengwa kwenye vitabu vinavyopitishwa na Kamati ya Bunge Zima. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, Dira ya Taifa 2025 na kurudi nyuma kwa sekta ya viwanda, biashara na uwekezaji. Mipango mbalimbali ya Serikali katika sekta ya viwanda biashara na uwekezaji inaongozwa na Dira ya Maendeleo ya Taifa (*Development Vision 2025*) dira ambayo inaelekea kufeli na kushindwa kwa kiwango kikubwa kutimiza malengo yaliyokusudiwa ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025 iliundwa mwaka 1995 na leo hii ninavyozungumza inatimiza miaka 21. Imebakia miaka tisa tu kufika mwaka 2025 ambapo dira ya hiyo itakuwa inatimiza miaka 30 bila kuwepo hata kwa dalili za mageuzi makubwa ya viwanda hapa nchini. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge lako Tukufu na Watanzania wote kwa ujumla kuwa itatumia mbinu zippi ndani ya miaka mitano ijayo kufikia lengo la kuifanya Tanzania kuwa nchi yenyе kipato cha katii? Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kueleza kwa Watanzania ni kwa kiasi gani mikakati hiyo ya kuifanya nchi kuwa ya kipato cha katii itashughulika na maendeleo ya watu na hayatakuwa maendeleo ya vitu kama ilivyo hivi sasa? Hali ilivyo sasa, tunaona maendeleo ya majengo ya wachache yasiokuwa na uhusiano na uhalisia wa maisha ya Watanzania zaidi ya asilimia 80 waishio vijijini katika ufukara wa kupindukia. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha sana kuwa wakati wa uhuru sekta ya viwanda ilichangia Pato la Taifa kwa asilimia tisa. Mwaka 2011 wakati Serikali ya CCM inatoa mafanikio ya miaka 50 ya Uhuru, mchango wa sekta ya viwanda

katika Pato la Taifa ulishuka mpaka kufikia asilimia 8.6 baada ya miaka 50 iliyopewa CCM kuondoa umaskini, ujingga na maradhi, badala yake takwimu zake yenye zinaonyesha kuwa hali ni mbaya zaidi. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka mitano ijayo ya Mhehsimiwa Rais Magufuli inayotumia llani ya Uchaguzi wa CCM ya mwaka 2015 haina jambo jipya katika maendeleo ya sekta ya viwanda hapa nchini. Llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 inazungumzia maendeleo ya sekta ya viwanda katika muktadha ule ule ulioshindwa kuzaa matunda kwa zaidi ya miaka 50 iliyopita. Llani hiyo ya CCM inasema kuwa katika kipindi cha utekelezaji wa ilani hii ya 2015 – 2020 Chama cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali kuweka nguvu kubwa katika kukamilisha utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda Awamu ya Tatu 2010 - 2020 ambayo malengo yake ni kuiwezesha sekta ya viwanda kuchangia katika kufikia malengo ya maendeleo ya muda mrefu kama ilivyopitishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025 ni dira isiyokuwa na mwelekeo wenyе afya kwa Taifa letu hata katika hatua za utekelezaji imeendelea kusisitiza kuwa ifikapo 2025 uchumi wa Tanzania utakuwa umebadilishwa kutoka kwenye uzalishaji duni wa uchumi wa kilimo mpaka kufikia uchumi wa viwanda wa kati (*semi industrialized economy*). Kambi ya Upinzani Bungeni haioni suala hilo likitokea ifikapo mwaka 2025 kwa kuwa mipango ya Serikali ya CCM ni ile ile na hajibadilika na haina mikakati mahsus ya kubadili hali hii. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kufanya mapitio makubwa (*comprehensive review*) ya Dira ya Maendeleo ya Taifa, mipango na mikakati ya ukuzaji wa sekta ya viwanda, biashara na uwekezaji ili kuja na hatua muafaka na za kulinusuru Taifa letu kutokupiga hatua na kurudi nyuma zaidi kama ilivyojitekeza ndani ya kipindi cha miaka 50 ya Uhuru wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya viwanda hapa nchini. Kwa mujibu wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013 inaonyesha kuwa Tanzania ina jumla ya viwanda 50,656, ambavyo vipo katika mikoa mbalimbali hapa nchini. Wakati huo huo, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji inazungumzia viwanda au mashirika 119 tu ambayo yamebinafsishwa na kati yake 74 vikiwa vinafanya kazi (vizima), 44 vinaendelea vizuri, 13 vinalegalega na 17 vimefungwa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 96.5 ya viwanda vyote ambavyo ni viwanda 48,887 ni viwanda vidogo vinavyoajiri wafanyakazi mmoja hadi tisa. Asilimia 3.5 ambayo ni viwanda 1,769 vinatoa ajira kuanzia watu kumi na kuendelea. Takwimu hizi hazitoi matumaini ya uhakika ya kuingia katika uchumi wa viwanda kama inavyohubiriwa na Serikali ya CCM. Sambamba na hayo ni

kwamba Serikali inasema ina mkakati wa kuendeleza viwanda vikubwa na vidogo na vile vilivyobinafsishwa na taarifa hiyo hiyo inasema changamoto kubwa inayovikabili viwanda vilivyobinafsishwa ni pamoja na ukosefu wa mitaji, teknolojia ya uzalishaji kuitwa na wakati, malighafi isiyokuwa na uhakika, umeme na maji.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kwamba changamoto hizi bado zipo na zitaendelea kuwepo kwa kuwa Serikali haina mkakati wowote maalum wa kibajeti wa kuondoa changamoto hizi ila ni nyimbo zile zile (*business as usual*). (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, sera mbovu ambazo haziangalii maendeleo ya watu katika sekta ya viwanda, biashara na uwekezaji. Ni wazi kuwa Serikali ya CCM imeshindwa kabisa kufanikisha azma ya maendeleo ya watu wa Taifa hili kwa kuwa maendeleo kwa mujibu wa nadharia na matendo ya Hayati Baba wa Taifa ni maendeleo ya watu na siyo maendeleo ya vitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imejiridhisha kuwa sera mbovu ya uagizaji wa bidhaa nje ya nchi ambaou umekuwa ni wa holela, usiojali maslahi ya Watanzania umeendelea kuua sekta ya viwanda hapa nchini. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuwataarifu Watanzania wote kwa ujumla kuwa kwa muda wa miaka 21 wa utekelezaji wa dira hii ya kisanii badala ya kujielekeza katika maendeleo ya watu, viongozi wa Serikali wa CCM wameishia katika kupiga deal za ukwapuaji wa fedha za umma zilizogharimu Taifa kama ilivyokuwa katika kashfa ya wizi wa fedha za Rada, kashfa ya ukwapuaji wa fedha za ESCROW, kashfa ya Rais Mkapa kujuzia Mgodi wa Kiwira, kashfa ya Lugumi na mikataba tata isiyozingatia maslahi ya Watanzania na kadhalika.

Kambi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kuwa sasa ijielekeze katika mikakati ya kusuka upya taasisi zinazoshughulikia viwanda, biashara na uwekezaji ili kuziba kabisa mianya ya ukwapuaji wa fedha za umma ambazo zingeweza kutumika katika kuendeleza sekta ya viwanda endapo zisingekwapuliwa na wajanja wachache. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, maandalizi ya kuwa wachuuzi wa Kimataifa. Kumbukumbu zinaonyesha kwamba Serikali inajitahidi kuhamasisha wananchi kufanya biashara kwa kujenga sehemu kama vile Machinga Complex na sasa Mradi wa Kituo cha Kimataifa cha Biashara na Huduma Kurasini kwa ajili ya bidhaa kutoka China kwa zaidi ya shilingi bilioni 64.19. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba shilingi bilioni 64.19 ni fedha nyingi na kwa mazingira ya kawaida kama fedha hizi zingewekezwa katika ujenzi wa kiwanda ni dhahiri kiwanda hicho kingkuwa kimeanza uzalishaji.

Mfano Kiwanda cha General Tyre, Arusha kwa mujibu wa menejimenti ya kiwanda hicho inahitaji shilingi bilioni 60 tu kuanza uzalishaji. Hili lingewezekana kama kweli Serikali imepania kuwa ya viwanda na inatoa uzito zaidi kwa viwanda vyake kuliko uchuuzi wa bidhaa za nchi nyingine. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mtazamo mpana ni kwamba sasa hivi nchi yetu ndiyo itakuwa inachuza bidhaa za Wachina na kuwa mlango mkuu wa wachuuzi kwa bidhaa za Wachina kwa Mataifa yanayotuzunguka, tunakuwa wachuuzi wa Kimataifa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inauliza hivi hiyo dhana ya viwanda kuwa ndiyo tegemeo kubwa kwa uchumi badala ya kilimo kwa tafsiri pana itafikiwa kweli kama Awamu ya Pili ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa inavyohitaji? (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uwekezaji hafifu katika sekta ya viwanda nchini, sekta ya viwanda hapa nchini haifanyi vizuri ukilinganisha na nchi zilizoendelea kiviwanda duniani. Ripoti ya Maendeleo ya Viwanda Duniani ya mwaka 2016 (*Industrial Development Report 2016*) imeitaja nchi ya Tanzania kuwa nyuma kiviwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi zilizoendelea kiviwanda duniani kama vile Ujerumani, Japan na Marekani zinatajwa na ripoti hiyo kuendelea kushika nafasi zao kutokana na kutunza maarifa na teknolojia ya juu kiviwanda ambayo ina rasilimali za kutosha na nishati toshelevu (*they did this by maintaining knowledge and high-tech industries that are resource efficient and energy efficient*). Uwekezaji katika msingi wa mageuzi ya viwanda unatajwa kuwa chanzo cha mafanikio ya nchi zilizoendelea kiviwanda duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo Kambi ya Upinzani Bungeni imepitia Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kuhusu sekta ya viwanda ambapo kwa ujumla Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 9.3 tu. Kati ya shilingi bilioni 9.3, shilingi bilioni sita zimetajwa kutengwa kwa ajili ya SIDO ambapo fedha hizo zinanufaisha mikoa minne tu ambayo ni Dar es Salaam, Mwanza, Morogoro na Mbeya wakati nchi hii ikiwa na jumla ya mikoa 32.

Aidha, kiasi hicho cha fedha hizo kitaishia kukarabati majengo ya SIDO na ujenzi wa majengo ya wajasiriamali bila kugusa kabisa mitaji ya wajasiriamali hao, teknolojia na mitambo. Kiasi hiki ni kidogo sana tena sana kufanikisha mahubiri ya kuwa na uchumi wa viwanda 2025 kama viongozi wa CCM wanavyohubiri. Kambi ya Upinzani Bungeni imebaini kuwa kauli ya Rais, Mheshimiwa Magufuli kuwa Tanzania itakuwa ni nchi ya viwanda, ni kauli ya mwendelezo wa sera za CCM kuwahadaa wananchi kwa kauli tamu ambazo hazina mikakati ya kuzitekeleza. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli ya Tanzania ya Magufuli ya viwanda imetoweka ghafla hata kabla ya Serikali ya Rais Magufuli haijamaliza muda wa mwaka mmoja madarakani kutokana na Serikali yake kushindwa kuwekeza vya kutosha katika sekta ya viwanda vidogo vidogo (*SIDO*) ambayo ndiyo njia sahihi ya kwenda kwenye uchumi kamili wa viwanda (*industrialised economy*). Kama Mheshimiwa Waziri alivyosema tunafanya graduation ya viwanda, viwanda vidogo, vya kati na baadaye viwanda vikubwa. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango huo wa mwaka 2016/2017 haujaweka bayana nia ya Serikali ya kurejesha umiliki wa viwanda 33 vilivyobinafsishwa kwa wawekezaji na vikafa mikononi mwao na uzalishaji kusitishwa. Jambo la kushangaza ni kuwa hata Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Miaka Mitano (*National Five Years Development Plan 2016/2017 - 2020/2021*), haujaweka bayana mkakati wa Serikali hii ya CCM kufufua viwanda hivyo kati ya viwanda 106 vilivyobinafsisha mbali na maneno ya mbwembwe tu. Kambi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kurejea upya Mpango wake wa Maendeleo wa Taifa kwa Miaka Mitano na Mpango wa mwaka wa fedha 2016/2017 na kueleza ni kwa namna gani Serikali itashiriki zoezi la kufufua viwanda 33 vilivyofia mikononi mwa wawekezaji waliomilikishwa viwanda hivyo kutokana na sera mbovu ya ubinafsishaji iliyolenga kuua sekta ya viwanda badala ya kuviendeleza. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya mazao ya biashara. Msingi wowote wa maendeleo ya viwanda duniani unaangalia maendeleo ya watu hasa wakulima wa mazao ya chakula na biashara. Kwa muda mrefu wananchi wa Tanzania wanaolima mazao kama korosho, mpira, pamba, mchikichi, katani, kahawa, mazao ya ufugaji, samaki, mbao, misitu, alizeti na kadhalika, wameshindwa kuinua hali zao za maisha kutokana na sera ya uwezeshaji wa kimitaji na mazingira magumu ya biashara kuwabana katika uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo kama vile vya kukamua mafuta ya alizeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano hai ni katika uzalishaji wa zao la korosho katika Mikoa ya Lindi na Mtwara ambapo korosho ghafi husafirishwa nje ya nchi bila kubanguliwa kutokana na kutokuwepo kwa kiwanda au viwanda vya ubanguaji wa korosho ghafi katika mikoa hiyo na vile vilivyokuwa vimejengwa wakati wa Mwalimu Nyerere vimebinafsishwa kwa wachuuzi na sasa vimegeuka kuwa maghala. Uuaji wa viwanda hivyo umenyima Taifa ajira. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo korosho zingeuzwa nje ya nchi zikiwa zimebanguliwa thamani yake ingepanda na mauzo yake nje ya nchi yangeweza kuwa mara mbili zaidi ya kiasi cha fedha zilizopatikana ndani ya mwaka 2015 pekee dola za Marekani 267.5 ambazo ni sawa na shilingi bilioni 584.12. Zaidi ya asilimia 90 ya korosho ghafi hununuliwa na wamiliki wa

makampuni ya ubanguaji kutoka India na wao huzibangua na kuziwa kwa bei kubwa zaidi katika masoko ya nchi za Marekani na Ulaya. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Korosho imeshindwa kusimamia vyema zao la korosho. Kambi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kuivunja mara moja Bodi hii ili kuunda Bodi mpya itakayoweza kusimamia vyema ubunifu na uwekezaji wa viwanda vya ubanguaji wa korosho katika ukanda wa Lindi, Mtwara na Pwani. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa ujenzi wa Kiwanda cha Kubangua Korosho haujawekwa katika Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano wala mwaka wa fedha 2016/2017 bado Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaikumbusha Serikali kuwa iache tabia ya kuwahadaa wananchi na itimizi ahadi za ujenzi wa Kiwanda cha Kubangua Korosho iliyotolewa na Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan aliyoitoa wakati wa kampeni za uchaguzi Wilayani Mkuranga ambapo alinukuliwa na gazeti linalomilikiwa na Serikali la Habari Leo lilichapishwa tarehe 14 Septemba, 2015. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya biashara na masoko. Mazingira ya kuanza biashara mpya hapa nchini ni magumu sana, endapo mtu anaanzisha biashara ndani ya mfumo rasmi. Tanzania imeshika rekodi mbaya katika hatua za kuanzisha biashara mpya. Kwa mujibu wa ripoti ya Benki ya Dunia iliyotolewa mwaka 2016 iitwayo *Doing Business 2016: Tanzania*, Taifa letu limeshika nafasi ya 129 katи ya nchi 189 duniani katika uharaka wa kuanzisha biashara mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huo wa *Doing Business 2016: Tanzania*, inagharimu siku 26 kuanza biashara mpya huku mfanyabiashara akitakiwa kuvuka vizingiti tisa ambapo ndizo hatua za utaratibu wa kuanzisha biashara. Jambo hili linaifanya nchi kukosa mapato mengi yatokanayo na kodi, linachochea biashara za magendo ambazo zinaongeza ukwepaji wa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwekezaji yeyote awe wa ndani au wa nje ya nchi kwa mujibu wa ripoti hiyo anapotaka umeme ndani ya kiwanda chake, inagharimu muda wa siku 109. Kambi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kuzingatia matokeo ya utafiti huo wa Benki ya Dunia kwa kuamua kupitia upya utaratibu wa kuanzisha biashara hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu katika ripoti yake ya 2013 ya Takwimu za Biashara Nje (*Foreign Trade Statistics*) imebaini kuwa thamani ya biashara ya Tanzania katika Soko la Dunia ilifikia shilingi trilioni 28.12 na kuonesha dhahiri kuwa nchi yetu haifanyi vizuri sana katika urari wa biashara. Kwa kuwa Taifa letu halizalishi vya kutosha, manunuzi ya nje (*imports*) ni makubwa zaidi ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi (*exports*). Takwimu

zinaonesha kuwa mauzo yetu ya bidhaa nje ya nchi yameshuka kwa asilimia tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni aibu kubwa kwa nchi yetu kuagiza mchele kutoka mataifa mengine wakati tuna mito inayotiririka maji mwaka mzima, tuna ardhi kubwa yenyе rutuba na vijana wetu wana nguvu za kuzalisha ila Serikali haijatilia maanani aibu hii mbele ya uso wa ulimwengu. Taifa linashindwa kuzalisha ngano na badala yake thamani ya manunuzi ya ngano nje ya nchi (*imports of wheat*) yamefikia dola milioni 225 kwa mwaka kwa mujibu wa *Global Agricultural Information Network*. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, ununuzi wa bidhaa nje ya nchi (*imports*) unachangia katika kuperomosha thamani ya shilingi ya Tanzania kiasi cha kulifanya Taifa kupoteza hazina yake ya fedha za kigeni na kuongezeka kwa pengo kubwa katika urari wa biashara. Nchi yoyote inayotaka kujitegemea kibajeti lazima iimarishe bidhaa zake zilizoongezewa thamani na kuuzwa nje ya nchi. Hii ni kauli ya Mtendaji Mkuu wa *Tanzania Private Sector Foundation*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa kilimo kwa kipindi cha msimu wa kilimo wa mwaka 2013/2014, wakulima wengi walilazimika kuza mahindi yao kwa hasara kutohana na utaratibu uliotumika wa kutumia wakala wachuuzi kwenda vijiji kununua mahindi kwa bei ndogo ya shilingi 200 kwa kilo na wao kuiuzia Serikali kwa shilingi 500 - 550 kwa kilo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kuwa mwaka 2009, Bunge la Jamhuri ya Muungano ilitunga Sheria ya Uanzishwaji wa Sheria ya Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, ambayo lengo kuu lilikuwa ni kuhakikisha bodi hiyo inaweka bei elekezi kwa maana kwamba italazimika kununua mazao kwa bei ambayo wanunuzi wengine itawalazimu kuifuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni inauliza katika mazingira kama haya, sera na sheria za uwekezaji zinawasaidia vipi Watanzania katika kushiriki na kumiliki sekta mbalimbali za uchumi wa nchi yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sera ya Uwezeshaji ya Taifa ya mwaka 2004 pamoja na sheria ya usimamizi wa sheria hiyo ya mwaka 2004 vilenga kuhakikisha kwamba Watanzania walio wengi wanapata fursa ya kushiriki katika shughuli za kiuchumi kwenye sekta mbalimbali. Mataifa mengine yamefanya hivyo mfano, Afrika ya Kusini mwaka 1994 walianzisha sera ya kuwawezesha Waafrika wazawa kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wetu Sheria na Sera ya Uwezeshaji na Uwekezaji ni dhahiri vimeshindwa kukidhi matakwa tajwa imebakia makabatini badala yake Mawaziri wa CCM wamekuwa wakiwabeza

Watanzania wazawa kila walipojaribu kutafuta fursa za kuwekeza kwa kuwaita wachuuzi. (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

**MHE. ANTONY C. KOMU - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hotuba bado ni ndefu, naomba yote ambayo sikuweza kuyasoma yaingie katika rekodi za Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (Makofi)

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI  
MHESHIMIWA ANTONY CALIST KOMU (MB) WIZARA YA VIWANDA  
BIASHARA NA UWEKEZAJI KUHUSU MAPITIO YA UTEKELEZAJI KWA  
MWAKA WA FEDHA 2015/2016 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA  
MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17  
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

(Inatolewa chini ya Kanuni 99(9) ya Kanuni  
za Bunge Toleo la mwaka 2016)

## **1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, Naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuweza kusimama mbele ya ukumbi huu nikiwa mwenye afya njema kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/17. Pia nikushukuru wewe Binafsi Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi ya kuweza kutoa maoni haya.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa heshima kubwa naomba kukishukuru chama changu kwa kuniamini na kunipatia nafasi ya kupeperusha bendera yake Jimbo la Moshi Vijijiini na ndio sababu niko hapa. Aidha nimshukuru Mheshimiwa Freeman Mboge (Mb) wa Hai na Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni (KRUB) kwa imani yake kubwa kwangu na kunipa jukumu la kuwa msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi wa wizara hii nyeti ambayo imebeba dhana nzima ya awamu ya pili ya mpango wa maendeleo wa miaka mitano ya kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu, (**nurturing Industrialization for Economic Transformation and Human Development**).

**Mheshimiwa Spika**, Niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Moshi vijijiini kwa imani yao kwangu, na ninaahidi kwamba nitawawakilisha vizuri na kwa umakini mkubwa. Aidha, niwashukuru na kuwapongeza waheshimiwa wabunge

wote hasa wajumbe wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa ushirikiano mzuri katika kuhakikisha Bunge linatimiza majukumu yake ya Kikatiba.

**Mheshimiwa Spika**, Mwisho lakini si kwa umuhimu ni kwa familia yangu ambayo imekuwa msaada mkubwa sana katika kutekeleza majukumu yangu.

## 1.1 UONGO WA SERIKALI KWA BUNGE –BAJETI IPI INAPITISHWA?

**Mheshimiwa Spika**, nakosa maneno sawia ya kueleza Bunge lako juu ya mambo ya ajabu ambayo serikali hii inayawasilisha kwenye Bunge lako hili kwani ukisoma vitabu na nyaraka za serikali wametuletea nyaraka tatu tofauti na zenyetakwimu tofauti juu ya jambo hilo hilo kiasi kwamba huwezi jua kama hii ni serikali moja ama ni serikali tatu tofauti zimeandaa nyaraka husika au ndio tuseme ni ushahidi wa kukosekana kwa 'Instrument of power'kwa ajili ya utendaji kazi wa Mawaziri ndio maana kila mmoja anajifanyia mambo yake huko serikalini.

**Mheshimiwa Spika**, ukisoma kitabu cha fedha zilizopangwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo 2016/2017 (**Volume 4**) utaona kuwa mradi wa kufufua kiwanda cha General tyre kasma (1210) zimetengwa **shilingi milioni 150** kwa ajili ya mradi huo. Ukisoma **randama** ya wizara ya viwanda na biashara General tyre kasma (1210) uk.148 imetengewa **shilingi 500 milioni** kwa ajili ya kufufua kiwanda hicho. Ila ukisoma mapendekezo ya **mpango wa Maendeleo** ambao ulitolewa na Wizara ya Fedha utaona kuwa General tyre kwa mwaka huu wa fedha zimetengwa **shilingi 2 Bilioni** fedha za ndani kwa ajili ya kufufua kiwanda hiki. Mpango wa Maendeleo sura ya nne uk. 38 'Mradi wa kufufua kiwanda cha General Tyre –Arusha', nanakuu '**katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 2 fedha za ndani kwa ajili ya ukarabati wa majengo na mitamboya kiwanda'**

**Mheshimiwa Spika**, hali ni hiyohiyo ukiutazama mradi wa Magadi soda – Bonde la Engaruka Arusha takwimu ziko tofauti na hazifanani na hii inaleta hofu hapa kuwa Bunge linapitisha nini haswa?, ukisoma randama uk .147 kasma (1122) zimetengwa **shilingi 1.7 Bilioni** kwa ajili ya mradi huu,lakini ukisoma mpango wa maendeleo 2016/17 uk.38 unasema zimetengwa **shilingi 700 milioni tu** kwa ajili ya mradi huu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwenendo huu wa takwimu zisizofanana ambazo zote zinazungumzia mradi mmoja maana yake ni kuwa serikali hii imekosa Uratibu 'Coordination' na hivyo kila wizara kuja na vitu vyake na takwimu zake kama ilivyobainika hapo juu, hali hii italiwia vigumu Bunge kupitisha bajeti hii kwani kwenye kamati tulijadili miradi iliyokuwa kwenye randama na fedha zilizoombwa , Bunge lako lilishapitisha mpango wa maendeleo na viwango vya fedha zilizoombwa kwa ajili ya kutekeleza mpango

, na leo tunajadili bajeti ya wizara na tutapitisha vifungu vilivyopo kwenye vitabu vyat matumizi na kile cha Maendeleo yaani VOLUME 4. Mhe Spika, huu ni sawa na mchezo wa kuigiza.

**Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inataka kupata majibu ya kina kabla ya kupitishwa kwa bajeti hii ni Mhe Waziri wa fedha anafanya "uhuni" wa kiasi hiki kwa kulidanganya Bunge? Kwani wizara ya fedha ndio wanaotoa viwango vyat mwisho vyat malipo kwa matumizi ya kawaida na kwa miradi ya maendeleo "ceilings", Au ni waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji?**

**Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kuelewa takwimu zilizopitishwa na Kamati kwa miradi husika kwa makubaliano na Serikali inakuwaje zinakuwa tofauti na takwimu zinazopitishwa na Kamati ya Bunge zima? Hapa ndipo "uhuni na utapeli" wanaofanyiwa wabunge na Serikali yao. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inawaasa waheshimiwa wabunge kuwa makini kwa kuoanisha takwimu za fedha zilizopo kwenye Randama na zile zilizotengwa kwenye vitabu vinavyopitishwa na Kamati ya Bunge zima.**

## **2.0 DIRA YA TAIFA 2025 NA KURUDI NYUMA KWA SEKTA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI**

**Mheshimiwa Spika;** Mipango mbalimbali ya Serikali katika Sekta ya viwanda, biashara na uwekezaji inaongozwa na Dira ya Maendeleo ya Taifa (Development Vision 2025, dira ambayo inaelekea kufeli na kushindwa kwa kiwango kikubwa kutimiza malengo yaliyokusudiwa ifikapo mwaka 2025. Kambi ya Upinzani Bungeni imeshazona dalili za anguko la dira hiyo kwa kushindwa kabisa kubadilisha maisha ya Watanzania kutoka katika lindi kubwa la umasikini unaowazunguka.

**Mheshimiwa Spika;** Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 iliundwa mwaka 1995 na leo hii ninavyozungumza imetimiza miaka 21, imebakia miaka 9 tu kufika mwaka 2025 ambapo Dira hiyo itakuwa imetimiza miaka 30 bila kuwepo hata kwa dalili za mageuzi makubwa ya kiviwanda hapa nchini.

Katika ukurasa wa pili wa kijitabu cha Dira ya Maendeleo ya Taifa mwaka 1995, dira hiyo ilisema wazi kuwa ifikapo mwaka 2025 Tanzania itakuwa imehama kutoka kuwa nchi iliyo nyuma kimaendeleo [least developed country] na kuwa nchi ya kipato cha kati yenye kiwango cha juu cha Maendeleo [ high level of human development].

**Mheshimiwa Spika;** Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza bunge lako tukufu na Watanzania wote kwa ujumla; kuwa inatumia mbinu zipi ndani ya miaka mitano ijayo kufikia lengo la kufanya Tanzania kuwa nchi yenye kipato cha kati? Aidha, Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka

Serikali kueleza Watanzania ni kwa kiasi gani mikakati hiyo ya kuifanya nchi kuwa ya kipato cha kati itashughulika na Maendeleo ya watu na hayatakuwa Maendeleo ya vitu kama ilivyo hivi sasa ? Hali ilivyo sasa tunaona maendeleo ya Majengo ya wachache yasiyokuwa na uhusianao na uhalisia wa maisha ya watanzania zaidi ya asilimia 80 waishio vijiji katika ufukara wa kupindukia .

**Mheshimiwa Spika;** Inasikitisha sana kuwa wakati wa Uhuru<sup>1</sup> sekta ya viwanda ilichangia pato la Taifa kwa asilimia 9 lakini mwaka 2011 wakati Serikali ya CCM inatoa mafanikio ya miaka 50 ya Uhuru, mchango wa sekta ya viwanda katika pato la Taifa ulishuka mpaka kufikia asilimia 8.6. baada ya miaka 50 iliyopewa CCM kuondoa umaskini ,ujinga na maradhi, badala yake takwimu zake yenewe zinaonyesha kuwa hali ni mbaya zaidi!

**Mheshimiwa Spika;** Miaka mitano ijayo ya Mhe. Rais Magufuli inayotumia ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015, haina jambo jipyä katika Maendeleo ya Sekta ya Viwanda hapa nchini . Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 inazungumzia Maendeleo ya sekta ya viwanda katika muktadha ule ule ulioshindwa kuzaa matunda kwa zaidi ya miaka 50 iliyopita. Ilani hiyo ya CCM inasema kuwa; “*Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii ya 2015–2020, Chama Cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali kuweka nguvu kubwa katika kukamilisha utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda Awamu ya Tatu (2010–2020) ambayo malengo yake ni kuiwezesha Sekta ya Viwanda kuchangia katika kufikia malengo ya maendeleo ya muda mrefu kama ilivyoanishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025.*”

**Mheshimiwa Spika;** Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 ni dira isiyokuwa na mwelekeo wenye afya kwa Taifa letu hata katika hatua za utekelezaji imeendelea kusitiza kuwa ifikapo mwaka 2025, uchumi wa Tanzania utakuwa umebadilishwa kutoka kwenye uzalishaji duni wa uchumi wa kilimo mpaka kufikia uchumi wa viwanda wa kati [semi-industrialized economy]

Kambi ya Upinzani Bungeni haioni suala hilo likitokea ifikapo mwaka 2025 kwa kuwa mipango ya Serikali ya CCM ni ile ile na haijabadilika na haina mikakati mahususi ya kubadili hali hii.

**Mheshimiwa Spika;** Kambi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kufanya mapitio makubwa [comprehensive review] ya Dira ya Maendeleo ya Taifa, mipango na mikakati ya ukuzaji wa sekta ya viwanda, biashara na uwekezaji ili kuja na hatua muafakana za kulinusuru Taifa letu kutokopiga hatua na kurudi nyuma zaidi kama ilivyojiteza ndani ya kipindi cha miaka 50 ya Uhuru wetu.

---

<sup>1</sup> Ukokotozi wa Ilani ya CHADEMA/UKAWA 2015, Ukurasa wa 43.

## 2.1 SEKTA YA VIWANDA HAPA NCHINI

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Waziri wa Fedha na Mpango inaonyesha kuwa mchango wa sekta ya viwanda katika pato la taifa kwa kipindi cha muongo mmoja uliopita ni wastani wa asilimia 7. Na kwa mujibu wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013, inaonyesha kuwa Tanzania ina jumla ya viwanda 50,656 ambavyo vipo katika mikoa mbalimbali hapa nchini, wakati huo huo wizara ya viwanda, Biashara na uwekezaji inazungumzia viwanda/mashirika 119 tu ambavyo vilibinafsishwa na kati yake 74 vikiwa vinafanya kazi (vizima), 44 vinaendelea vizuri, 13 vinalegalega na 17 vimefungwa kabisa. Takwimu hizi zinaonesha ushahidi mwingine wa ukosefu wa uratibu ndani ya serikali. Wizara kwa kushirikiana na msajili wa Hazina inafanya upembuzi wa utendaji na mikataba ya viwanda/mashirika ili kufikia uamuzi wa kunyang'anya viwanda/mashirika yanayolegalega nakuwapa wawekezaji wenye uwezo. Hoja hapa ni lini kazi hii itakamilika? Aidha bila aibu taarifa ya wizara inasema kuwa baadhi ya viwanda vilivyo binafishwa vilitumiks kama dhamana kukopa benki na fedha hizo zilitumika kwa shughuli nyingine baddala ya kuviendeleza, huu ni udhaifu kwa upande wa serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Asilimia 96.5 ya viwanda vyote ambayo ni viwanda 48,887 ni viwanda vidogo vinavyoajiri wafanyakazi 1 hadi 9. Asilimia 3.5 ambayo ni viwanda 1,769 vinatoa ajira kuanzia watu 10 na kuendelea.

**Mheshimiwa Spika**, Takwimu hizi hazitoi matumaini ya uhakika ya kuingia katika uchumi wa viwanda kama inavyohubiriwa na serikali ya CCM. Sambamba na hayo ni kwamba Serikali inasema ina mkakati wa kuendeleza viwanda vikubwa na vidogo na vile vilivyobinafsishwa. Na taarifa hiyo hiyo inasema kuwa changamoto kubwa inayovikabili viwanda vilivyobinafsishwa ni pamoja na ukosefu wa mitaji, teknolojia ya uzalishaji kuitwa na wakati, malighafi isiyokuwa na uhakika, umeme na maji.

**Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni**, inaona kwamba changamoto hizi bado zipo na zitaendelea kuwepo kwa kuwa serikali haina mkakati wowote maalumu wa kibajeti wa kuondoa changamoto hizi ila ni nyimbo zile zile (Business as usual).

## 2.2 SERA MBOVU AMBAZO HAZIANGALII MAENDELEO YA WATU KATIKA SEKTA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI

**Mheshimiwa Spika**; Ni wazi kuwa Serikali ya CCM imeshindwa kabisa kufanikisha azma ya Maendeleo ya watu wa Taifa hili, kwa kuwa Maendeleo kwa mujibu wa nadharia na matendo ya Hayati Baba wa Taifa ni Maendeleo ya watu na sio Maendeleo ya vitu.

**Mheshimiwa Spika;** Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni imejiridhisha kuwa sera mbovu ya uagizaji wa bidhaa nje ya nchi ambao umekuwa ni holela usiojali maslahi ya Watanzania umeendelea kuua sekta ya viwanda hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika;** Gazeti la Habari Leo linalomilikiwa na Serikali, katika toleo lake la mtandaoni lilitolewa tarehe 19 Agosti 2015, liliandika habari yenyeye kichwa kisemacho “**Bidhaa za nje zinavyoua sekta ya viwanda**” habari iliyoadikwa na mwandishi Sifa Lubasi<sup>2</sup> alimnukuu mmoja wa wamiliki wa viwanda vidogo hapa nchini Bwana, Ismail Manyana wa Kijiji cha Makutupa kata ya Lupeta wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma.

**Mheshimiwa Spika;** Mmiliki huyo wa kiwanda cha Kukamua mafuta ya alizeti, Bwana, Ismail Manyana alinukuliwa akisema “*Serikali inatakiwa kuangalia soko la ndani na kuliimarisha na si kama ilivyo sasa, bidhaa tunazozalisha zinakosa masoko. Wazalishaji wa mafuta ya alizeti ni wengi hapa nchini lakini mchango wao umekuwa hauthaminiwi na badala yake serikali inaangalia zaidi kuagiza mafuta nje hali inayoua soko la ndani,*”

**Mheshimiwa Spika;** Kambi ya Upinzani Bungeni inapenda kuwataarifu Watanzania wote kwa ujumla kuwa kwa muda wa miaka 21 wa utekelezaji wa Dira hii ya kisanii badala ya kujielekeza katika Maendeleo ya watu , viongozi wa Serikali ya CCM wameishia katika kupiga dili za ukwapuaji wa fedha za umma ziloligharimu taifa kama ilivyokuwa katika Kashfa ya wizi wa fedha za Rada, Kashfa ya ukwapuaji wa fedha za ESCROW, Kashfa ya Rais Mkapa kujuzia Mgodi wa Kiwira ambao baadaye, baada ya Kelele nyingi zilizopigwa na Kambi ya Upinzani Bungeni mgodi huo ulirejeshwa Serikalini, Kashfa ya Lugumi na mkataba tata isiyozingatia masalahi ya watanzania n.k.

**Mheshimiwa Spika;** Kambi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kuwa, sasa ijielekeze katika mikakati ya kusuka upya taasisi zinazoshughulikia viwanda, biashara na uwekezaji ili kuziba kabisa mianya ya ukwapuaji wa fedha za umma ambazo zingeweza kutumika katika kuendeleza sekta ya viwanda endapo zisingekwapuliwa na wajanja wachache.

## 2.3 MAANDALIZI YA KUWA WACHUUIZI WA KIMATAIFA

**Mheshimiwa Spika;** Kumbukumbu zinaonyesha kwamba Serikali inajitahidi kuhamasisha wananchi kufanya biashara, kwa kujenga sehemu kama vile machinga complex na sasa Mradi wa kituo cha kimataifa cha biashara na huduma kurasini kwa ajili ya bidhaa kutoka China kwa zaidi ya shilingi bilioni 64.19.

<sup>2</sup><http://habarileo.co.tz/index.php/makala/1023-bidhaa-za-nje-zinavyoua-sekta-ya-viwanda>

**Mheshimiwa Spika;**Ukweli ni kwamba shilingi bilioni 64.19 ni fedha nyingi na kwa mazingira ya kawaida kama fedha hizo zingewekezwa katika ujenzi wa kiwanda ni dhahiri kiwanda hicho kingekuwa kimeanza uzalishaji,mfano; Kiwanda cha General tyre Arusha kwa mujibu wa menejimenti ya kiwanda hicho inahitaji sh. Bilioni 60 tu kuanza uzalishaji. Hili lingewezekana kama kweli Serikali imepania kuwa ya Viwanda, na inatoa uzito zaidi kwa viwanda vyake kuliko uchuuzi wa bidhaa za nje. Dhana ya mradi huu ambao unaongelewa ni kuwapunguzia watanzania adha ya safari kwenda China kufuata bidhaa na badala yake wachina watakuwa wanaleta wenyewe hapa hapa.

**Mheshimiwa Spika;**Kwa mtazamo mpana ni kwamba sasa hivi nchi yetu ndio itakuwa inachuza bidhaa za wachina na kuwa **mlango mkuu wa wachuuzi** kwa bidhaa za wachina kwa mataifa yanayotuzunguka, tunakuwa wachuuzi wa kimataifa.

**Mheshimiwa Spika;**Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inauliza hivi hiyo dhana ya viwanda kuwa ndio tegemeo kubwa kwa uchumi badala ya kilimo kwa tafsiri pana itafikiwa kweli kama awamu ya pili ya mpango wa maendeleo ya Taifa unavyohitaji?

#### **2.4 UWEKEZAJI HAFIFU KATIKA SEKTA YA VIWANDA NCHINI**

**Mheshimiwa Spika;**Sekta ya viwanda hapa nchini haifanyi vizuri ukilinganisha na nchi zilizoendelea kiviwanda duniani. Ripoti ya Maendeleo ya Viwanda Duniani ya mwaka 2016 (Industrial Development Report 2016) imeitaja nchi ya Tanzania kuwa nyuma kiviwanda .

**Mheshimiwa Spika;**Nchi zilizoendelea kiviwanda duniani kama vile Ujeruman, Japan na Marekani zinatajwa na ripoti hiyo kuendelea kushika nafasi zao kutokana na kutunza maarifa na technolojia ya juu kiviwanda ambayo ina rasilimali za kutosha na nishati toshelevu (*They did this by maintaining knowledge and high-tech industries that are resource efficient and energy efficient.*)

Uwekezaji katika msingi wa mageuzi ya viwanda unatajwa kuwa chanzo cha mafanikio ya nchi zilizoendelea kiviwanda duniani.

**Mheshimiwa Spika;** Hata hivyo; Kambi ya Upinzani bungeni imepitia Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2016/17 kuhusu sekta ya viwanda, ambapo kwa ujumla Serikali imetenga jumla ya shilingi Bilioni 9.3 tu.

**Mheshimiwa Spika;**Kati ya Shilingi Bilioni 9.3, bilioni 6 zimetajwa kutengwa kwa ajili ya SIDO ambapo fedha hizo zitanufaisha mikoa minne tu (4) (ambayo ni Dar es Salaam, Mwanza, Morogoro na Mbeya) wakati nchi hii ikiwa na jumla

ya mikoa 32. Aidha kiasi hicho cha Fedha hizo kitaishia kukarabati majengo ya SIDO na ujenzi wa majengo ya wajasiriamali bila kugusa kabisa mitaji ya wajasiriamali hao, teknolojia na mitambo. Kiasi ni kidogo sana ten asana kufanikisha mahubiri ya kuwa na uchumi wa viwanda 2025.

**Mheshimiwa Spika;** Kambi ya Upinzani Bungeni imebaini kuwa kauli ya Rais Mhe . Magufuli kuwa Tanzana itakuwa ni nchi ya viwanda, ni kauli ya mwendelezo wa sera za CCM kuwahadaa wananchi kwa kauli tamu ambazo hazina mikakati ya kuzitekeleza.

**Mheshimiwa Spika;** Kauli ya Tanzania ya Magufuli ya Viwanda imetoweka ghafla hata kabla Serikali ya Rais Magufuli haijamaliza muda wa mwaka mmoja madarakani kutokana na Serikali yake kushindwa kuwekeza vyta kutosha katika Sekta ya viwanda vidogo vidogo (SIDO), ambayo ndiyo njia sahihi ya kwenda kwenye uchumi kamili wa viwanda (industrialized economy).

**Mheshimiwa Spika;** Mpango huo wa mwaka 2016/17 haujaweka bayana nia ya Serikali ya Kurejesha umiliki wa viwanda 33 vilivyobinafsishwa kwa wawekezaji na vikafa mikononi mwao na uzalishaji kusitishwa. Jambo la kushangaza ni kuwa hata Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa miaka 5 (National Five Year Development Plan 2016/17 – 2020/21) haujaweka bayana mkakati wa Serikali hii ya CCM kufufua viwanda hivyo kati ya viwanda 106 vilivyobinafishwa (**Tazama Kiambatanisho A**)

**Mheshimiwa Spika;** Kambi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kurejea upya mpango wake wa Maendeleo ya Taifa wa miaka 5 na mpango wa mwaka wa fedha 2016/17 na kueleza ni kwa namna gani Serikali itashiriki zoezi la kufufua viwanda 33 vilivyofia mikononi mwa wawekezaji waliomilikishwa viwanda hivyo kutokana na sera mbovu ya ubifsishaji iliyolenga kuua sekta ya viwanda badala ya kuiendeleza. Aidha, Kambi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kufanya mapitio upya ya uwekezaji uliofanyika katika msingi wa ujenzi wa viwanda hapa nchini ili kuja na hatua za makusudi katika Maendeleo ya sekta ya viwanda hapa nchini.

**Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni,** inapendekeza kuwa uwekezaji wa jumla ya shilingi Bilioni 9.3 katika Sekta ya viwanda ni mdogo na hautoshi. Tunashauri fedha zaidi zitengwe kwa ajili ya SIDO, katika mikoa yote iliyosalia ambayo haipo ndani ya mpango wa mwaka wa fedha 2016/17.

## 2.5 VIWANDA VYA MAZAO YA BIASHARA

**Mheshimiwa Spika;** Msingi wowote wa Maendeleo ya viwanda duniani unaangalia Maendeleo ya watu, hasa wakulima wa mazao ya chakula na biashara. Kwa muda mrefu wananchi wa Tanzania wanaolima mazao kama

Korosho, Mpira, Pamba, Mchikichi, Katani, Kahawa, Mazao ya ufugaji, Samaki, Mbao, Misitu, alizeti n.k wameshindwa kuinua hali zao za maisha kutokana na sera ya uwezeshaji wa kimitaji na mazingira magumu ya biashara kuwabana katika uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo kama vile vya kukamua mafuta ya alizeti.

**Mheshimiwa Spika;** Mfano hai ni katika uzalishaji wa zao la korosho katika mikoa ya Lindi na Mtwara ambapo korosho ghafi husafirishwa nje ya nchi bila kubanguliwa kutokana na kutokuwepo kwa kiwanda au viwanda vya ubanguaji wa korosho ghafi katika mikoa hiyo na vile vilivyokuwa vimejengwa wakati wa Mwl. Nyerere vimebinafsishwa kwa wachuuzi na sasa vimegeuka kuwa maghala. Uuaji wa viwanda hivyo umenyima Taifa ajira

**Mheshimiwa Spika;** Endapo korosho zingeuzwa nje ya nchi zikiwa zimebanguliwa thamani yake ingepanda na mauzo yake nje ya nchi yangeweza kuwa mara mbili zaidi ya kiasi cha fedha zilizopatikana ndani ya mwaka 2015 pekee dola za Marekani milioni 267.2 ambazo ni sawa na Shilingi Bilioni 584.12. Zaidi ya asilimia 90 ya korosho ghafi hununuliwa na wamiliki wa makampuni ya ubanguaji kutoka India, na wao huzibangua na kuzuza kwa bei kubwa zaidi katika masoko ya nchi za Marekani na Ulaya, jambo linalowatesa wakulima kutokana na kukosekana ushindani wa bei kwa kuwa nchi nyininge hazinunui korosho ghafi kwa wingi bali hununua korosho zilizobanguliwa, na hufanya ununuzi huo nchini India

**Mheshimiwa Spika;** Bodi ya Korosho imeshindwa kusimamia vyema zao la korosho. Kambi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kuivunja mara moja bodi hii ili kuunda bodi mpya itakayoweza kusimamia vema ubunifu na uwekezaji wa viwanda vya ubanguaji wa korosho katika ukanda wa Lindi, Mtwara na Pwani.

**Mheshimiwa Spika;** Pamoja na kuwa Ujenzi wa kiwanda cha kubangua korosho haujawekwa katika mpango wa Taifa wa miaka 5 wala mwaka wa fedha 2016/17, bado Kambi ya Upinzani Bungeni inaikumbusha Serikali kuwa iache tabia ya kuwahadaa wananchi na itimizie ahadi ya Ujenzi wa Kiwanda cha Kubangua Korosho iliyotolewa na Makamu wa Rais Mhe. Samia Suluhu Hassan aliyoitoa wakati wa kampeni za uchaguzi wilayani Mkuranga ambapo alinukuliwa na gazeti linalomilikiwa na Serikali, Habari leo lililochapwa tarehe 14 Septemba 2015, habari iliyoandikwa na Halima Mlacha<sup>3</sup> akisema kuwa “Tuchagulieni Dk Magufuli na wagombea ubunge na udiwani ili tulete maendeleo Mkuranga. Tumejipanga na tunaahidi kujenga kiwanda cha kubangua korosho hapa kwenu”

<sup>3</sup> Ahadi ya Kujenga Kiwanda cha Korosho:

<http://www.habarileo.co.tz/index.php/habari-za-kitaifa/1933-aahidi-kujenga-kiwanda-cha-korosho>

### 3.0 SEKTA YA BIASHARA NA MASOKO

#### 3.1 Sekta ya Biashara

**Mheshimiwa Spika;** Mazingira ya kuanza biashara mpya hapa nchini ni magumu sana endapo mtu anaanzisha biashara ndani ya mfumo rasmi. Tanzania imeshika rekodi mbaya katika hatua za kuanzisha biashara mpya. Kwa mujibu wa Ripoti ya Benki ya Dunia iliyotolewa mwaka 2016 iitwayo "Doing Business 2016: Tanzania" Taifa letu limeshika nafasi ya 129 kati ya nchi 189 duniani katika uharaka wa kuanzisha biashara mpya.

**Mheshimiwa Spika;** Kwa mujibu wa matokeo ya Utafiti huo wa "Doing Business 2016: Tanzania" inagharimu siku 26.0 kuanza biashara mpya huku mfanyakibashara akitakiwa kuvuka vizingiti 9 ambazo ndizo hatua za utaratibu wa kuanzisha biashara. Jambo hili linaifanya nchi kukosa mapato mengi yatokanayo na kodi lakini pia linachochea biashara za magendo ambazo zinaongeza ukwepaji wa kodi.

**Mheshimiwa Spika;** Mwekezaji yoyote awe wa ndani au wa nje ya nchi kwa mujibu wa ripoti hiyo anapotaka kuingiza umeme ndani ya kiwanda chake, inagharimu muda wa siku 109, huku akitakiwa kupitia vizingiti 4 ili aweze kuwekewa umeme katika kiwanda chake. Haya ni mazingira magumu sana na yanaichelewesha nchi yetu kupiga hatua za Maendeleo katika sekta ya biashara.

**Mheshimiwa Spika;** Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni, inaishauri Serikali kuzingatia matokeo ya Utafiti huo wa Benki ya Dunia kwa kuamua kupitia upya utaratibu wa kuanzisha biashara mpya nchini na kuangalia pia taratibu zake za kuunganisha umeme kwenye viwanda vinavyoanzishwa hapa nchini.

#### 3.2 Sekta ya Masoko

**Mheshimiwa Spika;** Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu katika ripoti yake ya mwaka 2013 ya "Takwimu za Biashara ya Nje" (Foreign Trade Statistics), imebainika kuwa thamani ya biashara ya Tanzania katika soko la dunia ilifikia Shilingi Trilioni 28.12 na kuonesha dhahiri kuwa nchi yetu haifanyi vizuri sana katika urari wa biashara kutokana na uzalishaji hafifu unaochangiwa na sera mbovu za Serikali ya CCM katika kuchochaea uzalishaji wa ndani. Urari wa biashara umefikia negative balance ya Shilingi Trilioni 11.68 yaani (negative Balance of Trade)

**Mheshimiwa Spika;** kwa kuwa Taifa letu halizalishi vya kutosha manunuzi ya bidhaa nje ya nchi (imports) ni makubwa zaidi ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi (exports). Takwimu zinaonesha kuwa mauzo yetu ya bidhaa nje ya nchi yameshuka kwa asilimia 5.0 ambayo ni sawa na shilingi Triliioni 8.22 wakati uagizaji wa bidhaa nje ya nchi ukiongezeka kwa asilimia 8.9 ambayo ni sawa na Shilingi Triliioni 19.90.

**Mheshimiwa Spika;** Sera mbovu za biashara zilizo asisiwa na Serikali hii ya CCM hazijaweza kumudu kuiondoa nchi katika hali mbaya kama hiyo. Nchi yetu imekuwa tegemezi na haizalishi vya kutosha kiasi cha kuagiza kutoka nje ya nchi hata chakula kama sukari, mchele, ngano na mahindi mazao ambayo yalipaswa kupatikana kwa wingi hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika;** Kwa sasa Tanzania inanunua mchele kutoka katika mataifa ya China, India, Indonesia, Pakistan na Vietnam, wakati uzalishaji wa ndani ukiwa mdogo ambapo asilimia 18 ya familia zinazojihusisha na kilimo ndio hulima zao la mchele. Jiji la Dar es Salaam pekee hutumia asilimia 60 ya mchele unaozalishwa ndani wakati asilimia 30 huliwa na wakulima wenyewe na asilimia 10 inayobakia huingia katika soko la ndani hasa maeneo ya mikoani. Hii ni kwa mujibu wa ripoti ya Global Agricultural Information Network iliyotolewa tarehe 21 Machi 2016 kama ilivyoandalishi na Benjamin Mtaki na kuidhinishwa na Kate Snipes.

**Mheshimiwa Spika;** Ni aibu kubwa kwa nchi yetu kuagiza mchele kutoka mataifa mengine wakati tuna mito inayotiririka maji mwaka mzima, tuna ardhii kubwa yenye rutuba, na vijana wetu wana nguvu za uzalishaji ila Serikali haijatilia maanani aibu hii mbele ya uso wa ulimwengu. Taifa linashindwa kuzalisha ngano na badala yake thamani ya manunuzi ya ngano nje ya nchi yaani “**imports of wheat**” yamefikia dola milioni 225 kwa mwaka kwa mujibu wa Global Agricultural Information Network.

**Mheshimiwa Spika;** Ununuzi wa bidhaa nje ya nchi (imports) unachangia katika kuporomosha thamani ya Shilingi ya Tanzania kiasi cha kulifanya taifa letu kupoteza hazina yake ya fedha za kigeni na kuongezeka kwa pengo kubwa katika urari wa biashara. Thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani imeporomoka kutoka shilingi 1,754.7 Januari 2015 mpaka kufikia Shilingi 2,189.1 mwezi Februari 2016. Sababu zinazotajwa na Serikali kuchangia uporomokaji huo ni pamoja na kupungua kwa mauzo ya nje ya nchi. Hapa Serikali imeendelea kukiri udhaifu wake kuwa inashindwa kabisa kusimamia thamani ya Shilingi dhidi ya dola ya Marekani katika soko la dunia.

**Mheshimiwa Spika, “nchi yoyote inayotaka kujitegemea kibajeti lazima iimarishwe na bidhaa zake zilizoongezewa thamani na kuuzwa nje ya nchi”** hii ni kauli ya mtendaji mkuu wa TPSF

**Mheshimiwa Spika;** Kambi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya CCM ichukue hatua za makusudi ili kuimarisha thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani katika soko la Dunia na soko la ndani. Aidha tunaitaka Serikali ieleze mkakati wake wa kuongeza uzalishaji wa ndani hasa katika mazao ya chakula ambayo takwimu zinaonesha uzalishaji umeshuka sana.

### **3.4 BIASHARA YA MAZAO NA UNYONYAJI WA WAKULIMA NCHINI**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa kilimo kwa kipindi cha msimu wa kilimo wa mwaka 2013/2014 na 2015, wakulima wengi walilazimika kuuza mahindi yao kwa hasara kutokana na utaratibu uliotumika wa NFRA kuwatumia mawakala (wachuuzi) kwenda vijijini kununua mahindi kwa bei ndogo ya Sh 200 na wao kuiuzia serikali kwa Sh 500 hadi 550 kwa kilo.<sup>4</sup>

Aidha, ili wakulima wawewe kulima ni dhahiri kuwa matumizi makubwa ya raslimali fedha na muda vinakuwa vimewekezwa, na pale ambapo Serikali inashindwa kupanga bei kulingana na hali halisi ya gharama zinazokuwa zimetumika ni hujuma ya dhahiri kwa wakulima (watanzania wa kawaida).

**Mheshimiwa Spika,** Tukumbuke kuwa mwaka 2009, Bunge la Jamhuri ya Muungano lilitunga sheria ya uanzishwaji wa Sheria ya Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko.<sup>5</sup> Ambayo lengo kuu ilikuwa ni kuhakikisha Bodi hiyo inaweka bei elekezi kwa maana kwamba italazimika kununua mazao kwa bei ambayo wanunuzi wengine itawalazimu kuifuata, kinyume na hivyo bodi ndiyo itakayokuwa mnunuzi wa mazao ambayo hayakuundiwa bodi yake, mazao kama vile mahindi, maharage, mpunga, ulezi, ufuta, mbaazi n.k

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inauliza katika mazingira kama hayo, Sera na sheria za uwezeshaji zinawasaidia vipi watanzania katika kushiriki na kumiliki sekta mbalimbali za uchumi wa nchi yetu? Ni dhahiri kuwa serikali imeshindwa kuwasaidia Watanzania kuingia katika biashara kubwa kwa makusudi au kwa kukosa uwezo wa kujenga mazingira wezeshi kwa Watanzania kuwekeza na kuwa sehemu ya wamiliki wa uchumi wao.

## **4.0 UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Sera ya Uwezeshaji ya Taifa ya mwaka 2004 pamoja na sheria ya usimamizi wa sheria hiyo ya mwaka 2004 vililenga kuhakikisha kwamba

<sup>4</sup>Gazeti la Habari Leo, Februari 3,2016- Wakulima wa Mahindi “waililia” Serikali

<sup>5</sup>Sheria namba 19 ya 2009, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (The Cereals and Other Produce Act 2009)

watanzania waliowengi wanapata fursa ya kushiriki katika shughuli za kiuchumi kwenye sekta mbalimbali. Mataifa mengine yamefanya hivyo, mfano; Afrika Kusini mwaka 1994 baada ya kumalizika kwa Ubaguzi wa Rangi walianzisha sera ya kuwawezesha Waafrika wazawa **Kiuchumi(Broad-Based Black Economic Empowerment (B-BBEE))**.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wetu, Sheria na Sera za Uwezesajji na Uwekezaji ni dhahiri vimeshindwa kukidhi matakwa tarajiwa, imebaki makabatini badala yake mawaziri wa CCM wamekuwa wakiwabeza watanzania wazawa kila walipojaribu kutafuta fursa za kuwekeza kwa kuwaita wachuuzi na huku wakiwasaidia wachuuzi wa kweli wa nje kwa wao wenyewe kunufaika na raslimali zetu. Mifano halisi ni ile iliyompata Dr Regnaldi Mengi alipojaribu kuinunua hoteli ya Kilimanjaro akaishia kuambiwa hana uwezo wa kuiendesha baadaye alipojaribu kutafuta fursa ya kuwekeza kwenye vitalu vya gesi akaishia kuitwa mchuuzi na Waziri ambaye leo yupo katika serikali ya awamu ya tano. KRUB inasikitishwa na hali hii na inajiliza kama mfanyakiashara aliyefanikiwa kama Dr Regnald Mengi anaweza kunyanyaswa hivyo, je Watanzania wa kawaida hufanywa je?

**Mheshimiwa Spika**, Serikali za CCM zimeshindwa kabisa kutumia ardhi na raslimali asilia za nchi yetu kama mtaji kwa watanzania katika ubia na wawekezaji wa nje.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kiasi kikubwa watanzania ambao walihamasishwa kujunga pamoja na kuwa na nguvu ya pamoja katika kupata kandarasi za Serikali hasa katika sekta ya ujenzi, dhana hiyo imepelekea wazawa kufilisika au kufilisiwa na mabenki kwani walikopa ili kufanya kazi za Serikali. Hadi Machi, 2015 Deni la ndani ni shilingi trilioni 9.4 ambazo ni sawa na asilimia 26.8 ya Deni la Taifa. Kati ya hizo deni la makandarasi, Wazabuni mbalimbali na Watumishi wa Serikali lilifikia sh. trilioni 1.3.<sup>6</sup>

**Mheshimiwa Spika**, Katika hali kama hii ambapo Serikali baada ya kupatiwa huduma hailipi au kuwawezesha watanzania ili wabaki katika biashara na badala yake inawalizimisha kujingiza katika madeni zaidi na mwishowe wanafilisika.

**Mheshimiwa Spika**, Mwaka jana Mhandisi aliyekuwa anamiliki kampuni ya ujenzi iliyokuwa inajenga barabara alijua kutokana na Serikali kutokulipa kwa wakati kampuni yake, Kambi ya Upinzani Bungeni inajiliza katika hali kama hii ya kuwadidimiza watanzania hicho kipato cha uchumi wa kati kinategemewa kuwanufaisha wakina nani? Kitafikiwa kwa hali kama hii?

<sup>6</sup>Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara iliyowasilishwa Bungeni February 4, 2015

#### 4.1 TIC NA UWEKEZAJI WA KUSUASUA NCHINI

**Mheshimiwa Spika**, Hali ya uwekezaji nchini hairidhishi hata kidogo hii ni kutokana na marekebisho ya mara kwa mara ya sheria zinazosimamia vivutio vya uwekezaji, urasimu, rushwa, ukosefu wa uratibu n.k. TIC katika taarifa yake ya machi 2016 ya hali ya uwekezaji 2005 – 2015 inaonyesha kuwa miradi imepungua toka 211 mwaka 2005 mpaka kufikia 5 tu 2014, hali inayothibitisha ukweli huo.

**Mheshimiwa Spika**, Sababu nyingine zinatokana na utawala mbovu kama ucheleweshaji wa vibali mbalimbali vya kuwasaidia wawekezaji kuendeleza miradi yao, umeme usiokuwa wa uhakika, ubovu na urasimu wa usafirishaji na bandari ya Dar es salaam kuwa na urasimu uliokithiri, migogoro ya ardhi isiyotatuliwa, raslimali fedha zisizokidhi mahitaji ya TIC mfano 2013/14 kilipang'iwa ruzuku (OC) ya sh. 700,000,000 lakini kilipewa sh. 350,000,000 tu ikilinganishwa na mahitaji halisi ya sh. Bilioni 3 mwaka huu 2016/17 hakikupewa hata senti moja, mlolongo wa kodi na ufanisi duni wa wakala wa serikali, bodi za mazao na riba kubwa zinazotozwa na taasisi za fedha .

#### 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**; Msimamo wa Kambi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na Ilani ya Uchaguzi ya CHADEMA/UKAWA iliyouzwa na Mgombea Urais wa CHADEMA/UKAWA Mhe. Edward Lowassa tuliwaahidi Watanzania kuwa katika kipindi cha miaka mitano yaani 2015 – 2020 naomba kunukuu tamko la Ilani, alisema kuwa<sup>7</sup> “**Tutainua mchango huu wa sekta hii muhimu (ya viwanda) ufikie siyo chini ya asilimia kumi na tano (15%) katika miaka yetu mitano ya kwanza**”. Tutafanya hivyo kwa:

- 1) Kuimarisha sekta ya viwanda kuwa mhimili wa uchumi kwa uzalishaji wa bidhaa na ajira endelevu;
- 2) Kujenga viwanda vipyta vya kusindika mazao ya kilimo, uvuvi na ufugaji;
- 3) kuingia mikataba ya kuleta technologia ya kutengeneza bidhaa badala ya kuleta bidhaa;
- 4) Kuhakikisha kuwa ndani ya miaka mitano asilimia (75%) ya mali ghafi zote za Tanzania zinasindikwa kabla ya kusafirishwa nje ili kuongeza mapato na ajira ya mamilioni ya vijana;

<sup>7</sup> ILANI YA CHADEMA/UKAWA ukurasa wa 45.

5) Kutoa kipaumbele na vishawishi maalum kwa viwanda vya kuendeleza kilimo. Kwa mfano, tutaendeleza viwanda vya mbolea kulingana na mahitaji ya taifa na uuzaji wa ziada ya bidhaa hiyo nje ya nchi; pili viwanda vya kutengeneza mbegu bora na madawa ya kilimo;

6) Hatutaruhusu uuzaji nje ya nchi wa korosho ambazo hazijabanguliwa na kuhakikisha kwamba asilimia mia moja ya korosho zote tunazozalisha (zaidi ya tani laki mbili) zitabanguliwa hapa Tanzania na kuuzwa kwa walaji wa ndani na nje;

7) Hatutaruhusu uuzaji nje ya nchi ngozi ambazo hazijasindikwa na kuhakikisha kwamba zinaongezewa thamani ya kuziwezesha zizalishe bidhaa zote zinazotokana na ngozi;

8) Kufufua na kuongeza viwanda vyetu vya nguo ili tuweze kusindika kiwango kitachofikia asilimia sabini na tano (75%) ya pamba inayozalishwa Tanzania.

9) Kuimarisha na kukuza usindikaji wa mazao ya katani, kahawa, tumbaku na chai ili kuhakikisha ongezeko kubwa la thamani katika mazao haya na ongezek kubwa la bidhaa zinazotokana na mazao haya.

10) Kuanzisha Benki ya Ukuzaji wa Viwanda yenyeye riba nafuu. Ingawaje tatizo la ukosefu wa benki limesababishwa na uholela, udhaifu, ubadhirifu na ufisadi katika sera na usimamizi katika Serikali za CCM. Tulikuwa na benki ya maendeleo Vijiji(CRDB), NMB, NBC, THB n.k zote zimechuuzwa na sasa tunaanza tena tulikotoka.

**Mheshimiwa Spika**, serikali za CCM kwa utamaduni wake wa kutaka kuonekana inafanya imekuwa ikijiwekea vipaumbele vingi na wasivyoweza kutekeleza kutokana na kujaribu kushika kila kitu na mwishowe kushindwa vyote . Tunataka utamaduni huu sasa ukome kwani unaliingizia taifa hasara kwa kutenga fedha kidogo kidogo kwenye miradi na hatimaye kushindwa kukamilisha miradi husika kwa wakati na huku gharama za miradi zikukua maradufu. Fidia kwa maeneo ya EPZ na SEZ sasa ni shs bilioni 190.9 toka shs.bilioni 60 tathmini ilivyofanyika.

**Mheshimiwa Spika, Kambi** rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kuwa msimamo huo ndio ulikuwa unatakiwa kupewa msukumo katika kipindi cha miaka mitano ijayo kuanzia sasa.

**Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni**, inasilitiza na kuendelea kuishauri Serikali kuwa bado inaweza kubadilisha mwelekeo wake kwa kuzingatia msimamo wa Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Maendeleo ya Sekta ya viwanda

katika kipindi cha miaka mitano ijayo, kwani huo ndio mwelekeo sahihi katika kufikia azima ya kuwa na Tanzania yenye viwanda, kinyume na hapo ni sawa na kukimbiza upepo.

**Mheshimiwa Spika**, kamwe tusijiaminishe kuwa eti tunaweza kufikia taifa la viwanda kwa kutenga **shilingi bilioni 42.159 kwenye bajeti ya mwaka**, kama fedha za Maendeleo kwa ajili ya Wizara ya Viwanda, Biashara na uwekezaji takriban asilimia 0.3 ya fedha zote za maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo kwa niaba ya kambi ya upinzani naomba kuwasilisha.

.....  
**ANTHONY CALIST KOMU (MB)**

MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI  
WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI

**06.05.2016**

**KIAMBATANISHO A.**

Orodha ya viwanda vilivyobinafsishwa na kushindwa kuendelea na uzalishaji kwa muda mrefu Nchini;

1. Central Maintenance Service Centre
2. Tanzania Bag Corporation Ltd-Moshi
3. Kisarawe Brick Manufacturers Ltd.
4. Mbeya Ceramics Company Ltd
5. Steel Rolling Mills
6. Tanganyika Packers Ltd- Shinyanga Meat Plat
7. Lupembe Tea Factory- Njombe
8. Mlingali Tea Estate
9. Ubungo Garments Limited
10. Tanzania China Friendship Textile Mills
11. Dakawa Rice Mill Complex
12. Poly sacks Company Ltd
13. LRT Motors Ltd
14. Moproco
15. Tanzania Shoe Company
16. Illemela Fish Processing Plant
17. Nyanza Engineering Foundry Company Ltd
18. CDA Zuzu Factory
19. Aggregates Processing Plat
20. Vipe Vibrated Concrete Plant

21. Asphalt Plant
22. Kagera Regional Transport Company
23. Arusha Metal Industries
24. Mang'ula Mechanical and Machine Tools Ltd (MMMT)
25. Mwanza Tanneries Ltd
26. Morogoro Shoes Ltd
27. Morogoro Ceramics Ltd
28. Kilimanjaro Textile Mills Ltd
29. Express Tanzania Ltd
30. Zana za Kilimo Mbeya
31. Iringa RTC
32. Moshi Hand Tools Ltd

**NAIBU NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tutaendelea na uchangiaji. Tutaanza na Mheshimiwa Khatib Said Haji atafuatiwa na Mheshimiwa Raphael Michael Japhary na Mheshimiwa Masoud Suleiman Nchambi ajiandae.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuwa mchangiaji wa mwanzo katika hotuba hii Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na kuweza kusimama hapa. Napenda ni-declare interest mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naanza kwa masikitiko, hotuba ya Mheshimiwa Waziri ambayo naamini maneno yale mengi kama yatakelezwani mwendelezo mzuri na ningependa na ningetamani sana Watanzania waisikie na pia wasikie maoni ya Kambi ya Upinzani ili kuonesha mwelekeo sahihi wa ile kauli ya Rais ya Tanzania ya Viwanda, nilitamani sana. Kwa bahati mbaya sana Bunge hili bado tumeendelea kukaa gizani, tutaambiana sisi kwa sisi, tunaendelea kuambiana haya tulioambiana kwenye Kamati, mengi tunayajua.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nifarijike jana tu kwa Wabunge wawili wa CCM, niwapongeze sana kwa kitendo chao kizuri sana walichoionesa jamii ya Watanzania kwamba sisi siyo wapinzani tu tunaopenda haya tunayoyasema hapa kwamba Bunge hili lionekane live. Wao walitumia jitihada ya kupigana picha za video, Mheshimiwa Abuu na Mheshimiwa Aeshi na gazeti la Nipashe likaonesha Watanzania kumbe letu ni moja, lakini tunatofautiana tu kimtazamo.

Mwimbaji mmoja kule Zanzibar aliimba nyimbo akasema kisebusebu na kiroho kiko papo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya tuendelee kuambiana katika njia za upole nadhani tutaelewana tu, hakuna haja, muone tu umuhimu wa haya mambo. Mheshimiwa Mwijage leo katika majibu yako ya maswali hapa, kuna raia wangu alinipigia akasema nilitamani nimwone Mwijage kila muda lakini wapi umeyatupa ndugu yangu hulitetei hili. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kwamba Msemaji wa Kamati, Makamu Mwenyekiti alizungumzia jambo moja zuri. Alizungumzia umuhimu wa biashara na namna Serikali inavyowa-treat watu wanaoingiza bidhaa kutoka nje kutokana na ukadiriaji wa kodi ambazo wakati mwingine tunasema hazina mashiko. Kwa mfano, hivi sasa Watanzania wengi wanafilisiwa magari yao katika Bandari ya Dar es Salaam kwa tatizo moja tu. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe hukuwepo Bunge la Kumi, nilisimama hapa wakati Waziri wa Fedha akiwa Mheshimiwa Saada Mkuya nikasema ikiwa Serikali mmeweza kuweka Maafisa wa TBS katika nchi tunazochukua bidhaa kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa ubora wa bidhaa, ni kipi kinachowashinda katika suala hili la bei? Kwa sababu nchi ambazo Watanzania tunachukua magari kubwa ni tatu tu hapa duniani, ni Uingereza, Japan na Dubai, wakaweka usahihi wa ile bei ya gari Mtanzania analonunua ili akifika hapa atozwe kodi kulingana na thamani halisi ya gari. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa sababu kauli ile ilitoka *left hand* ikaonekana haifai. Leo Wabunge wenyewe wameonja bakora hii, wameagiza magari, thamani ya gari anavyolinunua akija hapa TRA tayari wameweka bei yao ambayo hiyo ni bei *astaghfirullah* wameifanya kama bei ya Msahafu maana Msahafu na Bibilia ndiyo ambayo haipingiki. Hii inapelekea watu kuona ugumu kiasi fulani wa kufanya biashara na watu wengi kufilisiwa gari zao zinapofika pale bandarini. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, naweka msisitizo wa hili, gari aina ya Suzuki Carry inauzwa si zaidi ya dola 500 Japan na ukiingia kwenye mitandao utaziona hizo bei, leo inachukuliwa hata *carry* ni gari ya anasa? Tungeondoa kutumia wanyama huko vijijini, mkulima mdogo mdogo analima mazao yake badala ya kutumia wanyama na kuokoa muda na kufikisha bidhaa zake katika soko angeweza kununua *carry* kwa dola 500 akija hapa akalipishwa kwa thamani ya ununuza na usafirishaji ambayo haizidi dola 800, dola 1500 ikapigwa thamani lakini ukifikisha hicho kigari TRA wanakuambia thamani yake ni dola 2,500. Hii si haki, ni dhuluma na ni aibu sana kwa Serikali kuwadhulumu raia wake, tuliangalieni hili. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kumekuwa na wigo na maneno mengi juu ya biashara ya magendo baina ya Tanzania Bara na Zanzibar. Yamekuwa yakisemwa njia za panya zimekithiri katika ukanda wa bahari, lakini sababu ni moja. Sababu inayochangia hili ni vikwazo vya wafanyabiashara wa Zanzibar wanapoingiza bidhaa katika soko la Tanzania Bara. Kumekuwa na vikwazo na ugumu mkubwa sana ambao unasababishwa na Mamlaka ya Bandari na TRA Dar es Salaam kuwafanya wafanyabiashara wa Zanzibar watafute njia mbadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata katika hali ya kawaida ukimziba mdomo lazima atatoa pumzi kwenye pua. Wafanyabiashara wale wa Zanzibar cha kushangaza TRA ni moja, maafisa wa TRA wanateuliwa na Kamishna Mkuu wanafanya kazi kule Zanzibar, hakuna TRA mbili. Leo hii bidhaa kutoka Zanzibar zinapofika Dar es Salaam zinatazamwa kwa mtazamo hasi na kuonekana ni bidhaa ambazo hazifai kuingia ndani ya nchi yaani zinaangaliwa kwa ukakasi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na Tume za Pamoja toka miaka ishirini ya Bunge hili kujadili kuondoa vikwazo vya wafanyabiashara wa Tanzania Bara na Zanzibar lakini hili nalo linaonekana ni jipu. Ninukuu usemi wa Mheshimiwa Nahodha, Waziri Kiongozi Mstaafu wa Zanzibar namheshimu sana kwamba ni jukumu la uchumi mkubwa kusaidia uchumi mdogo. Kwa hiyo, badala ya kuitazama Zanzibar kwa jicho hasi na wafanyabiashara wake lazima sasa muwatazame kwa mtazamo wa huruma na kuwaongoza katika njia stahiki ili biashara ifanyike pasipo na vikwazo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo, nilisema na ninarudia raia wa nchi yoyote jirani ana haki ya kutoka na gari lake akaingia Tanzania, akitumia ruhusa ya kibali maalum kwa kukaa ndani ya nchi karibu miezi mitatu. Hilo kwa Zanzibar limeondoka na halipo, hawezি Mzanzibar kutamani kwenda Mikumi na gari yake na watoto wake ku-enjoy akaingiza gari lile na akapewa *permit* ya kwamba utakaa miezi mitatu gari kwa sababu labda kodi ya Zanzibar na hapa ina tofauti ukimaliza miezi mitatu urudi Zanzibar, hilo halipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii raia wa Burundi ambaye hayupo kwenye Muungano ataingia na gari lake na ata-enjoy kukaa nchi hii anavyotaka Wakongo halikadhalika. Kwa hiyo, hili nalo ni jambo linalotakiwa liwekewe utaratibu. Wapo wanaoleta magari yao kwa biashara wapitie ule utaratibu wote wa kiforodha na kama kuna makusanyo ya kodi ni sawa lakini anayekusudia kuja kukaa na gari lake katika kipindi kifupi kuna tatizo gani kupewa *temporary document* ya kukaa hapa? (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, mbona mkitoka na gari zenu hapa mkiingia kule hakuna kikwazo hiki, kwa nini? Leo hii ukitoka na gari lako Tanzania Bara

ukiingia nalo Zanzibar njoo Konde uta-enjoy utaenda kulala under water room kule Jimboni kwangu hakuna tatizo lakini hapa kwa nini? Tatizo ni kwamba ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda umeisha Mheshimiwa.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Hatujipambi wakati wa kuolewa twajipamba wakati wa kuachwa. (Makofij)

**NAIBU SPIKA:** Sawa. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Raphael Michael Japhary atafuatiwa na Mheshimiwa Masoud Suleiman Nchambi na Mheshimiwa Ezekiel Maige ajiandae.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kushukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia. Pia niipongeze sana hotuba ya msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa namna ambavyo ipo katika mtazamo wa kuisaidia Serikali kuboresha mpango wake wa kuifanya Tanzania ya viwanda. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maeneo machache ya kutoa mchango wangu. Mpango wa kuifanya Tanzania kuwa ya viwanda ni mwema na maombi yetu sote tufikie hapo. Lakini mashaka yangu mimi ni sababu zilizotusababisha tukashindwa kufikia hapo siku za nyuma. Kwa sababu miaka ya 80 tulikuwa tunaenda vizuri, ni kizungumkuti gani kilituingia mpaka tukaamua kuruhusu mipango isiyo mizuri ambayo imelifikisha Taifa hapa mpaka leo ndiyo tunaanza kutafakari namna ya kuifikisha Tanzania kuwa nchi ya viwanda. Hofu yangu ni kwamba inawezekana mpango huu wa Serikali ukawa ni mpango unaosikika vizuri masikioni lakini bado ukawa na shida katika utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nini ambavyo tunavikosa katika Taifa hili? Ukiangalia Serikali ya Awamu ya Tano inafanya kazi kama vile Serikali imeanguka leo, haikuwepo tangu huko nyuma, kama vile ni chama kipyka kimeanza kutawala Taifa hili wala sio Chama cha Mapinduzi kilichokuwa kinatawala. Kwa hiyo, hakuna muunganiko kati ya mfumo wa Serikali iliyopita na mfumo wa Serikali inayofuata sasa ambao ungesaidia kujuu ni mabaya yapi mnayaacha, ni mazuri yapi mnayapokea. Matokeo yake kila mtu anakuja na mtazamo kama vile anataka kuizaa Tanzania leo wakati Tanzania ina miaka 50 tangu imeitwa Tanzania. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, hofu yangu kubwa ni consistency ya government. Hiyo ndiyo inanipa mashaka kwamba kuna uwezekano mkubwa wa kutofikia hii mipango yote ambayo tumeipanga. Mimi ukiniuliza leo

ningekuambia kilichokosekana katika Serikali zilizopita, ya Awamu ya Tatu na ya Nne ni dhamira na uzalendo kwa viongozi waliopewa dhamana, ndicho ambacho ningekujibu. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo kama Rais wetu kweli ana dhamira na kama Waziri wa Viwanda leo alivyotoa hotuba yake kweli ndiyo dhamira yake hivyo ana wajibu wa kuhakikisha kwamba anaambukiza hiyo dhamira kwa watu wote wanaomzunguka ili Tanzania ifike hapo inapotaka kufika kuwa Tanzania ya viwanda. Kama hatutaweza kuibadilisha *culture* ya rushwa, ubadhirifu na ujisadi zilizopo katika Taifa hili hizi zitakuwa ni nyimbo na ngojera ambazo zitaimbwa kila mwaka na hatufiki popote. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nachoshauri ni kwamba Serikali ijiandae katika hilo, kwanza kwa kubadilisha utamaduni wa watendaji wetu wa kuliibia na kuliumiza Taifa ili kidogo tunachokipata sasa tukielekeze kwenye maendeleo. Nina hakika tukifanya hivyo tunaweze kufika mahali fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utangulizi huo, nataka niongelee suala la wafanyabiashara kama wenzangu waliotangulia walivyosema. Taifa hili bado halijaonyesha kiukweli, kama maneno nitakayotumia siyo mazuri sana lakini nadhani hivyo kwamba Taifa hili bado halijaonyesha kiukweli kwamba lina haja ya kuwasaidia wafanyabiashara wake wa ndani, bado halijaonyesha kwa dhoni. Ndiyo haya unasikia mambo ya kodi watu wanapoingiza mali lakini hata wafanyabiashara wa ndani mazingira yao waliokekewa vikwazo vyao vimeduwa ni vingi sana kiasi kwamba uwezo wa wafanyabiashara hawa kufanya kazi yao vizuri wakawa ni sehemu ya wawekezaji muhimu katika Taifa hili umeduwa ni mdogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wakati tumejikuta tunathamini wawekezaji wa nje kuliko wa ndani, siyo jambo bayo lakini siyo vizuri kushindwa kuwatengenezea fursa na mipango mizuri wafanyabishara wa ndani ili waweze kuwa wawekezaji ambao wana uhakika kuliko wawekezaji wa nje na watakaohakikisha Taifa hili kubaki na pato lake la ndani na uchumi wake kukua kwa haraka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu kwa Serikali ni vizuri tuhakikishe tunaondoa vikwazo kwa wafanyabiashara wetu wa ndani, tozo zimekuwa nyingi mmo. Leo ukiuliza hivi ni kwa nini bado corporate tax ni kubwa kwa wafanyabiashara hakuna majibu ambayo ni ya msingi sana. Ukiuliza kwa nini VAT bado ni kubwa kwa wafanyabiashara hakuna jibu ambalo ni la msingi sana. Kanuni mojawapo ya kodi ni kuwa na compliance ili mfanyakibashara aweze kulipa kodi hiyo. Sasa leo kodi inatumika kumfilisi mfanyakibashara, anaingia kwenye uchumi kesho, kesho kutwa anafilisiwa na kodi na anafilisiwa na Watanzania wenzake halafu mnakwenda kufikiri kuwaneemesha watu wa

nje waje kuwekeza wakati mnashindwa kuwawezesha wafanyabiashara wa ndani wakafanya vizuri maana yake ni kwamba hamsaidii wafanyabiashara wenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo pamoja na jithada ya kuvutia wawekezaji wa nje ni vizuri tusaidie wafanyabiashara wetu wa ndani ili wafanye biashara zao vizuri. Hebu tuangalieni tax regime yetu kama ipo sawa sawa na inawasaidia wafanyabiashara wa ndani? Kodi ya Taifa hili imekuwa ni kikwazo kikubwa kwa wafanyabiashara. Leo katika nchi hii mfanyakibashara akimuona mtu wa TRA ni afadhali amuone simba kwa jinsi ambavyo muda wote anafikiri kufilisiwa. Bahati mbaya Serikali inajenga taswira hasi kwa wafanyabiashara kwamba wote ni wizi, ndiyo inavyoonekana hivyo, hakuna wakati maafisa wa TRA wamekuwa tayari kuamini taarifa halisi za wafanyabiashara na ndiyo maana leo unaskia gari inanunuliwa nje shilingi dola 500 inakuja kuchajiwa kodi ya dola 2,000 kwa sababu ya kutoamini wafanyabiashara. Nadhani ni muhimu sana kuangalia eneo hili kama tuna dhamira ya kuwafanya wafanyabiashara hao wawekeze katika sekta ya viwanda. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niongelee suala la sekta isiyo rasmi. Kama Mheshimiwa Waziri alivyoonyesha dhamira ya Serikali ya kuhakikisha anasaidia viwanda vidogo, vidogo sana na vya kati na wafanyabiashara wadogo sana na wa kati, ni lazima sekta hii ipewe kipaumbele. Kipaumbele nachozungumzia siyo kwa maneno ya kisiasa, siyo kwa kuzungumzia habari ya asilimia tano ya Halmashauri kwa akina mama ambayo haipatikani, ni lazima tujenge mkakati rasmi wa kuhakikisha kwamba tunatengeneza mazingira ya kuwasaidia wafanyabiashara wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo katika Taifa hili Mheshimiwa Rais anasema wafanyabiashara wadogo wasibugudhiwe, wasisumbuliwe katika Halmashauri zao lakini huko chini Wakurugenzi wanaumbua wafanyabiashara hao. Ni lini wafanyabiashara hawa wataweza kwenda mbele? Rais anatoa maagizo, huko chini maagizo ni mengine. Rais anaagiza kwamba watu watengewe maeneo ya kufanya biashara, hakuna maeneo ya kufanya biashara kila siku watu hawa wanaishi kama swala anayemuogopa simba katika Taifa hili. Hatuwezi kupeleka Taifa hili mbele, ile sekta ni muhimu sana na ina uwezo ikitumika vizuri. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimekuwa Meya katika Halmashauri yangu najua ikitumika vizuri ina uwezo wa kulitoa Taifa hili hapa kulipeleka mahali pengine na wana uwezo hao kuwekeza vizuri katika eneo la viwanda. Kwa hiyo, ni vizuri mtengeneze mkakati thabiti wa kuwasaidia hawa watu kule chini. Toeni maelekezo kwa Wakurugenzi wawe creative, wabuni namna gani wawasaidie wale wafanyabiashara rather than kuwapiga na kuwasumbua katika maeneo yao wanayofanya biashara ili nao waishi kama Watanzania wengine na wapate faida ya matunda haya tunayotaka kuyafikia ya lengo la

kuwa na Tanzania mpya ya viwanda. Nilidhani hiyo sekta ni muhimu sana na muione kama engine muhimu sana inayoweza kutusaidia kufika tunapotaka kwenda. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nizungumzie kidogo kwenye suala la forward and backward linkage ya sekta zetu. Bado tuna tatizo kama wengi walivyosema la kilimo, ni vizuri tuone sasa kwamba kama tunataka kweli kufika kwenye viwanda pamoja na matatizo hayo huko nyuma ambayo tunaweza tukayarekebisha, lakini ki ukweli ni lazima tukiinue kilimo chetu kiwe ni kilimo chenye sura ya viwanda. Kama hatutafanikiwa hili bado tutaimba tu viwanda na hatutafikia lengo. Bila kumung'unya maneno...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa mzungumzaji)

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha hoja yangu, ahsante sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Masoud Suleiman Nchambi atafuatiwa na Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige.

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nikushukuru sana na nikupongeze kwa moyo wako wa kijasiri wakati kina mama wenzako walipokuwa wakijaribu kukuzomea. Nikutie moyo kwani hata Yesu Kristo wakati akitangaza injili alipokuwa akipita katika mitaa wengi walimbeza, wengi walimuuliza eti wewe ni mwana wa Mungu, eti wewe ni mtakatifu na yeye aliwajibu ninyi mwasema. (Makofi)

Kwa hiyo, hicho wanachokisema wao ni wao wanakisema. Mimi nikutie moyo mama yangu umeanza vizuri, ongeza kasi na sisi Wabunge shapu tutaendelea kukunoa uwe shapu, mambo yako yaende kwa ushapu na Bunge hili lifanye kazi ya kutekeleza mipango mizuri ambayo wananchi wameingia mkataba na Chama cha Mapinduzi wakati wa uchaguzi na Chama cha Mapinduzi kimekabidhi llani ambayo inatekelezwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, maandiko matakatifu yanasema na wala msifanane na hao kwa kuwa baba yenu anayajua mahitaji yenu kabla ninyi hamjamuomba. Kwa hiyo, sisi tunayo imani Watanzania lipo jambo waliliomba na kupitia Serikali ya Chama cha Mapinduzi Mungu amekabidhi usukani wakiwa na imani wakati wanaomba kama maandiko yanavyosema, niombeni na mkiamini mtapata, Bwana Asifiwe. (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Amini.

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa niwape hesabu rahisi sana Waheshimiwa Wabunge. Mbunge mmoja wa Upinzani amesifu sana hotuba yao ya Upinzani, kitabu hiki kilichowasilishwa na kambi ya wenzetu kina kurasa 28 wakati kitabu cha Mheshimiwa Mwijage kina kurasa 217. Katika kurasa 28 zilizowasilishwa na Kambi ya Upinzani, ukurasa wa kwanza, mwasilishaji amewashukuru wapiga kura wake, ukurasa wa pili ametukana, ukurasa wa nne ametoa lawama tu, ukurasa wa nane imetukana na kukisema Chama cha Mapinduzi, ukurasa wa 27 na 28 ni kama viambatanisho. Kwa hiyo, ni dhahiri katika kurasa hizi sita zimebaki 22 ambazo asilimia 70 ya mistari iliyopo katika kitabu hiki kinachowasilishwa na wenzetu wa upinzani ni lawama, kejeli, matusi na mengineyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ukipiga hesabu rahisi kurasa 217 ukigawanya kwa kurasa 22 ni kwamba wapinzani hawayajui matatizo ya Watanzania na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuitia Waziri mchapakazi, hodari Mheshimiwa Mwijage amekwenda mara kumi zaidi ya matatizo wao wanavyoyajua, hiyo ni hesabu rahisi.

Kwa hiyo, ndugu zangu Wabunge mimi niwatie moyo kazi wanayoifanya wenzetu kwa sisi wafugaji tunapokwenda na ng'ombe zetu kwenye mabwawa ama malambo, huwa wanaangalia saa hiyo sauti ya vyura ipo wapi ili wajue maji pale ndiyo yana kina kirefu wanakwenda wanakunywa. Kwa hiyo, wao wanapiga kelele kama vyura sisi tunanywesha ng'ombe zetu, Watanzania wanapata maziwa, wanapata nyama ambazo sasa ndizo shughuli za maendeleo na matatizo na kero zao. Hawa ndiyo kazi iliyowaleta Bungeni wala msiwalaumu, wataendelea kupiga kelele kama vyura na ninyi Mawaziri chapeni kazi sisi Wabunge tutawasaidia na Wabunge wa CCM tufanye kazi ya kuishauri na kuikosoa na kuielekeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Magufuli amekuja na mkakati wa mabadiliko. Nilikuwa napitapita mtaani naongea na wenzangu kule wanasema kazi anayoifanya Mheshimiwa Magufuli ndiyo haswa ilikuwa kazi yetu sisi UKAWA, tena wengine wenzangu wa Zanzibar maana kuna Wabunge wenzangu kule Zanzibar wanakalia Dole, wengine wanakalia Mkanyageni, wengine wapo Mwembemchomeke, ni rafiki zangu huwa nakwenda kuwatemebelea wakati mwagine katika maeneo yao hayo niliyoyataja wana Kiswahili ambacho kinazingatia misingi ya neno waliloliongea wanasema haswa anachokifanya Mheshimiwa Magufuli ndiyo ilikuwa hoja ya UKAWA kutekeleza mambo anayoyafanya yeye. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka niwaambie ndugu zangu wakati fulani niliwahi kumwambia Waziri fulani wa CCM humu ndani nisingependa kumtaja, muda mwagine mtu akisoma sana akafika mwisho huwa nahisi mimi

akili inarudi reverse. Sasa inategemea, inarudi reverse pengine dhamira yake ama ubongo wake umepata frustration fulani maana shetani huwa haonekani, unaona matendo unasema huyu matendo yake yanafanana na shetani. Maneno yake na matamshi yake yanafanana na shetani lakini mimi sijawahi kumuona na sina reference ya kitabu chochote cha Mungu ambacho kiliwahi kumuona shetani kuititia binadamu hapa duniani, lakini matendo ya mtu ndio yanamfanya aonekane ni mtakatifu ama shetani. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ndugu zangu zipo lugha zinatumika ambazo Wabunge hao hao wanaotumia lugha hizo wanakuja na madai ya wao kuheshimika katika Taifa hili na Bunge hili, haiwezekani! Waziri anayechukua dhamana ya Wizara katika Wizara yake leo anaitwa muhuni, tapeli na maneno mengine.

**MBUNGE FULANI:** Muda unaisha.

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Wacha muda uishe lakini nataka niwaeleze ukweli, kwa sababu kazi zenu ninyi ndizo hizo mnazozifanya. Lugha hizi hazipendezi sana...

**MBUNGE FULANI:** Mwambie utachangia kwa maandishi.

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Nitachangia kwa maandishi msiwe na haraka, mbona sindano zikiwa zinawaingia upande wenu mnapiga kelele, quinine huwasha baadaye masikioni, tulieni kwanza tuwape vidonge vyenu maana mmekuja kufanya kazi ambayo mnaifanya. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi hawa kelele zao wala hzinipi shida mimi ni Mbunge shapu wala sina matatizo na wao.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hoja iliyoko mezani ni hii hapa.

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo tatizo la baadhi ya majimbo kuruhusu watu ambao hawakuwa na sifa na wala hawakujandaa kuja kutetea wananchi wao kuingia ndani ya nyumba hii lakini angekuwa amejiandaa, amejipanga na anajua wajibu wake wa kibunge ndani ya jumba hili takatifu asingekuwa anaropoka kama mwendawazimu. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikuhakikishie Watanzania wanaona na wanasikia. Nakuapia Mungu niliwahi kuwaambia wenzeni, shemeji zangu wa Kigoma akina Kafulila, niliwaambia kasomeni Luka 6:38, mtalipwa kwa kile mnachokifanya ndani ya jumba hili leo wako wapi? Akina Machali, Kafulila na Mkosamali wako wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu anayeropoka maneno haya wapiga kura wake watamuona, watamsikia, mwaka 2020 tutaagana naye kwa sababu kazi aliyoifanya ndiyo hiyo ya kuzomea na kutukana, hatarudi humu wala asiwape shida yoyote. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwaeleza wenzangu na kuwakumbusha misingi na wajibu wao ndani ya Bunge nieleze machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko tatizo kubwa juu ya wakulima wetu, wakulima wetu wanapata tabu sana. Nikuombe Mheshimiwa Mwijage katika maeneo machache kulingana na muda na mengine nitachangia kwa maandishi. Mkitaka wakulima wa pamba waendelee ni lazima Serikali ijiandae kudhibiti bidhaa zote zinazotokana na mazao ya pamba zinazoingia nchini. Wako Wabunge humu walipiga kampeni tukatoa ushuru wa mazao mengi ya pamba kuingia katika Taifa hili tumewakandamiza Wasukuma wenzangu. Nataka nikuhakikishie zao la pamba nenda ka-review ili viwanda viwepo kutokana na zao la pamba. (Makofi)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nchambi muda umeisha.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, ubarikiwe sana.

**MBUNGE FULANI:** Huyo siyo Msukuma, anajipendekeza.

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Naunga mkono hoja. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimwia Ezekiel Magolyo Maige.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie bajeti hii ya Wizara ya Biashara. Naomba nianze kwanza kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kuwa hivi nilivyo leo. Kipekee niwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Msalala kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Heche naomba tumsikilize Mheshimiwa Maige.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa kuwa wananchi hawa wa Jimbo langu la Msalala wamenipa nafasi kwa mara

nyingine ya kuja kuwawakilisha hapa Bungeni, wamenipa heshima kubwa, naamini nitaitumia vizuri ...

**MBUNGE FULANI:** Hawakuoni.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Kwa ajili ya maslahi na maendeleo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais na timu yake ambayo kwa kweli dhahiri kazi inayofanyika kila Mtanzania anaikubali.

Mimi naamini kampeni nzuri inafanywa na Serikali yetu kupitia matendo ambayo yanafanywa na kwa maana hiyo wana-CCM wenzangu wala tusipate hofu mwaka 2020 kama siyo robo basi watakuwa wamebaki theluthi au watakuwa wamepungua zaidi kwa sababu kazi inafanyika vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa rafiki yangu sana Waziri wa Viwanda. Hotuba yake imesheheni matumaini makubwa sana. Kwa kweli naamini, endapo nia ya Waziri itatekelezwa kama ambavyo mwenyewe anatamani tutafika kwenye nchi ya viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimsaidie Mheshimiwa Waziri baadhi ya maeneo ambayo yanaweza kumsaidia sana. Cha kwanza naomba ufahamu kwamba Wizara yake ni kiungo. Serikali kwa miaka mingi ilishajitoa kwenye uzalishaji na kwenye biashara moja kwa moja. Serikali haijengi viwanda, haina mashamba, haifanyi chochote zaidi ya kuweka mazingira mazuri kwa biashara kufanyika. Ili biashara ziweze kufanyika cha kwanza ni muhimu kuangalia mazingira yanayoweza yakaruhusu biashara hizi kushamiri. Ili tuweze kufika huko, nikuombe Mheshimiwa Waziri rejea kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais alipolihutubia Bunge tarehe 20 Novemba, 2015, alituwekea dira kwamba anapenda ndani ya miaka mitano hii asilimia 40 ya ajira zitokane na viwanda. Ni suala kubwa ambalo nilitegemea kwenye hotuba yako kwa kiasi fulani ungeweza kuwa umeligusia. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nini kinachopaswa kufanyika kwenye eneo hili ambacho sijakisikia, ninachosikia tu ni kwamba tutakuwa na viwanda na kadhalika.

Nilipenda kupitia kauli hiyo ya Mheshimiwa Rais Waziri atufanyie study na atuletee ili nasi tuweze kuwa tunafuatilia na kumshauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kwanza, ni vizuri angeweza kutupa baseline data kwamba hivi sasa ajira zilizopo ni kiasi gani na zinazalishwa ngapi

kwa mwaka. Kati ya hizo ajira kiasi gani au asilimia ngapi inatokana na viwanda. Akishapata hiyo takwimu atuambie mwaka 2020, 40% ya ajira zote zitatokana na viwanda maana yake tutakuwa na ajira ngapi zitakazotokana na viwanda. Ili kufika huko aende mbele zaidi ajaribu kuangalia ni sekta zifi zinaweza zikampa hizo ajira zinazohitajika na kuzitazama hizo sekta ni vizuri pia akaangali ni vitu gani vya kufanya katika sekta hizo. Eneo mojawapo la muhimu la kuliangalia ni mazingira ya kodi, upatikanaji wa malighafi pia aina na upatikanaji wa wafanyakazi watakaofanya kazi kwenye hivyo viwanda na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la malighafi ambalo mimi nalionna ni muhimu sana hakuna eneo litakalotoa malighafi nyingi za ku-feed viwanda vyetu zaidi ya eneo ambalo rafiki yako na rafiki yangu na mdogo wangu Mheshimiwa Mwigulu Nchemba analisimamia, Wizara ya Kilimo. Wizara hii ya Kilimo ni Wizara pacha na Wizara hii, naomba mfanye kazi kwa pamoja. Sekta hii Mheshimiwa Waziri itakupa 95% ya malighafi zote unazohitaji. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano wa eneo moja, malighafi moja muhimu na kubwa inayoweza ikasaidia viwanda ni inayotokana na zao la pamba. Pamba inatoa nyuzi, nguo, mafuta, mashudu yanayotumika kulishia mifugo na vitu vingi ambavyo vyote vinakwenda kutumika kwenye viwanda. Angalia hali ya zao hili ambalo ndiyo malighafi muhimu kwa viwanda unavyohitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1995 pamba tuliozalisha nchini ilikuwa zaidi ya tani 600,000. Kwa takwimu za Mheshimiwa Mwigulu ambazo alizosoma hapa juzi mwaka 2014/2015 tumezalisha pamba tani 245,000 na tunategemea mwaka 2016 tutazalisha pamba tani 145,000 ina maana uzalishaji wa pamba umeshuka kutoka tani 600,000 miaka mitano iliyopita au kama siyo mitano ni kumi hadi wastani wa tani 150,000. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini uzalishaji wa zao la pamba umeanguka? Kama uzalishaji wa pamba unaendelea kuanguka maana yake hautapata malighafi na bila malighafi maana yake hautapata viwanda na usipopata viwanda, ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kufikia 40% ya ajira zitokane na viwanda haitatimia. Kuna nini kwenye pamba? Yapo matatizo mengi, kaeni na Mheshimiwa Mwigulu mshirikiane kupata majibu ya msingi ya matatizo ya eneo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo wanayokabiliana nayo wakulima wa pamba moja ni bei inayoratibiwa na soko la dunia. Ni lazima tutafute namna ya kupambana na tatizo la bei. Tuliwahi kupendekeza hapa kwamba ni vizuri tukaanzisha mfuko wa ku-stabilize bei ya pamba (*price stabilization fund*) ya pamba ili pale bei inapoanguka kwenye soko la duni mkulima aweze kupata

fidia. Ni wapi suala hili limefikia? Kaeni na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo mpate namna ya kutatua tatizo hili. (Makof)

Mhehimiwa Naibu Spika, tatizo la pili linalojitokeza ni suala la dawa. Mwaka huu tumeletewa dawa inaitwa “ninja” haiwi wadudu. Kimsingi kilichofanyika ni wizi, ni uhujumu uchumi. Mheshimiwa Mwigulu nakufahamu, nakuamini, naomba ufahamu kwamba mwaka huu pamba uzalishaji utakuwa chini ya nusu ya ile uliyotarajia kwa sababu dawa ilioletwa hii inayoitwa “ninja” haiwi kabisa wadudu badala yake wadudu wanafurahia kuwa kwenye maji maji ya ile dawa kwa sababu yanawapunguzia joto. Wanakula vizuri zaidi yale matunda ya pamba na pamba haikomai. Kwa hiyo, suala la dawa ya “ninja” naomba tupate taarifa ni nani aliye-supply na kwa nini haiui na hatua gani zinachukuliwa kwenye jambo hili ambalo ni uhujumu uchumi? (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni suala la mizani kwenye pamba. Kwa kawaida ninavyojuu mimi ni kwamba unapoenda kuuza kitu anayemiliki mizani ni yule muuzaji. Ukienda kwa mtu anayeaza sukari mzani utaukuta kwa muuza sukari, ukienda kwa mtu anayeaza kitu kingine chochote hata petrol station mzani au pump iko kwa muuzaji. Kwa zao la pamba pump au mizani anayo mnunuzi au wakala wake, jambo hili si sawa. Katika mazingira hayo, wanachezea mizani, tulianza na ile mizani ya ruler ikawa haitumiki, sasa hivi wanatumia mizani ya digital ndiyo wanaharibu kabisa wanawaibia wakulima wa pamba. Naomba shirikianeni hizi Wizara mbili mpate ufumbuzi wa tatizo la mizani ya pamba. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine kwenye suala hili la pamba ni kodi kwenye mafuta ambayo yanatokana na pamba hasa VAT ambayo inawanyima nafasi ya kushindana na mafuta yanayotoka nje lakini kubwa na mafuta wanayozalishwa na viwanda vingine. Kwa mfano, pale Shinyanga kuna kiwanda cha Mchina ambacho kimewekwa kwenye mazingira ya uwekezaji ya EPZ, amesamehewa kodi nyingi, wakulima wa kawaida na wenyi viwanda vidogo vidogo vingine vya ukamuaji wa mafuta ya pamba hawana misamaha hiyo, kwa hiyo mafuta wanayozalisha wanashindwa kushindana naye. Niombe eneo hili nalo mlirekebishe. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine hata yale mashudu wanayozalisha kutoka kwenye makapi yanayotokana na matunda ya pamba nayo yanatozwa VAT. Mimi navyojuu mali zote au vitu vyote vinavyotumika kwa ajili ya kuendeleza mifugo vinapaswa kusamehewa kodi. Mashudu yanayotokana na pamba yanatozwa VAT matokeo yake wafugaji wanashindwa kuyanunua na kunenepesha mifugo yao. Niombe Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Waziri Viwanda na Biashara shirikianeni kupata ufumbuzi, hizi kodi ambazo kimsingi wala hazina maana yoyote zaidi ya kuleta bugudha kwa wakulima na wafugaji ziweze kuondolewa. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuomba sana, Mheshimiwa Waziri kaa na wafanyabiashara, watakusaidia sana. Kwa kuwa wewe huwezi ukajenga viwanda basi ukae nao watakueleza wana matatizo makubwa ya jinsi kodi zinavyokokotolewa, wana matatizo makubwa jinsi wanavyopata malighafi, wana matatizo makubwa jinsi wafanyakazi wanaoajiriwa kwenye viwanda vyao wanavyo-behave. Sheria ya Kazi na Mahusiano Kazini kwa kiasi kikubwa inajenga mazingira ya wafanyakazi kutofanya vizuri kama ambavyo wawekezaji wanapenda. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache, naomba kusema kwamba naunga mkono sana hoja hii, namshauri Mheshimiwa Waziri aondoe vikwazo kwenye upatikanaji wa malighafi. Ahsante sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa. Sasa tutamsikia Mheshimiwa Ahmed Ally Salum.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii. Kwanza kabisa, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa hoja yake. Vilevile nimpongeze msaidizi wake mkuu, Dkt. Meru, Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara alikuwa EPZ, ni Katibu Mkuu mmoja mzuri sana, anafanya kazi vizuri, tulikuwa naye, namfahamu atakusaidia sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaka kuanzisha kiwanda au ili Tanzania iwe nchi ya viwanda, taasisi ya dunia inayotoa hali halisi ya mazingira mazuri ya kuanzisha viwanda nchi ya Tanzania ni ya 139 kati ya 184. Maana yake utaona Tanzania bado kuna vikwazo vingi sana katika kuanzisha bishara au viwanda katika nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ameongea hoja nzuri sana lakini naomba nitoe mifano miwili, mitatu ili uone namna gani vikwazo hivi bado viko Tanzania. Ukienda *TIC* pale wako *TRA*, kipo *Kitengo* cha Ardhi na kipo *Kitengo* cha Uhamaaji lakini wale hawana mamlaka. Unapotuma *application* ya aina yoyote ili kupata huduma pale lazima sasa utoke tena uende *Immigration* au Ardhi. Wanasema kuna Benki ya Ardhi hawana, siyo kweli! Ukitaka kuwekeza pale wanaweza wakakupeleka kwenye pori ambalo linatakiwa lilipiwe, ufanye kazi kubwa, uanze kuendesha na mambo mengine mengi sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, *TIC* ni kitengo kizuri sana lakini Mheshimiwa Waziri ungefanya utafiti wa kina sana, One Stop Center siyo vile, ungeongeza na *TBS* na *NEMC* na wawe na maamuzi pale, ukipata certificate *TIC* wanakuambia nenda kafanye kazi, ukienda kuanzisha kiwanda, naomba ni-declare interest mimi nina kiwanda, raha ya ngoma uingie ucheze,

natengeneza air cleaner zipo hapa, mwaka mmoja na nusu kupata certificate ya TBS, mimi sijapata mpaka leo. Nimeenda kwa Katibu Mkuu na wewe nimekueleza mmenielewa. Sasa kama mimi nasumbuliwa hivi wengine inakuwaje? Kwa kweli T/C inatakiwa iwe ni One Stop Center. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu umesema kuna viwanda zaidi ya 49,000, sawa, umefanya utafiti ni Watanzania wangapi wanamiliki na wageni wangapi wanamiliki? Tusipotazama huko tunakokwenda Watanzania watakuwa wasindikizaji na hauwezi kukataa wawekezaji wa nje kuja hakuna kitu kama hicho. Tunawahitaji kweli lakini kuwepo na mfumo mzuri. Mimi nitakuja na hoja binafsi namna gani bora ya kuwasaidia Watanzania waweze ku-penetrate kwenye suala zima la kumiliki viwanda. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme vikwazo vingine. Ukiwa na kiwanda cha maji TFDA anaingia humo, ukitaka kupata kibali TBS humo humo, OSHA humo humo na hao wote wanafanya kitu kimoja. Kwa nini wasikubaliane tu kwamba taasisi hii moja ikitoa kibali kwa ajili ya maji basi biashara yangu imeisha. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye cement, ili uweze kuuza cement kwenye soko la Afrika Mashariki unatakiwa upate kibali cha Mkemia Mkuu ambapo unalipa 2.5% ya thamani lakini ukienda Kenya haipo, ukienda Uganda haipo. Unamwambia nini mwenye kiwanda? Ni kwamba ondoa kiwanda chako peleka Kenya, peleka Uganda ndiyo maana yake. Ndiyo maana sisi tumekuwa wa 139. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa wenyе viwanda vya alizeti walisema wana uwezo wa kuwaajiri Watanzania milioni saba mpaka kumi lakini waondoe vikwazo vya kuagiza malighafi. Ukienda Uganda kupata kibali cha kuagiza malighafi ya mafuta ya alizeti kwa maana ya mbegu za alizeti ni miezi sita, Tanzania miaka saba, huu ni utafiti umefanyika. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri afanye utafiti wa kina sana, anaweza akaongea vizuri sana hapo lakini bado hatuko vizuri sana katika kuwasaidia Watanzania wawekeze. Kutana na wafanyabiashara wenyе viwanda, wa kati na wa juu wakupe ya kwao uanzie pale, ukitoka na vile vitu vizuri ukavifanyie kazi kwa mfano suala zima la sera na kubadilisha sheria. Kwa mfano, mtu akiwekeza kiwanda cha mashudu hapa, akiagiza malighafi kwa ajili ya mashudu anapigwa ushuru mkubwa sana lakini ukileta mashudu kutoka Kenya unaingia bila VAT, ni msamaha tu! Maana yake unamwambia nini? Ondoa kiwanda chako cha mashudu peleka Kenya ili mashudu yaje Tanzania, ndio hivyo ilivyo. Kuna contradiction kubwa sana. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina kiwanda cha *air filter*, naagiza malighafi kutoka nchi mbalimbali kama Korea na sehemu nyingine, unapigwa as if ni *finished product* lakini ukiagiza *air filter* ni 10% only *finished product*. Hivi una Mtanzania kweli unamsaidia? Yako mambo mengi tu lakini kwa kweli vikwazo ni vingi sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, bandari, Kenya wanatoa container milioni sita na nusu kwa mwaka lakini Tanzania ni container milioni moja na nusu wakati ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuongelea *transit containers* siongelei *container* za ndani, hiyo ni biashara. *Transit containers* ni *direct foreign income* kwa nchi kama vile utalii tu, mtu ana-container lake anatoka DRC anakuja kulichukua hapa, anaacha pesa yake, anachukua container lake anaondoka. (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

**MHE. AHMED A. SALUM:** Dakika ya saba hiyo.

**MBUNGE FULANI:** Malizia.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Tunapofanya maamuzi ndugu zangu, tuwe tunafanya utafiti nchi jirani kama Malawi, ninyi mnajua uhusiano wa Tanzania na Malawi. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa naomba umalize.

**MBUNGE FULANI:** Anamalizia.

**MBUNGE FULANI:** Endelea.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, Malawi ni nchi ambayo mahusiano yetu mnayajua wanatupiga vita kwenye bandari yetu hii, Kenya ni hivyo hivyo wanatupiga vita. Kwa hiyo, tunapofanya maamuzi ya aina yoyote ile tuwe tunatazama huku kwa sababu port ya Dar es Salam ni bandari. Sasa hivi ma-container yamepungua pale ni ma-container ya DRC, Zambia na Burundi yameondoka kwa sababu ya vikwazo vilivyokuwa ndani ya bandari yetu, yameondoka kabisa hivi hivi tu. Tumeweka VAT on the transit goods for what reason kuna checks point sita for what reason? (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa malizia.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja, dakika kumi ni ndogo sana, ahsante. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo machache hapa.

Tangazo la kwanza linatoka kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Taifa wa Chama cha Mapinduzi, anawaalika Wabunge wote kushiriki kuchangia damu ili kuokoa maisha ya mama na mtoto. Tangazo linasema zoezi hilo litafanyika kuanzia leo tarehe 6 - 8 hospitali ya Mkao wa Dodoma.

Tangazo lingine linatoka kwa Katibu wa Wabunge Wanawake wa CCM, anawatangazia Wabunge wake wa CCM wa Majimbo na Viti Maalum kuhudhuria kikao cha Baraza Kuu la UWT kitakachofanyika kesho tarehe 7 Mei, 2016 katika ukumbi wa NEC uliopo CCM Makao Makuu kuanzia saa moja na nusu asubuhi. Aidha, anasisitiza tangazo la kwenda kujitolea damu kwa ajili ya kuokoa maisha ya mama na mtoto.

Tangazo lingine ni la semina, Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kwamba kesho Jumamosi tarehe 7 Mei, 2016 kutakuwa na semina kwa Wabunge wote kuhusu nafasi ya Wabunge katika kukuza na kuimarisha usawa wa watu wenye ulemavu nchini. Semina hiyo itafanyika katika ukumbi wa Pius Msekwa kuanzia saa tano asubuhi. Mnakaribishwa sana kwenye semina hiyo.

Tangazo lingine ni la majina ya wachangiaji watakoanza mchana, Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima, Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, Mheshimiwa Joel Mwaka Makanya, Mheshimiwa Deogratias Ngalawa, Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vulu, Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter kafumu, Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe.

Pia tuna Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk, Mheshimiwa Vedasto Edgar Ngombale na Mheshimiwa Peter Lijualikali, Mheshimiwa Waitara Mwita Mwikwabe, Mheshimiwa Saed Ahmed Kubenea, Mheshimiwa Antony Calist Komu na Mheshimiwa Kasuku Samson Bilago. Hao ndiyo watakoanza kuchangia mchana wa leo tutakaporejea.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni.

(Saa 7.00 mchana Bunge lilitishwa mpaka saa 10.00 jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilitrudia)

Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alikalia Kiti

**MWENYEKITI:** Tukae. Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA - KATIBU MEZANI:** Hoja za Serikali, Hoja ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwamba Bunge sasa likubali kupidisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Majadiliano yanaendelea.

## HOJA ZA SERIKALI

### **Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2016/2017**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuendelee na mjadala. Asubuhi tulipata wachangiaji watano sasa tuendelee kwa utaratibu huo huo. Anayefuata ni Mheshimiwa Mussa Sima atafuatiwa na Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nami nimshukuru Mwenyezi Mungu lakini kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kutoa mchango wangu katika Bunge hili, nichukue fursa hii kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Singida Mjini walionipa ridhaa hii na mimi niwaahidi utumishi uliotukuka.

Pia nichukue fursa hii kushukuru Chama changu cha Mapinduzi, lakini pia niishukuru Kamati yangu ya Viwanda na nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri ambapo mambo mengi ambayo na mimi niliyatarajia sasa nimeyaona yakiwa humo. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye kuchangia hoja ya viwanda. Nianze na EPZA kwa maana ya pale Kurasini, eneo lile ni muhimu sana na niipongeze sana Serikali kwa uwekezaji mkubwa ambao unaendelea pale. Mambo yaliyomo mule ni mengi sana na nimejifunza vitu vingi mle ndani na ni vizuri sana Watanzania wakajua kwamba leo hii Serikali yetu kwenda kwenye viwanda wala haijakosea. Kuna uwekezaji mkubwa na pale wanatengeneza jeans ya grade A, suruali ile inauzwa Marekani, Uingereza na German, ina-compete kwenye soko la Kimataifa. Hali kadhalika pale wanatengeneza mpaka ATM card mpaka voucher tunayoweza kuitumua. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hoja yangu ni nini hapa? Hatuwezi kuendelea kuwa-entertain wawekezaji halafu wakawekeza na sisi tukabaki tu kutumika. Niombe Serikali ifike mahali tuwe na mpango wa ku-adopt teknolojia kutoka kwa wenzetu hawa wageni lakini isitoshe ku-adopt kama inawezekana kuinunua teknolojia ifike mahali tuinunue teknolojia. Baada ya huo muda wakiweza kuondoka na sisi tuweze kuendesha hivyo viwanda ambavyo vipo. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ni la ajira. Tumezungumzia kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi asilimia 40% ya ajira. Nataka jambo hili tuliweke wazi. Tunao vijana zaidi ya 800,000 wanaingia mtaani kila mwaka na wote hawa tunazungumzia ajira. Hapa palihitaji ufanuzi mpana kidogo. Najua utafiti ulifanyika ndani ya chama changu na Serikali yangu wanajua kabisa kwamba ajira hii inawezekana. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tuliweke vizuri, ni vizuri tukaliweka katika mazingira ambayo yanaeleweka. Tunayo service industry, tuna kiwanda cha huduma, kote huku unakokuona hotelini, kwenye masoko, usafirishaji, mazingira haya yote yanazungumzia ajira ya Watanzania. Hoja yangu hapa ya msingi ni lazima sasa Serikali ijikite kwenda kuangalia mikataba ya hawa Watanzania wanaoajiriwa kwenye haya maeneo. Ni namna gani wanafaidika na namna gani wanaweza kujikimu kwenye maisha yao. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo wenzangu walizungumza awali lazima Serikali ijikite kwenye agro-product. Tuna kila sababu sasa ya kuwekeza zaidi kwa wakulima wetu ambao tunajua kila mkoa sasa hivi unazalisha na hiyo ago-product itatusaidia sasa kuboresha viwanda vyetu. Connectivity ioneckane ya mkulima, ya mchuumizi na mtumiaji, hii pia inaongeza wigo wa ajira. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja ya kulinda viwanda vyetu vya ndani. Amejaribu kuizungumza Mheshimiwa Waziri namna ya kulinda viwanda vyetu vya ndani, mimi nilitaka nishauri na lazima tuliweke wazi. Ufanuzi hapa ultakiwa uwekwe bayana, tunapovipeleka viwanda vyetu vya ndani kwenye tenders kwa maana kwamba tumetangaza tender na vyenyewe vinakwenda ku-compete, kazi ile ni ngumu sana. Tunatakiwa katika asilimia 100% tuwape kwanza viwanda vya ndani asilimia 40% halafu asilimia 60% waingie kwenda ku-compete na viwanda vingine vya nje, hapa tutakuwa tumeweza kulinda viwanda vyetu vya ndani. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe mfano mdogo, tuna Kiwanda cha TANALEC kinachotoa transformer bora East Africa na sisi Serikali mle ndani ni wabia. NDC wana 10% lakini TANESCO wana 20%, sisi ni wabia, maana yake sisi ni member wa Bodi ya TANALEC lakini kwa bahati mbaya sana tunaagiza transformer kutoka India. Ukiagiza transformer kutoka India, wenzetu Serikali ya

India inatoa ruzuku ya 10% kwenye viwanda vyake vya ndani, kwa hiyo, uzalishaji unakuwa mkubwa inafikia mahali wanatafuta masoko kwa cheap price. Kwa hiyo, ukija ukiwaingiza TANELEC kwenda ku-compete wenzetu wanakuwa chini halafu hawa wa TANALEC wanakuwa wako juu na ukizingatia TANALEC wako Tanzania na sisi tunamiliki percent ya TANALEC. Kwa hiyo, niwaombe sana tunapokwenda kuhakikisha tunalinda viwanda vyetu vya ndani ni lazima tuzingatia mambo haya ya msingi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine, tuna kiwanda cha Urafiki, tuna asilimia 49% pale kwenye kiwanda kile na Wachina wana asilimia 51%, ndiyo wasemaji wakubwa wa kiwanda, lakini uzalishaji wa pale ni hafifu na Kamati imeeleza pale kuna madeni ya kutisha. Kwa hiyo, nigombe sana Mheshimiwa Waziri tufike mahali kama ambavyo tumeshauri sisi ndiyo tu-hold share ya Kiwanda cha Urafiki. Sasa leo tunavaa khanga na vitenge kutoka China lakini tuna Kiwanda cha Urafiki, niombe sana Serikali iliangularie suala hili. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mahali siku za nyuma tulijaribu kulinda viwanda, niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge, tuna *Mufindi Paper Mills*. Kiwanda hiki cha Mufindi kinatumia rasilimali za Tanzania na ikumbukwe miaka ya nyuma 2007 cubic meter moja walikuwa wanauziwa nusu ya bei badala ya 28,000 wanauziwa 14,000 na bado ile *pulp* wana safirisha kwenda Kenya na wakitoka Kenya importation ya huku tumewapunguzia mpaka 10% Serikali inaingia hasara. Wakenya hawana misitu, misitu iko Tanzania. Kwa hiyo, niombe Serikali iende ikaliangularie hili, hili jambo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niende moja kwa moja nizungumzie sekta ya ngozi. Mheshimiwa Waziri amezungumzia sekta ya ngozi hapa kwamba wataiangularie na wataboresha mpaka kufikia kiwango cha *wet blue*. *Wet blue* jamani ni sawa na kutengeneza raw material, ni sawa na kutengeneza ghafi. Leo hivi viwanda vilivyopo vya *wet blue* tunazungumzia temporary turning maana yake ni sawa na mtu anakwenda kwenye harusi unamuogesha tu halafu anaenda hana viatu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi leo tumepeleka fedha kwenye SIDO nimeona pale, zaidi ya shillingi bilioni sita lakini tunasafirisha ngozi hatuwezi kwenda huko. Mheshimiwa Waziri ni shahidi maghala yamejaa ngozi. Niombe sana Serikali sasa ichukue hatua ya haraka kuhusu suala hili. Vile viwanda ni temporary, umezungumzia viwanda nane hakuna viwanda nane Mheshimiwa Waziri, kama vinazidi sana ni vinne na bado ni temporary kwa hiyo Tanzania bado hatuna viwanda hivyo. Niombe sana jambo hili liangaliwe. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nishukuru tumezungumzia habari ya regulatory bodies, tu-harmonise vifanye kazi kwa pamoja kuondoa mlolongo

mrefu ambao hauna tija. Jambo lingine tumezungumzia model, nimeona kwenye kitabu hapa, wenzetu wa Vietnam, China, Korea Kusini na wengine wote walianzia hapa tulipo. Kwa hiyo, niombe sana tuangalie hili tabaka la katika maana ya *middle class* ndiko mahali ambapo tunatakiwa kujikita zaidi kuhakikisha kwamba Watanzania wanaweza kujikimu na maisha yao juu ya uwepo wa viwanda. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunapozungumzia SIDO lazima tuweke connection na VETA. Hivi vitu lazima vihusiane, SIDO na VETA. Hatuwezi kuishia tu SIDO, VETA inafanya nini ili iweze kutusaidia? (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Waziri jambo la mwisho kwamba sasa wakati umefika kama tumeamua Tanzania iwe nchi ya viwanda, tuwe na siku ya viwanda Tanzania. Jambo hili litawarahisishia wafanyabiashara na wenye viwanda kukutana na kujadili changamoto wanazokutana nazo hata kila mwaka, hata kila baada ya miezi sita, jambo hili litatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niende mbali zaidi. Leo wenzetu wa Rwanda wanazalisha alizeti. Singida sisi ni maarufu sana kwa alizeti na bahati mbaya sana sijaona kama tunaenda kuanzisha kiwanda cha alizeti Singida, niombe sana suala hili liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sisi Singida ni wafanyabiashara wazuri sana wa vitunguu. Mheshimiwa Waziri karibu sana tuje tuanzishe soko la Kimataifa pale Singida ili tuweze kuwasaidia wananchi wa pale. Rwanda leo wameweka 25% ya kodi hata Kenya wenye nao wanaweka lakini sisi tukitaka kuweka hapa mpaka tukafulize *East Africa*. Mheshimiwa Waziri naomba agenda hii uilete vizuri ili tuweze...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makof)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Sima. Tunaendelea na Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga atafuatiwa na Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nianze kumshukuru Waziri wa Viwanda na Biashara kwa hotuba yake nzuri ambayo imeelekeza changamoto za Watanzania. Nitaanza na ku-declare interest kwa maana ya kwamba ni mmiliki wa kiwanda. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia viwanda tunazungumzia viwanda vya aina gani? Sisi wakulima wa pamba tunakotoka tulikuwa na viwanda 77 leo vimebaki 40 na hivi 40 na vyenyewe vipo katika hali tete. Nini mpango wa Serikali kuvisaidia viwanda hivi ili viweze kufanya kazi? (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizungumza na ukifuatilia suala la viwanda kwanza malighafi yenyewe haipo ni kwa sababu Serikali hajjaweka kipaumbele kwa mazao yanayozalishwa hapa nchini ili yaweze kuwa na bei kubwa. Kwa mfano, pale Morogoro tunacho Kiwanda cha Ngozi baada ya Serikali kuzuia ngozi zetu zisisafirishwe bei zimeshuka. Leo bei ya kilo moja ya ngozi ya ng'ombe ni shilingi 400 lakini enzi zile wakati wanasaferisha ilikuwa ni shilingi 1,500, ya mbuzi ilikuwa shilingi 1,000, ya kondoo ilikuwa shilingi 800, leo unazungumzia ya kondoo shilingi 100 kwa kilo na ya mbuzi unazungumzia shilingi 200, kwa jinsi hii tunalindaje viwanda vyetu vya ndani? Ifike mahali sasa Serikali ijaribu kuangalia kwa undani na kwa umakini zaidi ili kuhakikisha mali tunayoizalisha hapa nchini inakuwa na viwanda vya kuzalisha vizuri zaidi. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ione ni jinsi gani ya kuongeza bei, hili jambo kwa kweli linanipa taabu. Unakuta mazao yetu ya ndani kodi inaongezwa, mfano kama pamba. Mashudu yana kodi, mafuta yana kodi lakini mali inayotoka nje inakuwa haina kodi, unategemea hii mali itapanda kwa utaratibu upi? Ukizungumzia zao la pamba, zao la pamba linajumuisha vitu vingi, utachukua mapumba yale makapi, utachukua mbegu zake utauza lakini kwa hali iliyopo ukigusa kila kitu kina kodi kwa sababu sisi soko la nje hatuli-control hatuwezi kuongeza bei na mkulima bei yake ikiongezeka ni sehemu ya kichecheo kwa wakulima kuweza kuzalisha kwa mwaka unaofuata. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Wizara ya Kilimo imezungumza, kwa mwaka 2004 nchi ilizalisha roba 700,000 lakini leo tunazungumzia uzalishaji wa tani 150,000, ni tayari nchi imeingia hasara kwa aina gani? Tumekosa dola lakini vilevile tumekosa ajira kwa vijana wetu. Mimi niiombe sana Serikali, Waziri atenge muda wa kukutana na wenye viwanda hawa ili aweze kuzungumza nao wamwambie ni changamoto za aina gani wanazokabiliana nazo. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani nchi inazungumza kila siku masuala ya viwanda lakini bado kuna watu ambao wana viwanda lakini wameshindwa kuvientesha kwa sababu ya mambo mengi. Tuna kiwanda pale Arusha kipyaa na kizuri kabisa lakini kimeshindwa kufanya kazi. Hata huyu Mchina ambaye yuko pale Shinyanga amefungua Kiwanda cha Nyuzi pamoja na Kiwanda cha Oil Mill haviwezi kufanya kazi kwa sababu ya malighafi na gharama inakuwa kubwa. Kwa hiyo, ifike mahali tuangalie ni jinsi gani tunataka kuwasaidia Watanzania lakini tuangalie ni jinsi gani tunataka tusimamie mazao yetu ya ndani ili kuyaongezea thamani ili wakulima wetu waweze kupata bei zilizokuwa nzuri. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mambo mengi ambayo yanababisha tushindwe kusonga mbele. Ukiangalia mfano mwaka huu tumekosa pamba na mtu anayehusika na viwanda anapaswa sana kusimama kwa sababu ni sehemu yake ili viwanda vyake viweze kufanya kazi. Mwaka huu tuna maeneo mengi ambayo yamesababishiwa hasara na baadhi ya wataalam wa *TPRI* kwa sababu ya kuleta dawa mabovu hivyo hatuna pamba ya kutosha. Hili jambo lazima Waziri wa Viwanda aliangalie kwa umakini zaidi na kuhakikisha wanakuwa wamoja ili wasukume gurudumu la maendeleo kuhakikisha nchi yetu tunipeleka mahali tunakokusudia. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna changamoto nyingine kwenye suala la viwanda. Viwanda vyetu lazima tukubali, kwanza suala la umeme bado halijakaa vizuri, lazima ongezeko la umeme wa kutosha liwepo. Kiwanda unakiendesha ndani ya miezi miwili, lakini ndani ya miezi hiyo miwili utalipa miezi mitatu inayofuata, kama ni bili ya shilingi milioni 100 utalipa miezi mitatu mfululizo, tayari pale yule mwenye kiwanda hawezikuendelea atasimama tu hivyo hivyo na mwisho wa siku nchi yetu itaingia kwenye matatizo makubwa sana.

Niombe sana Wizara inayohusiana na jambo hili ilishughulikie kwa umakini zaidi na kuona jinsi gani sasa tunasonga mbele na kauli mbiu ya Mheshimiwa Rais inayositisizia suala la viwanda. Viwanda vina changamoto na lazima Mheshimiwa Waziri aingie ndani zaidi, ajifunze zaidi najua ni mtaalam na jinsi anavyojibu yuko shapu kama Mbunge wa Kishapu akiweka mambo yake vizuri tunaweza tukapiga hatua kubwa sana lakini bila kufanya hivyo tutazungmza hapa miaka mitano itaisha na viwanda havitaenda ni kwa sababu mambo hayako wazi tunaelewa kabisa. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu walioendelea, kuna nchi kama Bangladesh, ina sehemu tu ya viwanda, kiwanda kimoja kina wafanyakazi 25,000, kila kitu kipo na masaa yote kinafanya kazi lakini sisi Tanzania hapa hatujipanga vizuri. Hata hivyo, kwa kasi hii ya Awamu ya Tano naamini imojiwekea utaratibu mzuri. Niwaombe sana Waziri wa Kiwanda pamoja na Waziri wa Nishati na Madini muweke kasi kwenye mambo ya umeme kwa sababu viwanda vyetu vina *fail*, vinaunguza vitu kutokana na mambo mengi. Yote haya tukiyazingatia na kuyachukulia maanani tutapiga hatua na nchi yetu itabadilika. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mambo magumu sana ambayo tunayaona lakini mambo mepesi sana tukishirikiana na wananchi wetu, tunavyo viwanda vya *SIDO*. Mfano mimi kwenye Jimbo langu pale Luguru, maana Mwenyekiti wewe ni Mtemi kule, kuna Kiwanda cha *SIDO* kipo siku nyingi tu. Kile tayari kikitengenezewa utaratibu kinafanya kazi maana majengo tunayo zile teknolojia zipo zinabadilika kila siku tu ni kwenda kutoa zilizokuwepo unaweka

mitambo mingine kazi inaendelea, lakini bado sasa tunazunguka na tunazungumza sana. Kama tunataka vijana wawe na ajira ni pamoja na vitu kama hivi tukiviwekea kipaumbele tunaweza tukapiga hatua na nchi yetu tukaipelekea pale panapokusudiwa. (Makof)

Suala lingine ni alizeti. Sasa hivi pamba inaenda inashuka lakini alizeti sasa nayo imeingia kwenye soko. Nimuombe Waziri wa Viwanda ajaribu kuangalia na kutoa ushauri kwenye Wizara ya Kilimo kwa sababu ni wamoja wanaweza wakaungana wakafanya kazi ya pamoja ili kusudi kuhakikisha Taifa letu sasa linapiga hatua. Kwenye alizeti, niishauri Serikali tuna mifumo kwenye nchi hii mingi sana, mkiingiza bodi na kadhalika tayari lile soko litashuka. Leo mwenzangu wa Singida amezungumzia ni walimaji wazuri sana ni kwa sababu hakuna bodi pale ukiingiza tu bodi lazima patakuwa na tatizo, itaanza kushuka na kadhalika. Tuyaangalie sana hizi bodi wakati mwingine yanaliingiza Taifa kwenye matatizo na migongano isiyokuwa na maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante sana. (Makof)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga atafuatiwa na Mheshimiwa Deogratias Ngalawa.

**MHE. JOEL M. MAKANYAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa mmoja kati ya wachangiaji wa hotuba ya Waziri wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hilo niendelee kumpongeza sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kwa kazi yake kubwa anayoifanya. Hapa tunapiga kelele ya vitu vingi lakini wenyewe kusikia wamesikia. Leo akiwa safarini kwenda Arusha amezungumza mambo mazito juu ya watu wanaoleta fujo na biashara yetu ya sukari. Ni jambo ambalo linawagusa wananchi na yeye mwenyewe linamgusa sana nadiyo maana analikemea kila anapokwenda. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa hotuba yake nzuri aliyoiwasilisha kwa umakini kabisa. Wakati akianza nilikuwa naangalia kitabu chake kilivyo kikubwa nikasema hii itakuwa kazi hapa lakini ikawa kazi kweli. Amei-summarize kwa uzuri kabisa, hakuna kitu alichoacha ambacho mtu hakuelewa. Utapitia na utapata details za yale aliyokuwa ameya-summarize, nampongeza sana. Amezungumzia kwa undani kuhusu viwanda kwamba Serikali yetu ya Awamu ya Tano inajipanga kufanya nini kwenye viwanda,

akizungumzia viwanda vidogo sana, viwanda vidogo na viwanda vikubwa. Amezungumzia biashara na uwekezaji wake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba namuunga mkono na naunga mkono hoja hiyo. Naiunga mkono kwa dhati kabisa nikitambua kwamba safari tuliyonayo ambayo tumejiwekea ya kuingia kwenye uchumi wa kati hatujakosea njia. Njia sahihi ni hii ya kupitia viwanda, kwa nini? Tunapozungumzia kuelekea kwenye uchumi wa kati maana yake tunazungumzia kipato cha mtu mmoja mmoja ambapo mwisho tunazungumzia kipato cha Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tuna shida ya ajira, kama mtu hufanyi kazi hakuna jinsi utajiongezea kipato lakini unapokwenda kuwainua wananchi kwa viwanda maana yake unakwenda kunyanya vipato vyao. Unaponyanua vipato vyao maana yake unapandisha kipato cha Taifa na hii ndiyo njia sahihi ya kutupeleka kwenye uchumi wa kati. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia kilimo, ili kilimo kiweze kuboreshwa lazima soko la uhakika liwepo. Kilimo kipo lakini soko halina uhakika, kwa hiyo kilimo kiko katika *levels* za chini. Tutakapoweka viwanda vitakavyofanya *processing* ya mazao yetu ya viwandani maana yake nini? Maana yake watu wengi zaidi wataji-engage kwenye kilimo ambacho soko lake lipo. Tunapozungumzia ufugaji vilevile, tunataka watu wafuge wakiwa na uhakika wa masoko yao. Tunapozungumzia uvuvi tunataka watu wavue wakiwa na uhakika wa masoko ya mazao wanayoyapata. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia viwanda maana yake tunazungumzia *value addition* ya *products* zetu tunazozipata. Hili ndilo tatizo kubwa ambalo tumekuwa nalo Watanzania, tatizo hili pia nchi za Afrika tumekuwa nalo sana, kazi yetu ni kuzalisha malighafi na kuwapelekea Wazungu na nchi za nje, wao wanaenda ku-add value, wanatengeneza faida kubwa na kuturudishia sisi tena.

Kwa hiyo, tunapokwenda kwenye hatua hii ya kuzalisha wenyewe, tunapata ajira. Tunapoweka viwanda maana yake kuna watu wanapata ajira viwandani kwa ajili ya ku-process yale mazao lakini mazao yanapotoka pale lazima yafanyiwe biashara, tayari watu wanapata biashara pale pale. Kwa hiyo, ukiangalia *chain* nzima, hii ndiyo njia sahihi ya kumuongezea kipato Mtanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda sasa nijikite kwangu kwenye Mkoa wa Dodoma, Wilaya ya Chamwino na hasa Jimboni kwangu Jimbo la Chilonwa. Jimboni kwangu ni wakulima na ni wafugaji. Tunalima kiasi cha kutosha pamoja na shida ya mvua iliyopo lakini Mungu anatujalia tunapata kiasi cha kutosha

lakini tatizo kubwa ni soko. Nilizungumza juzi kwamba kama tukipata soko la uhakika watu watalima kwa wingi na viwanda vitapata malighafi za kutosha. Tunalima alizeti, ufuta na mahindi lakini soko lake ni duni. Kwa sababu hakuna soko la kuaminika wafanyabiashara wanakuja wanunua kwa bei wanazotaka. Kama tukiwa na uhakika wa viwanda kwamba nalima alizeti najua naipeleka kiwanda gani akinifuata mfanyabiashara nitamuuzia bei ambayo najua hii inanilipa mimi, inalipa muda wangu niliokuwa shambani, inalipa pembejeo zangu nilizotumia shambani na kupata faida kidogo lakini kwa sasa tunauza maadam tuuze. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika upande wa viwanda na mazao yetu, kuna mazao yanahitaji viwanda vidogo vidogo, vidogo sana lakini kuna mazao yanahitaji viwanda vikubwa na vya kati kwa upande wa alizeti, ufuta na mahindi. Ninachokiomba kwa Serikali na kuitia kwako wewe Waziri hebu tuangalie namna ya kuwawezesha wananchi wapate mikopo ya kuweza kuanzisha hivi viwanda vidogo vidogo vya ku-process mazao yao kama alizeti, ufuta na mahindi. Sisi kwetu Chilonwa tuna biashara ya uhakika ya zabibu yenyе shida ya soko.

Naomba nikuombe wewe sasa Waziri kuitia kwako Mwenyekiti tunahitaji tupewe kiwanda cha uhakika cha kutengeneza mvinyo. Tukipata kiwanda cha uhakika cha kutengeneza mvinyo maana yake watu kwa wingi sana watajitokeza kulima zao la zabibu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda hili niliweke sawa kidogo. Kuna mchangiaji mwenzangu mmoja alisema kuna viwanda vya aina mbalimbali, naomba nishauri katika hili tusikimbilie viwanda tu, tunapofikiria viwanda basi tuweke viwanda vyenye teknolojia ya kisasa. Kwa mfano, unapozungumzia Kiwanda cha Mvinyo ambavyo ndiyo vingi viko hapa Dodoma vidogo vidogo, kazi yao ni kukamua ile zabibu na kutengeneza mvinyo, basi! Hayo siyo mazao peke yake unayoweza kuyapata kutokana na zabibu. Viwanda vya wenzetu vina-process unapata juice lakini unaweza ukai-ferment ukapata mvinyo (wine) lakini vilevile unaweza ukai-concentrate ukapata kitu kinaitwa concentrates hizi ambazo tunapigia kelele hapa kwamba wafanyabiashara wengi wa viwanda vya mvinyo wengi wana-import concentrates wanakuja kutengeneza mvinyo hapa wakisema kwamba wametumia zabibu za hapa nchini, sio kweli! Basi na sisi tuanzishe kiwanda cha namna hiyo tuweze kutengeneza juice, mvinyo na concentrates. Tukifanya hivyo tutakuwa tumefanya value addition kubwa sana na kuipatia nchi hii hata fedha za kigeni hasa tukizungumzia concentrates ambazo zina soko la uhakika huko nje. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nitamke kwamba naunga mkono hoja na ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa kutuokolea na muda pia na kwa mchango wako mzuri. Kama nilivyosema tunaendelea na Mheshimiwa Deogratias Ngalawa atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Lijuakali. Mheshimiwa Ngalawa hayupo, haya ngoja nivute kidogo Mheshimiwa Lijuakali.

**MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Lijualikali siyo Lijuakali.

**MWENYEKITI:** Lijualikali.

**MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI:** Naam!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuzungumza kidogo. Naomba nizungumzie kwamba kama tunataka kutengeneza nchi ya viwanda ili twende kwenye uchumi wa katilimi nafikiri kiwanda ni matokeo ya uwekezaji katika umeme. Lazima tuwe na umeme utakaoweza kufanya viwanda vifanye kazi. Kwa hiyo, niishauri Serikali kwamba iijitahidi sana kuwekeza katika umeme ili tuwe na umeme wa uhakika. Tukiwa na umeme wa uhakika viwanda ambavyo tunataka vije ama tuvifufue basi viweze kupata uwezo wa kufanya kazi vizuri. Huo ulikuwa ni ushauri wa kwanza. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie hoja hii ya sukari. Tanzania kuna viwanda vinne ambavyo vinazalisha sukari. Kuna kiwanda cha Ilovo, kipo Jimboni kwangu Kilombero, kuna kiwanda cha Mtibwa, kuna cha TPC na kuna Kagera. Kiwanda cha Ilovo kimefunga uzalishaji wake tangu mwezi wa kwanza na hii ni kwa sababu ya *maintenance*, lakini leo ajabu karibu tani nane za sukari kutoka Ilovo zilikuwa kwenye godown hapo Tabata zimeuzwa leo. Hili godown lipo Tabata limeuza tani nane. Tafsiri yake ni nini? Tafsiri yake ni kwamba tuna sukari ambayo imefichwa na wafanyabiashara. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Rais akiwa na nia safi, mimi nasema safi kwa sababu anazungumza vizuri ya sisi tuweze kupata sukari na viwanda viendelee, watu wanaficha sukari, wanasubiri *maintenance* za viwanda zikifanyika wao ndiyo watoe mzigo. Kibaya zaidi baada ya huu upungufu wa sukari hawa watu wanataka wapewe vibali vya kwenda kuagiza sukari yaani watu wanaoficha sukari kwenye ma-godown leo wanataka wao ndiyo wapewe vibali vya kwenda kuagiza sukari. Tafsiri yake ni nini? Tafsiri yake ni kwamba hao watu kwa tabia yao hii ya kuficha kwanza hatuna uhakika kama wataagiza ambacho wameruhusiwa, maana yake ni kwamba wataongeza. Wakiongeza viwanda vyetu hivi vinne vya Ilovo, Mtibwa, TPC na Kagera vikianza production vitakuta tayari kuna mzigo mkubwa upo kwenye soko vitapunguza uzalishaji. Vikipunguza uzalishaji maana yake hawa wakulima

wetu mfano wakulima wangu kule Sanje, Kidatu, Mkula wataathirika. Tunakwenda kuua hawa wananchi ambao wanaendesha kilimo hiki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu sasa, niiombe Serikali isiruhusu kabisa wafanyabiashara waagize sukari nje. Mimi najua kuna watu wamewekwa humu ndani waweze kuongea maneno haya, wamewekwa humu ili waweze kusema kwamba wafanyabiashara waruhusiwe, niombe Serikali, hivi viwanda vinne na kwa sababu Serikali hii inaweza sana, hawa Mawaziri wanafanya kazi bila kuwa na sheria, hawana kazi, basi niombe kama huo ndiyo utaratibu wetu hata kama viwanda hivi watasema kwamba sijui havina mamlaka haya, tuendelee hivi hivi tu, tufunike hivi hivi hawa wenye viwanda, viwanda hivi ndiyo viagize sukari ili kulinda viwanda hivi na wakulima. Nilikuwa nataka hili niliweke sawa watu wajue na Serikali ijue kwamba kuruhusu wafanyabiashara binafsi kuagiza sukari ni kuua viwanda na kuwa wananchi watu wa Sanje na sehemu zingine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu Morogoro. Morogoro ina viwanda vingi sana lakini viwanda hivi watu wanafuga mbuzi, hapa ndipo wanaposema *we have killed our past and we are busy killing our future*. Tumeua *past yetu na tuko busy future yetu*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi huwa najiuliza hivi nia ya Serikali ya privatization (kubinafsisha) hivi viwanda ilikuwa ni nini? Ilikuwa ni kuwapa watu nafasi ya kupata maeneo ya kufuga, kuuza mashine zetu kama scraper au nia ilikuwa tuongeze uzalishaji na ajira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nia ilikuwa ni kuongeza ajira na uzalishaji hivi inakuwaje tunakuwa na viwanda yaani kama Taifa tumejiminya, tumepata viwanda, tukasema wenzetu mviendeleze halafu wanachukua hivyo viwanda wanaanza kufugia mbuzi, wanakata mashine, wanauzu kama scraper, kama Taifa hii ni aibu! Sidhani kama Serikali hii ya Awamu ya Tano inayosema Hapa Kazi Tu itaruhusu kwamba hizi ndizo kazi zenyewe. Yaani kazi ya Mwalimu Nyerere ilikuwa kuunda viwanda halafu watu wengine waje kukata scraper! Sidhani kama hii ndiyo kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mifano hapa, pale kwangu Mang'ula pana kiwanda kinaitwa MMT, nina handover letter hapa ambayo hii Serikali ilikabidhi hiki kiwanda kwa Mama Rwakatare, Mama Rwakatare huyu huyu ambaye alikuwa Mbunge, handover hii hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu walikuwa hawajui kama mlikuwa mnaona vifaa kama mapanga na kadhalika vyenye picha ya mamba ilikuwa ni Mang'ula. Kiwanda tumekabidhiwa kikiwa kizuri, kikiwa kina kila kitu lakini pale sasa hivi kuna mbuzi tu ndiyo wanachungwa pale lakini unakuta eti mtu naye

anajiita mwekezaji, amewekeza nini huyu? Umewekeza kwa kuua uchumi wa nchi? Kile kiwanda kilikuwa kinatoa ajira pale, Serikali ikaamua kutoa, ikasema endeleva na nimuombe Waziri twende kule akaone kiwanda hiki ambacho kilikuwa kina manufaa katika nchi yetu leo kimekuwa cha kufunga mbuzi. Hatuwezi kujenga Taifa la hivi na tukiongea hivi hatumuonei mtu, tunaongea ukweli kwa sababu ya faida ya Taifa letu. Kuna watu huko hawana ajira, tumetoa viwanda watu wanafugia mbuzi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo kama haitoshi, kuna kiwanda kingine kilikuwepo pale Mang'ula, wengine mnafahamu vizuri wakati reli hii ya TAZARA inajengwa vifaa vyta kutengeneza yale mataruma vilikuwa pale Mang'ula. Mwalimu Nyerere kaacha viwanda vizuri, kiwanda vyta ilovo, kiwanda vyta Mtibwa spare zake ilikuwa wanazipata Mang'ula. Leo kiwanda mtu anachukua semi-trailer anapakia chuma chakavu anapeleka kuuza, sisi tupo tu hapa, Taifa lipo, Serikali ipo! Kiwanda kinahujumiwa, nchi inaliwa tunasema wawekezaji, what kind of this business? Are we serious?

**MBUNGE FULANI:** No!

**MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI:** We are not serious and never be serious. We have killed our past and we are busy killing our future. Ukiuliza, anaongea mpinzani, anaongea UKAWA, come on lets be serious! Tunazungumzia uchumi wa nchi hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Waziri twende tukaone kule! Kiwanda ambacho mnasema mmempa mtu mkaone...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, muda wako ndiyo huo.

**MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vulu, hayupo, tunaendelea na Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, nifikishe ule uwiano wetu baada ya kumkosa Mheshimiwa Ngalawa.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi naomba kwanza nianze kwa kuipongeza Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli pamoja na timu yake yote ya watendaji wakiwemo Mawaziri wote kwa kazi nzuri ambayo wameendelea kuifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja ili nisije nikasahau ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa Charles Mwijage na nampongeza kwa hotuba yake na uwasilishaji wake mzuri wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuanza na utangulizi huo, nianze kuchangia kuhusiana na wafanyabiashara wadogo. Wafanyabiashara wadogo kama ambavyo Mheshimiwa Mwijage, Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji alivyooanisha kwenye kitabu chake kwamba nchi kama Korea Kusini, Singapore na Malaysia wakati sisi tunapata uhuru nchi hizi tulikuwa tunalingana kiuchumi, sasa leo wenzetu wako mbali mno, sijui sisi tatizo letu ni wapi. Moja ya tatizo ninaloliona ni urasimu kwa wafanyabiashara hawa wadogo ambao tumekuwa tukiimba kwamba kwetu wako karibu asilimia 99 na hata nchi zingine ambao kwa kiasi kikubwa ndiyo wanachangia pato kubwa la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisema mfanyabiashara mdogo mdogo, tunaanza na wale wanaopata leseni za kawaida, mtu ana mtaji wake wa shilingi laki mbili, tatu mpaka milioni moja. Kwa urasimu ambao tunao kwenye biashara, kwa mfano, mfanyabiashara anakata leseni ya kawaida shilingi elfu themanini, anataka kuja kuomba tender ya Serikali, kuna viainishi vingine anatakiwa kuwa navyo. Kwa mfano, awe na cheti kutoka Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) wakati anataka kuomba tender hapo hajapata, hii nayo ina gharama yake. Kwenye Sheria ya Manunuzi (PPRA) kuna GPSA, ukitaka kujisajili GPSA kununua kitabu chao tu kile cha kuomba kujisajili siyo kupata biashara ni shilingi laki moja. Mimi nina mashaka makubwa mfanyabiashara wa mtaji wa shilingi laki mbili mpaka tano au milioni moja atawezza kufanikisha milolongo hii yote. Pia huwa kunakuwa na mwingiliano wa kazi kati ya PPRA na TFDA (Mamlaka ya Chakula na Dawa). Unaweza ukakuta hawa PPRA nao wanakagua chakula, sijui kwa mamlaka yapi, mimi nashindwa kuelewa kwa sababu TFDA na hawa PPRA wanachanganyana. Kwa hiyo, ile Sheria ya Manunuzi kama walivyosema wenzangu nadhani sasa imepitwa na wakati. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nichangie suala la gharama ambayo wafanyabiashara wanakutana nayo hasa pale bandarini. Kuna ushuru wa uzembe unaofanyika zile damage charges, ule uzembe unaofanyika pale haumhusu mteja. Vitu vinavyoendelea pale kwa mfano wengine waliongelea mambo ya magari lakini kuna mizigo pia, mteja unafuatilia toka siku ya kwanza unajua meli imeingia na ina gari lako, sijui wengine lakini mimi nimetoa magari mara nyingi pale, haijawahi kutokea zile siku wanazokupa kama free ukawenza kutoa gari. Wao wana kisingizio, wakati wewe unataka kwenda kulipia wanakuambia system iko down.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wasafirishaji kwa mfano wa mabasi na reli, tunaona kabisa kwamba kama gari kwa mfano limekwama njiani wataleta basi lingine kwa gharama zao kwa sababu siyo kosa la msafiri. Vivyo hivyo hata kwenye reli tumeona reli ya kati hapa ikitokea matatizo wanakodisha magari kwa gharama zao.

Sasa hawa *TRA* mitandao yao inapokuwa iko down kwa nini gharama zile aingie mteja? Mimi nadhani gharama zile zilikuwa zinapaswa kubaki *TRA*. Hili ni jipu kwa sababu kama kweli kila siku mitandao iko down, mtu anataka kwenda kulipia pesa wanasema kuna tatizo la mitandao sasa hivi huwezi kulipia, ni mapato ya Serikali yanachelewa kukusanya. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kwenye suala la Sera hii ya Viwanda. Kama alivyoainisha Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni kwamba nchi yetu itakuwa ya viwanda kwa asilimia zisizopungua 40, hapa nirudi kwenye Mkoa wangu wa Tabora, mimi ni Mbunge wa Tabora Mjini, nimeshasema mara nyingi mwamba ngoma anavutia kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tabora ni mkoa wa kihistoria hata kura zile za uhuru tatu zilifanyika Tabora. Tabora inalima tumbaku kwa wingi kuliko sehemu yoyote Tanzania hii. Tabora ilikuwa na kiwanda cha nyuzi lakini Kiwanda hiki cha Nyuzi, siku moja Mheshimiwa Mwijage wakati anajibu swalii moja hapa alisema kwamba wame-respond vizuri wale watu kwamba wanasema nyuzi hazina soko. Siyo kweli Mheshimiwa Mwijage, naomba siku ukipata nafasi katembelee Tabora pale na mimi nikiwepo, kimefungwa na mitambo iliyopo mle ndani inasadikiwa imeuzwa kama chuma chakavu kama walivyosema wengine na huwa hawakufungulii unapokwenda pale. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwijage hii sababu wanayotoa si kweli, kile kiwanda aliyebinafsishiwa siyo. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hivyo tu kuna asali Tabora. Naomba Mheshimiwa Mwijage hata kama viwanda itashindikana kama niko sahihi hapa Tanzania hatuna maabara ya kupima ubora wa asali kwa maana ya maabara. Naomba basi hata tutakapojenga maabara tujenge Tabora ili wale wanafunzi ambapo vyuo viko vingi pale waweze kupata hiyo ajira ambayo tunasema sasa tutakuwa watu wa viwanda na biashara. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia naomba nimalize kwa hizi taasisi ambazo ni za utafiti kama *TIRDO*, *TEMDO* na *CARMATEC*. Naomba wanapofanya utafiti waikumbuke na Tabora. Kwa mfano, wanapotengeneza matofali ya saruji ambayo yamechanganyika na udongo, wanatoa matofali ambayo unajenga nyumba za kisasa, mafunzo yale yakifanyika Tabora yatawawezesha pia vijana kupata ujasiriamali kwa kutumia taasisi hizi za utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya machache, narudia kuunga mkono hoja na ahsante kwa kunipa nafasi. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka. Tunaendelea, Mheshimiwa Waitara Mwita Mwikwabe atafuatiwa, niwe huko huko na ...

**MBUNGE FULANI:** Huko huko UKAWA.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk halafu tutaendelea. Karibu Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nipongeze hotuba nzuri ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwenye idara hii ya viwanda. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru kwa kupata nafasi hii nichangie. Nikupongeze sana wewe binafsi, kulikuwa na maneno sana, sasa najaribu kulinganisha maneno yale juu yako na uongozi wako, wewe ni Mwenyekiti *smart* kweli kweli, hongera sana Mheshimiwa. Nitakuomba kwa umri wako na uzoefu umsaidia Naibu Spika asiharibu hili Bunge, kwa kweli nasema haya ni muhimu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara tuchangie hoja. (Kicheko)

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana Mheshimiwa maana msema ukweli ni mpenzi wa Mungu kama unafanya vizuri tukupongeze, ukifanya vibaya tunakusema lakini sitarajii kwamba wewe utafanya vibaya. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni Wizara ya Viwanda na Biashara na nina hoja hapa ambazo ningeomba Mheshimiwa Waziri mhusika asikilize. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Waziri kwamba hoja za msingi sehemu kubwa ya hoja hizo zinatoka Upinzani naomba utusikilize vizuri, yale mambo mengine wayapuuze. Kwa sababu kwa mfano mtu akikusikiliza vizuri Mheshimiwa Waziri na akatafakari na mimi nimekusikiliza hapa mara kadhaa nikaenda nikakaa, nikarudi hapa nikaona maneno yako yale kama utaweza kuyatekeleza utakuwa ni Waziri wa kwanza ndani ya CCM kufanya kazi kubwa sana na mimi nakutakia kila la kheri. Siyo kwa sababu ni mtani wangu umekula senene hapana, lakini unavyozungumza nitaomba hayo mazungumzo ya-reflect actions pamoja kwamba kuna kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie, CBE ipo chini ya Wizara yake na Mheshimiwa Waziri wa Elimu asikilize hapa. Nimepata

taarifa kwamba CBE pale kuna majipu, ninazo document hapa ambazo Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana anazo, Mheshimiwa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo anazo tena ni Profesa, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Bodi ambaye ni Profesa wangu wakati nikiwa Chuo Kikuu Dar es Salaam nikiwa Rais wa Chuo kile alikuwa anaendesha Baraza la Chuo nikiwepo, Mheshimiwa Profesa Luhanga na wadau wengine. Wameleta malalamiko wanadai kwamba katika kile chuo, Mkuu wa Chuo pamoja na Mkurugenzi wa Fedha, chini ya Idara yako na hii sasa inaweza ikapunguza maneno yako haya nikatafsiri tofauti, kwamba kuna Mkurugenzi wa Fedha amekusanya zaidi ya shilingi milioni 400 bila kutoa stakabadhi anatoa risiti za karatasi zile baadaye hazionekani, vielelezo hivi hapa viro, hii ni Idara yako na ulipopata taarifa hapa, wale watu ambao wameleta document hapa wakapigiwa simu wanatishiwa kwa nini wameleta taarifa kwako. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hizi tuhuma Katibu Mkuu alipoandikiwa, yaani shilingi milioni 400 zimekusanya, CBE pale kuna campus nne, nazungumzia Dar es Salaam wamekusanya fedha zaidi shilingi milioni 400 kwa utaratibu ambao kimsingi ni kinyume na utaratibu. Wanasema kuna wanafunzi ambao hawalipi ada wakiongea na Mkurugenzi wa Fedha wanamkatia kidogo anaenda anafuta zile kumbukumbu, wale wataalam wa fedha wanasema bad debtors kwa maana ya kupoteza ushahidi, pia haya ni malalamiko ambayo yapo kule. Kwa maelezo yao inaonesha kwamba Mkuu wa Chuo anaelekeza alama 50 ziongezwe kwa wanafunzi ambao wamefeli ambao yeye ana maslahi nao. Hii inaingia kwenye standard ya elimu na hivi vyuo vimekuwa na malalamiko muda mrefu kwamba wanafanya kazi pale kuonesha urembo CBE almost zote wanashiriki sana haya mambo yako.

Kwa hiyo, ina maana hapa inahusu vilevile na Waziri wa Elimu atambue kwamba ni suala la Wizara ya Biashara lakini pia kuna jambo hilo linazungumzwa. Kuna Mkaguzi wa Nje alipelekwa pale alikuwa hired na chuo, akaahidiwa kupewa shilingi milioni 13 akakubali kufanya forgery kwenye ukaguzi wake, aka-abuse profession lakini badaye akapewa shilingi milioni 3.5 sasa hivi analalamika mtaani kwamba amedhulumiwa, huyu naye ni jipu. Nilipoleta malalamiko kwamba kile chuo kichunguzwe, Mkuu wa Chuo kwa kuzungumza na Mkurugenzi wake wakazunguka hilo zoezi halijafanyika kufanya ukaguzi wa fedha. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, CBE ya Mwanza na yenyewe ina malalamiko, kuna mtu pale anaitwa Rose yupo Gerezani Segerea tangu mwaka 2011 lakini kapandishwa mshahara analipwa mshahara. Sasa unatafuta wafanyakazi hewa kumbe wapo, document hizi zipo, Waziri anazo, Katibu Mkuu anayo, Bodi inajua na Mkuu wa Chuo anafahamu. Sasa haya mambo Mheshimiwa Mwijage yatapunguza kasi na maneno yako yanaweza yakatia wasiwasi katika mazungumzo. Vielelezo hapa viro mpaka risiti, mpaka bank statement hizi

hana zimetolewa. Kwa hiyo, ni muhimu sana haya mambo unapopanga uyaangalie, haya makandokando tunaposema wala siyo kuzomea huu ni ukweli mambo yapo, yafanyieni kazi haya, nendeni mkaapeleke *special audit*, CAG akague hivi vyuo alete taarifa, hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, mimi ni Mbunge wa Jimbo la Ukonga. Kule Ukonga tunayo shida ya sehemu ya kupata vifaranga, vingi vinatoka nje ya Jimbo na vingine hata nje ya nchi. Wananchi wengi wanafuga kuku, akina mama, vijana wa bodaboda, wauza maandazi wamekopa VICOBA wanafanya biashara ile kwa maana ya kujikimu. Mtu analisha almost miezi miwili, mitatu kwa gharama kubwa vinakufa vyote na hakuna fidia. Unakuja kutafuta unaambiwa eti havikuchanjwa, nani alipaswa kuchanja, nani ana-control standard, bidhaa inatoka wapi, kiwanda kinalipaje, hayo mambo yote wananchi wangu wanapata shida sana. Kwa hiyo, nitaomba unapokuja hapa pia ni muhimu tukapata majibu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunajua kwamba kulikuwa na mpango hapa unazungumzia habari ya biashara lakini Serikali hii ya chama changu cha zamani na mimi huwa nazungumza nawashangaa ambao wanapiga humu. Mimi nilikuwa kada wa hicho chama yalinishinda nikabwaga manyanga, lakini niko vizuri kweli kweli. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa namwambia Mheshimiwa Nape kama wakiruhusu kuongea pumba sisi tunaweza kutengeneza pumba tukaitumia vizuri kuliko mtu anayeokota pumba. Kwa hiyo, ni muhimu sana tukazungumza mambo serious. Kule kuna kitu kinaitwa *DECI* na MALINGUMU, fedha zinapandwa, Serikali ilisajili watu wakawa wanalipa kodi, wakafungua na ofisi, hili jambo na lenyewe mpaka leo wananchi wangu wamepata shida. Watu wa Dar es Salaam wamedhulumiwa fedha kesi imeenda Mahakamani inaendelea au haiendelei haijulikani. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ulivyozungumzia wafanyabiashara wadogo wasaidie hawa watu, hii *DECI* na MALINGUMU uje na majibu nani alisajili na Mawaziri wastaafu walihusika na fedha zilikusanywa zikaenda Hazina mpaka leo hawajarudishiwa mitaji yao, hawajalipwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo ndiyo maana tukasema viwanda vilikufa watu wakauziana, leo mnakiri wenyewe na mnajua kwamba viwanda vingi vimekuwa scraper. Sasa watu hawa watengenezee matumaini waone hali sasa ni nzuri, makandokando yameondoka, viwanda vikianzishwa vitaendelea kudumu, vitazalisha, watapata ajira, ni muhimu sana kujua hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeenda kwenye kiwanda cha Mbagala kule, kuna kiwanda pale Ukonga cha Nguo kinaitwa Namel, hivi viwanda mmepitisha mshahara wa wafanyakazi maskini wetu wale wanalipwa shilingi laki moja kwa mwezi, nataka utuambie hivi unavyoanzisha sasa na vyenyewe

mshahara shilingi laki moja inasaidia kitu gani. Wanafanya overtime wanalipwa shilingi elfu mbili, hawana gumboot, hakuna usalama mle ndani, wanafanya kazi zaidi ya masaa ya kazi, mikataba hawapewi, kwa hiyo ina maana watu wanaonewa. Kwa hiyo, viwanda vinaweza vikaja mkafurahi kupata kodi, hii milolongo ambayo hamjarekibisha wananchi wakaendelea kuumia na hiyo ni shida tutaomba pia uoneshe kama kuna mazingira rafiki ambayo yametengenezwa ili watu wetu waweze kufanya kazi. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, chakula cha kuku Dar es Salaam ni shida sana, bei ni kubwa, kilikuwa kinauzwa shilingi 36,000 kimepanda mpaka shilingi 60,000. Nimejaribu kuuliza wananiambia mahindi, pamba na alizeti zinapelekwa nje bila kuwa processed na wafanyabiashara wakubwa wanaificha kwa hiyo inavyorudi bei inakuwa ni kubwa sana, hatuwezi ku-control.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeuliza kwa mfano dawa zikoje, zile dawa za chanjo za kuku hata ng'ombe nyingi hazina TBS, nendeni pale Ukonga mkague maduka yale hakuna TBS, hawalipii, kwa hiyo bei wanajipangia wenyewe. Kuna biashara holela na hili linaweza kuhatarisha maisha yetu kwa sababu tunakula mayai ya kuku hawa kumbe yako *below standard* tunapata magonjwa mengine ya kutisha. Kwa hiyo, Mheshimiwa naomba utusaidie pia katika hilo. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nataka unisaidie ni kuhusu mifuko ile ya kijamii. Kumekuwa na malalamiko hapa kwamba wafanyakazi wale michango yao haipelekwi kwenye mifuko hii ya jamii. Sasa lazima uweke mazingira rafiki kwamba hili nalo ikitokea unafanyaje...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako ndiyo huo.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Dah, ahsante sana, siungi mkono hoja, ila nawasilisha. (Makof)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Mbarouk.

**MHE. MUSSA BAKARI MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Na mimi kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha na mimi leo kusimama hapa kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Vilevile nitakuwa ni mchoyo wa shukrani kama sikuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo langu la Tanga Mjini ambao kwa mara ya kwanza

wamebadilisha historia ya Tanzania kwa kupatikana Mbunge wa Upinzani katika Jimbo la Tanga iliyokuwa ngome kuu ya CCM. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia viwanda, biashara na ubinafsishaji. Kwanza nisema bila umeme wa uhakika basi Tanzania ya viwanda itakuwa ni ndoto za alinacha. Nasema hivi kwa sababu nchi yetu imekuwa kama nchi ya kufikirika. Baada ya kugundulika gesi na makaa ya mawe tumekuwa tukiambiwa kwamba umeme kukatikakatika utakuwa kama historia ya vita ya Majimaji iliyopiganwa mwaka 1905 lakini leo umeme umekuwa hauna uhakika, humu humu ndani ya Bunge pia umeme unakatika, sasa sijui Tanzania ya viwanda itakuwa ni Tanzania ipi hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba viwanda, biashara, reli na barabara ni vitu vinavyoambatana. Imefika mahali sisi Tanzania tumekuwa tunafanya vichekesho, kwa nini? Leo reli inayotoka Tanga kuja kuungana na reli ya kati imekufa, lakini vilevile pia viwanda vingi, hakuna asiyejua kwamba Tanga ulikuwa ni mji wa viwanda. Tulikuwa na Kiwanda cha Chuma – Steel Rolling Mills, tulikuwa na kiwanda cha Sick Saw Mill, tulikuwa na Kiwanda cha Mbolea, tulikuwa na Kiwanda cha Kamba – Ngomeni, tulikuwa na NMC, tulikuwa na karakana kubwa ya reli, vyote hivyo vimeuliwa chini ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, kutokana na kufa viwanda hivi, leo Mji wa Tanga umekuwa hauna ajira. Tukumbuke Tanga ulikuwa siyo mji wa mazao ya vyakula, ilikuwa ni mashamba ya mkonge nayo pia yamekufa. Sasa imefika mahali Tanga umekuwa kama mji ambao ulikuwa na vita kama Baghdad vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia kuuliwa viwanda vya Tanga matokeo yake sasa miaka 55 baada ya uhuru Tanzania leo tunaongoza kwa kilimo cha pamba lakini nepi za watoto wachanga *made in China*. Sindano ya kushonea kwa mkono *made in China!* Vijiti vya kuchokolea meno (*tooth pick*) *made in China!* Miti ya kuchomea mishikaki pia *made in China!* Basi hata handkerchief pia! Bado tukikaa humu ndani tunajisifu kwamba sisi tuna viwanda na tunataka kuifanya Tanzania ya viwanda, mimi sikubaliani na suala hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasema kama tunataka kuifanya Tanzania ya viwanda kwanza tufufue vile viwanda vingi vilivyouliwa katika mji wa Tanga! Hakuna asiyejua, ukienda Tanga, Muheza ni wazalishaji wakubwa wa mazao ya matunda hususan machungwa lakini leo tunanunua packet ya juice kutoka Saudi Arabia kwa shilingi 5,000. Hakuna asiyejua kwamba ukienda maeneo ya Hale na Korogwe kuna maembe ya kutosha lakini hakuna hata viwanda vya ku-process matunda hayo tukaweza kuza sisi katika nchi nyingine. Leo matunda na juice zote zinatoka nje wanaoleta huku wanachukua pesa zetu za kigeni wakaenda kununulia. Unapokuwa una-import zaidi kuliko ku-export maana yake unajikaribishia umaskini lakini wenzetu hilo hawalion! Anayezungumza hapa ataanza kupongeza, ataanza kusifu llani ya Chama cha

Mapinduzi lakini yanapoharibika hasemi kwamba ni llani ya Chama cha Mapinduzi ndiyo inayoharibu! (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mimi nashangazwa, mbona nchi nyingi duniani zinafanya maendeleo lakini hawataji ilani za chama! Kenya shule zinajengwa, maabara zinajengwa, ukienda Malawi barabara zinajengwa na maendeleo mengine yanafanyika lakini watu hawataji llani ya Chama! Mimi naona tatizo hapa ni Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, lazima tubadilike, Serikali yoyote inayokusanya kodi kazi yake ni kurudisha kodi hiyo kwa kuwapelekea wananchi maendeleo. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye suala la biashara, Watanzania leo wamekuwa wakihangaika hususan akina mama, ukienda katika kila nyumba sasa hivi katika mikoa yetu na miji yetu mikuu, kila nyumba ina frame za maduka kwa sababu ajira hakuna na viwanda hakuna. Leo akina mama ndiyo wanaolea familia, wanahangaika wanafungua biashara lakini cha kushangaza sheria ya biashara ya Tanzania ni tofauti na sehemu nyingine. Kawaida ya biashara, mfanyakibashara anapoanza biashara upya lazima apewe *tax holiday* ili ajiweke vizuri aweze kupata faida alipe kodi. Hata hapa ndiyo sheria inavyosema kwamba usilipe kodi kabla ya kupata faida lakini Tanzania mtu anakwenda TRA akishapata *TIN Number* anafanyiwa assessment, analipa kodi kabla hajafanya biashara! Matokeo yake sasa akina mama wanaokopa mikopo katika taasisi za kifedha kama BRAC, Poverty Africa na wengine wamekuwa wakichukuliwa vyombo vyao, wamekuwa wengine wakijinyonga na wengine wamekuwa wakikimbia familia zao kwa kuogopa madeni wanayodaiwa na taasisi za fedha. Sasa kwa nini Serikali yetu haiwasaidii wananchi wake katika biashara? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda Rwanda na Burundi anayekuwa na nia ya kufanya biashara baada ya mtaji aliokuwa nao Serikali inamuongezea fedha na kuambiwa kwamba tunakuongezea fedha uajiri Waburundi wenzako au Warwanda wenzako wawili usaidie kukuza ajira katika nchi yetu lakini Tanzania ni kinyume. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, nakuomba ulizingatie hili, Tanga viwanda vingi vimeuliwa, hususan reli. Panazungumzwa hapa reli ya kati itajengwa katika kiwango cha standard gauge, lakini Waswahili wana usemi wao wanasema, mwiba uingiapo ndiyo unapotokea hapo hapo. Reli ya kati ilianza kujengwa na Wajerumanî katika miaka ya 1905 na ilianza Tanga, vipi leo twataja reli ya kati ijengwa kuanzia Dar es Salaam! Tumesahau kwamba mwiba uingiapo ndio utokeapo? Mimi naomba kama reli ya kati inataka kufanyiwa ukarabati basi ianzie Tanga, Bandarini pale ambapo ndio reli ilipoanza. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nalotaka kusema, tumeambishiwa hapa na wazungumzaji wengi kwamba viwanda vilifanyiwa ubinafsishaji na

vingine kuuzwa. Amesema Mheshimiwa Lijualikali kwamba kule kwake kuna mbuzi katika kiwanda cha sukari lakini hata Tanga kwenye kiwanda cha chuma! Cha kushangaza walikuja wawekezaji wa Bulgaria, wakaja Wajerumani wakataka kiwanda kile cha chuma lakini matokeo yake wakanyimwa, wakapewa wawekezaji waliotakiwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Matokeo yake sasa kiwanda kile imekuwa ndani kunafugwa mbuzi napo kama vile ilivyokuwa Morogoro. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda cha chuma cha Tanga kilikuwa kinazalisha *two products same time*, kulikuwa pana misumari bora kabisa katika Afrika Mashariki na nondo zinazozalishwa Tanga zilikuwa ni bora. Sasa na mimi naijuliza, chuma bado kinahitajika siku hadi siku katika ujenzi wa maghorofa, katika ujenzi wa madaraja lakini hata katika body za magari, inakuwaje kiwanda cha chuma kipate hasara mpaka kife? Huu ni ushahidi kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeshindwa kusimamia viwanda vyetu. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme Mheshimiwa Waziri, hoja yako siiungi mkono naunga mkono hoja iliyotolewa na Upinzani lakini kwanza iangalie Tanga! Katika viwanda vingine usisahau viwanda vya matunda, Tanga ni mji unaozalisha matunda kwa wingi, tunahitaji viwanda vya matunda navyo vijengwe Tanga ili Tanga iweze kurudia hadhi yake kama zamani. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nikumbushe historia kidogo, hata ukiangalia jina la nchi hii kabla ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar ilikuwa inaitwa Tanganyika. Sasa hebu angalia Tanga ilivyokuwa na umuhimu katika nchi hii, Tanga na nyika zake ndio tukapata hii Tanganyika lakini bado watu wamesahau historia kwamba Tanga imechangia mchango mkubwa katika kuleta uhuru wa nchi hii, leo Tanga imekuwaimeachwa kama mtoto yatima! Hata ukiangalia bajeti ya mwaka huu 2016/2017, Tanga tuna mambo mengi ambayo tumeachwa, tutakuja kuzungumza. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata vilevile pia katika huo Muungano wa Tanganyika na Zanzibar palikuwa pana mahusiano mazuri sana kati ya watu wa Zanzibar na watu wa Tanga na hususan katika masuala ya kibiashara. Mpaka leo watu wanaingiliana katika biashara, watu wanawekeza upande wa Bara na Visiwani, lakini Serikali imekuwa haitii nguvu kwa hawa wafanyabiashara ambao ni wazalendo.

Vilevile pia tumeacha sasa kuikumbuka na kuisaidia Tanga kwamba ndio yenye historia ya uhuru wa nchi yetu, lakini tunaomba Mheshimiwa Waziri asisahau kwamba hata yeye yawezekana akawa ana jamaa zake na ndugu zake Tanga, kwa nini? Kwa sababu Tanga ulikuwa ni mji wa viwanda, uliweza kukusanya makabila yote ya Tanzania 122 lakini hata nchi jirani kutoka Burundi,

tunao Warundi wengi kule, kutoka Malawi tunao watu wanaitwa Wanyasa kule, kutoka Kenya, Uganda, Zambia watu walikuja kufuata ajira Tanga, sasa inakuwaje viwanda vya Tanga vife. Mimi naomba kama Waziri una nia ya kweli ya kuifanya Tanzania ya viwanda hakuna haja ya kujenga viwanda vipyta, tukifufua viwanda vya Tanga peke yake na maeneo mengine ya Tanzania kweli tutakuwa Tanzania ya viwanda. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa kabisa tuisahau kwamba bila ya umeme wa uhakika viwanda vitakuwa ni kama vile mchezo wa alinacha. Lazima kwanza tuwe na umeme wa uhakika, iwe tuna dhamira ya kweli kwamba kweli tumegundua gesi, tumegundua makaa ya mawe lakini hata upo umeme pia wa upepo lazima tushirikishe umeme wote huo. Wenzetu wa baadhi ya nchi kama Ujerumani pamoja na ukubwa wake wanatumia solar power system na sisi kwa nini hatuna mpango wa muda mrefu wa Serikali wa kujenga mtambo mkubwa wa umeme wa kutumia solar power system? Kama tuki-fail katika hydro-electric power twende katika gesi, Kama kwenye gesi tumeshindwa, tungekwenda katika solar power. Sasa Waziri unapozungumzia viwanda bila ya kutuhakikisha kwanza kwamba tuna umeme wa uhakika, mimi hapo inakuwa sielewi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri, hakuna haja ya kujenga viwanda vipyta, tufufue viwanda vingi zaidi ya 70 viliviyokuwa Tanga ambavyo vimekufa lakini tufufue na viwanda vingine ambavyo vya zamani kama alivyotaja Mheshimiwa mmoja kiwanda cha Nyuzi Tabora na vinginge ili tuweze kufikia maendeleo ambayo Watanzania wanayatarajia. (Makofii)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa muda wako ndio huo. Tunaendelea na Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mheshimiwa Shally Josepha Raymond ajipange.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Na mimi nataka nitoe mchango wangu kuhusiana na Wizara hii ya Viwanda. Mheshimiwa Waziri nashukuru umekuwa unaongea sana na unapojibu maswali kama vile bado tuko kwenye kampeni. Tunatagemea sasa hivi hapa utupe data za uhalisia namna utakavyokwenda ku-earth majukumu yale ambayo Mheshimiwa Rais amekupa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua Mheshimiwa Rais amesema anataka nchi hii, jambo ambalo ni jema, iwe ni nchi ya viwanda kwa maana ya uchumi wa viwanda. Nchi hii wahitimu kwa mwaka ni 800,000. Katika majukumu ambayo Mheshimiwa Rais amekupa wewe kama Waziri amesema 40% ya

wahitimu 800,000 anataka waende kwenye viwanda. Katika 40% ya hao watu 800,000 ni watu 320,000 maana yake hawa tunawaingiza kwenye viwanda. Kwa nchi hii kiwanda kikubwa ambacho kimewahi kuajiri watu wengi sana hawazidi 5,000. Sasa twende kwenye hesabu za haraka haraka maana ukija hapa unakuwa kama unafanya kampeni, twende kwenye hesabu za haraka haraka za kawaida tu. Ili lengo lako hilo la kuajiri watu 320,000 kwa mwaka lifikiwe maana yake unatakiwa uwe na viwanda 530 katika kipindi cha miaka mitano ya llani yenu ya Uchaguzi ambayo mnajisifu nayo. Hoja inakuja hapa mwaka huu sasa tunakwenda nusu una viwanda vingapi? Naomba utujibu hapo, una viwanda vingapi mpaka sasa? Utatutajia cha Dangote, alikiacha Mheshimiwa Kikwete ambaye sasa hivi mnamzomea, ninyi hamjatengeneza hata kimoja, una viwanda vingapi? (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii wafanyabiashara wanataka kuongea na Serikali yako, mnawakatalia, mnawa-frustrate, hamkai nao. Bado mnasema mna wawekezaji kutoka nje wakati hawa hawa waliomo ndani hamuwezi kuwa-handle vizuri. Ningekuomba Mheshimiwa Waziri hebu tuache mbwembwe tuwe *realistic*, hizi hesabu zinakataa, huna uwezo huo. Saa hizi hata viwanda viwili vipyta huna! Ukinionesha viwanda vitatu umetengeneza nitakupa *Land Cruiser* yangu hapo nje kama unavyo, toka mmeingia Serikali hii, huna hivyo viwanda. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mnakuja hapa mnatupa takwimu za uongo, za kutuaminisha matumaini ambayo hayapo, hauna viwanda hivyo. Ukipiga hesabu hawa watu huwezi kuwapeleka, kiwanda kikubwa kinachoajiri watu sasa hivi ni Breweries inapeleka watu 3,000. Hawa watu 320,000 kwa mwaka where are you going to employ them, wapi utaenda kuwaajiri? Tunaomba unapokuja utuambie hesabu za uhalsia, hatuko kwenye kampeni, tunataka utuambie ukweli! Naomba hilo usije na majibu mepesi mepesi, hivyo viwanda hauna. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ndugu yangu hapa amezungumza, *infrastructure* ya umeme iko wapi, umeme wa uhakika uko wapi mpaka sasa unaowaita hao. Umetuambia Jumatatu tuje tugawane hapo, hatuwezi kugawana watu kama njugu wakati hakuna *infrastructure* yaani mimi nitaondoka na mwekezaji nasema naenda naye lringa naenda naye wapi! Tukafanye nini? Mazingira yaliyoandaliwa yako wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri mimi ningeomba hebu tuambizane ukweli na ninyi ndio mtakaokwenda kumuangusha Mheshimiwa Magufuli kama mkija na mbwembwe ambazo hazina uhalsia. Mtupe mambo ambayo yanawezekana. Nimekupa hii takwimu uikatae! Unahitaji kuwa na viwanda 530 ndiyo uwapeleke hawa 40% kwenye hivyo viwanda unavyosema unakwenda kutupa na kuwaaminisha Watanzania

kwamba nchi itakuwa ya viwanda, mambo yatakuwa mazuri, utupe figure ambazo ni za uhalisia. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine amezungumza Mheshimiwa mwenzangu hapa kuhusiana na hawa wafanyabiashara wadogo wadogo ambao tumezungumza sana hata miaka mitano iliyopita tunawaona kama ni kero katika nchi yetu badala ya kuwaona ni fursa. Kwa hiyo, hebu tu-change, is a *mindset thing*. Change what you see by changing how you see. Tunapowaona wale watu ni kero ndiyo tunagombana nao na mabomu badala ya kuweka mikakati ya kuwafanya hawa watu wawe na tija kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu ni wengi sana wangetafutiwa maeneo. Tumezungumza sana na mwaka jana tulitoa mpaka na maazimio kwenye eneo hilo kuhakikisha miji yote yatengwe maeneo walao kila weekend maeneo yale yafunguliwe, haya mambo yamekuwa yakusuasua katika maeneo mbalimbali. Naona hapa kwa mfano Dodoma imeshaanza na maeneo mengine lakini tumekuwa tukiwapiga hawa Wamachinga, tumekuwa tukiwaonea, hatuwatengenezei mkakati mzuri. Kwa sababu wao kama alivyosema ndugu yangu hapa, ndiyo wako kwenye field wengine wote hapa tunaongea nadharia tu lakini wao wako kwenye field ndio wanalionia soko lilivyo.

Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri, tungeomba hili tatizo nalo lipate ufumbuzi wa kudumu na wa moja kwa moja badala ya kuwaona hawa watu ni kero tuone kama ni fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi kwenye suala la viwanda, kwa mfano Mwanza kuna kiwanda kilikuwa cha nyama ambacho kilikuwa cha Tanganyika Packers, wakaja wakawekeza wawekezaji hakikwenda vizuri. Wakaja watu wa nje, baadaye wakaja Wamarekani, Wamarekani baada ya matatizo yao ya uchumi, hakipo. Leo Mheshimiwa unasema kwamba watu waje, kile kiwanda kule tatizo ni nini? Vilivyopo vimeshindwa nini na sasa hivi unatuaminisha kitu gani kitasababisha hivyo viwanda vilivyopo kwenda mbele? Vile vilivyoshindwa vilishindwa kwa nini na sasa hivi kwa nini unatuaminisha kwamba hivyo vilivyopo tutasonga mbele? (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hebu tuache mambo ya kampeni. Uchaguzi mlishashinda whether mliuibia kwa magoli ya mkono, *it is fine*, mlisashinda, Serikali ni ya kwenu.

Sasa hapa hatuhitaji kampeni, tupeni vitu ambavyo mnakwenda ku-earth. Hatutaki mbwembwe! Mheshimiwa Mwijage acha mbwembwe, tipe vitu ambavyo ni practical. Mwalimu wangu alikuwa anasema how can you earth it?

Tuambie unawezaje kutuambia kwenye ground? Tuna viwanda vingi sana, Iringa tulikuwa na viwanda vingi vya akina-TANCUT vile vyote vimekufa. Ukienda Mbeya hivyohivyo, ukienda Morogoro hivyohivyo. Sasa hivi mnakuja na lugha nzuri sana, very testy lakini ukienda kwenye uhalsia, hii hesabu ni ndogo sana nimekupa, *it doesn't work brother.* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba atakaporudi hapa atatupa majibu. Hii ni hesabu ndogo sana huhitaji kuwa na elimu ya Chuo Kikuu, ndogo tu. Utupe majibu namna gani hii kazi aliyokupa Mheshimiwa Magufuli ya kuhakikisha 40% ya wahitimu 800,000 wanaingia kwenye viwanda, ni viwanda vipi? Mpaka saa hizi huna hata kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niliweke wazi hilo, tuache mbwembwe, tuambizane ukweli hapa ili tuisimamie Serikali. Nikushukuru sana kwa kunipa nafasi. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea kama nilivyosema na Mheshimiwa Dkt. Kafumu atafuatiwa na Mheshimiwa Shally Raymond na Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe ajiandae.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba nianze kwa kumshukuru tena Mungu kupata nafasi hii kutoa na mimi mchango wangu. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara na Mazingira, na ni Mwenyekiti. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitoe mchango wangu baada ya kuwa nimekutana na wadau wengi sana pamoja na Kamati yangu, tulikutana na wadau wenye viwanda, wafanyabiashara lakini pia tulikutana na mamlaka za udhibiti, ziko nydingi, tulikutana nazo kama 19 hivi. Tulikutana pia na waagizaji wa bidhaa na wale ambao wanapeleka bidhaa nje. Pia tulikutana na Wizara ya Viwanda na Biashara. Kila tulipokutana swalilangu la kwanza kwa Waziri lilikuwa ni kwamba hivi tunafanya muujiza gani ili tuweze kutekeleza hii azma ya Mheshimiwa Rais ya kuwa na viwanda katika miaka 10 ijayo? Waziri ni shahidi na hata Wajumbe wenzangu ni mashahidi, tuliuliza sana swalihili na kwa kweli hatukupata jibu kwa maana kwamba yale yote yaliyowasilishwa kwenye Kamati ni *business as usual.* Kwa kweli ni vizuri sisi Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani na sisi wa Chama cha Mapinduzi tutoe ushauri ambaotutuo hapa tulipo utupeleke mbele. (Makofi)

Baada ya kutafakari, naomba niseme mambo kama sita hivi kwa kifupi, nadhani muda utanitosha. Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano una maneno mazuri sana na unasema vizuri sana, *naturing industrialization in Tanzania.* Maneno haya ni mazuri na Mheshimiwa Rais ameya-reflect wakati

anafanya kampeni na sisi sote lazima tufikirie kwenda huko. Tukifanya kazi kama tunavyofanya tunaweza tusifike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, ni lazima tuwe na quick wins sasa, vitu ambavyo tutavifanya kwa haraka tuone mabadiliko. Jambo la kwanza katika quick wins, ni viwanda vilivyopo na wafanyabiashara waliopo; tuwaondolee kero zao, tutengeneze mazingira mazuri, waweze kupanuka badala ya kufa. Walituambia wana kero sana na Waheshimiwa Wabunge wamesema, kero ni nyingi. *Regulation* ya udhibiti, kila mtu anakuja kudhibiti kiwanda kidogo. OSHA anakuja, nani anakuja mpaka unafunga. Kwa hiyo, *Regulatory Authorities* hizo bado zinachelewesha huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walisema mambo mengi; utitiri wa kodi, tozo na vitu vingi sana. Jambo lingine walilosema hao wenye viwanda vilivyopo, walisema service wanayopewa na hizi *institutions*, wakati mwingine wanazilipia kwa bei kubwa. Serikali inatakiwa itoe service hii bure kwa hivi viwanda ili viweze kuendelea. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, walilosema miundombinu. Umeme unakatika sana. Pamoja na kwamba tuna mipango mizuri, tunaishukuru Serikali, lakini bado umeme uwe *stable, reliable*. Siyo unakatika! Kwenye kiwanda ukikata dakika tano, umechelewesha *production* kwa muda mrefu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia walisema kulinda bidhaa za ndani. Kuna hatua tunaona zinachukuliwa, tunaishukuru Serikali. Tulinde bidhaa za ndani dhidi ya bidhaa za nje. Viwanda na wafanyabiashara waliopo wana mambo mengi sana ambayo siwezi kuyasema, lakini Waheshimiwa Wabunge wamesema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Serikali mmeonesha vizuri sana kwenye hotuba, lakini pia kkwenye Mpango, viwanda vya kimkakati. Ukioma kwenye mpango vimejatwa vizuri; viwanda vya chuma, vimetajwa viwanda vinavyotumia mazao ya kilimo na viwanda vingine kama vya mazao ya uvuvi na mazao ya mifugo. Ukienda kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, unaona ni kiwanda kimoja tu cha chuma ndio cha kimkakati, lakini viwanda vingine; sijui kiwanda cha kutengeneza dawa za kuua mbu, sio cha kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima tuangalie hasa viwanda vinavyotumia mazao ya kilimo. Hivi ni vya kimkakati kweli, sivioni kwenye speech! Kwa hiyo, tunaomba hilo liwe jambo la pili. Tunavyotaka kujenga viwanda vipyta, ni hivi vitakavyohamasisha *industrialization* katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni kuhamasisha wawekezaji. Tuliongea na wawekezaji wengi wa ndani na nje, wote walisema wanaonekana

kama wezi. Mtazamo wa Watanzania wengi na mtazamo wa hata viongozi wengine, mwekezaji wa ndani anayepewa eneo kubwa anasumbuliwa, anaonekana mwizi, yule wa nje ndio kabisa! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana, wawekezaji hawa wanahitaji misamaha. Japokuwa tulipitisha sheria mwaka jana, ile ya VAT ya mwaka 2015 nadhani, na mimi nilisimama hapa nikasema hii VAT ukiweka kwenye vifaa kwa ajili ya kutafuta madini, kwa ajili ya kuanzisha kiwanda, utafukuza wawekezaji. Kwa hiyo, nasema tena, tutazame hii misamaha tusiigope.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne ni kufufua viwanda vilivyokufa. Kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge, viko viwanda vya mazao ya kilimo kama pamba. Igunga kule tulikuwa na Manonga Ginnery, ilikufa. Hatutazamii kufufua viwanda vya namna hii. Kule Tabora ndugu yangu amesema; viwanda vya nyama Mwanza, Shinyanga na kadhalika tumeviacha; viwanda vya chuma Tanga na kadhalika, tuvifufue hivi. Kuna viwanda vingine kama CAMATECH na Mang'ula, vitu vya namna hii tuvitazame, tuvifufue. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, niseme maeneo ya kuwekeza (EPZA), tulipe madeni. Serikali itafute fedha ilipe madeni, Shilingi bilioni 191. Fedha hizi zitatuteni mlipe ili mpate maeneo mengine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, naomba nimalizie kwa kusema, tulikubaliana na Mheshimiwa Waziri kwamba ili tuweze kupata *gist* ya mambo haya, tuitishe Mkutono wa wadau na tulikubaliana tuitishe Dodoma kabla ya bajeti. Tulisema wadau ambao tunataka tuwaitishe, tuzungumze tufanye dialogue hii, tujue; tukipata yale maneno ndiyo tuyaingize kwenye mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua mwaka kesho tutakuwa na mpango mzuri zaidi kwa sababu tutakuwa tumepeata mawazo ya wenzetu. Kwa hiyo, wadau ambao tulikubaliana, Mheshimiwa Waziri na hii lazima uitishe labda hata wiki ijayo ili tupate mambo haya kwa ajili ya mwaka kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea, Mheshimiwa Shally Joseph Raymond, atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Bashe na baadaye Mheshimiwa Zaynabu Matity Vullu.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa hii; na jina langu ni Shally Josepha Raymond, lakini kwa vile baba yangu alikuwa anaitwa Joseph, mkiita hivyo naitika na nakubali pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mungu sana kwamba ametuweka wote hapa tuweze kuzungumzia mambo ya maendeleo ya nchi yetu. Kipekee naomba shukrani hizi ziwafikie wanawake wa Mkoa wa Kilimanjaro ambao ndio walionipigia kura nikaingia hapa kupitia Viti Maalum. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunazungumzia Wizara ambayo ni nzito na Wizara ambayo kwa kweli llani ya CCM inazungumza wazi kwamba sasa twende kwenye uchumi wa viwanda kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Iko kwenye ilani! Mwasilishaji wa hotuba hii, Waziri wetu yuko makini na ni mzungumzaji mzuri, ameongea kwa makini, wataalam wameandaa hotuba vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla yangu amezungumza Mwenyekiti wa Kamati hii, na mimi niseme kwamba naungana naye na yote aliyosema, lakini na mimi nataka nihoji kupitia kwako Mwenyekiti, Kamati ilipokaa ilikuwa na nia nzuri na imetuambia, ila kuna mambo magumu nimeyaona kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna shida ya uwasilishwaji wa fedha za maendeleo. Hadi kufikia mwezi huu wa tatu walikuwa wamepewa shilingi bilioni moja tu. Sasa shilingi bilioni 1.6 kwa viwanda vya Tanzania nzima, itafanya nini? Nirudi pia kwa Waziri wangu, yeye leo hapa amekuja na kitabu chake hiki, anatuomba hapa tumpitishie shilingi bilioni 81.8, Tanzania nzima! Hivi kweli fedha hiyo ndiyo italeta mabadiliko ya viwanda? Haifiki hata trillioni moja! (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipitia hiki kitabu cha Mpango wa Maendeleo, nikidhani kwamba labda hiyo ndiyo Wizara iliyopewa fedha nydingi kutokana na mabadiliko tunayotarajia, lakini nikakuta hapana, kuna Wizara ambazo zimepewa mpaka shilingi trillioni tatu. Sasa hii Wizara ya Viwanda na Biashara inashindikana nini kuipa hata shilingi trillioni mbili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuwaombea fedha ili hii mipango mizuri iliyoinishwa kwenye kitabu hiki iweze kutekelezeka. Niseme wazi kuna jambo ambalo linanikera. Wakati sisi huku tunawaombea fedha au tunaona kwamba fedha hii haitoshi, Mawaziri wetu wanatuambia hiyo hiyo, tutaenda kigumu kigumu! Hii siyo kazi ya mtu! Ni kazi ya nchi hii, sisi tumeona, na ninyi mnatakiwa mwone! Fedha hii haitoshi! (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye miaka ya 1980, SIDO ilikuwa inafanya vizuri sana nchini. SIDO zikuwepo katika Mikoa yote na sasa hivi SIDO zimebaki mfumfu tu, haziko vizuri. Sasa najua tunapoongelea viwanda, kuna viwanda vidogo, vya katika na vikubwa. Mimi kwa ajili ya ajira ya vijana wetu, naomba nibaki kwenye viwanda vya katika au vidogo kiasi ili nianzie hapo SIDO.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila Mkoa una eneo la *SIDO* limetengwa na wapo sasa watu wandafanya shughuli kule ndani ya *SIDO*, lakini Serikali kiasi imetoa mkono wake. Mimi nilikuwa naomba maeneo haya ya *SIDO* na viwanda hivi vilivyokuwa vimeanzishwa kwenye *SIDO*, sasa vifanyiwe kazi maalum ya kivifufua. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika shughulil za viwanda, wengi tunazungumzia tu mashine, lakini nguvu kubwa ya kiwanda ni rasilimali watu, na sisi watu tunao. Tunao vijana wetu ambao wanatafuta ajira. Ndiyo maana unakuta hata zile nchi zinazoendelea, zinatafuta nchi ambayo ina *labor*, yaani *cheap labor* inakwenda kufanya huko viwanda vyao. Sisi iko hapa hapa, tunataka kufanya viwanda hapa. Kwa hiyo, tuna hao vijana watakaopata ajira. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumbukumbu zangu sahihi kabisa, kila kitu kilikuwa kinapatikana *SIDO*, vijiko vizuri vya *SIDO*, makufuli mazuri ya *SIDO*, vitasa vizuri vya *SIDO*, makarai, mabeseni, leo imekuwaje? Kwa nini hatuvipati vitu hivyo? Eti tunaagiza, tunataka vitu *imported*, vitusaidie nini? Matokeo yake ndio hata vitu vingine tunaishia kwenye mitumba, wenzetu wamechoka wametupa, sisi tunaletewa huku, hapana!

Naomba kupitia kwako, Wizara hii isimamie *SIDO*, vijana wetu wapate ajira na ndiyo hiyo sasa tuanze kuona tunafufua viwanda kwa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna viwanda vikubwa ambavyo vilikuwa nchini na bado baadhi visto. Wakati huo nitoe mfano wa Kiwanda cha Kuzalisha Sukari (*TPC*), kiwanda cha kuzalisha sukari. Ajira yake ni watu 5,000, lakini haikuishia tu ajira, kiwanda hicho kilikuwa pia kina *training school*. Wale vijana wanakuwa *trained pale*, wanakuwa na shule ya kuwafundisha, wanaweza kuchonga vyuma, wanaweza kukarabati vyuma hivyo, wanaweza kuvitumia. (Makofi)

Sasa nilikuwa naomba kila mwekezaji anayekuja akaweka kiwanda, awe pia na nafasi ya *ku-train* vijana wetu ili wawe ni watu ambao wana ujuzi katika jambo lile linalofanyika. Hili linaweza kufanyika pia kwenye viwanda vya sementi, bia labda na viwanda vingine. Pia kwenye hicho kiwanda cha *TPC* ningependa pia wafufue ile *training school*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi nyumbani. Naelewa kwamba charity starts at home. Mimi nitokako ni Kilimanjaro, viwanda vyetu vyote vimekufa, sasa hivi tunacho hicho kiwanda kimoja cha *TPC* na labda kile cha Bonite ambacho ni private na kiwanda kingine ambacho kipo ni kiwanda kidogo tu cha kutengeneza bia. Tena ni bia ya Serengeti maana ile Kibo imeshakufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Rais anapita katika kampeni zake za kuomba kura za Urais, alisema haitachukua muda mrefu viwanda vyote vitafufuliwa. Kwa haraka haraka naomba nivitaje tu; najua haviwezi kufufuliwa mwaka huu au mwaka ujao, lakini ianze sasa basi process ya kifufua. Tuna *Kilimanjaro Machine Tools*, tuna Kiwanda kile cha Magunia na hiki ni kiwanda muhimu kwa sababu pale Kilimanjaro ni wakulima wa kahawa na hii kahawa haiwekwi kwenye gunia lingine labda kama la sulfate, hapana, unyevu utabakia. kwenye kahawa. Gunia moja tu linalofaa kuweka kahawa ni lile la jute. Kwa hiyo, bado kuna soko la magunia hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri wangu ajue kwamba sasa kuna kazi kufufua kile Kiwanda cha Magunia. Hailishii hapo, pia kuna Kiwanda cha Ngozi. Kwenye kiwanda cha ngozi, kuna private sector ambayo kuna muhindi, ni *Shaha Industries*, anatengeneza vifaa vya ngozi ila umeme unakuwa ni shida na pia kodi zimemuwia ngumu amefunga, aweze pia kuzungumza naye ili kiwanda hicho kifunguliwe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tuna shauku kubwa, tuna hamu ya kuona kwamba tunapiga hatua. Naomba nimtakie kila la heri na ninaunga mkono hoja. Ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Shally kwa mchango wako. Mheshimiwa Vulu!

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote nami nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyenzi Mungu, mwingi wa rehema, ametujalia na leo tumeiona siku yetu ya Ijumaa, basi azidi kutupa heri na baraka na atuongoze kwa kila jambo lilokuwa na heri na sisi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbele yetu kuna hoja inayohusu viwanda. Viwanda tunavyovizungumzia tunataka vitulee mabadiliko ambayo tayari Watanzania tulianza kuwanayo katika miaka ya nyuma. Kwenye miaka ya 1970 tulikuwa na viwanda vingi kwenye maeneo mbalimbali. Msimamizi mkuu katika shughuli hizo za viwanda ilikuwa ni NDC.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapozungumzia uchumi wa viwanda, nasi Watanzania tuko tayari, tumesema tutaupokea uchumi wa viwanda. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri aliyotuwasilishia; ameyataja maeneo mbalimbali ya Tanzania kwamba tutapata viwanda ikiwemo Mkao wa Pwani ninakotoka mimi. Ninamuomba Mheshimiwa Waziri, kwanza atufufulie viwanda ambavyo vilikuwepo na vimekufa. Viliuzwa kwa watu, iweje mpaka leo hakuna kitu chochote ambacho kimeendelezwa au kimefanyika katika viwanda hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika hotuba yake ameelezea kwamba kutakuwa na utaratibu wa viwanda ambapo wenyewe viwanda watashirikiana na wananchi waliokuwepo katika maeneo yale kwa maana ya kuwa wakulima watakaotumia maeneo yale kwa kilimo na vile viwanda vitatumia mazao yale kuzalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai au ushauri kwake, sasa hivi tumeona kuna viwanda vingi nchini, ikiwemo Mkuranga na Bagamoyo, lakini kwa nini jambo hili la kuchukua wakulima wadogo wadogo wanaozalisha mazao yao wasianze sasa hivi tukaona mfano? Hata sisi Wabunge tutakapokwa tunazungumzia suala la kuhimiza na kushawishi watu kuja kutengeneza viwanda kwa maeneo yetu, tuwe na mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano Arusha kuna maeneo wanazalisha maua, lakini pia kuna wakulima wadogo wadogo ambao wanazalisha yale maua, yanauzwa kwenye viwanda, wao wanaasidia zile mbegu na dawa za kuzuia uharibifu wa mazao kwa maana ya maua. Kwa hiyo, naomba na huku kwetu uwezekano wa wakulima wadogo wadogo waweze kununuliwa mazao yao kwa sababu Mkoa wa Pwani, mfano, tuna machungwa mengi, maembe mengi, na matunda ya aina mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka kuthibitisha hilo, msimu wa matunda pita katika maeneo mbalimbali ya Mkao wa Pwani uone mazao yanavyoharibika kwa sababu hakuna pa kuyapeleka. Mkulima hasa mwanamke; asilimia 80 ya wanawake ni wakulima wadogo wadogo. Naomba basi uwezekano Serikali kufikiria ni vipi watakwenda kununua mazao hayo kwa wakulima kuwawezesha na wao wainue kipato chao? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunapozungumzia viwanda, nilizungunguzia kwenye hotuba ya Waziri Mkuu. Kwenye viwanda vyetu vilivyokuwepo sasa hivi nchini, vijana wetu wanatumika vibaya sana. Wao wanaajiriwa kwa mshahara mdogo sana, wakati sisi tunatarajia waajiriwe wapate fedha zitakazowaendesha katika maisha yao, lakini kinyume chake wanapewa mshahara wa shilingi 150,000 kwa mwezi. Shilingi 150,000 kwa mwezi anaifanyia nini kijana yule, mama yule, dada yule, kaka yule? Naomba kama tunakwenda kwenye mtindo wa kuwa na viwanda vingi, basi hata mshahara uwekwe kabisa, aambiwe mwekezaji kwamba mshahara wa kima cha chini isiwe shilingi 5,000 kwa siku.

Mhehimiwa Mwenyekiti, naomba sana, kama kutakuwa na uwezekano kwa Serikali yetu ichukue hata vile viwanda ambavyo vilikufa, vikawezeshwa na wakachukuliwa akina mama wakapewa kiwanda kile waendeshe wao. Wako ma-engineer, wako wataalam wa aina mbalimbali, iwe mfano wa kiwanda kile tuone uzalishaji utakotoka pale. Akina mama ni wachapakazi! Sisemi kama

wanaume hawafanyi kazi, lakini nasema uchumi wa viwanda umkomboe na mwanamke katika viwanda hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema viwanda, tuangalie na mazao tunayoyalima katika maeneo yetu. Mkoa wa Pwani tunalima nyanya nyingi sana, lakini mwisho wa siku tunanunua nyanya za kopo, zinazotoka nje ya nchi, haipendezi! Tuwe na viwanda vyetu, tuwe na nyanya tunazotengeneza wenyewe, tuwe na matunda ya aina mbalimbali ambayo akina mama wanaweza wakatengeneza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nimalizie na hotuba ya Wapinzani kwenye ukurasa kama sikukosea ni wa 16, waligusia ahadi ya Mheshimiwa Rais, kwamba aliahidi atajenga kiwanda cha Korosho, Mkuranga na Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie neno moja tu, Waswahili wana msemo wao wanasema hivi, tena hata waimbaji waliimba, "mtoto acha kupiga mayowe, waache watu waje waone wenyewe."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi toka imetolewa hata miezi sita haijakkamilika. Subirini muone kazi itakavyokwenda. Nawaomba himizeni wapiga kura wenu, wananchi wetu, wasimamie uzalishaji wa korosho, wasimamie uzalishaji wa mazao ya aina mbalimbali ili tuweze kuhakikisha viwanda vyetu vitakuwa na malighafi, inayotoka ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, nasema ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli, kwa ajenda yake ya uchumi wa viwanda. Watanzania na hasa akina mama, tumesimama imara, tutaifanya kazi katika viwanda vitakavyoletwa. Ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunakushukuru. Tunaendelea! Anayefuata Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, atafuatiwa na Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene na Mheshimiwa Zainab Nuhu Mwamwindi ajiandae na Mheshimiwa Balozi Adadi. Nimeshamalizia kwa upande huo.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuchangia.

Jambo la kwanza nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais, ameongelea suala la sukari huko alikokuwa anaelekea Arusha, kwa sababu jambo hili ni jambo la dharura, ni jambo kubwa, kwa sababu leo tu pale Choma cha Nkola sukari ni shilingi 5,000, Nzega Mjini ni shilingi 4,000, Igunga Mjini ni shilingi 3,200, Kibaha hapo kwenye mzani ni shilingi 3,000.

Kwa hiyo, naiomba Serikali, alichokisema Mheshimiwa Rais huu mchakato wa kuagiza sukari na sukari kuingia nchini, kwa sababu mwezi wa Ramadhani umebaki siku chache na kwa tabia ya soko bidhaa huwa zinapanda sana na moja ya bidhaa ambayo huwa inapanda ni sukari. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kumwambia kaka yangu Mwijage, mimi nitakuunga mkono leo. Bajeti hii nitakuunga mkono, ila ya mwaka kesho ukija kwa style hii sitakuunga mkono. Nasema hivi kwa sababu moja, ukisoma ripoti ya Kamati ya Viwanda na Biashara katika miradi ya kimkakati iliyotajwa na Mheshimiwa Waziri, moja ni kufufua General Tyre. Serikali inataka kutenga two billion, lakini Kamati inasema ili uifufue General Tyre unahitaji shilingi bilioni 60. Bajeti ya Serikali ni bilioni 80! Kwa hiyo, namwonea huruma Mheshimiwa Mwijage, anaenda kufanya muujiza gani? Mimi namtakia kila la kheri. (Kicheko/Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivi? Ukisoma hotuba ya kaka yangu Mheshimiwa Mwijage, page namba 43 mpaka 49 anasema uendelezaji wa viwanda vya kimkakati. Kiwanda cha kwanza nachokitaja ni Kiwanda cha Makaa ya Mawe cha Mchuchuma na Liganga ambacho CAG amesema mkataba wake una harufu ya ujisadi, *strategic partnership* tunayotaka kufanya na hawa Wachina, ina walakini. Nasema namtakia kila la kheri kaka yangu, Mheshimiwa Mwijage.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa pili ni wa Magadi Soda wa Engaruka; mradi wa tatu ni wa Viwatilifu TAMCO Kibaha. Najiuliza swali dogo, nimeamua kwenda hadi kwenye dictionary kutafuta tafsiri sahihi iliyotajwa katika Mpango wa miaka mitano, lakini vilevile iliyotajwa na Mheshimiwa Mwijage, ya nini *strategic industries?* *Strategic industries* kutokana na dictionary ya Cambridge inasema kwa kiingereza, nanukuu; “*an industry that a country considers very important for economic development.*” Hii ndiyo tafsiri. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *I am asking myself, kama tunataka kuuondoa umaskini wa nchi hii, ni wapi pa kuanzia? Engaruka? General Tyre? Ukisoma Mpango alichokisema ukurasa wa 62, flagship project, kipengele cha kwanza, anasema maamuzi ya uwekezaji yote yatakuwa based on the countries comparative advantage.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *my question is, do we have comparative advantage over others in the world, kwenye uwekezaji huu wa kutengeneza matairi? Hili ni swali najiuliza namtakia kila la kheri kaka yangu Mheshimiwa Mwijage. Huo muujiza mwaka kesho niuone.* (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulisema wakati tunachangia Mpango Bunge lililopita, nchi hii 65% ya wananchi wetu wako kwenye sekta ya kilimo, kwa nini

hatusemi precisely kwenye documents zetu, kwamba our focus itakuwa ni Agro Processing Industries? Ninayo hotuba ya kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu, nendeni page namba 23 pamba; mwaka 2013/2014 uzalishaji ulikuwa 245,000; mwaka 2015/2016 uzalishaji ulikuwa 149,000, una nosedive! Uzalishaji unaporomoka! Tumbaku uzalishaji unaporomoka! Kila sehemu uzalishaji unaporomoka. What are we doing?

**MBUNGE FULANI: Nothing!**

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kosa letu la kwanza, ni utangulizi wa kauli yetu ya Mpango wa mwaka mmoja; hili ndilo kosa la kimkakati tulilofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema hivi, naomba ninukuu; "Mpango unakusudiwa kuwa na maeneo ya vipaumbele vinne, viwanda vya kuimarisha kasi ya ukuaji uchumi, miradi mikubwa ya kielelezo, miradi wezeshi kwa maendeleo ya viwanda ikiwemo barabara, reli, nishati, bandari, maji, mawasiliano, maendeleo ya viwanda; maeneo yatakayolenga kufungamanisha maendeleo ya viwanda na watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema tunataka maeneo yatakayofungamanisha maendeleo ya viwanda na watu, halafu hayo maeneo hatuvekezi. Hatuvekezi kwenye pamba, hatuvekezi kwenye katani, hatuvekezi kwenye korosho, hatuvekezi kwenye alizeti, hatuvekezi popote, halafu tunatarajia muujiza! Nawaombeni Mawaziri, ushauri wangu wa kwanza kwenu, Mheshimiwa Waziri Mwijage kwanza *in your mind*, wewe ni mtoto, ni matokeo ya wengine. Mkae mtengeneze strategic unit ili muongee lugha moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia hotuba ya Mheshimiwa Mwigulu, nimeangalia ya kwako, nimekata tama. We are planning to fail kaka zangu! Hatuezi kujadili kufanya revolution kwenye uchumi wa nchi hii bila kuamua kuweka vipaumbele vya maeneo yanayogusa watu. Tutakuja hapa kusema uchumi wetu umekuwa kwa asilimia nane, umaskini bado upo kwa sababu mipango yetu yote inaacha watu wetu wengi nje. Hakuna inclusion! Hatuwa-include watu wengi kwenye mipango yetu; na hili ni tatizo. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia uwekezaji, nataka nikwambie Mheshimiwa Waziri, nenda kwenye database ya Wizara, miaka minne iliyopita kilo moja ya ngozi, raw, kwa mchunaji machinjioni ilikuwa shilingi 3,000 leo ni shilingi 400. (Makof)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakutana mwaka kesho, namuunga mkono kaka yangu. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea, Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwamwindi Zainab Nuhu na Mheshimiwa Balozi Adadi ajiandae.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami naomba nichangie hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda kwa kuanza kwa pongezi kwake kwa maandalizi mazuri ya hotuba iliyosheheni mpangilio mzuri unaoonesha azma ya Serikali kutupeleka katika uchumi wa viwanda. Nimefurahishwa na suala zima la kuangalia umuhimu wa kuzingatia miundombinu muhimu, wezeshi kwa ajili ya kuanzisha viwanda au kuviendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka na mimi niongezee hapo kuwa kwa sasa hivi kwa uzoefu tuliokuanao huko nyuma, kila Wizara inafanya kazi peke yake. Napenda kuona atakaporudi kuja kuwasilisha maadhimisho ya hotuba yake, atufahamishe juhudhi ambazo anazifanya kushirikiana na Wizara nyingine ambazo moja kwa moja zinahusiana na masuala ya maendeleo ya viwanda kama nishati, maji, miundombinu, elimu, kazi ili kuhakikisha kuwa mipango yake itaweza kutekelezwa na masuala yote muhimu yatakuwa yamezingatiwa. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tuna viwanda ambavyo tayari vinaendeshwa, vingine vipyta, vingine vya zamani, lakini kwa bahati mbaya bado kuna matatizo ya kimsingi ya miundombinu muhimu, wezeshi kwa viwanda hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua mipango iliyopo kwa viwanda vilivypo kwanza kwa sasa hivi, ya kuhakikisha kuwa vinapata umeme wa kutosha, vinapata *allocation* ya gas kwa ajili ya kuzalisha umeme wa kuendesha shughuli zao, vinapata maji ya kutosha na zaidi ya yote miundombinu bora itakayowezesha mazao kwenda na kuondolewa kwenye viwanda hivi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna matatizo ya kimsingi ambayo lazima tuyatatu sasa kabla hata hatujafikiria kuanzisha viwanda vingine. Hii itakuwa ndiyo njia peke yake ya kuwavutia wawekezaji wa ndani na wa nje kuja kuwekeza katika viwanda nchi hii, baada ya kuona mifano mizuri ya viwanda ambavyo tayari viko nchini. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vilevile kutoa rai kwa Serikali kuwa hadi sasa tunavyozungumza, naamini kutokana na hilo kuwa kila Wizara inajienda yenye kazi bila kuangalia mahusiano ya karibu yaliyo katika Wizara

hizo, tunakuwa na migongano ya sera na sheria, hata taratibu za kiuendeshaji zinazosababisha kuwe na kulinzana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mdogo, ukizungumzia viwanda vinataka kuwekeza, lakini unakuta labda viwanda vinapotaka kuwekezwa sehemu fulani, mweka umeme yeye ile sehemu siyo kipaumbele kwake. Kwa hiyo, moja kwa moja kunakuwa kuna kulinzana. Kiwanda kinaweza kuanzhishwa, soko linaweza kuanzhishwa, lakini linachelewa kuanza kazi kwa sababu halijapata miundombinu muhimu ya umeme, maji na hata barabara. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa kuona jinsi gani Serikali imejipanga, Wizara muhimu zikae pamoja kupanga mipango tangu mwanzo wanapotengeneza *road map* ya viwanda, hadi inapofika utekelezaji kuwa kila kitu kiko *in place* ili viwanda vikianza vianze kufanya kazi bila kusuasua. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuzungumzia suala zima la mambo ya vipimo na viwango. Tuna tatizo kubwa sana hata kwa viwanda vilivyopo katika uzalishaji uliopo wa viwango na vipimo sahihi vinavyoweza kuhakikisha kuwa bidhaa zetu zinapata ushindani unaostahiki. Tuna taasisi ziko chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara ambazo kazi yake ni kuhakiki viwango na vipimo. Kwa bahati mbaya, havina uwezo wa kutosha. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri sasa wakati tunajipanga kwenda kwenye uchumi wa viwanda, kuhakikisha taasisi muhimu kama hizi zinawezeshwa kwa maana ya taaluma, maabara, nyenzo zote zitakazowawezesha wao kuhakikisha kuwa viwango na vipimo viko sahihi ili bidhaa tunazouziwa ziwe zile ambazo zina ubora unaotakiwa au ubora ambaa unaweza kushindana na bidhaa zinazotoka nje ya nchi. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahi kuona katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri, ameelezea kuwa kutakuwa na mgawanyo wa viwanda nchi nzima kufuatana na rasilimali zilizopo. Hili ni wazo jema kwa sababu hii itaondoa ule mtindo wa zamani kuwa kila kitu kinalundikwa katika Miji Mikuu na sisi wa pembenzoni tunakuwa kila siku ni wa kuzalisha malighafi na tunashindwa mahali pa kuzipeleka. (Makof)

Napenda kuona sasa kuona ramani kamili ya viwanda hivi hasa maeneo ya pembezoni au vijijini ambako kilimo kinaendeshwa kwa wingi na jinsi gani viwanda vya aina mbalimbali, vikianzia vile vidogo kabisa, vya kati na hata vikubwa vitakavyokuwa vimeainishwa. Hii itahakikisha Watanzania wengi wanashiriki katika uchumi wa viwanda, wanapata kipato, ajira na vile vile na maisha yao yanainuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia kwa ufupi suala zima la kukuza soko la ndani. Tumekuwa ni watu wa kuagiza bidhaa ambazo hatuzalishi na kuzalisha bidhaa ambazo hatuzitumii. Napenda kuona hili linabadilika kwa sababu bidhaa nyingi tunazoagiza kutoka nje kwa fedha nyingi, kwanza hazina ubora ambaao tungeutegemea, lakini vilevile zinaua soko la ndani na vilevile zinaua ajira zetu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalima mazao mengi sana nchi hii ya kutosha kulisha nchi yetu hata na majirani. Huo ni mwanzo mzuri kwetu kwa ajili ya viwanda. Sasa napenda kupata kutoka kwa Waziri mkakati alionao wa kukuza soko la ndani kwa maana ya kuanza kuwekeza katika viwanda ambavyo vinazingatia mahitaji ya ndani kabla ya kuzungumzia masuala ya ku-export. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kujua, Mheshimiwa Waziri ana mkakati gani wa kupunguza uagizwaji wa bidhaa kutoka nje ambazo kwa kweli hatuzihitaji, ukizingatia kwa sisi wenyewe tunao uwezo wa kuzalisha? Tungependa kuona anaanza kupunguza kidogo kidogo uagizwaji wa bidhaa za nje ambazo haziitajiki na kuongeza uzalishaji wa bidhaa za ndani. Hii itawezekana akishirikiana na Wizara zinazozalisha mazao ya kilimo, ufugaji na uvuvi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la uwezeshaji wa wajasiriamali. Tanzania hii kuna mwenzangu mmoja ni Mheshimiwa Mbunge amesema kuwa kila mahali kuna frame. Mimi lile sioni kama ni jambo baya, ule ni ujasiriamali. Kinachotakiwa sasa ni je, wanawezeshwa vipi hawa wajasiriamali kwa maana ya mafunzo, nyenzo na mitaji? Napenda sana kuona Wizara hii ya Viwanda inaboresha kitengo kinachoshughulika na wajasiriamali ili tuone jinsi gani wamejipanga kuwasaidia wajasiriamali wale wadogo kabisa, wa kati, hata wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ndiyo ina taasisi muhimu zinazosaidia kujenga uwezo wa wajasiriamali kwa maana ya tafiti, masoko na uzalishaji, lakini hatujaona moja kwa moja jinsi ambavyo wajasiriamali wetu wengi wananufaishwa na hizi taasisi. Tungependa sasa kuona ule mpango ambaao upo chini ya Wizara wa *industrial upgrading* unatumika na kufanya kazi vizuri zaidi; kutoa mafunzo kuwatafutia masoko, kuwapa mbinu za uzalishaji na viwango na kuwaanzishia viwanda na kuwasimamia hadi wakomae. Kwa kuanzia na ngozi, nguo, usindikaji chakula, mafuta ya kula na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba sekta ndogo ndogo mbalimbali zichukuliwe na kupewa mafunzo, nyenzo bora za jinsi ya kuzalisha, jinsi ya kuanzisha viwanda na ku-maintain ubora na ku-maintain kufungasha vizuri katika njia ambayo inavutia walaji, lakini vilevile kuuza katika soko la ndani

na hata la nje kwa maana ya masoko ya Afrika Mashariki na Afrika kwa ujumla. Wizara hii ni muhimu na ya kimkakati sana katika masuala ya kukuza uchumi na kuondoa umaskini. Hata hivyo, tungependa kuona moja kwa moja mchango wake unavyoonekana kufuatana na mipango yake. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikatai sasa hivi ndiyo tumeanza hizi mbio za kwenda kwenye uchumi wa viwanda na kwa mwaka huu tunaweza fusione viwanda moja kwa moja; lakini japo ile mipango ioneshe mwelekeo wa Serikali katika kuhakikisha kweli hivi viwanda tutavifika. Tuondoe hizi kejeli ambazo tunazisikia hapa kuwa ooh, mnasemasema tu! Oooh, mnapanga panga tu, uwezo wa nchi hii kuwa na uchumi wa viwanda upo, lakini tujipange vizuri, tuwe *realistic*, tusijiwekee malengo ambayo tutashindwa kuyafikia, lakini tuanze pole pole kwa mwelekeo mzuri utakaotuhakikishia kuwa mwisho wa siku tunaweza kufanya hili jambo. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa sijawatendea haki akina mama na vijana kama sitazungumzia suala zima la mchango na ushiriki wa wanawake na vijana katika suala zima la viwanda. Wanawake na vijana ni wazalishaji wakubwa na wana jeshi kubwa nyuma yao. Hili ni lazima lichukuliwe maanani wakati wa mipango yote ya viwanda. Viwanda vidogo vidogo, biashara ndogo ndogo nyingi zinaendeshwa na makundi haya makubwa mawili, sasa tunapozungumzia viwanda vilevile lazima na wao tuwabebe, tuhakikishe kuwa akina mama na wao wanawezeshwa katika masuala ya usindikaji, vifungashio na mafunzo muhimu ya jinsi gani ya kuboresha huduma anazozitoa. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, akina mama wamekuwa ni wafumaji wa nguo; masweta, wengine tunatoka kwenye Mikoa yenyе baridi sana, akina mama wangeweza kuwekewa viwanda vya kufuma masweta na soksi na nini, badala ya kuagiza sweta na *uniform* za watoto kutoka China, eeh wakawekewa mifumo hiyo wakafuma masweta wakawa wanauzwa katika nchi yetu hata nje ya nchi, hiyo ingekuwa ni ajira tosha na ingeinua kipato na maisha ya akina mama wengi sana. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wengi sana wanamaliza vyuo vikuu na shule mbalimbali katika ngazi mbalimbali, wangetengewa hawa utaratibu kwa kupitia BRELA ambayo ndiyo inaandikisha makampuni wakawekewa namna ya kuandikisha makampuni yao, wakawekewa namna ya kufundishwa jinsi ya kuzalisha na kuanzisha biashara mbalimbali au uzalishaji mbalimbali wakapata ujuzi huo, wakaunganishwa na mitaji kutoka benki, wakaanzisha biashara zao wenyewe bila kungojea kuhangaika kuajiriwa na mtu yeyote. Hiyo ingekuwa ni njia moja ni rahisi sana ya kukuza viwanda nchini kwetu kuanzia vile vidogo na kadri wanavyoendelea kuwa wakubwa wakakua mpaka wakaja kuwa na viwanda vikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Roma haikujengwa siku moja ndugu zangu, lakini tukianza vizuri tunaweza tukafikia malengo yetu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizugumzie sasa kidogo Mgodi wa Kiwira. Mgodi wa Makaa ya Mawe wa Kiwira ni mgodi ambao uko lleje, Jimbo ambalo mimi ndio Mbunge wake. Mgodi huu haujawahi kunufaisha lleje. Kwanza ulikuwa hautambuliki kama uko lleje wakati kijigrafia na kwa njia nyingine zote uko lleje. Haya, hayo tuyaaache, hiyo ni historia!

Sasa hivi tunaambiwa mgodi ule upo tayari kufufuliwa na ule mgodi ulianzishwa ili makaa ya mawe yale yatumike kwa ajili ya umeme. Lleje ni Wilaya mojawapo ambayo haina umeme, viwanda, barabara, haina kitu chochote ambacho unaweza ukakizungumza kuwa ni cha maendeleo zaidi ya kilimo, lakini rasilimali zimejaa pale, zimetuzunguka. Napenda sasa Mheshimiwa Waziri utakapokuja hapa, uwaeleze wana lleje mgodi ule utafufuliwa lini? (Makofii)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea! Mheshimiwa Zainabu Nuhu Mwamwindi, atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Adadi. Mwamwindi hayupo! Tunaendelea na Mheshimiwa Balozi Adadi.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii kuweza kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Viwanda. Pia nawashukuru wapiga kura wangu, Wanamuheza kwa kuendelea kuniamini na kuweza kunifanya niendelee kuongea hapa leo. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Viwanda ni Wizara muhimu sana. Ni Wizara muhimu kwa sababu inaendana na malengo ya Awamu ya Tano; wananchi wa Tanzania wengi wana mategemeo makubwa sana na Wizara hii; wana mategemeo ya mabadiliko mengi sana kwenye Wizara hii; wana mategemeo ya kupata ajira nyingi kutokana na viwanda ambavyo Awamu ya Tano inategemea kuviveka. Kwahiyoo, Wizara hii ni Wizara ambayo ni ya muhimu na Wizara ambayo tunaitegemea itakuza uchumi wetu, italeta ajira nyingi na itatuondolea umaskini kwa kiwango kikubwa. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda ambavyo vilikuwepo tangu enzi za Mwalimu ni viwanda vingi, lakini vile viwanda vingi vimekufa. Sasa hivi kinachofanyika ni kutaka kuvifufua hivyo viwanda. Mkoo wa Tanga ulikuwa ni mmoja wa Mkoo ambao tulikuwa tunaongoza kwa viwanda hapa nchini.

Tuikuwa na viwanda karibu 180 na sasa hivi viwanda ambavyo viko ni 50 tu, ndio viwanda vikubwa na vidogo ambavyo tunaweza kusema kwamba ndio vinafanya kazi katika Mkoa wa Tanga. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama alivyosema Waziri kwenye hotuba yake kwamba malengo ya kwanza ni kuanza kuvifufua viwanda hivi, lakini hatuwezi kufufua viwanda hivi kama hatujajua vile viliviyokufa vilikufa kwa sababu gani. Kwa hiyo, tutakapovifufua viwanda hivi tutakuwa tunajua kwamba vile ambavyo vimekufa vimekufa kwa sababu gani, tusirudie hayo makosa tena. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muheza ni sehemu mojawapo tulikuwa na kiwanda. Tulikuwa na kiwanda cha matunda. Matunda ambayo yanazaliwa Muheza ni matunda ambayo yanajulikana hii Afrika na ulimwengu mzima. Sisi tunaweza kutoa matunda tani 100,000 kwa mwaka. Ni matunda ambayo yanaweza kuwa ya pili au ya tatu katika Bara la Africa baada ya South Africa na Egypt.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Muheza tunatoa machungwa mengi, lakini sasa hivi hatuna kiwanda cha machungwa. Wanakuja Wakenya, wanajaa pale, wanajaza hoteli za Muheza, miezi miwili iliyopita ilikuwa ukija Muheza huwezi kupata nafasi kwasababu wamejaa Wakenya pale kuchukua machungwa yetu ku-cross kupeleka Mombasa kwenye viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nategemea Mheshimiwa Waziri, atakapokuja ku-wind up kwenye hotuba hii, atatoa matumaini ya kiwanda cha matunda cha Muheza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuhitaji kiwanda cha matunda Muheza, lakini pia tunazalisha viungo vingi kuna pilipili manga, hiliki pale baada ya Zanzibar, kuna karafuu na mdalasini. Wanakuja watu kutoka nchi za nje wanajaa Wilayani pale kwa ajili ya kuchukua malighafi hizo na kuzipeleka nje. Kwa nini tusiweke hata kiwanda kidogo pale? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ame-present hotuba yake kwa nguvu sana na inaonekana inatoka moyoni kwake. Kwa hiyo, tunategemea utekelezaji wake utakuwa ni mkubwa ili wananchi wa Muheza na wenyewe waweze kufaidika na Mheshimiwa Waziri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunategemea kwamba viwanda hivi basi vitakapozalisha vitalindwa. Nimefurahishwa sana na Mheshimiwa Rais aliposema kwamba kuanzia leo basi furniture zote za maofisini ziwe zinatokana na malighafi yetu ya humu humu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuna kiwanda chetu cha kamba, kama unavyojua katani, ni zao letu kubwa Mkoani Tanga, ni zao letu kubwa Wilayani Muheza. Kiwanda cha Ngomeni cha kamba ambacho ni kiwanda kikubwa Afrika Mashariki na Kati, ni kiwanda kimojawapo ambacho watu wanalipa hela kabla hata hawajapata hayo mazao yake ambayo wanayataka pale. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunategemea kwamba kiwanda kile kinatakiwa sasa kisaidiwe na Serikali. Nilikwenda pale na kuongea na uongozi, wakaniomba. Wao wanaomba kitu kimoja tu, wanaomba Serikali iwave tender ya wao kutengeneza mazulia ya maofisi zote za Serikali kwenye nchi hii na uwezo huo wanao, ni suala la kubadilisha zile mashine zao pale na kuwapa mashine nydingine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namtegemea Waziri ataweza kuwapa upendeleo kiwanda hicho, kukuza kiwanda hicho kiweze kuzalisha mazulia yote ambayo yanatengenezwa kwenye ofisi zote za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niongelee suala la EPZA. Kwanza nawashukuru sana EPZA kwa sababu wameweza kujaribu kuweka maeneo ambayo wawekezaji wakija wanaweza wakaoneshwa, ni hatua moja nzuri sana. EPZA imejikita zaidi kwenye Foreign Direct Investment (FDI). Vitu vyote wanaelekeza nje, vinapelekwa nje; vikitoka kule, vinatengenezwa, then vinarudishwa hapa hapa. Sasa nilitaka wapanue wigo wa kuweza kuwfanya Watanzania na wenyewe waweze kuelimika na kuwa wataalam na waweze kufanya vitu hivyo wao wenyewe na kuviuza hapa hapa nchini; kuleta mashine ambazo zinaweza kufanya kila kitu hapa hapa nchini na kuweza kutoa mali ambayo inaweza kuwa ni nzuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanga tunataka tufaidike na bomba hili la mafuta la kwenda Kampala.

Kwanza tunaisifu sana Serikali kwa kuweza kupata hiyo zabuni ya kutengeneza hilo bomba la mafuta, lakini tunataka tuhakikishe kwamba tunaongeza value kwenye hilo bomba ili wananchi wa Tanga, wananchi ambaao bomba hilo litapita sehemu zote, waweze kufaidika nalo. Wanaweza kufaidika nalo namna gani?

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea! Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, atafuatiwa na Mheshimiwa Vedasto Edgar Ngombale.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na ni mara yangu ya kwanza kwenye bajeti hii ukiacha maoni ya Kamati niliyoyatao hapo mbele kuchangia kwenye bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana na kumpongeza sana Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa hotuba nzuri iliyojaa takwimu ambazo tunazihitaji, na mimi sihitaji kurudia takwimu hizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna Taifa lilioendelea bila viwanda. Viwanda kwanza vinatumia teknolojia, lakini viwanda vinazalisha teknolojia kwa ajili ya sekta nyingine. Kama viwanda ndiyo vinavyozalisha teknolojia ya kuboresha sekta nyingine, itakuwaje nchi hii iondokane na umaskini bila ya kuwa na msingi wa viwanda? Kwa hiyo, naishukuru Serikali kupitia Mpango wa miaka mitano kufanya msingi wa maendeleo uwe ni viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na umuhimu wa viwanda, mimi nilisomea uchumi wa viwanda, maisha yangu mengi sana nilifanya kazi viwandani kama Ofisa mdogo mpaka nikawa Meneja Mkuu. Siwezi hata siku moja nikaongelea maendeleo bila viwanda. Napenda kusema kwamba uendelevu wa viwanda unategemea sana sekta ya kilimo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya kilimondiyo inayotoa chakula kwa wale watakaofanya kazi viwandani. Sekta ya kilimo ikiongeza tija ndiyo itakayoleta ajira kwenda viwandani, ikisaidiana na sekta ya elimu. Kwa hiyo, ndugu zangu, hatuwezi tukaongelea maendeleo ya viwanda na msingi wa uchumi wetu na maendeleo yetu kama hatutatilia nguvu sana sekta ya kilimo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya kilimo ili iweze kutekeleza wajibu wake katika kuendeleza viwanda, ni lazima iwe ni kilimo cha kisasa. Tutumie zana bora na kisasa, tutumie mbolea na mbegu za kisasa; tutumie viwatilifu, lakini hatimaye ni viwanda ambavyo vitaongeza maisha ya malighafi na chakula kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri, ninampongeza sana.

Kwa hiyo, sisi wote ili tuweze kui-support Serikali au kuipa msukumo kwa msingi huu wa viwanda ili tufikie uchumi wa kati na wa viwanda, tukubaliane kwamba bila ya kuongeza bajeti kwenye kilimo, tusahau maendeleo ya viwanda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema kwamba wakati wa ukoloni mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo ulivunjika nchi hii. Tulikuwa tunakula tusichozaalisha na kutumia tusivyozaalisha na tunapeleka nje vitu ambavyo tungepaswa vitumike kwenye viwanda vyetu. Sasa ni lazima turudishe mnyororo

wa thamani ya mazao ya kilimo. Namna moja ya kurudisha mnyororo huu ni kupitia viwanda, kwasababu baada ya kufanya kazi mashambani, lazima mazao yale yatakayozalishwa na wakulima yasipopata masoko viwandani ni sawa na kutupa shilingi chooni. (Makofii)

Kwa hiyo ndugu zangu, wakati tunakazania sana kilimo, namna moja ni kukazania viwanda ambavyo vitachakata au vitasindika mazao ya kilimo. Na mimi naomba Bunge hili liazimie kwamba viwanda ambavyo tutaanza navyo ni hivi ambavyo vitakuwa na uhusiano wa karibu na kilimo ambavyo vitaipa kilimo malighafi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hivyo waliotangulia kutoa mchango kwa viwanda wamesema miundombinu ni jambo muhimu, na mimi naungana nao kwamba bila miundombinu viwanda haviwezi vikaendelea. Ndiyo maana hapa katikati kutohana na ukosefu wa umeme hatukuweza kuanzisha na kuendeleza viwanda vingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Muhongo aangalie sana mgao wa umeme kuelekea kwenye viwanda kama tunataka kuwa na viwanda. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niongelee jambo moja; ndugu zangu, kuna viwanda mama, kuna viwanda vya katì na kuna viwanda vya kuchakata. Bila viwanda mama hatuwezi kuwa na viwanda vingine. Kwa hiyo, napenda kwa muda uliobaki niongelee umuhimu wa Liganga na Mchuchuma. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Liganga na Mchuchuma ni viwanda mama. Mchuchuma itatoa makaa kwenda kwenye mradi wa chuma. Kwa hiyo ndugu zangu, tuna jambo moja ambalo Wabunge wengi hawalifahamu kuhusu chuma cha Liganga. Chuma cha Liganga siyo kama maeneo mengine ya migodi ya chuma ina kitu kinaitwa mchanginyiko wa madini mengine ambayo kama huna teknolojia sahihi huwezi ukapata chuma safi kutoka Liganga. Kwa hiyo, siyo rahisi kupata wawekezaji ambao wana ujuzi huo, naomba mjue hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana tutoe msukumo kuanza utekelezaji wa mradi huo. Ilituchukua muda mrefu kupata mwekezaji wa Liganga; na naomba niseme kwamba nilishawahidi kuwa Waziri wa Viwanda ili mjue kwamba ninaposema hivyo, nasema mambo ambayo nafahamu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipotangaza tender ya Mchuchuma, ilituchukua muda mrefu kupata teknolojia sahihi. Teknolojia hiyo watu wengi wanaipiga vita ili sisi tuendelee kutokuwa na chuma tuagize nje. MJUE KWAMBA

kuagiza chuma nje itakuwa ni ghali kwa viwanda vyetu kwa sababu mazao ya chuma ni mazito na kwa hiyo ni lazima zitakuwa na gharama ya kuleta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna nchi yenye bahati kama Tanzania, Liganga na Mchuchuma ni mwendo mfupi tu! Kwa hiyo, tutakapotengeneza chuma, makaa ya mawe tunayoyahitaji yatakuwa pale karibu. Naomba sana tupiganie mradi wa Liganga uanze mapema inavyowezekana kama kweli tunataka kuwa na viwanda Tanzania. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunataka tuwe na viwanda na kilimo bora, tukazanie viwanda vya mbolea vile vile. Tuna gesi lakini wale wanaoleta mbolea kutoka nje, hawataki tuwe na viwanda vya mbolea. Ninawaombeni sana hilo mliljue. Mtwara ina gesi na mambo yanayowezekana tuyafanye sasa, tuanzishe viwanda na hivi ndivyo vinaitwa viwanda mama. Kiwanda cha Chuma, Kiwanda cha Mbolea na mashamba ya mbegu ndiyo yatakuwa ni msingi wa uchumi wa kati wa viwanda. Tukifanya hivyo, tutafanikiwa na mpango huu wa miaka mitano au utabaki kwenye vitabu kama ilivyokuwa muda uliopita. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoka mbali, sasa hivi nimetoka Hanang, naomba niwakumbuke watu wa Hanang tena kuendelea kuwashukuru sana kwa ajili ya kunipa kura na nitaendelea kuwajibika kwao. Naomba ushirikiano wa dhati na ninaomba ushirikiano wa Wizara ya Viwanda na Bunge hili ili kweli nchi hii iwe nchi ya viwanda na uchumi wa kati kupitia kilimo cha kisasa na haiwezi kuwa kilimo cha jembe. Ahsanteni sana na Mungu awabariki. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana kwa kutunza muda, lakini kwa mchango wako mzuri. Mchangiaji wetu anayefuata kama nlivyosema ni Mheshimiwa Vedasto Edgar Ngombale atafuatiwa na Mheshimiwa Saed Ahmed Kubenea.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pia nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu na kwa mara nyingine tena kwa namna ya kipekee niwashukuru wapiga kura wa Jimbo la Kilwa Kaskazini. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala zima la uwekezaji wa viwanda katika mazao ya bahari. Mikoa ya Kusini ambayo inapakana na Bahari ya Hindi haina viwanda vinavyosindika mazao ya bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kwamba Mikoa ya Kusini inapitiwa na mkondo wa Kilwa (*Kilwa Channel*), mkondo ambao unafanya eneo la Kilwa na Mikoa ya Kusini liwe ni mionganini mwa maeneo machache yanayozalisha samaki kwa wingi. Kwa bahati mbaya kabisa mpaka leo baada ya miaka zaidi ya 54 ya Uhuru hatuna kiwanda cha kusindika mazao ya bahari. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Lindi pia unapakana na Mto Rufiji na delta za Mto Rufiji. Delta za Mto Rufiji zimetokana na Mto Rufiji ambao unatiririsha mboji nyingi kutoka Mikoa ya Bara. Maeneo haya yanababisha bahari hii ya kusini iwe maarufu kwa uzalishaji wa kamba. Tunazalisha kamba wengi, lakini kwa bahati mbaya hatuna kiwanda cha kusindika mazao ya bahari. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, sisi watu wa Mikoa ya Kusini tuna mazingira wezeshi ambayo yanaweza kupelekea kuanzhishwa kwa kiwanda katika maeneo yetu. Tuna barabara nzuri ya lami, tuna umeme wa uhakika unaotokana na gesi, lakini tuna ardhi ya kutosha. Kwa mfano, katika Jimbo langu maeneo ya Miteja pale, pana ardhi ya kutosha inayowezesha kuanzhishwa mchakato wa kuanzhishwa kiwanda, lakini kwa bahati mbaya hatuna kiwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hilo sasa wavuvi wetu kutokana na kukosa hilo bado wanajihuisha na ku-preserve samaki kwa njia ya kukausha, zile njia za kijima kwamba sasa inalazimika wakaushe ili wapate ng'onda. Bado tunawafanya wavuvi waendeshe shughuli zao katika njia za kijima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme ukianzia maeneo ya Moa - Tanga mpaka Msimbati - Mtwara, kuna viwanda viwili tu vya kusindika mazao ya samaki. Hii haitengenezi ustawi wa wavuvi wetu wa maeneo ya mikoa ya Kusini. Sasa naomba commitment ya Serikali kwamba Mheshimiwa Waziri atakapokuja atuelekeze ana mpango gani wa kujenga kiwanda cha kusindika mazao ya bahari katika maeneo ya mikoa ya Kusini? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, niende moja kwa moja kwenye suala zima la uwekezaji katika kilimo cha muhogo. Nilipata kumsikia Mheshimiwa Waziri akisema kwamba Serikali sasa imewezesha kutuletea wawekezaji wa China na wamechagua eneo la mikoa ya Kusini hususan katika Jimbo langu la Kilwa Kaskazini kwamba wataanzisha kilimo cha mashamba makubwa ya mihogo. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hilo, naipongeza sana na nichukue fursa hii kuwakaribisha wawekezaji hao, waje, maeneo yapo, tuna ardhi ya kutosha, watu wapo na kwa bahati nzuri sasa tuna umeme huu wa REA. Kwa hiyo, wazo la uwekezaji wa kilimo cha muhogo liende sambamba na kujenga kiwanda cha kusindika mazao ya muhogo. Bila kumung'unya maneno, napendekeza kiwanda hicho kijengwe katika Jimbo langu katika Tarafa ya Njinjo. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala zima la kiwanda cha kuzalisha mbolea Kilwa Masoko maeneo ya Kilamko. Wakati harakati za kusafirisha gesi zinaanza kutoka maeneo ya Kilwa kuja Dar es Salaam, kati ya

ahadi zilizotolewa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi wakati wa mfumo wa chama kimoja mwishoni mwa miaka ya 1980 ni kwamba gesi ile ije Dar es Salaam lakini watu wa Kilwa walihidiwa kujengewa Kiwanda cha Mbolea maeneo yaa Kilamko. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa ninavyozungumza, hakuna kiwanda zimebakia hadithi. Kilichotokea ni kwamba, watu wa TPDC walichukua zaidi ya hekari 800 maeneo ya Kilwa Masoko na hawajaziendeza mpaka leo. Kinachotokea sasa ni kwamba wao walisema watawalipa fidia watu 28 tu. Toka mwaka 1989 walipochukua maeneo hayo mpaka leo ninavyozungumza, kuna zaidi ya watu 1,000 wako pale. Kwa hiyo, watu wa TPDC wamekuja lakini kwa msimamo wa kwamba wao watafidia watu 28 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naitaka Serikali ihakikishe kwamba wakati wa mchakato wa kujenga kiwanda kama mlivyotuhidi, wakati tunakumbuka maumivu makubwa ya kuondokewa na gesi yetu kwenda Dar es Salaam, tuwakumbuke pia wale wananchi ambao wapo katika eneo lile. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la muhimu ni kwamba sasa hivi sisi watu wa mikoa ya Lindi na maeneo ya Kilwa ni wazalishaji wakubwa wa zao la ufuta. Wilaya ya Kilwa peke yake inazalisha zaidi ya tani 25,000 za ufuta, lakini mpaka leo bei ya zao la ufuta inasuasua kwa sababu hatuna kiwanda cha kusindika mazao ya ufuta. Sijapata kusikia kama kuna kiwanda cha kusindika mazao ya ufuta. Ninaona tu kwamba Serikali inaendelea ku-entertain kwamba zao la ufuta lisafirishwe kama zao ghafi kitu ambacho kinawaumiza wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate maelezo ya Mheshimiwa Waziri atakapokuja atuambie Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha sasa zao hili la ufuta linapata viwanda vya usindikaji ndani ya nchi? Nashukuru, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako, Mheshimiwa Saed Ahmed Kubenea atafuatiwa na Mheshimiwa Mwalimu Kasuku Samson Bilago.

**MHE. SAED A. KUBNEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kupongeza hotuba ya Msemaji wa Upinzani Bungeni aliyoitao leo asubuhi. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeambiwa na nimemsikiliza Waziri wa Viwanda akizungumza jinsi ya kuifanya Tanzania iwe ya viwanda, lakini katika hotuba nzima sijasikia Serikali ikitisema kwa nini viwanda vyetu vilikufa? Nchi hii ilikuwa na viwanda vingi, ilikuwa na mashamba, ilikuwa na migodi na mabenki,

yamegawanywa na yameuzwa kwa bei ya kutupa, halafu leo Serikali inakuja inasema inaaniszisha viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea kwamba wangkuja na mkakati wa kutueleza kwanza viwanda vyetu vilikufaje. Tumeambiwa, baadhi ya Wabunge wamezungumza humu kwamba viwanda vyetu vimekufa kwa sababu Taifa hili halina uzalendo. Nikiangalia Waheshimiwa Wabunge na Mawaziri waliomo humu ndani upande huu wa pili, asilimia kubwa sio wazalendo. Viwanda hivi hata vikianzishwa vitakufa! Hata kuanzishwa, havitaanzishwa! (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna fedha kwenye bajeti hii ya kuanzisha viwanda. Bajeti nzima imetengewa shilingi bilioni 80. Kiwanda kimoja zaidi ya shilingi bilioni 60, unajenga wapi hivyo viwanda? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikimwangalia huyu Waziri na mbwembwe alizokuja nazo asubuhi kwamba ataanzisha viwanda, namfananisha na yule aliyekuwa Waziri wa Habari wa Iraaq wakati wa vita vya Ghuba ya Pili Al-Sahaf; ndiye mwenye mbwembwe kama hizi. Anaweza kukuaminisha pepo wakati bado uko hai, hujafa, akakwambia kuna chakula kiko hapo, kula, chakula hakipo! Huyu anafaa kuwa Waziri asiye na Wizara Maalum, ahamasishe kuzibua mito, ahamasishe kuzibua mitaro, hiyo ndiyo kazi anayoiweza, siyo kazi kubwa kama hii. Viwanda haviwezi kujengwa kwa namna hii. Huyu anaweza kufanya kazi ya uhamasishaji, ile ambayo inaweza kufanya na watu wale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2015 nilipata nafasi ya kwenda Uingereza. Nikiwa pale Uingereza nilitembelea kituo chetu cha biashara cha London. Nilikwenda Ubalozi, wakatueleza, pale London kuna kituo chetu cha biashara kinaitwa *London Trade Center*.

Kituo hiki kilianzishwa baada ya maelekezo ya Rais wa wakati huo mwaka 1989. Hali ya kituo cha London inasikitisha! Wafanyakazi wa Kituo cha London hawajalipwa mishahara toka Disemba mwaka 2015. Mkurugenzi wa Kituo cha London, nyumba yake inadaiwa kodi, hajalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameandika barua chungu nzima kwenye Wizara, Mheshimiwa Waziri anazo barua hizo, wanakumbushia juu ya malipo ya mishahara, wanakumbushia malipo ya pango, lakini Serikali haijapeleka fedha London. Wakati Waziri anajibu hoja za Wabunge nataka alieleze Bunge hili Tukufu ni lini Serikali itapeleka fedha za mishahara London?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo hiki kimefanya kazi kubwa sana ya kuitangaza Tanzania nje, lakini wafanyakazi wa kituo hiki wameachwa solemba, wameachwa yatima. Wameandika barua, kuna barua hapa ya tarehe 22 Februari, 2016. Kuna barua wanaeleza jinsi ambavyo wasivyokuwa na fedha,

wako hoi, hata kazini hawawezi kwenda, hawana nauli, halafu mnaweka watu nje wadhalilike! Wamekopa, mpaka mzigo wa madeni umewazidi! Kama hamuwezi, warudisheni Tanzania, badala ya kuja na mbwembwe hapa mtaanzisha viwanda; mnashindwa kulipa wafanyakazi wenu walipo London, mtaanzishaje viwanda? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni mchungu. Bahati mbaya sana, tukizungumza sisi tunaitwa wapinzani. Amezungumza Mheshimiwa Bashe, amewaambia mnahitaji miujiza ili muweze kutekeleza hii bajeti. Sisi tunazungumza kama Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kujenga nchi kama huna bandari. Sisi Mungu ametujalia tuna bandari, lakini bandari yetu tumeiua. Leo mizigo inayopita bandarini asilimia 40 ya mzigo imeshuka kwenye makontena. Matokeo yake, badala ya kuiendeleza bandari, kila siku tunakwenda kuvunja Bodi ya Bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Harrison Mwakyembe amekuwa Waziri wa Uchukuzi, amekwenda kuvunja Bodi ya Bandari, akamfukuza na Mkurugenzi wa Bandari Mheshimiwa Mgawe; amekuja akaunda Bodi yake. Akaja Mheshimiwa Sitta akafukuza Bodi ya Mwakyembe; akaja Waziri Mkuu akafukuza Bodi ya Mheshimiwa Sitta na mionganoni mwa Wajumbe waliofukuzwa ni Naibu Spika. Sasa haya ni mambo gani? (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo bandari miezi mitano haina Bodi, haina Management, unaendeshaje nchi? Bandari haina Mkurugenzi, unaendeshaje nchi? Halafu unasema unaweza ukaleta Tanzania ya viwanda; viwanda vipi bila bandari? Ndiyo maana Waziri katika bajeti yake yote, anazungumza juu ya bomba la gesi linalotoka Uganda kwenda Tanga. Pia kuna reli inajengwa kutoka Uganda kwenda Rwanda. Katika mipango hii ya Waziri hakuna reli ya kutoka Kagera ambako ndiko karibu na Uganda, lakini hakuna mpango mkakati wa biashara katika mkoa huu; na huo ndiyo mkoa Waziri anakotoka! Mkoa wake! Hakuna biashara! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisemi afanye upendeleo, lakini hii ni kuonesha kwamba hakuna connection kati ya Waziri wa Viwanda na Biashara na Waziri wa Miundombinu, hakuna! Hiyo ndiyo Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefika mwaka 2015 wakati wa kampeni, mimi sio mwenyeji sana huko, Rais Magufuli aliongelea Special Economic Zone Kagera. Katika eneo alilolisema nadhani ni Omukanjuguti, labda akina Mheshimiwa Tibaijuka na Mheshimiwa Lwakatare wanaotoka huko, wanaweza kujua zaidi. Utueleze basi katika majibu yako, mipango gani ya kibiashara

unayopanga kwa ajili ya kilimo cha mboga na matunda kinachohitajika uwanja wa ndege? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo ya kuzungumza bila kuleta hoja nzuri hatutafika. Hapa tunazungumza juu ya mradi wa Mchuchuma na Liganga, lakini wale Wachina, nyaraka zilizopo na Serikalini mnazo, zinaonesha Wachina hawana fedha ya kuendesha huu mradi, wanataka kukopa dola milioni sita kutoka Benki ya Exim na dhamana yao ni Mchuchuma na Liganga.

Sasa mali yetu inachukuliwa dhamana halafu Mheshimiwa Nagu anasimama hapa anasema tuwe na viwanda. Alikuwa Waziri wa Viwanda na Biashara na ripoti ya CAG imesema ule mkataba ni fake, uvunjwe; Mheshimiwa Mama Nagu akiwa Waziri. Mambo gani? Mnaambiwa mnasema tunatukana. Sisi tunawaeleza! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii haitaenda kwa ngonjera na usanii na kwa mtu kuwa Al-Sahaf. Nchi hii itakwenda kwa uchumi endelevu kwa watu kukaa kwenye meza, kuchora uchumi, kuendesha nchi kwa data, hesabu, numbers. Bila hesabu, bila namba, hakuna uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalize kwa kusema kwamba Taifa letu limebahati, lina utajiri mkubwa, lakini tusije tukarudia makosa wakati wa ubinafishaji. Tuliiza mabenki, tukauza viwanda...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SAED A. KUBENA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea. Mheshimiwa Mwalimu Kasuku Samson Bilago, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Seif Ungando.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii adhimu. Awali ya yote, nawapa pole wanawake wote waliodhalilishwa jana, maana pande zote walidhalilika; wanawake hawana chama; kudhalilishwa hakuangalii chama. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kwanza nijue suala la viwanda kama ni vision ya nchi au ni vision ya Mheshimiwa Rais? Mheshimiwa Waziri baadaye akija atusaidie, atuambie kama ni ya Mheshimiwa Rais atusaidie. Atakapovianzisha, hawataviuza wengine? Maana vilikuwepo, wakauza. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nashauri, kama inawezekana, kwa baadhi ya vitu tunavyoanzisha tuwe tunatunga sheria ya kuivilinda hivyo

tulivyovianzisha. Yaani siyo tunaanzisha, anakuja mtu mwingine baada ya miaka mitano, naye anabadilisha anakuja na mambo mapya mengine kabisa, kama vile hatukuwahi kuwa na kitu chochote hapa nchini. Kwa hiyo, hata hiki kitu kama kingefanikiwa, kitungiwe sheria ya kudhibiti, atakayekuja asikiharibu! (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingekuwa nchi zilizoendelea, waliouza viwanda vyetu wangkuwa ndani, jela! Walitakiwa wawe jela, maana mlilia kabisa ili twende kwenye uchumi imara wa nchi hii ni kuwa na viwanda na lilijulikana mapema, lakini sasa hivi ndiyo linatokea, linashamiri baada ya kuwa tumeviuza vile tulivyokuanavyo. Maana yake nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba wale walioviuza ndio wametufikisha kwenye uchumi mbovu tulionao! Kwa hiyo, nchi za wenzetu zilizoendelea, hawa walitakiwa watangulie Segerea ili watusaidie kujibu kwa nini wameifanya nchi kuwa maskini kwa kuza viwanda ambavyo vingetupeleka mahali pazuri? (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nzungumze mambo madogo kabisa yanayohusiana na viwanda. Wala tusiende kwenye viwanda vikubwa sana vya mtani wangu Mheshimiwa Mwijage, akiyaeleza unaweza ukadhani kesho asubuhi hii nchi inakuwa mbinguni. Hii nchi ni Tanzania ile ile, hii hii! Haiwezi kubadilika katika wiki moja, mbili, miaka mitano au kumi, haiwezekani! Atusaidie! Tena nimshauri, ni mtani wangu, aongee machache, atende mengi. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni hii hii ambayo machungwa yanaiza, hakuna anayeshituka; maembe ya wakulima yanaiza, hakuna anayeshituka; nyanya za Watanzania zinaiza, mnaagiza tomato sauce Ulaya na mko hapa hapa! Nanasi zinazooza ni nyingi! Nani kiongozi wa Serikali anaona uchungu kwa mazao yanayoweza kufanyiwa process ya viwanda na akashituka akasema hapa tuweke kiwanda? Tunaangalia tu! Wala havihitajiki viwanda vikubwa sana. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya kawaida sana vingeweza kututoa hapa tulipo kwenda mbele zaidi. Tunafikiria makubwa wakati uwezo wa makubwa hatuna. Hii bajeti ya Mheshimiwa Waziri haiwezi kutengeneza hayo yote tuliyoyasema na wafadhili tunaowategemea, Mheshimiwa Waziri atuambie, walikaa mkutano wapi, kwamba watakuja waweke viwanda Tanzania? Watakuja wawekeze viwanda vyetu Tanzania; uwekezaji Tanzania sasa hivi nao unaanza kuwa shida na unaanza kuwa taabu! Masharti lundo! Kwa hiyo, tungeanza na vitu vya kawaida, vya chini mno! (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi za wenzetu; nimeona Uingereza, mwananchi mkulima wa kawaida mazao yakiharibika, Serikali ina-compensate.

Sisi hapa halipo! Tunaliona la kawaida tu! Tena mazao yakiharibika ndiyo mnakwenda, jamani poleni, zile nyanya vipi, zimeharibika? Yaani ni jambo la kawaida tu, lakini hatujui nguvu aliyotumia, familia yake itaishije kwa taabu kabisa katika mazingira kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umezungumzia viwanda Kigoma kwenye swalii asubuhi. Mpango ule wa Kiwanda cha miwa na sukari Kigoma kilianza Bunge la Kumi. Mpaka leo hakuna muwa hata mmoja pale Kigoma! Kwenye kitabu chako hiki, hakuna hata ukurasa uliotaja ile miwa ya Kigoma, hakuna! Sasa watakuje humu hawamo? Hata hao wawekezaji wenyewe ambao wangkuja! (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kweli tunahitaji kukaa vizuri na hili suala la viwanda. Tusiwaaminishe sana Watanzania, baadaye watatuuliza maswali haya haya, humu humu kwamba hivi mlisema viwanda yaani kwa mbwembwe kwa mkwara kweli kweli, mmefika wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo naona linaleta shida, ni biashara ambayo iko chini ya Waziri mwenyewe. Nchi hii kufanya biashara ni *risk* yaani *owners risk*. Hakuna mazingira rafiki ya kufanya biashara katika nchi hii. Wakati wa uchaguzi mimi huwa naupenda sana, ni kwa sababu tu unakuwa ni muda mfupi. Watu wanafaidika na mambo yote mabaya yanasmama ili watu wapate kura, baada ya hapo yanarudi yale yale mabaya waliotendewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna watu wanateseka nchi hii kama bodaboda! Wanakimbizwa na polisi kila asubuhi! Tujiulize, wale watu wa bodaboda wangkuwa hawana hizo bodaboda, nani angekuta side *mirror* kwenye gari lake? Ujambazi ungekuwa mkubwa kiasi gani? Watu wametafuta ajira binafisi, lakini wanakimbizana na polisi kila asubuhi! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimboni kwangu, Wilayani kwangu Kakonko ili uweze kupata *TIN Number* unakwenda kilometra 300 za barabara zisizo na lami, kuifua Kigoma Mjini. Unamwambia mtoto wa watu afuate hiyo *TIN Number*, halafu afuate na leseni, sijui na vidude gani, kilometra 300, anakimbizana na oolisi tu! Bodaboda wangapi wamekufa wakiwa wanakimbizwa na polisi ili wawakamate tu wachukue fedha? Matokeo yake sasa umekuwa ni mradi wa polisi na mwenye bodaboda. Bwana eeh, una leseni? Wewe unaniulizaje leseni na jana sikuwanayo, unaniuliza leo tena? Anachukua fedha zake, anaweka mfukoni. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawakatisha tamaa wafanyabiashara wa nchi hii. Biashara ya maduka, VAT inasema hivi ili uweze kulipa VAT TRA, mwenye biashara awe na bidhaa inayozalisha shilingi milioni nne kwa mwaka. Wanakimbizana na wauza soda vikreti viwili, anakuja anampigia hesabu mtu

wa TRA, wewe unaiza soda, eeh, kreti tano kwa siku mara siku 30 mara mwaka mzima, anamtoza kodi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Ndiyo ya mwisho hiyo?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, muda ndiyo huo.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana! (Makofii)

**MWENYEKITI:** Mchangiaji wetu anayefuata ni Mheshimiwa Ally Seif Ungando atafuatiwa na Mheshimiwa Omari Tebweta Mgumba na Mheshimiwa Stanslaus Mabula ajiandae.

Mheshimiwa Mgando hayupo! Haya, tunaendelea. Mheshimiwa Omari Mgumba!

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Pili, namshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia kufika siku ya leo, kunipa afya na uzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, naomba niwape pole Wapiga Kura wangu wa Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki na Morogoro Vijiji kwa ujumla kwa mafuriko makubwa yaliyowakuta ya mvua ambapo mashamba yao yote yameharibika na mvua hiyo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mheshimiwa Dkt. Kebwe na Mkuu wa Wilaya kwa hatua yao waliyoichukuwa ya kutusaidia chakula ingawa kidogo lakini siyo haba, kimesaidia sana waathirika hawa! Nachukua fursa hii kuiomba Serikali, tunaomba misaada zaidi ya chakula katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nampongeza sana Waziri wa Viwanda na Biashara kwa hotuba yake nzuri ambayo inaonyesha dhamana aliyobeba ya kutimiza matakwa na ndoto za Rais wa Awamu ya Tano, Mheshimiwa John Pombe Magufuli. Kwa sababu Rais wa Awamu ya Tano tangu anaomba kura mpaka sasa anajipambanua kwamba Serikali yake itakuwa ni ya viwanda. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtie moyo Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara angalau ameanza kuleta mpango. Pamoja na wengine wanasesma

kwamba umekuja na mpango lakini fedha ambazo umeziomba ni chache sana, kuna tatizo moja ambalo kama wazungu wanavyosema, ukitaka kumnyima kitu Mwafrika, kiweke kwenye maandishi. Kwa sababu umeongelea vizuri kwenye ukurasa wa 140 kwenye mikakati yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza kabisa naomba ninukuu na umesema; "kuhamasisha sekta binafisi, kuanzisha na kuendeleza viwanda vinavyotumia malighafi za hapa nchini na kuvutia wawekezaji kujenga viwanda vya vifungishio (*packaging*) na kadhalika."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni nini maana yake? Maana yake ni kwamba siyo Serikali ndiyo itajenga viwanda, bali ni sekta binafisi ndiyo itajenga viwanda. Kazi ya Serikali itakuwa ni kuweka mazingira mazuri ya kuivutia sekta binafisi kuja kuwekeza katika viwanda na hatimaye kutoa ajira. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wenzetu wanaosema kwamba bajeti ni ndogo, nafikiri kwamba hiki kitabu kama ulivyosema au tulivyokiona ni kikubwa sana, watu wanaona uvivu kukisoma chote. (Makofii)

La pili, Mheshimiwa Waziri unalaumiwa na unaambiwa kwamba mpaka leo miezi sita haujaanzisha kiwanda chochote. Hawa wenzetu ndiyo maana tunasema wenzetu vigeugeu! Juzi tu hapa wamekuja walikuwa wanailaumu Serikali hii kuhusu kuhamisha fedha kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyininge kuwashudumia Watanzania. Leo hii ndani ya miezi sita, hili ndilo Bunge la Bajeti ya kwanza la Serikali ya Awamu ya Tano; kwa fedha gani ungeweza kuitumia kujenga viwanda hivyo ndani ya miezi sita? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri ndiyo maana ameleta hapa sasa tumpe ili mwakani akija ndiyo tumkabe koo. Kwa hiyo, niwaombe tu ndugu zangu kwamba pamoja na kwamba tunatamani sana hivyo viwanda vijengwe, lakini haviwezi kujengwa bila kupitisha bajeti na mipango aliyoileta katika Bunge hili na hiyo ndiyo kazi yetu sisi Wabunge, tumpitishie halafu tuje tumhukumu mwakani akija. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, naomba nichangie katika mpango wenywewe aliouleta. Mheshimiwa Waziri kama ulivyosema, mionganoni mwa changamoto zinazowakabili wawekezaji wengi ni malighafi isiyokuwa ya uhakika, maana yake nazungumzia viwanda ambavyo viro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitangaze *interest*, maana unaweza kusema mimi nazungumzia korosho. Mimi niliwhi kufanya kazi katika kampuni inayohusika na mazao ya biashara miaka 19 kwa ajili ya exportation.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachoongelea nina uzoefu kidogo wa kujua ni changamoto gani ambazo wanakumbana nazo hususan kwenye korosho, pamba, kahawa, mbaazi, dengu, choroko, mpunga na kadhalika. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie changamoto zinazowakabili wawekezaji wa viwanda vya korosho, kwa sababu viwanda hivi vinabeba uchumi mkubwa sana hasa kwa wakulima wa Mikoa ya Lindi, Mtwara, Pwani na sehemu ndogo ya Mkoa wa Morogoro katika upande wa Mkulazi kule tulikopakana na Kisarawe. Ndiyo maana nafarijika na hili kulizungumzia mara nyingi kwenye upande wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda hivi kama nilivyowahi kusema mwanzoni, sababu mojawapo ambayo wawekezaji wengi wamefunga viwanda vya kubangua korosho, mionganoni mwa sababu mojawapo ni mfumo wa stakabadhi ghalani ambao hauwapi fursa wawekezaji wa ndani kupata raw materials.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ule mfumo unaoenda kuwashindanisha wawekezaji wa ndani wenye viwanda pamoja na wabanguaji wa India kwenye uwanja mmoja. Haiwezekani hata siku moja mwenye kiwanda cha ndani atafute raw materials mpeleke kwenye mnada akashindane na wabanguaji wa India, hawezi kupata raw material. Ndiyo maana uliona sababu, kulianzishwa viwanda zaidi ya 10, tulishafikia kubangua zaidi ya tani 50,000, nchini leo vyote vimefungwa vimebaki viwili tena vinasuasua!

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo jambo jepesi, mtu kawekeza mtaji wake, karun kiwanda zaidi ya miaka mitano, leo anafunga na Serikali tumekaa kimya, wanahamishia nchi za wenzetu za jirani, kuna tatizo! Naomba kushauri katika hili, kama kweli tunataka kuwavutia wawekezaji wengi waje kwenye kuwekeza Tanzania husasan katika viwanda vinavyotumia malighafi za Tanzania, kwa mfano kama korosho, ni lazima tuwatengenezee mazingira mazuri ya kuhakikisha wanapata malighafi hiyo, la sivyo itakuwa ni ndoto. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupa mfano tu, kwa mfano, huwezi kushindana na India kwa sababu India wenyewe ukizungumza korosho, unazungumza siasa za India. Wale wana uwezo wa kubangua tani 1,600,000, lakini uzalishaji wao ni tani 600,000 tu. Kwa hiyo, ni lazima wanahitaji tani milioni moja kutoka nchi mbalimbali. Ndiyo maana wanawapa mpaka incentive ya 2% kwa ajili ya mtu ku-export korosho iliyobaguliwa kutoka India, Tanzania kwetu hakuna! Pia mtu akibangua kule, by product kwa maana ya vipande vya korosho, kwa maana ya maganda ya korosho, yote ni biashara lakini Tanzania hakuna. Kwa hiyo, kuna incentive kubwa zaidi India kuliko Tanzania. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu katika hili, tuweke kabisa Sera ambayo inatambulika na itawavutia wawekezaji kwamba mtu yoyote anayewekeza kwenye Korosho hapa Tanzania, tutahakikisha anapata raw material kwanza kwa ajili ya kutosheleza kiwanda chake kwa mwaka mzima, ndiyo turuhusu mnada mwingine kwa ajili ya kupeleka nje ya nchi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo watakuja, kwa sababu hata sera yetu nchini hairuhusu *ku-import raw material* kutoka nje, wakati nchi nyingine kama Vietnam na India wanaruhusu *ku-import raw material* kutoka nchi nyingine. Sababu ni nini? Kumpunguzia gharama za uzalishaji huyu mwekezaji. Kwa sababu usipomruhusu *a-import raw material* kutoka nchi nyingine, ukizingatia korosho ni biashara ya msimu ya miezi mitatu, maana yake unamlazimisha mwekezaji wa Tanzania, kama ana kiwanda cha kubangua tani 50,000 anunue hiyo raw material ya 50,000 kwa miezi mitatu na ai-store.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana nyingine gharama itakuwa kubwa kwenye storage, kwenye mtaji, kwenye weight loss, kwenye running na kwenye mishahara kwa ajili ya walinzi na wafanyakazi wengine kulinda hiyo, kitu ambacho kwingine hamna. Wanaruhusu ndani ya miezi mitatu kwa sababu biashara ya korosho ni *rotation business in the world*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii biashara, watu wanazunguka, wanunuzi ni hao hao. Miezi mitatu wako Tanzania, baada ya Machi wanakwenda India mpaka Juni; baada ya Juni wanakwenda Afrika Magharibi kwa maana ya Nigeria, Guinea Bissau na Ivory Coast. Kwa hiyo, mtu ana fursa, atakuja kununua hiyo mwezi Oktoba kwa ajili tu ya kutumia hiyo miezi mitatu, baada ya hapo anakwenda sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu muda siyo rafiki sana, nitakuona Mheshimiwa Waziri nikupe mchango zaidi katika hili ili ukusaidie katika kuwekeza katika kilimo hususan mazao ya kilimo. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nisije kusahau nyumbani, sisi ni wakulima wa matunda na ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mwijage kwa juhudzi zako kubwa unazozifanya kwa ajili ya kutukumbuka watu wa Morogoro hususan kwenye kilimo cha ndizi na kututafutia wawekezaji kwa ajili ya kiwanda cha ndizi ili tuweze kupata soko la uhakika kwa ajili ya matunda yetu, mananasi, ndizi na menginyo yanayopatikana ndani ya Morogoro Vijijiini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo naomba nitoe ushauri mwingine. Kwa sababu hii korosho tukibangua hapa tutapata ile korosho iliyobanguliwa ambayo kitalaam inaitwa kernel, lakini baada ya kernel kuna vile

vipande vipande. Hivi vipande vipande, soko hakuna kwingine zaidi ya India. Ila kudhibiti kutaka watu wakabangue kule, India wameweka *import duty* kubwa.

Nakuomba Mheshimiwa Waziri uende kwenye Ubalozi wa India ukawaombe angalau ili kuvutia wawekezaji waje wawekeze hapa, waondoe ushuru huu wa vipande ili tupate soko la hao wanaobangua hapa, vile vipande tukauze India.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nakuomba kwa sababu wewe ndio Waziri wa Uwekezaji na Biashara, katika suala la mchakato wa kupata leseni za biashara, ni vizuri ukafungua dawati moja ambalo litarahisisha hao wawekezaji kwa maana ya sehemu zote kupatikana katika...

*(Hapa kengele ililia kuashria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mgumba! Unaona na Mwenyekiti alinogewa kidogo, lakini ndiyo hali hiyo, umetusaidia sana. Tunaendelea Mheshimiwa Stanslaus Mabula atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christina Ishengoma na Mheshimiwa Ibrahim Raza ajiandae.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia na mimi angalau kidogo na nitajikita zaidi kwenye viwanda vyetu katika Jiji letu la Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kupata fursa nydingine tena leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka miaka michache iliyopita Mji wa Mwanza ulikuwa maarufu sana kwa viwanda vya samaki na watu wake wengi sana walipata nafasi za maendeleo, za kiuchumi na uchumi kwa kweli ulikuwa sana. Hata asilimia tunayoizungumza leo inayochangiwa kwenye pato la Taifa na Mkoa wa Mwanza imetokana sana na imetengenezwa na viwanda vya samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa viwanda hivi vya samaki leo ni viwanda ambavyo vinajiendesha kwa hali dhoofu sana. Nasema dhoofu sana kwa sababu zao hili la samaki miaka mitatu nyuma kiwanda kimoja cha samaki peke yake kilikuwa na uwezo wa kukata tani 250 kwa siku kikiwa kimeajiri wafanyakazi wasiopungua 600; na hawa walikuwa ni vijana kabisa wa kike na wa kiume. Leo tunapozungumza hapa, kiwanda kimoja cha samaki kati ya viwanda saba

kinakata tani zisizopungua 20 mpaka 72 kwa siku, kikiwa kimepunguza wafanyakazi kutoka 500 mpaka 750 kufikia wafanyakazi 96 mpaka 120. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri yake ni kwamba vijana wengi wamepoteza ajira lakini vijana wengi hawana pa kwenda ndiyo sababu unaona Mji wa Mwanza unazidi kujaa kwa vijana ambaa hawana kazi, kila mmoja anatamani kufanya biashara ya umachinga, kila mmoja anatamani kufanya biashara ya umama lishe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu! Tatizo liko kubwa! Mheshimiwa Waziri viwanda hivi vinakufa kwa sababu zao la samaki linapungua. Zao la samaki linapungua kwa sababu gani? Uvuaji wa njia za sumu umekuwa ni mkubwa zaidi na badala yake samaki hazipatikani kwa njia rahisi, lakini wenzetu wamezalisha samaki hizi na kwenda kuzivuna na kuzipanda makwao, leo unaweza kupata samaki wengi sana kutoka Ugiriki na kutoka Urusi na wameongeza ushindani zaidi kwenye soko letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *quality* ya samaki wanaovuliwa sasa kwa sababu uvuvi haramu umekithiri, hii sumu inasambaa sana. Unapozungumzia uvuaji katika Ziwa Victoria, mikoa hii inayotumia sana uvuaji huu kwa Ziwa Victoria, lakini zipo nchi za jirani, Uganda na Kenya, wanafanya biashara kama sisi. Sasa wazo langu hapo Mheshimiwa Waziri, ni lazima tuangalie njia mbadala. Tutafanyaje kuhakikisha tunaokoa, uvuvi huu haramu unaondoka na tunabaki na uvuvi sahihi ambaa unaweza kusaidia viwanda hivi?

Mheshimiwa Waziri, Mwanza kwa sasa ukipata mbinu mbadala ya kuhakikisha viwanda hivi vinaendelea na uzalishaji wake kama zamani, vinarudisha ajira kubwa iliyoangaka. Huna sababu ya kufikiria kujenga viwanda vipyta vya samaki kwa sasa Mwanza. Hivi tulivyonavyo, kama tunakwenda kujenga viwanda vipyta, hivi tunaviweka kwenye kundi gani? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kiwanda cha Mwatex pale, miaka kumi iliyopita, tangu tukibinafsisha mpaka leo, wafanyakazi kutoka 700 na kitu mpaka 30 na kitu kwa siku. Hata walioondoka hawajalipwa mpaka leo, imekuwa ni kero na kasheshe kila kukicha. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tuangalie hivi tulivyonavyo kwanza kabla ya kufikiria mbele. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunacho kiwanda cha Tanneries pale, nilikuwa nataka kumpa taarifa rafiki yangu Mheshimiwa Msigwa, bahati mbaya tu nilichelewa, nilitaka tu nimtaarifu kwamba unapozungumza Kiwanda cha Tanneries hakihuksiki na kuzalisha nyama, bali kinahusika na kutengeneza na kuzalisha mazao yanayotokana na ngozi. Kiwanda hiki kimeuzwa na kimekuwa godown, hakuna shughuli inayofanyika pale na tumepoteza vijana wengi ambaa naamini Serikali mngefikiria vizuri, leo vijana wetu wangekuwa

wanafanya kazi pale. Kwa maana siyo kwamba ng'ombe nao wamekufa, ngozi hazipatikani. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, majeshi yetu leo yanekuwa yanapata bidhaa za viatu kutoka pale, mikanda yao wangetoa pale na kadhalika. Sasa hivi tunavyozungumza, makampuni ya ulinzi yamekuwa mengi na maarufu sana nchini hapa. Wote hawa wanahitaji bidhaa za viatu hizi na mikanda yao ni hii hii ya bei za kawaida. Leo hata mikanda tunaagiza kutoka China na bahati mbaya sana inakuja ya plastiki ambayo haidumu, unanunua leo, kesho imekatika inabidi ununue mwengine.

Mheshimiwa Waziri nakuomba, tunayo kila sababu ya kuangalia umuhimu wa kiwanda hiki ambacho kilikuwa kinasaidia watu wa Mwanza kupata ajira na kadhalika, uangalie uwezekano wa kukifanya kirudi na sisi tukitumie kwa manufaa ya Watanzania wote. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza suala la uboreshaji wa viwanda tulivyonavyo, tunazungumza suala la anguko kubwa la ajira. Kama ajira hii ambayo vijana wengi wanaitegemea, leo kila tukija hapa, nami kila nikisimama nazungumza juu ya ukuaji wa Mji wa Mwanza. Leo yapo maeneo tupetenga kwa ajili ya EPZ, hizi EPZ zinafanya nini? Tunajenga leo, tunatenga leo, matokeo yake ni baada ya miaka 30. Waachiwe watu maeneo haya wafanye biashara zao nydingine za kawaida, maana kuendelea kutunza maeneo makubwa, na mimi nikupe mfano, walikuja watu wa NDC toka mwaka 1974 wakachukua eneo la zaidi ya ekari 305, sawa na ekari 705. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo haya yamekaa toka miaka ya 1980 mpaka leo, eneo halijaendelezwa na tumeambiwa eneo hili ni kwa ajili ya viwanda vidogo vidogo. Pia maeneo mengi yanayochukuliwa hayalipwi fidia kwa wakati. Tunajua Halmashauri zetu hazina uwezo mkubwa wa ukusanyaji wa mapato. Hebu nikuombe Wizara yako ione umuhimu na maana halisi ya kuhakikisha maeneo yote yanapotengwa kwa ajili ya viwanda, aidha vidogo vidogo au viwanda vikubwa, tafsiri yake tunataka kupunguza mzigo, lakini tunataka kukuza uchumi, zaidi ya yote tunataka kuajiri vijana wengi zaidi ili tufikie kwenye malengo ambayo ilani yetu inasema. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatuwezi kuboresha maeneo haya, hatuwezi kuokoa kundi kubwa la vijana ambao wanamaliza vyuo. Sio wanaomaliza vyuo tu, wako watu wana vipaji wanaweza kufanya kazi. Viwanda hivi tunavyovizungumza ni viwanda vinavyochukua watu wenye tabia tatu, wenye elimu ya chini, elimu ya katni na elimu ya juu, wote hawa wanataka ajira. Ni lazima tufike sehemu, kama tunataka kuepukana na matatizo ya msongamano wa vijana machinga, mama lishe na kadhalika kwenye maeneo

mengi, lazima tuhakikishe tunajenga viwanda, lazima tuhakikishe viwanda hivi vinahimishwa, vinakuwa sawasawa na vinafanya kazi zake kwa wakati. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nakuomba tu kwamba nitakuunga sana mkono lakini kubwa ninalotaka kulisema, Mheshimiwa Mwijage sisi tuna imani na wewe. Tunayo imani kubwa, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano amekuamini na sisi tunakuamini. Imani yetu tuliyonayo kwako tunataka kuona, tunajua huu ndiyo mwanzo, tunataka kuona hapo ulipo na hayo unayoyasema unayasimamia, unayafanya kazi. Na wewe ni jembe la shoka, hatuna shaka, hizi nyiningine ni kelele tu tumeshazizoea. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka uone watu hawana adabu, haiwezekani unazungumza, unatukana, unamaliza unaondoka bila kusubiri majibu. Hawana nia njema na Watanzania hawa. (Makofi)

**MHE. MBUNGE FULANI:** Wewe! (Makofi)

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Meshimiwa Mwenyekiti, tunataka watu ambaeo ukitoa hoja ya misingi kwa ajili ya Watanzania, ukitoa hoja kutetea vijana kwamba wanatafuta ajira, lazima ubaki upate majibu yake. Waangalie wako wapi? Mheshimiwa Kubenea yuko wapi hapa? Mheshimiwa Msigwa yuko wapi hapa? Wametukana, wameondoka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nataka niseme Waheshimiwa Wabunge, iko tofauti na lazima tukubali. Tofauti ya Mbunge wa CCM na Mbunge wa Upinzani ni kubwa na itabaki pale pale. Sisi ndio Wabunge wenye Serikali na hiyo ndiyo tofauti, hakuna namna nyiningine. Sisi ndio wenye Serikali, ni lazima tuiunge mkono Serikali hii, tufikie malengo ya watu wetu kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi. (Makofi)

Mhesimiwa Mwenyekiti, mtu mwengine, rafiki yangu Mheshimiwa Mussa pale anashangaa kila tunachokisema tunazungumzia llani. Kwenye ushindani kule si kila mtu alinadi llani yake. Haya ndiyo matunda ya llani ya Chama cha Mapinduzi. Leo ukisimama hapa unazungumza, mwisho wa siku unaomba. Ndugu yangu Mheshimiwa Mussa ameomba reli ya kati ianzie Tanga. Bila llani ya CCM usingeomba reli ya kati. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwashukuru sana na niendelee kuhimiza, naunga mkono bajeti asilimia mia moja, viwanda kwa ajira za vijana wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (Makofi/Vigelegel)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mabula kwa mchango wako. Mheshimiwa Dkt. Christina Ishengoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Ibrahim Raza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia kwenye bajeti ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa. Pili, nawashukuru wanawake wa Morogoro kwa kunileta tena humu Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri Charles Mwijage kwa mipango yake mizuri yote aliyoitaoa kwenye kitabu chake cha bajeti. Mheshimiwa Waziri unaweza, nakuamini, naomba ufanye kazi, yale yote uliyoyaandika kwenye kitabu na Kamati yako na Wizara yako muweze kuyatekeleza kama yalivyopangwa pamoja na Wizara yako. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa yote, hata wewe mwenyewe unavyoendesa Bunge lako hili Tukufu. Nianze kabisa na wafanyabiashara. Hapa naanza na sekta hii kwa sababu ya wafanyabiashara wadogo wadogo na hasa akina mama na vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mmoja ni shuhuda kuwa sekta hii kwa upande wa biashara, akina mama wengi sasa hivi, hakuna mama anayelala, kila mama anafanya biashara; na biashara nyingi wanazozifanya kama tulivyo sema kuwa viwanda sana sana ni usindikaji kutokana na malighafi ya kutoka kwenye kilimo. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasindika, lakini Mheshimiwa Waziri tatizo wanadolipata hawa akina mama, jambo la kwanza ni tatizo la kupata kibali cha TBS. Wanahangaika sana, mikoa yote. Watu wengi wanahangaika sana, hasa akina mama, kupata mambo ya TBS. Wanafanya usindikaji mzuri, usindikija wa mvinyo, usindikaji wa achali na mambo mengine. Kwa hiyo, naomba sana waelekezwe jinsi ya kupata TBS na minyororo yote ya kupata TBS iweze kufupishwa kusudi wapate TBS kwa urahisi. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwa wafanyabiashara hawa wadogo wadogo, naomba waweze kujengewa mazingira mazuri hasa kwa kupata mikopo ambayo kuwawezesha kufanya hii biashara yao kwa urahisi, kwa sababu wakifanya biashara ndiyo hapo hapo wanainua pato lao na pato la nchi kwa ujumla. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, ni kweli Serikali haifanyi biashara, lakini tunatafuta wawekezaji. Naomba sana

wawekezaji wanapopatikana, jaribuni kuwasambaza kwenye mikoa yote ya Tanzania. Kuna mikoa ambayo haijafaidika na viwanda hivi. Mikoa ya pembezoni bado haijafaidika sana na viwanda. Kwa hiyo, naomba uiangalie vizuri na yenyewe iweze kupata wawekezaji ilimradi cha msingi wawekezaji waweze kupewa miundombinu. Sana sana ni *land bank*, ili iweze kutiliwa maanani. Kwa sababu unampeleka mwekezaji, kwa mfano, unampeleka Morogoro, Iringa, Kagera au Pwani, lakini unakuta huko hakuna area ambapo anaweza akafanya. Huyo mwekezaji anahangaika, mwisho anarudi na inaonekana hana pa kufanya biashara na mwisho wake anahama anakwenda kwenye nchi nyingine. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee kuhusu viwanda. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais, amesema kuwa nchi yetu inabidi iwe nchi ya uchumi wa viwanda. Ni kweli inawezekana sisi yenyewe tukijituma. Tukijituma inawezekana. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri aangalie viwanda vilivyokuwepo, hasa miaka ya 1980, nchi yetu ilikuwa na viwanda vingi sana. Kwa mfano, nikianza na Mkoa wangu wa Morogoro, tulikuwa na viwanda vingi. Nianze na Kiwanda cha Juusi ambacho huwa nakisemea mara kwa mara kwa sababu mimi mwenyewe napenda sana juusi. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Juusi cha Morogoro na mikoa mingine iliyo karibu kwa mfano tumesema Mkoa wa Tanga, Muheza, Lushoto, Iringa na mikoa mingine wanalima sana matunda na mboga mboga. Kwa upande wa juusi naomba sana kiwanda hiki kiweze kuangaliwa. Mheshimiwa Waziri nakuomba sana kiweze kufanya kazi. Ni kweli ni aibu kuona watu wananunua juusi kutoka Saudi Arabia ambao kweli nchi yao siyo *fertile* kama nchi yetu. Kwa hiyo, naomba sana hili tuliangalie. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili siku moja niliongea lakini ikaonekana kuwa hivi viwanda, pamoja na Kiwanda cha Azam nikiunganisha pamoja, wanaleta sana sana *concentrate* ambayo siyo nzuri. Nchi yetu ni nzuri ambapo tunalima matunda. Kama kuna tatizo la ubora wa matunda, tulifanyie kazi. Tuna watafiti wetu, waweze kufanya kazi, huu ubora unaweza ukawaje ukatoa juusi ambayo haiwezi kuchacha mara moja. Tuifanyie kazi pamoja na maabara ziweze kuwepo za *ku-test shelf life* ya hii juusi iweze kuendelea kwa muda mrefu. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu bado niko hapo hapo, niongelee kiwanda cha ngozi. Tulikuwa na Kiwanda cha Ngozi - Morogoro ambacho sidhani kama kinafanya kazi. Kilikuwa kinatoa bidhaa ya ngozi, lakini sasa haipo. Kuna Kiwanda cha Kioo, tulikuwa tunapata sahani na vikombe lakini hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa upande wa kiwanda cha 21<sup>st</sup> Century hicho kinafanya kazi vizuri, lakini Mheshimiwa Waziri naomba ukiangalie mazingira yake kusudi kiweze kuzalisha kwa wingi na kitumie mazingira ambayo ni rafiki kwa mazingira, kiache kuharibu mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Waziri hivi viwanda viweze kusambaa mijini pamoja na vijiji, hasa mahali pale penye umeme. Naomba ushirikiane na Wizara nyingine kama Wizara inayoshughulika na mambo ya Nishati na Madini pamoja na Wizara ya Maji pamoja na Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda kingine ni Kiwanda cha Magunia. Tulikuwa na Kiwanda cha Magunia Morogoro, tulikuwa na viwanda vingi Morogoro, Morogoro ulikuwa ni Mkoa wa viwanda, lakini sasa hivi viwanda vyote kwa wastani havifanyi kazi. Siyo Morogoro tu, tulikuwa na Tanganyika Packers ya Dar es Salaam, tulikuwa tunakula nyama za makopo na samaki za makopo na kila kitu, lakini sasa hivi tuna-import vitu hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia kwa Mheshimiwa Waziri ambaye namuamini kuwa atafanya kazi hii, naamini kuwa viwanda vyote, kama alivyosema kwenye hotuba yake, viwanda vyote vilivyokufa atavifufua, naomba kweli vifufuliwe kusudi tuweze kupata ajira kwa vijana wetu, tuweze kupata ajira kwa akina mama, tuweze kupata masoko ya mazao ya kilimo ambayo wakulima wengi wanalima, lakini mpaka sasa hivi hawapati soko. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna viwanda vya korosho. Kwa mfano, Kiwanda cha Korosho Kibaha (TANITA), hakifanyi kazi. Najua hakifanyi kazi lakini na wewe Mheshimiwa Waziri unaelewa kwa nini hakifanyi kazi, naomba kifanye kazi ili wananchi wa Mkoa wa Pwani waweze kukitumia kwa kuuza korosho zao kupitia kwenye kiwanda hicho. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wenyewe naomba tuhamasishe wananchi waweze kufungua na kuanzisha viwanda vidogo vidogo hasa huku vijiji mahali ambapo kuna umeme. Tunashukuru sana kwa sababu sasa hivi vijiji angalau vingi vingi vina umeme wa REA... (Makofij)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa!

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa hayo machache ambayo nimechangia. Naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Haya! Tunaendelea, Mheshimiwa Ibrahim Raza, atafuatiwa na Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, mtani wangu, Mafia hiyo na binti yangu Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo ajiandae.

**MHE. IBRAHIM HASSANALI MOHAMMEDALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya nzuri kusimama hapa mbele ya jengo hili na niweze kusema kwamba ni mara yangu ya kwanza kuchangia katika Bunge hili. Nawashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Kiembe Samaki kwa imani yao kwa kunileta katika jengo hili, nawaambia ahsanteni sana wananchi wa Jimbo la Kiembe Samaki. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli, kwa kweli ameonyesha kwamba anataka kubadilisha Tanzania katika sekta zote za uchumi na hususan Tanzania yenye viwanda. (Makofii)

Katika kipindi kifupi Mheshimiwa Rais, ameweza kweli kuleta mabadiliko na matumaini kwa Watanzania wanyonge ambayo sisi Wabunge lazima tumuunge mkono kwa asilimia mia. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza vilevile ndugu yangu Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara kwa hotuba yake nzuri. Kwa kweli naweza kusema Mheshimiwa Waziri ambaye kapata hii Wizara ni kweli Mheshimiwa Rais hakufanya makosa kumchagua ndugu yangu. Nina imani ni mtu ambaye amebobeaa, ni mtu ambaye anajua, nasi tumuunge mkono katika kufanikisha yale ambayo yeye amejipanga, na sisi tuwe nyuma yake. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianze kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara. Kwanza nilikuwa namuomba Mheshimiwa Waziri kwamba hawa *TIC* wawe serious kidogo katika hao wawekezaji ambao wanakuja Tanzania kutaka kuwekeza. Kwa sababu Serikali inategemea *TIC* na kama *TIC* hawatakuwa serious katika suala hili kwa kweli tutawavunja moyo wafanyabiashara ambao kwa nia moja nzuri kabisa wanataka kuja kuwekeza Tanzania, kwa sababu Tanzania ni kisiwa cha amani. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri katika jengo la *TIC* pawepo na One Stop Centre ambayo mambo yote yanaishia kwenye jengo lile. Mfanyabiashara, tena mwekezaji asihangaike kwenda katika masuala mengine ya kutafuta vibali ambayo mwisho tunamvunja nguvu mwekezaji na huondoka hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nilikuwa nataka Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara aweke vivutio maalum kwa wale wawekezaji ambao wanataka kwenda kuwekeza Mikoani, kwa sababu sasa hivi wawekezaji wengi sana wanawekeza katika Mkoa wa Dar es Salaam. Kwa hiyo, pawepo na vivutio maalum kwa wale ambao wanataka kwenda kuwekeza Tanga, Mtwara au mikoa mingine ya Kigoma. Kuwe na vivutio vizuri vyatatu wajembe hapa. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwa ruksa yako ni kuhusu soko. Kwa kweli sisi Tanzania tuna nafasi nzuri sana ya kuzalisha mambo mengi sana. Mungu ametupa ardhi yenyewe rutuba nzuri sana, lakini hatukitumii ile ardhi, hatukitumii kile ambacho Mwenyezi Mungu aliyetupa. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara awaangalie katika kutafuta masoko. Tanzania leo hii tuna mananasi mpaka yanaiza yanatupwa. Leo Tanzania hii tuna embe mpaka yanaiza yanatupwa na matunda mengine, kwa kweli soko lipo nje, lakini hao ambao wanazalisha mashambani upeo wao mdogo kwenda kutafuta soko. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza kusema kwamba embe hapa Tanzania ukiuziwa shilingi 500 au shilingi 700 unaona nyingi sana, lakini embe hii hii ikiipelekwa nchi za Arabuni, basi tunanunua kwa dola moja au dola moja na nusu. Kwa hiyo, naweza kusema kwamba soko lipo lakini hawa wakulima bado hawajasaidiwa katika kutafuta masoko ya nchi za nje.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, kwa kweli Tanzania tumejaliwa kuwa na ardhi na matunda tunayo ya kutosha, kwa hiyo, tuwasaidie wakulima wetu katika kuwatafutia masoko. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine tuje katika hawa ndugu zetu Watanzania waliowekeza katika Kiwanda cha Saruji. Kwa kweli wanajitahidi kuzalisha saruji katika kiwango kizuri ambapo sasa hivi tunafurahi tofauti na siku za nyuma tulikuwa tunanunua saruji kutoka nchi nyingine lakini ilikuwa haina *quality*. Leo wenzetu ambao wamewekeza Tanzania katika viwanda vyatatu saruji wanatupa saruji nzuri na tuwapongeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilio chao hawa viwanda vyatatu saruji wanakuwa wanalipa *ten percent* ya *clinker*. Kwa hiyo, naomba Wizara ya Viwanda na Biashara iwaangalie katika hiyo kulipa *ten percent* kama kuna uwezekano wa kutolipa au wa wapunguziwe hiyo *ten percent* ili saruji tupate kwa bei nzuri ambayo sisi Watanzania wengi ambao sasa hivi tuko katika kujenga majumba, hata tukitembea mikoani huko vijiji, watu sasa hivi hawajengi tena kwa udongo, wanatumia saruji, Tanzania hii inabadilika! (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri aliangalie na suala hili. Vile vile nami niko tayari kumsaidia Mheshimiwa Waziri kama atataka nimtafutie masoko, kwa sababu mimi ni mfanyakibashara, ninakwenda nchi mbalimbali. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri niko tayari kufanya kazi na Wizara yako, niko tayari kukutumikia na *Inshallah* tutafika mahali ambapo Mwenyezi Mungu atatusaidia, Tanzania hii itakuwa ya viwanda na biashara. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, namshukuru tena Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii adhimu katika jengo hili Tukufu na ninamwombea dua Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, Mungu ampe nguvu, kutekeleza yale ambayo yeye mwenyewe, sisi tunayajua na tunayaona na nataka kumthibitishia Mheshimiwa Rais kwamba tutamuunga mkono kwa asilimia mia moja, wapinzani wetu wataisoma namba. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache, kwa heshima zote, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii adhimu na naunga mkono hoja hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara. (Makof)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea, Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, atafuatiwa na Mheshimiwa Taska Mbogo. Dau! Ehe, Mheshimiwa Mbogo atafuatiwa na Mheshimiwa Salim Turkey. Mheshimiwa Mbogo hayupo. Mheshimiwa Turkey!

**MHE. SALIM HASSAN ABDULLAH TURKY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata fursa hii. Na mimi nachukua fursa hii kumshukuru Allah Subhanah-Wataallah kwa kutujaalia afya njema, tuko mjengoni tunafanya vitu vya uhakika, hatujui kutukana, tunahakikisha nchi yetu inaenda mbele, uchumi unakua na wala hatutatoka hata siku moja ndani ya mjengo huu tunahakikisha Tanzania inakuwa na amani. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongesa sana Rais wetu Bwana Magufuli na hali kadhalika Rais wetu wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Shein kwa ushindi wake wa kishindo. Kwa sababu leo kama unavyojuu, timu za mpira zikiitwa, timu kama haijahudhuria, timu iliyohudhuria inapewa kombe. Sasa sioni sababu ya watu kunung'unika kwamba aah, kuna hili na lile. Umeitwa njo kwenye mech, hujaja, shukuru Mungu jipange tena kwa mech ijayo. (Makof)

Mhesjimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, nataka sasa nichangie katika uchumi wa nchi yetu. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara na wewe nataka nikupongeze sana kwa sababu una nia ya dhati ya kutekeleza kauli aliyoitangaza mwenyewe mkubwa wa nchi hii kwamba hii safari itakuwa ni nchi ya viwanda. Na wewe umekuwa kweli askari wake wa kwanza wa kuhakikisha hili linakuwa na unajitahidi sana! (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mawazo ambayo nataka niyatoe; tutake, tusitake Mji wetu wa Dar es Salaam, ndiyo soko kubwa la wenyewe viwanda, wenyewe biashara na kila kitu ni Dar es Salaam na hasa wazalendo wamewekeza sana katika viwanda vyetu. Naomba sana Serikali nayo kama inataka viwanda basi ihakikishe pale Dar es Salaam inajipanga kutafuta eneo na kuwaita wawekezaji wetu wa nchini kwanza waulizwe kwamba wao wana shida gani na tuweze kushirikiana nao kuona kwamba uchumi huu tunakuwa pamoja tunaendeleza vipi nchi yetu kwa ujumla. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili kama litawezekana Mheshimiwa Waziri, ninaamini kwamba Tanzania hii itabadijika. Vilevile nataka nizumgumze jambo lingine ambalo kwa kweli siyo Wizara husika hii, lakini nataka kusema kwamba Dar es Salaam ni mji wa biashara. Sasa hivi umefika wakati, na mimi naamini Rais wetu yule analiweza, Makao Makuu yahamie Dodoma, Dar es Salaam ubaki kuwa mji wa biashara. Pale ndiyo tutapata hali halisi ya uchumi wetu utakavyokuwa. Kwa hilo wala hatuna haja ya kutafuta fedha, majengo ya Serikali yote yale yaliyokuwepo kama utayabinafsisha kwa bei ya soko la dunia, basi pesa zile zinatosha kabisa kujenga Dodoma yetu mpya na Wizara zote zikahamia hapa. Kwa hiyo, hili nalo litazamwe. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja katika uchumi wetu baina ya Bara na Visiwani. Nataka kusema kwamba Zanzibar mara nyingi sana katika Muungano wetu tunakuwa tunaitazama Zanzibar kama mshindani katika uchumi wa Tanzania. Hii fikra nataka tuiondoe. Tanzania ni moja, kwa sababu leo kama Zanzibar itakua kiuchumi, basi tujue kwamba na Tanzania imekua ka sababu Bank of Tanzania ni moja ambayo ndiyo inahimili fedha yetu. Kwa hiyo, uchumi unapokua kokote, sote wawili tunakuwa pamoja. Kwa hili, naomba sana kwamba Wazanzibar wao mashallah wamejaliwa kwamba ni bingwa wa kufanya biashara. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnayoju Tanzania hii tuna wafanyabiashara wakubwa wawili, tuna Wachaga huku, tunao na Wazanzibar kule wakiongozwa na Wapemba. Sasa ninachotaka kusema ni kwamba lazima tupange uchumi ambao utakua kwa nchi yetu. Nimeshawahi kutoa wazo hapa, sasa hivi, vijana kama tunavyoona wanataka ajira; na ili ajira hizi zipatikane, basi Zanzibar tuitazame kama inakuwa center moja ya uchumi. Sisi sasa hivi ushindani wetu mkubwa ni Dubai. Kila kitu tukienda kununua, tunaenda Dubai. Watu wana ma-account Dubai, wana majumba Dubai, watu wanaenda kununua magari Dubai. Hii Dubai kwa nini tusiisogeze ikawa Zanzibar yetu pale? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Watanzania wote tusikubaliane kwamba sasa Dubai ya Tanzania ni Zanzibar na uchumi wote uje pale magari yaje pale bidhaa zote zikae pale na ugomvi wa kudaiana ushuru baina ya Bara

na Visiwani utaisha. Kwa sababu kama Zanzibar itakuwa freeport leo ukichukua mzigo Zanzibar ukileta Bara unalipa kodi kama zinavyotakiwa. Isipokuwa ukisema leo bandari hii kwamba Bagamoyo au Mtwara iwe freeport, utajizonga mwenyewe, kwa sababu utakamata vipi watu wasikuibie katika nchi moja? Bahari utai-control mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili naomba sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu tulismamie kwa nguvu zetu, ikiwezekana mwaka huu tuweke azimio la kuhakikisha kwamba Zanzibar inakuwa Dubai ya Tanzania. Hili lazima tufanye kazi pamoja na hapo ndipo uchumi wetu utakapobadilika. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nataka kueleza, Mheshimiwa Waziri toka ameingia madarakani FCC (*Fair Competition Commission*) pale kuna Bodi ambayo toka mwaka 2015 haipo. Sasa hivi tuna viwanda, tuna makampuni kibao, watu wameuziana share na kila kitu. Hatuwezi kwenda mbele kwa sababu Bodi inatakiwa iwepo pale ndiyo iamue. Sasa hivi kwa kweli ni mwaka wa pili, kesi nyngi ziko pale hazipati maamuzi. Naomba sana wewe ni mtu wa speed, hili ulisamamie kwa nguvu sana liweze kukaa vizuri. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka niseme, na-declare interest, mimi ni mfanyabiashara. Sasa hivi nchi yetu ina ukata mkubwa sana wa sukari. Leo inasikitisha sana kuona kwamba nchi hii watu wanahangaika kutafuta sukari. Miaka 21 iliyopita nchi hii tulibinafsisha viwanda vyetu vya sukari na watu ambao tuliwapa viwanda hivi walituhidi kwamba katika miaka mitatu mpaka mitano, Tanzania itajitosheleza kwa sukari. Leo wenye viwanda hawa inabidi tuwaalize, ni kipi ambacho kimefanya mpaka leo hatujaweza kujitosheleza? Wawekezaji wapya wakija hapa, baada ya muda unaona hawapo, ni kwa sababu gani? Isije kuwa kuna mitikasi ambayo inafanywa kuweza kuendelea na mfumo huu wa kila siku ikifika sukari hamna Tanzania, haitoshelezi. Hapa nataka Serikali iwe macho sana. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili jana nilikuwa na Mheshimiwa Adam Malima. Mheshimiwa Adam alipokuwepo hapa aliulizwa swalii kwamba tunataka kujua cost of production ya sukari katika nchi yetu, mpaka ameondoka Wizara ya Kilimo jibu hilo halikupatikana.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, nawe nakupa swalii hili, naomba ukija hapa utupe majibu ya cost of production ya sukari yetu ndani ya nchi hii ni kiasi gani? Halafu lingine mara nyngi sana watu huwa wanazungumza lugha hapa kwamba nchi nyngine zina-subsidize, lakini je, ile figure ya subsidize ni kiasi gani? Pia hatujui? (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, subsidization wanayopata kule, utakuta ni mtu anapata 10 percent to 12 percent. Leo sisi hapa tunavilinda viwanda hivi kwa kuweka 100 percent protection. Kwa nini tunaweka ushuru wa kiasi hicho? Kwanini tusiweke ushuru wa asilimia 25 au 45 mpaka 50 ili wakati bei duniani ikishuka, basi mtu aweze kufanya biashara hiyo kuweza kuwalisha Watanzania. (Makofi)

Leo katika Tanzania yetu hii, nani anayemtetea mlaji? Hebu niambieni! Sisi tuko wakulima pengine labda milioni mbili, wafanyakazi pengine milioni mbili, lakini watu milioni 40, mfumuko wa bei unawaumiza. Mishahara ambayo kwa kweli iko chini na maisha haya yakipanda kwa kweli hatumtetei haki mlaji huyu, wala hatumlindi. Naomba sana hili litazamwe kwa nguvu zote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nazungumzia...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji*)

**MHE. SALIM HASSAN ABDULLAH TURKY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja kwa nguvu zote. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mchangiaji wetu wa mwisho baada ya kuwasoma wengine ambao hawapo, Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Na mimi sina budi kuungana na wachangiaji wa awali kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara kwa kazi nzuri. Ni pacha wangu kabisa lakini pia ni mwanangu, kwa lugha ya upendeleo naona kwamba tuna sababu sasa baada ya kuangalia andiko lake hili, ni kwamba kweli tunaingia katika awamu ya viwanda na biashara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kabisa kwa kusema kwamba mpango uliopo mbele yetu ukitekelezwa na ninaona kila nia ya kuutekeleza, utatupeleka mbele. Napenda tu nisimame hapa kuchangia kwa kuboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini na ninafahamu kabisa kinadharia kama mwanauchumi kwamba ili uwe na viwanda na Mheshimiwa Waziri analijua na atakaposimama kujibu atueleze, ni lazima viwanda vinaendana na kilimo, maana yake wanasema ni *Agricultural Development* na *industrialization*, hivi vina kwenda pamoja. Huwezi kuendeleza viwanda kama hujaendeleza kilimo. Hutapata malighafi ya ku-feed hivyo viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyosema wachangiaji wengine, na mimi naomba nisisitize kwamba ni lazima tuwe na malighafi. Sasa mazao ambayo unayo, kwa mfano zao la sukari, mchele na alizeti; ukiniuliza mimi kwa uelewa wangu wa mambo kama mchumi, nitasema kwamba Taifa hili halina

sababu yoyote isipokuwa katika hali ya dharura kukubali kuingiza sukari, mchele au alizeti kutoka nje. Kwa sababu mafuta, kama unataka *industrialization* na hii inaitwa *nascent industrial development*. Lazima uwe na mkakati wa kulinda viwanda. Kila nchi zimelinda, Marekani, Uingereza na Ulaya imelinda. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha zaidi sasa, Jumuiya ya Kimataifa katika WTO inatulinda sisi tulinde mazao haya. Mheshimiwa Waziri utakaposimama, una mwambata wako yuko Geneva ambaye anaafuatilia mambo haya katika *World Trade Organisation, under special and differential treatment for least developed countries*. Mazao haya yamelindwa na Sheria za Kimataifa. World Bank wanapokuja hapa kutuambia tufungue milango, wanakuwa wanatuonea.

Kwa hiyo, katika zana ya biashara, hili nalo naomba lieleweke na Mheshimiwa Waziri utufafanulie utakavyofuatilia sasa na waambata wako wa biashara walioko Geneva ambao wanafuatilia mazungumzo ya Kimataifa kuhusu biashara duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri jambo hili litatusaidia sisi, kwa mfano mimi nasimama hapa kuzungumzia viwanda na biashara nikitoka pembezoni, Mkoa wa Kagera. Nadhani alikuwa Mheshimiwa Kubenea. Hapa ni lazima niseme kwamba na-declare *interest* nakubaliana na Mheshimiwa Kubenea kabisa kwamba sikuona mkakati wako kwa mikoa ya pembezoni. Watu wanasema Rwanda ni nchi ambayo haina bandari, lakini Kagera, Kigoma na Katavi ni mikoa ambayo haina bandari. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima tuwe na mkakati wa kusaidia mikoa ya mbali kuweza kufika bandarini. Mimi nafikiria suala ambalo Mheshimiwa Rais amelitilia mkazo na tunashukuru kumuunga mkono kwa nia yote, ni suala la hii *standard gauge* na reli inajengwa. Na mimi naomba niseme, reli hiyo ni lazima pia iwe na spur au mikondo inayoingia mikoa mingine ya pembezoni itakapokuwa inapita kusudi wote tuweze kuzifikia bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima hapa nikiri kwamba, Rais Museveni nataka nimpongeze kabisa, hatua hii tuliyofikia kwamba bomba la gesi sasa litapita Tanga. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi najua na naweza nikatoa taarifa kabisa kwamba Rais Museveni ilikuwa ni azma yake kwa sababu alikaa hapa Tanzania kama mkimbizi, alikaa Muleba pale kwako Mheshimiwa Waziri, Muleba Kaskazini, ndiye alikuwa anakaa pale anapigania uhuru. Sasa unaona kwamba ametoa shukrani, anatukumbuka na katika hilo lazima tumpongeze na tujipongeze. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika hali hiyo, tujipange sasa. Sisi walio wengi ni wakulima, wavuvi na wafugaji, na sisi ndio viwanda. Hivyo viwanda

vitahitaji malighafi. Sasa mnatuwezeshaje? Mnatuwezesha kwa miundombinu, lakini pia mnatuwezesha kwa mifumo ya kuweza kuwafanya waingie kwenye uzalishaji wa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaposema sukari isiingie, sukari ikiingia itaua viwanda vya sukari. Hata mtoto wa shule anajua hilo. Ili kusudi Watanzania wapate sukari ni lazima Wizara ya Kilimo iwe na utaratibu wa kuingiza sukari, lakini siyo kutumia wafanyabiashara. Wafanyabiashara wale ukiwapa nafasi wataingiza sukari ya zaidi na viwanda vyetu ndani vitakufa. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kabisa kwa mfano kiwanda cha Kagera sasa hivi hakizalishi kwa sababu mvua ni nyingi, mashine haziwezi kuvuna muwa, vitu kama hivyo.

Kwa hiyo, nataka kusema kwamba itatosha kabisa kwa sisi kuwasaidia wavuvi wetu wapate viwanda. Wavuvi sasa hivi wanahangaika kwa sababu ya nyavi, lakini pia na viwanda vya samaki vingi viko katika mikono ya watu binafsi. Mheshimiwa Waziri naomba uviangalie pia viwanda vya samaki, vinawezeshaje wavuvi? Viwanda vya samaki wenyewe havina utaratibu wowote wa kusaidia wavuvi, lakini utakuta hawapati bei wanayostahili na wakati mwengine mauzo hayaendi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukishajipanga ndani, sasa tunajipanga nje; na dunia ya Kimataifa inatusubiri. Nimeona Mheshimiwa Waziri umezungumzia vizuri AGOA (African Growth Opportunity Act), lakini kama unavyojua, Tanzania inasuasua na AGOA. Hatupati faida yoyote. Ninaweza nikasema kabisa, nilipokuwa bado Umoja wa Mataifa kwenye Shirika la Biashara nilipoanza kazi, Ulaya wametupa pia, AGOA ya Ulaya inaitwa ABA (All But Arms), unaweza ukaingiza kitu chochote Ulaya isipokuwa silaha. Hii ni trade offer waliyotupa, lakini kwa sababu hatujajiandaa... (Makofij)

(Hapa kengele ya kwanza ililia)

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni kengele ya kwanza eeh? (Makofij)

Sasa nataka kusema hivi, vijana wetu sasa; *trade presupposes exchange of goods and services*, yaani ni lazima muwe mnabadilishana kitu. Sasa vijana wetu wanapokuja kufanya biashara, tumewawezeshaje vijana wetu?

Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, naomba nisikie mkakati wako wa kuwasaidia vijana waanze kufanya biashara. Wale ambao wamemaliza darasa la saba lakini wana ujanja unaweza wakapewa hata *tuition* ya kuzungumza kiingereza kusudi waweeze kwenda kufanya biashara, maana yake huwezi

kufanya biashara za Kimataifa na wewe hujui lugha. Hiyo nayo tusidanganyane. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wachina hawa sasa hivi wanajifundisha kiingereza kila mahali. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba kwa upande wa biashara, tujue yaani tunajiandaaje na masoko? Vijana wetu wanapomaliza form four, form six, chuo kikuu, napenda kuona mkakati Mheshimiwa Waziri unaposimama hapa kujibu, utuambie. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa kabla kengele haijanigongea, Mkoa wa Kagera sisi tuko mbali; nimeshangaa kuona kwamba Omukajunguti hajijatajwa hapa. Pale Mheshimiwa Rais Magufuli, alituahidi kwamba ataweka Export Processing Zone.

Sasa napenda kujua kwamba hii Export Processing Zone ambayo itatukomboa sisi Wandakagera kuweza kuingia kwenye horticulture kwenda kuza mboga (vegetables), kama huna ndege huwezi. Kule Kilimanjaro wanafanya kwasababu kule kuna airport. Sasa kule Bukoba, huwezi. Hata ukienda kule kila kitu kwetu ni green lakini hamna miundombinu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huo ndiyo mchango wangu. Tunapozungumzia viwanda na biashara, Serikali hii imejipanga, napongeza sana juhudhi za Serikali, naunga mkono hoja, lakini na mimi nimechangia kinadharia kwa kusema kwamba inaendana na sekta nyingine. Huwezi kuzungumza viwanda na biashara *in a vacuum*, lazima uangalie kwamba itakwendaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo, naunga mkono hoja na kumpongeza mwanangu Mheshimiwa Mwijage, amefanya kazi nzuri. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Profesa tunakushukuru.

Waheshimiwa Wabunge, hapo ndio mwisho wa shughuli zetu kwa jioni ya leo. Nawashukuruni sana kwa michango yenu kwa hoja hii. Hoja hii itaendelea tena siku ya Jumatatu tarehe 9, ndiyo atahitimisha mtoa hoja.

Nina matangazo. Tangazo la kwanza linawahuwa Waheshimiwa Wabunge Wanawake wa Chama cha Mapinduzi, wanakumbushwa kufika Makao Makuu ya Chama cha Mapinduzi, saa mbili yaani kesho, bila kukosa. Mna kikao ambacho mnakifahamu.

Tangazo la pili, linahusu semina yetu kesho kwa Waheshimiwa Wabunge. Ni rudio hili, nimeombwa na Mheshimiwa Naibu Spika tulirudie tena.

Kesho Jumamosi tarehe 7 Mei, kutakuwa na Semina kwa Wabunge wote kuhusu nafasi ya Wabunge katika kukuza na kuimairisha usawa wa watu wenye ulemavu nchini. Semina hiyo itafanyika kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa na itaanza saa 5.00 asubuhi. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa. Ni semina muhimu sana hiyo.

Tangazo la tatu, itakumbukwa tangu Jumatatu ya wiki hii kumekuwa na utaratibu mpya wa kuthibitisha mahudhurio ya Waheshimiwa Wabunge, humu Bungeni. Naelewa bado suala hili, kwa sababu kitu kipyta kinakuwa na changamoto zake, lakini Uongozi wa Ofisi ya Katibu wa Bunge unataka uwathibitishie Wabunge wote kwamba mahudhurio yenu tangu utaratibu huu uenze yako salama, kwa maana kwamba kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanaenda kwenye centre ile kufanya zoezi hilo hata kwenye Ofisi ya Wahasibu kuulizia kama wamo. Uthibitisho ni kwamba mmo wote. Kwa hiyo, hilo halina tatizo lakini wataendelea kuli-perfect. (Makofii)

Tangazo la mwisho na lenyewe lilitangazwa mchana, linahusu mchezo wa kirafiki wa mpira wa miguu katika Bunge Sports Club na Maafisa wa Jeshi la Wananchi, Kikosi cha Ihumwa, kwenye uwanja wa Jamhuri, kesho tarehe 7 Mei, 2016 ndiyo, tukaone sasa mambo. Ni saa 10.00 jioni uwanja wa Jamhuri, karibuni Waheshimiwa Wabunge wote tuishangilie timu yetu. Hayo ndiyo matangazo manne ambayo nilikuwa nimepewa hapa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, naahirisha shughuli za Bunge hadi siku ya Jumatatu, tarehe 9 Mei, 2016, wiki ijayo saa 3.00 asubuhi.

(Saa 1.50 Usiku Bunge lilahirisha mpaka Siku ya Jumatatu,  
Tarehe 9 Mei, 2016 Taa Tatu Asubuhi)